

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Nane – Tarehe 8 Februari, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. THEONEST RUHILABAKE– KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU – MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:

Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea, Katibu!

NDG. THEONEST RUHILABAKE– KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali la kwanza leo linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mbunge wa Kiwengwa. Kwa niaba yake Mheshimiwa Abbas.

Na. 81

Zuio la Sherehe za Muungano

MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI (K.n.y. MHE. KHAMIS MTUMWA ALI) aliuliza:-

Serikali ilizuia sherehe za kuadhimisha muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuelekeza kusheherekea kwa kufanya usafi wa mazingira. Wakati ziuo hilo linatolewa maandalizi ya sherehe hizo yalikuwishaanza na gharama mbalimbali zilitumika ikiwemo mafunzo ya halaiki ya watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafidia wale waliotumia gharama binafsi wakiwemo wakufunzi wa maandalizi ya sherehe hizo?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mbunge wa Kiwengwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho ya sherehe za miaka 52 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 2016 yalifanyika kwa wananchi kupumzika siku hiyo na kuendelea kutafakari umuhimu wa Muungano wetu ambao unazidi kuimarika na hivyo kufanya shughuli mbalimbali kama vile usafi wa mazingira, kujitolea katika shughuli mbalimbali za maendeleo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali haina kumbukumbu zozote za watu binafsi waliotumia rasilimali zao kwa maandalizi ya sherehe hizo. Maandalizi hufanyika baada ya idhini kutolewa na viongozi wakuu hivyo hakuna mtu, kikundi au taasisi itakayofidiwa kwa namna yoyote ile.

MWENYEKITI: Ahsante. Swali la nyongeza kama lipo Mheshimiwa Abbas.

MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI: Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yamejitosheleza kwa hiyo hakuna swali la nyongeza.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali la pili ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel.

Na. 82

Gawio kwa Wanachama wa Hifadhi ya Jamii

MHE. RUTH H. MOLLEL aliuliza:-

Mashirika ya Hifadhi ya Jamii yamewekeza katika miradi mbalimbali kwa kutumia michango ya wanachama:-

Je, wanachama wamepata gawio kiasi gani na faida ya uwekezaji?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya hifadhi ya jamii imegawanyika katika makundi makuu mawili. Mifuko inayoendeshwa kwa mfumo wa pensheni yaani *defined benefits schemes*

na mifuko inayoendeshwa kwa mfumo wa akiba yaani *defined contribution schemes*. Mfumo unaotumika Tanzania ni mfumo bayana wa pensheni (*defined benefits schemes*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mfumo huu, malipo ya mafao ni ahadi ambayo mfuko huahidi kumlipa mwanachama pindi anapojiunga na mfuko kupitia vikokotoo maalum vya mafao vilivyowekwa kisheria. Hivyo, katika mfumo huu hakuna utaratibu wa kumlipa mwanachama gawio badala yake ukokotoaji wa mafao ya mwanachama huzingatia mshahara wa mwanachama na muda wa uchangiaji. Kwa mwanachama aliyechangia kwa kipindi kinachostahili (*vesting period*) na ambaye mshahara wake ulikuwa ukiongezeka katika kipindi cha ajira yake kiasi cha mafao anacholipwa wakati wa kustaafu ni kikubwa zaidi kuliko kiasi alichochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha pensheni wanacholipwa wastaafu nchini ni asilimia 72 ya mishahara yao ya mwisho. Kiasi hiki hulipwa kila mwezi kwa muda wote wa uhai wa mwanachama. Hivyo, uwekezaji na faida yote inayopatikana katika uwekezaji unaofanywa na mifuko ya hifadhi ya jamii husaidia mfuko husika kuweza kulipa mafao kama ulivyoahidi pamoja na mafao mengine ya muda mfupi kama vile mafao ya uzazi, matibabu na mazishi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo sijayafurahia sana mimi kama mstaafu, napenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pensheni hii ambayo tunalipwa kila mwezi kwa kadri miaka inavyokwenda gharama zinapanda na shilingi inashuka thamani. Nimemshuhudia hata baba yangu mzazi Mungu alimjalila umri wa miaka 90 lakini ile pensheni aliyokuwa anapata na alikuwa mtu mkubwa sana Serikalini ilikuwa kidogo sana kama asingekuwa na watoto wenye uwezo angekuwa ombaomba. Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba pensheni hizi za wastaafu zinawekewa hata *percentage* kidogo kusudi wasiwe ombaomba baada ya miaka kadhaa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hifadhi hizi za jamii zimewekeza sana kwenye majengo, Mheshimiwa Rais juzi alisema wawekeze kwenye viwanda. Je, imefanyika *actuarial study* kuona kwamba hii mifuko haitafilisika na baadaye kuleta adha kwa wanachama? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza la pensheni kidogo na kutaka kujua mkakati wa Serikali, katika utaratibu wa ulipaji wa mafao kipo kitu kinaitwa *indexation* ambacho ndiyo imekuwa ni nyongeza ya kiwango ambacho kimekuwa kikilipwa kila mara kwa wastaafu. Kwa takwimu zilizopo, wastaafu wengi walikuwa wakilipwa kima cha chini cha Sh.50,000 mpaka pale ambapo lilitoka tamko kupitia SSRA ambapo sasa hivi wastaafu wanaanza kulipwa kuanzia Sh.100,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko uliobaki ni mfuko wa LAPF tu lakini mifuko mingine yote sasa wataanza kuwalipa wastaafu kima kile cha malipo kuanzia Sh.100,000 na kuendelea na wamekwishaanza. Kwa hiyo, nimwondoe tu wasiwasi kwamba mifuko hii kadri inavyozidi kufanya uwekezaji wake na kadri ambavyo *returns* za *investment* zinaongezeka, watafanya kitu

kinaitwa *indexation* kuweza kusaidia ili wastaafu wao waweze kukidhi maisha na mahitaji ya dunia ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili lilikuwa ni la wasiwasi ya kwamba, je, mifuko hii ikienda katika uwekezaji wa viwanda haitashindwa kweli kutimiza majukumu yake ya msingi? Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, katika utaratibu wa uendeshaji wa mifuko hii, kuna kitu kinaitwa *actuarial valuation* ambapo huwa inafanya tathmini ya afya ya mfuko. Mpaka maamuzi haya yanafanyika ni kwamba mifuko hii tayari inao uwezo wa kwenda kufanya uwekezaji huo pasipo kuathiri michango au mafao ambayo wanachama wanastahili. Kwa hiyo, nimwondoe hofu kwamba *study* ya uhakika imefanyika ya kuifanya mifuko hii iende kufanya uwekezaji katika uchumi wa viwanda.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwalimu Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika majibu ya swali la msingi, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba mifuko hii iko imara. Kama kweli mifuko iko imara, kuna Walimu waliostaafu zaidi ya 6,000 hawajalipwa mafao yao zaidi ya shilingi bilioni 550. Walimu hawa wanateseka wakiwemo Walimu wangu wa Jimbo la Buyungu ambao kila wakati nahangaika kufuatilia mafao yao ya kustaafu. Ni kwa nini anayestaafu halipwi mafao yake kwa mujibu wa mkataba ndani ya miezi miwili baada ya kustaafu? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ni kwamba mifuko hii imeanza kulipa mafao na kwa hivi sasa SSRA inawasimamia kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanastahili kulipwa mafao wanalipwa. Zamani hapa lilikuwa linazungumzwa deni kubwa ambalo lilikuwepo hasa katika mfuko ambao unashughulika na watumishi wa umma ambao Serikali ilikuwa inadaiwa takribani shilingi trilioni 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninavyozungumza hivi sasa Serikali imeshalipa shilingi trilioni 1.2 na deni lililobaki ambalo Serikali inadaiwa ni shilingi bilioni 128 tu. Mfuko wa PSPF mpaka ninavyozungumza hivi sasa wameshalipwa takribani shilingi bilioni 720. Kwa hiyo, Mwalimu Kasuku kama bado kuna usumbufu huo, naomba unilettee nitazungumza na SSRA waweze kulifanyia kazi ili Walimu waweze kulipwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata linalizwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatere, Mbunge wa Bukoba Mjini.

Na. 83

Kulika kwa Kingo za Ziwa Victoria-Bukoba

MHE. WILFRED M. LWAKATARE aliuliza:-

Kingo za Ziwa Victoria katika mwambao wa Manispaa ya Bukoba katika maeneo ya Kalobela Bandarini, Hoteli ya Spice, Kiroyela, Nyamukazi na Kifungwa zimelika na maji na mawimbi ya maji kusogea kiasi cha kuingia kwenye nyumba zilizoko kandokando mwa ziwa hilo na kuhatarisha maisha ya watu:-

(a) Je, Serikali inachukuliaje hali hii na inawatolea tamko gani wakazi wa maeneo hayo?

(b)Je, Serikali iko tayari kutafuta mfadhili au kuchukua hatua za kujenga ukuta imara wa kuzuia maji kusogea jambo linalooneka kuhatarisha ofisi za Makao Makuu ya Mkoa, nyumba ya Mkuu wa Mkoa na majengo ya Mahakama?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa mmomonyoko katika fukwe za Ziwa Victoria mwambao wa Manispaa ya Bukoba hali inayohatarisha baadhi ya majengo na miundombinu iliyojengwa karibu na maeneo hayo. Hali hii inawezekana kuwa imesababishwa na kuongezeka kwa kina cha maji na kasi ya mawimbi katika Ziwa Victoria kutokana na matukio ya vimbunga, upepo mkali na mvua nyingi yanayohusishwa na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, hali hii pia yaweza kuwa inasababishwa na uharibifu wa mazingira kando ya ziwa na mito inayoingiza maji ziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa tamko kwa wakazi wa maeneo ya fukwe za Ziwa Victoria na maeneo mengine nchini kuacha kufanya shughuli za kudumu za kibinadamu zenye athari kwa mazingira ndani ya eneo la mita 60 kutoka kwenye kingo za ziwa kwa mujibu wa kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Hatua hii itasaidia kuzuia uharibifu wa mazingira na madhara yanayoweza kutokea kutokana na mmomonyoko wa kingo za Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafanya tathmini ya kina ili kutambua chanzo na ukubwa wa tatizo na kuchukua hatua stahiki za kuhimili athari hizo mara baada ya tathmini kufanyika. Ufadhili unaweza kutokana na vyanzo vya ndani, mifuko mbalimbali ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kama vile *Adaptation Fund, Least Developed Countries Fund, Green Climate Fund* na wadau wengine wa maendeleo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lwakatatare.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Swali la kwanza, kufuatia majibu ambayo yametolewa na Serikali na kukubaliana na ukweli kwamba kweli kingo za Ziwa Victoria zinalika na maji kusogea. Kutokana na majibu ya Serikali itakubaliana nami kwamba mita 60 za mwaka juzi siyo mita 60 za mwaka jana na mita 60 za mwaka jana siyo mita 60 za mwaka huu kiasi kwamba inaondoa hata usahihi wa majibu au ushauri uliotolewa wa kuwazuia wananchi wasifanye maendeleo ndani ya mita 60 kufuatana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Kutokana na ukweli huo, Serikali inatoa maelekezo gani kwa *experience* hii ya Ziwa Victoria ambalo linaendelea kusogea na kuondoa usahihi wa *application* ya sheria hiyo ya mita 60 kama ambavyo Serikali imeshauri? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kifungu cha 57(1) na kufuatia ukweli wa kijiografia wa Bukoba town na Mkoa wa Kagera kwa ujumla ambao kimsingi una milima, mabonde na mtiririko wa mito mingi na kwamba wananchi hawawezi kuwa na mahali pa kuweka makazi yao, Serikali inatoa maelekezo gani kwa *experience* hiyo? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza anazungumzia usahihi wa ziwa kusogelea wananchi na kwamba inaleta shida katika kutambua zile mita 60. Nilisema katika jibu langu la msingi kwamba tutaenda kufanya utafiti ili tuweze kuona hali halisi yenyewe ikoje. Kama maji haya yamesogea, yamesogeeje kwenda kwenye makazi ya watu ili tuweze kujua. Tutakapofanya hiyo tathmini ndiyo itakayotupa majibu kwamba ni ziwa lenyewe limewasogelea wananchi au wananchi wenyewe wamejenga ndani ya mita 60 au wamejenga ndani ya mwambao wa ziwa ambao hauruhusiwi. Kwa hiyo, tathmini ndiyo ambayo itatupa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopata majibu haya ya tathmini huwa kuna njia nne za kufanya:-

(a) Unaweza usichukue hatua yaani *not doing anything* katika ulichokiona.

(b) Unaweza ku-*accommodate* tatizo kwamba wananchi waishi kulingana na hali ya mazingira ilivyo kwa maana ya kwamba sasa wao wenyewe wazuie uharibifu wa mazingira, wakubali hali ya mazingira ilivyo, wajenge nyumba na miundombinu ambayo inaendana na hali halisi.

(c) Unaweza kupeleka njia za kuwazuia (*protection*) kama ambazo alipendekeza mwenyewe Mheshimiwa Lwakatare kwamba unaweza ukajenga ukuta, unaweza ukapanda miti, unaweza ukafanya mbinu nyingine za kuzuia maji yale yasiendelee kuwasogelea wananchi.

(d) Unaweza uka-*retreat* ambapo sasa unawataka wananchi wao wenyewe wahame na wasipotaka kuhama unawahamisha kwa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapofanya tathmini tutakuja na jibu la usahihi wa ziwa hilo na hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahali pa kuweka makazi na lenyewe vilevile linategemea tathmini tutakayoifanya ndipo hapo tutakapopata mwanya mzuri wa kuwashauri wananchi wa Bukoba nini cha kufanya. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na linaelekezwa kwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Na. 84

Changamoto Zinazokabili Zao la Korosho

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Zao la korosho linakabiliwa na changamoto kadhaa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Chuo cha Utafiti wa Kilimo – Naliendele kinapanuliwa ili kiweze kufanya tafiti mbalimbali za magonjwa yote ya korosho badala ya sampuli kupelekwa nje ya nchi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Utafiti Naliendele ni kituo mahiri cha kufanya utafiti wa kugundua na kutathmini aina bora za korosho zinazotoa mavuno mengi na zinazopendwa katika soko. Vilevile kituo kinafanya utafiti kuhusu mbinu bora za uzalishaji, magonjwa na wadudu wanaoshambulia korosho na utafiti wa kuongeza thamani ya zao la korosho. Pia ni kituo cha kwanza Afrika kutoa mbegu bora za korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naliendele ilipeleka sampuli za korosho nje ya nchi ili kupata ufafanuzi kama vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa ukungu au *blight* ni aina moja au tofauti. Ufafanuzi wa aina hii wa aina za vimelea utasaidia kuweza kupata viatilifu vya ugonjwa huu. Maabara za nje ya nchi ni maalum (*specialized laboratories*) ambazo hufanya uchunguzi wa magonjwa ya mazao mbalimbali ikiwemo zao la korosho kutoka katika nchi tofauti. Maabara za aina hizi ni ghali kuendesha hivyo kuwa na maabara ya aina hii hapa nchini itakuwa ni hasara kwa vile matumizi yake yatakuwa chini yaani *underutilized* ukilinganisha na fedha zitakazotumika kujenga na kutunza maabara hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kama alivyosema kwenye jibu lake la msingi kwamba kituo hiki kinafanya tafiti mbalimbali lakini wanashindwa kuhaulisha yale maarifa wanayopata kwenye tafiti zao kwa wakulima kwa sababu hawana fedha za kutosha za kuweza kwenda kwa wakulima Mtwara, Lindi na Pwani na kuwapa matokeo mapya ya utafiti. Serikali ina mpango gani wa kukiongezea fedha kituo hiki ili waweze kuwafikia wakulima wengi wa korosho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kiutilifu muhimu katika uzalishaji wa zao la korosho ni *sulfur dust*. Napenda kujua mpango wa muda mfupi wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inawashawishi wawekezaji wakubwa waje kujenga kiwanda cha kutengeneza *sulfur* Mikoa ya Lindi na Mtwara ili *sulfur* hiyo iuzwe kwa bei ya chini kama ilivyo sasa hivi kwa viwanda vya mbolea badala ya kuagiza *sulfur* hii kwa fedha nyingi za kigeni kutoka nchi za nje? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwepo na changamoto ya kibajeti itakayoweza Kituo cha Naliendele kuhaulisha teknolojia ya korosho kwa wakulima na Serikali mwaka hata mwaka bado inaendelea kuongeza bajeti, lakini lazima niseme kwamba mafanikio makubwa ambayo tumepata kwenye zao la korosho na hasa katika msimu uliopita umechangiwa vilevile na teknolojia ambayo imetoka Naliendele. Kwa hiyo, nakubali kwamba kuna haja ya kuongeza bajeti na Serikali iko tayari kufikiria katika bajeti inayokuja lakini lazima vilevile tuseme kwamba pamoja na changamoto hiyo Naliendele imesaidia sana katika kukuza zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa kiwanda cha *sulfur*, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba namna mojawapo ya kupunguza gharama kubwa za *sulfur* kwa wakulima wetu ni kuhakikisha kwamba tunazalisha katika viwanda vyetu vya ndani. Nipende tu

kumhakikishia Mheshimwa Mbunge kwamba tayari Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anafuatilia ujenzi wa kiwanda cha *sulfur* akishirikiana na Mheshimiwa Hawa Ghasia. Kwa hiyo, tunatumaini kwamba kitakapojengwa changamoto hii itakuwa imeondoka.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka kufahamu kwamba kwa muda mrefu Serikali kupitia Mfuko wa Wakfu wa kuendeleza zao la korosho umekuwa ukiruhusu pesa kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali kwenye kuongeza thamani ya mazao ya wakulima ikiwemo mabibo kwa ajili ya kupata *juice* ambayo inaonekana ina uwezo mara tano zaidi wa kupata *vitamin c* kuliko ilivyo kwenye machungwa. Pia mabaki ya korosho kavu ambayo ni kochoko na yenyewe kuna uwezekano mkubwa sana wa kuweza kupata *gin*. Baada ya tafiti hizi kukamilika ni muda mrefu sana umepita, je, Serikali iko tayari kuanzisha viwanda kwa ajili ya kutengeneza *juice* pamoja na *gin* ili kuweza kuongezea wakulima hawa kipato kwa sababu mabibo pamoja na kochoko sasa vitakuwa rasmi na vitaweza kununuliwa na Serikali?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilijibu swali la Mheshimiwa Conchesta na naomba nirudie kwa maslahi ya Wabunge wote na Watanzania. Serikali kazi yake ni kuweka mazingira bora ya wawekezaji. Mheshimiwa Mbunge, nakuomba uje tukae wote kusudi hizo taarifa ulizonazo za fursa ya uwekezaji tuweze kuziweka pamoja kwenye andiko zuri, tutangaze ili tuweze kupata wabia wa kuweza kuwekeza kwenye kiwanda hicho. Hata hivyo, mwekezaji mzuri ni Mtanzania, ni mwananchi wa Jimbo lako, ni wewe mwenyewe Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo na sisi tutafute rasilimali tuweze kujenga viwanda sisi wenyewe.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bilakatwe Innocent.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lilivyo swali la msingi, kwa zao la kahawa na migomba kuna ugonjwa uitwao mnyauko kwa jina lingine unaitwa ugonjwa wa manjano. Ugonjwa huu umeshambulia migomba pamoja na kahawa. Je, Serikali imefanya utafiti upi ili kulipatia ufumbuzi zao hili lisije likapotea? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kati ya magonjwa ambayo yameleta changamoto katika zao la migomba na kahawa ni ugonjwa wa mnyauko na kwa kipindi fulani umeleta matatizo makubwa sana katika Mkoa wa Kagera. Serikali ilichukua hatua mahsusi za kutafuta namna ya kuzuia ugonjwa huo na tayari kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya kampeni kubwa iliyofanyika kuudhibiti, Serikali ilishaudhibiti na sasa hali siyo mbaya sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na sasa tunahamia kwenye swali la zao muhimu la tumbaku, linaulizwa na Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima. (*Kicheko*)

Na. 85

Kuwatambua Wakulima wa Tumbaku

MHE. HASNA S. K. MWILIMA aliuliza:-

Tarafa ya Nguruka na Uvinza zinalima zao la tumbaku na kuiingizia Halmashauri ya Uvinza fedha nyingi kwenye makusanyo ya ndani lakini wamekuwa wakinyonywa kwenye bei ya uuzaji na upangaji wa viwango vya pamoja vya soko:-

Je, ni lini Serikali itawatambua wakulima wa tumbaku wa Uvinza ili nao wapate chama kikuu ndani ya Mkoa wa Kigoma na kuwapunguzia gharama za usafirishaji kwenda hadi Tabora?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa wakulima wa tumbaku kuendelea kunufaika na huduma zitolewazo kupitia vyama vya ushirika. Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni za mwaka 2015 ili chama cha ushirika kiweze kusajiliwa kinapaswa, pamoja na kutimiza masharti mengine, kikidhi kigezo cha kuwa na uhai wa kiuchumi katika maana ya *economic viability*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa chama kikuu kuanzishwa, uhai wa kiuchumi unazingatia viwango vya uzalishaji kwa mwaka wa vyama vya msingi vinavyohudumiwa na chama kikuu hicho na ufanisi wa mfumo wake wa masoko. Kwa mujibu wa matakwa hayo ya kisheria ili chama kikuu cha ushirika wa tumbaku kiweze kusajiliwa kinapaswa kiwe kinazalisha na kuuza angalau kilogramu milioni kumi za tumbaku kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa katika Mkoa wa Kigoma kipo chama kikuu kiitwacho *Kigoma Tobacco Growers Cooperative Union (KITCU)*. Chama kikuu hicho kinahudumia Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Uvinza. Takwimu zinaonesha kuwa kutokana na wanunuzi wa tumbaku kupunguza mahitaji ya tumbaku kwa mwaka, uzalishaji wa chama kikuu hicho umepungua hadi kufikia wastani wa kilogramu milioni nane kwa mwaka. Wilaya ya Uvinza ambayo inajumuisha Tarafa za Nguruka na Uvinza inazalisha takriban 55% ya tumbaku yote ya *KITCU*, ambazo ni takriban kilogramu milioni 4.5. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wilaya hiyo imezalisha kilogramu 3,586,175 za tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa hiyo na umuhimu wa kuzingatia Sheria ya Ushirika katika kuanzisha vyama vya ushirika, kwa sasa chama kikuu kingine cha ushirika kinachojishughulisha na zao la tumbaku katika Mkoa wa Kigoma hakiwezi kuanzishwa. Badala yake Serikali inajielekeza katika kuimarisha nguvu za uzalishaji za *KITCU*, chama ambacho makao yake makuu yako Nguruka katika Wilaya ya Uvinza ili kiweze kukidhi vigezo vya kiuchumi na kisheria na hivyo kuendelea kuwahudumia wanachama wake kwa ufanisi zaidi, wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Uvinza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hasna Mwilima.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, tarehe 16 Desemba 2016, wadau wote wa zao la tumbaku walikuwa na mkutano Morogoro na mgeni rasmi alikuwa ni Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba. Katika mkutano huo vyama vililalamika kuhusiana na kuwa na madeni ya muda mrefu yanayowasababishia kukosa mikopo ya pembejeo kwenye mablenki. Mheshimiwa Waziri alitoa tamko kwenye mkutano huo hapo Morogoro kwamba mablenki sasa wachukue yale madeni ya muda mrefu badala ya kuvibebesha mizigo vyama vya msingi yapelekwe moja kwa moja kwa mwanachama au mkulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwa msimu huu, mablenki hayajatekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri kutaka madeni yale yaelekezwe kwa mtu mmoja mmoja badala ya vyama. Je, nini kauli ya Serikali kwa wakulima wa vyama vya msingi kwenye zao hili la tumbaku waliokosa mkopo wa pembejeo kwenye msimu huu wa 2016? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kilimo cha tumbaku kinahitaji utunzaji wa mazingira na kwa mujibu wa kanuni ya zao hili kila mkulima anatakiwa kwenye hekta moja anayopanda tumbaku apande miti 150 na miti 200 apande kwenye mashamba yanayomilikiwa na vyama vya msingi. Kwenye Halmashauri yetu ya Uvinza vyama vya msingi tulivyonavyo vinahitaji jumla ya hekta 240 sawa na hekari 600. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvisaidia vyama vya msingi vya zao la tumbaku kupata maeneo ya kupanda miti?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama alivyoeleza kwamba mwaka jana Mheshimiwa Waziri alitoa kauli ya kuelekeza namna bora ya kulipa madeni ya muda mrefu yanayovikabili vyama vya msingi na alielekeza kwamba ufanyike utaratibu ili madeni yale yaweze vilevile kulipwa na wale wanaodaiwa moja kwa moja badala ya kuleta mzigo kwenye chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado huu ndiyo msimamo wa Serikali. Serikali itaendelea kufuatilia kwamba kwa nini hili halijatokea kama ilivyotakiwa kwa sababu tunaamini kuendelea kuvibebesha vyama vya msingi mzigo ndiyo chanzo cha vyama hivyo kuporomoka na hatimaye zao la tumbaku kuanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utunzaji wa mazingira, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ana uelewa mzuri sana kuhusu namna zao la tumbaku linavyotakiwa kuendeshwa kwamba ili uweze kuzalisha tumbaku ambayo ina vigezo vya kimataifa lazima iwe *environmentally compliant* (ikidhi vigezo vya mazingira) na ndiyo maana kuna hitaji la kupanda miti. Nitaongea na Mheshimiwa Mbunge ili niangalie namna ya kuongea na Halmashauri za Mkoa wake kuhusu namna ya kupata ardhi kwa ajili ya kupanda miti hiyo ambayo inatakiwa kwa ajili ya zao la tumbaku.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, angalieni na ninyi muda umekwenda. Tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi.

Na. 86

**Mazingira Magumu kwa Utendaji
Kazi kwa Askari Polisi Masasi**

MHE. RASHID M. CHUACHUA aliuliza:-

Jeshi la Polisi limekuwa likifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na uchakavu wa vitendea kazi pamoja na kukosekana kwa magari ya kutosha:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawapatia magari Askari Polisi wa Wilaya ya Masasi ili kupunguza ugumu wa mazingira ya kazi?
- (b) Je, ni lini Serikali itarekebisha utaratibu uliopo ambapo inafikia wakati askari wanalazimika kutoa pesa zao mfukoni ili kuwapa chakula mahabusu?
- (c) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za askari katika Wilaya ya Masasi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Wilaya ya Masasi kina magari mawili yanayohudumia Wilaya nzima. Hata hivyo, Serikali inatambua kuwa magari hayo hayatoshelezi mahitaji ya Wilaya. Aidha, Serikali inatarajia kupokea magari kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi wakati wowote kuanzia sasa na mara magari hayo yatakapowasili, Wilaya ya Masasi itakuwa miongoni mwa Wilaya zitakazogawiwa magari hayo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuwahudumia mahabusu wanapokuwa mikononi mwa polisi ili kupata huduma muhimu za kijamii. Mathalani katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali ilitenga zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuhudumia mahabusu walioko vituo vya polisi, mwaka wa 2016/2017, Serikali ilitenga zaidi ya shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya kuhudumia mahabusu walioko Vituo vya Polisi Tanzania Bara na Zanzibar.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la ukosefu wa nyumba za askari hapa nchini. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali ina mpango wa ujenzi wa nyumba kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha. Ndiyo maana Serikali inao mpango wa kujenga nyumba 4,136 kwa kupitia mkopo wa bei nafuu kutoka Serikali ya China kupitia Kampuni ya *Polytech* utakaogharimu dola za Kimarekani milioni 500.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chuachua.

MHE. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kuwahudumia mahabusu na kwa kuwa fedha hizo huwa hazitoshi kuwahudumia mahabusu wao. Je, Serikali ina mpango gani kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ili kuhakikisha kwamba Askari Polisi hawatoitena fedha mifukoni kuwahudumia mahabusu wanaowekwa ndani kenye vituo vyao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali imesema ina mpango wa kujenga nyumba 4,136 kwa awamu. Je, kati ya nyumba hizo ni nyumba ngapi zitajengwa katika Wilaya ya Masasi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kifupi tu. Naona swali hili lina mvuto kwa Wabunge wengi lakini muda ndiyo huo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la msingi nilionyesha takwimu ambazo zinaonesha kuongezeka kwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mahabusu ambapo nilisema kwamba mwaka 2015/2016 tulitenga zaidi ya shilingi bilioni 1.5 na mwaka unaofuata kwa maana ya mwaka huu tulionao tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 1.7. Hii inaonesha kwamba kadri tunavyokwenda mbele bajeti kwa ajili ya kuhudumia mahabusu inaongezeka. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha tunaongeza bajeti kila mwaka ili kuweza kutoa huduma za mahabusu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na nyumba ngapi zitajengwa Masasi, migao katika ngazi ya Wilaya bado haijafanyika, lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapofanya mgao kwa ajili ya Mkoa wa Mtwara vilevile tutazingatia na Jimbo au Wilaya yake ya Masasi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Niongezee tu sehemu ndogo ile ya upande wa vyakula kwa mahabusu na niunganishe pamoja na wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tatizo la kibajeti lakini pamoja na tatizo hilo pia kuna tatizo la matumizi ya fursa tulizonazo za uzalishaji katika taasisi zetu za Wizara ya Mambo ya Ndani. Mpango wa muda mrefu tunaopanga ikiwa ni ziada ya majibu aliyoyatoa ya kibajeti ni namna ya kutumia fursa tulizonazo hasa hasa katika magereza yetu. Magereza yetu yana mashamba makubwa, juzi nilienda Kigoma, mkoa ambao mazao yanakubali kuliko mikoa yote kwa msimu kama huu ambao una ukame lakini kwenye shamba lile lenye ekari karibuni 10,000 walilima kama ekari 50 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika magereza yote tukilima vizuri, tutalisha magereza, tutalisha mahabusu na tunaweza tukalisha mpaka na shule za sekondari. Kwa hiyo, mpango tulionao ni kwenda kujitegemea katika uzalishaji ili tuweze kulisha wafungwa na mahabusu. Tunamwomba ndugu yetu Mheshimiwa Dkt. Tizeba na Mheshimiwa Mwijage watusaidie tu matrekta ili tuweze kwenda kulima kisasa hata NFRA tutawauzia mazao kwa ajili ya kuisaidia Serikali. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa hayo uliyosema fika na Gereza la Matongo - Bariadi, wana eneo kubwa ambalo sisi tunalitaka. Mheshimiwa Kapufi. (Makofi/Kicheko)

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mazingira magumu ya ukosefu wa vitendea kazi kama magari, mafuta na makazi ya askari yanayowakabili askari wa Masasi yanaakisi hali halisi ilivyo Wilayani Mpanda. Je, ni lini Serikali itafikiria kujenga makazi ya Askari Polisi Wilayani Mpanda? Katika hili nafarijika Waziri alikuwa huko na alijionea hali ilivyo ya askari wetu Wilayani Mpanda.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi anachozungumza Mheshimiwa Kapufi hasa ukitilia maanani Mkoa wa Katavi kama ilivyo mikoa mingine mipya, ina changamoto siyo tu za makazi hata ofisi za vyombo vya usalama. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba katika mgao ambao tumezungumza maeneo ambayo ni mapya kimkoa na kiwilaya yatapelele kipaumbele ikiwemo Jimbo la Mpanda Mjini.

MWENYEKITI: Ahsante! Tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

Na. 87

**Uhaba wa Nyumba za Askari Polisi na
Magereza Wilaya ya Tunduru.**

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia nyumba za makazi Askari Polisi na Magereza katika Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma?

(b) Je, Serikali imejipangaje kufanya ukarabati kwa nyumba za askari zilizopo Wilayani Tunduru ambazo kwa muda mrefu hazijafanyiwa ukarabati?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa nyumba za makazi, maafisa na askari, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mpango wa kujenga nyumba mpya kwenye baadhi ya magereza nchini kwa kutumia fedha zinazotengwa katika fungu la bajeti ya maendeleo kila mwaka. Kwa kutambua uhaba na uchakavu wa nyumba za Askari Polisi na Magereza, Serikali ina mpango wa kuwajengea askari nyumba 9,500 nchi nzima ikiwemo kwenye Gereza la Wilaya ya Tunduru pamoja na nyumba 4,136 kwa upande wa polisi, ikijumuisha Wilaya ya Tunduru.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo la uchakavu wa nyumba za makazi za maafisa na askari, Serikali itaendelea kuzifanyia ukarabati nyumba za Askari Magereza na Polisi nchini zikiwemo za Wilaya ya Tunduru kwa kutenga bajeti ya ukarabati kwa kila mwaka wa fedha kutegemeana na bajeti itakavyoruhusu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikambo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ifahamike kwamba Wilaya nyingi zilizopo Mkoani Ruvuma zipo mpakani, kwa mfano Wilaya ya Nyasa inapakana na Malawi, Wilaya ya Tunduru inapakana na Msumbiji. Kuwa na makazi bora ya polisi katika maeneo haya kutahamasisha polisi wetu kuishi katika makazi salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri ameeleza kuna nyumba 9,500 zinategemewa kujengwa nchi nzima. Napenda kujua kati ya nyumba hizo ni ngapi zitajengwa Mkoani Ruvuma? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pale Wilayani Tunduru kulikuwa na jengo ambalo lilikuwa linatumia na Askari Polisi wanapokuja kuhamia, jengo lile liliungua moto. Jengo lile lilikuwa linasaidia sana na hasa kwa askari wa kike kupata makazi pale wanapokuja kuhamia. Naomba kujua Serikali imejipangaje katika kuhakikisha jengo lile linajengwa tena ili liwasaidie askari wale?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu mafupi tu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na nyumba ngapi zinatarajiwa kujengwa Mkoa wa Ruvuma ni 320.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na jengo hilo ambalo amelizungumza tunachukua *concern* yake tuone ni hatua gani tutachukua ili kuweza kulifanyia ukarabati ikiwezekana katika bajeti zinazofuata.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Manyinyi halafu Mheshimiwa Selasini.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kule Musoma nako tumekuwa na tatizo kubwa sana la nyumba za askari na kwa bahati nzuri Serikali ilisikia kilio chetu. Hivi ninavyozungumza ni zaidi ya miaka mitatu sasa kuna jengo kubwa la ghorofa ambalo limejengwa pale Musoma Mjini. Cha kushangaza mpaka leo askari wetu hawajakabidhiwa. Nataka kujua Serikali inasubiri nini kukabidhi jengo hilo ili liweze kusaidia kuondoa ile adha kubwa wanayopata maaskari wetu?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mnasubiri nini kukabidhi jengo?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge linapofika suala la maslahi ya askari, robo ya tatu ya Bunge huwa wanasimama kutaka askari wetu wapewe maslahi hayo. Nitakapokuwa nakutana nao nitawaambia kwamba Wabunge huwa wanawasemea ili mnapopita majimboni wawape ushirikiano. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jengo la Mara, kuna hatua za ukamilishwaji ambazo ndiyo zilikuwa zinafanyika kutoka kwa mkandarasi wetu. Ni moja ya majengo ambayo yapo kwenye hatua za ukamilishwaji na yatakapokuwa yamekamilika yatakabidhiwa ili askari wetu wasipate shida hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wengi mlikuwa bado mnafuatilia, nimeshazunguka mikoa yote kasoro mikoa minne na kwa Mheshimiwa Sikudhani nitafika, bado Ruvuma, Njombe, Songwe, Geita pamoja na Singida. Nimetambua ukubwa wa tatizo hili na sisi ndani ya Serikali tunaendelea kuwasiliana kuweza kuhakikisha kwamba tunalibeba kwa ukubwa wake na hivyo tutalifanyia kazi ili kuweza kupatikana jawabu la kudumu linalohusu makazi ya askari wetu ili waweze kuendana na hadhi ya kazi wanazozifanya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni miaka saba sasa nikiwa hapa Bungeni swali hili linapoulizwa majibu ni haya haya, hayajawahi kubadilika hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna changamoto kubwa zaidi kwa hao wenzetu polisi kwa sababu kuwalaza polisi uraiani wakati huohuo ukawatuma kwenda kufanya operesheni ambazo zitapelekea kuwapiga wananchi, ni hatari kwao na kwa familia zao. Ni lini Serikali itafanya mkakati wa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba imeleta majibu tofauti na haya ili wananchi wa Rombo waone nyumba za polisi zinajengwa, waone nyumba za askari magereza zinajengwa, badala ya majibu haya ya kisiasa yanatolewa kila mwaka? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niliweke sawa swali la shemeji yangu Mheshimiwa Selasini. Suala la majibu kuwa yanafanana ni kwa sababu kila mwaka pia tunaajiri, kwa hiyo tutatarajia upungufu uendelee kuwepo, hiyo ni *mathematically*. Suala la jibu kuwa lililile si kwamba Serikali haifanyi kitu, hivi tunavyoongea ukiangalia Dar es Salaam tu kuna nyumba zaidi ya 300 zinajengwa lakini hazitatosha kwa sababu mwaka jana pia tumeendelea kuajiri na kwa kuwa tunaendelea kuajiri maana yake mahitaji yale yataendelea kuongezeka kadri tunavyoajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu iliyopita mmeona imejenga majengo mengi tu tena ya ghorofa, ndiyo mengine kama haya ya Mara ambayo Mheshimiwa Vedastus ameyaongelea. Mwezi uliopita, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 10 kwa upande wa magereza na ujenzi unaendelea. Kwa maana hiyo ujenzi utaendelea lakini na mahitaji yataendelea kwa sababu tunaendelea kuajiri, hata mwaka huu tunategemea tuendelee kuajiri kwa sababu bado idadi ya askari ambao wanatakiwa haijatosheleza. Kwa maana hiyo tumelipa uzito unaostahili suala hili lakini hatuwezi kuacha kuongeza vijana kwa sababu hakuna nyumba, tutaendelea kuongeza vijana lakini tutaendelea kujenga nyumba ili vijana waweze kupata nyumba hizo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Kilolo imeanza toka mwaka 2002 takribani sasa ni miaka 15, lakini kwa muda mrefu OCD amekuwa akikaa tarafa nyingine na makao makuu yako Tarafa nyingine na inabidi kuwasafirisha mahabusu kwani wako kule anakokaa OCD zaidi ya kilomita 100 kuwapeleka katika tarafa nyingine ya Kilolo. Kama Serikali yenyewe bado haijajiweka vizuri, kwa nini isitumie *National Housing* au *NSSF* kujenga nyumba pale Kilolo?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumekuwa tukieleza kila siku na leo vilevile, mipango ya ujenzi wa nyumba upo njiani. Kwa hiyo, hakuna haja ya kufikiria kwamba labda suala la OCD wa Kilolo kutokuwa na nyumba halijatiliwa maanani. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, pale ambapo mipangilio yetu itakapokamilika na mikataba itakapokuwa imesainiwa, basi ujenzi huo utaanza na tatizo ambalo linamkumba OCD wetu huyo wa Kilolo na Ma-OCD wengine popote nchini litakuwa limepata ufumbuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini.

Na. 88

Fidia kwa Waathirika wa Vita vya Majimaji

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE aliuliza:-

Tanzania ni moja ya nchi duniani zilizoathirika kutokana na Tawala za Kikoloni na Vita ya Majimaji ni moja ya vielelezo vya athari hizo ambapo vita hiyo vilianza Wilayani Kilwa katika Kijiji cha Nandete mwaka 1905-1907:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha waathirika wa Vita vya Majimaji wanapata fidia kutoka kwa utawala wa kikoloni wa Kijerumani?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, harakati za kupambana kivita dhidi ya ukoloni zilifanywa na makabila mbalimbali hapa nchini ikiwemo Vita vya Majimaji na nyingine nyingi. Vita hivyo vilifanywa na Watemi wa baadhi ya makabila wakiwemo Mtemi Mirambo wa Tabora, Mtemi Mkwawa wa Iringa na Chifu Abushir Bin Salim wa Uzigua Tanga. Aidha, madhila ya ukoloni kwa wananchi ni mengi yakiwa ni pamoja na utumwa, ubaguzi wa rangi, ukandamizwaji, uporwaji wa mali zetu na ardhi bora za kilimo pamoja na kuuawa kwa tamaduni zetu za asili. Haya ni baadhi tu ya madhila ya ukoloni. Maksud ya vita za watawala wetu wa jadi ilikuwa kupinga ukoloni na kutaka kujitawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ihakikishe kwamba Wajerumani wanawalipa fidia waathirika ni wazo zuri. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu itaandikia rasmi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili waangalie utaratibu bora wa kufikisha kwa wahusika madai haya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngombale.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, lakini pia kukishukuru Kiti chako kwa sababu swali hili nililileta kwa mara ya kwanza halikupata majibu muafaka ya Serikali. Kwa majibu haya kidogo napata faraja kwamba ndugu zangu wale wa Kilwa watakwenda kupata fidia kutoka Serikali ya Ujerumani chini ya usimamizi wa Serikali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri pia Serikali katika suala hili kwamba wenzetu wa Kenya waliendesha mchakato wa kudai fidia za waathirika wa Vita ya Maumau na Serikali ya Uingereza ikatoa fidia kwa waathirika wale. Kwa hiyo, nishauri Serikali nayo ikajifunze kutoka Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa historia ya Vita ya Majimaji imechanganywachanganywa na kuvurugwa; na kwa kuwa Taifa hili limedanganywa eti kwamba Kinjekitile Ngwale ndiyo kiongozi wa Vita ya Majimaji. Ukweli ni kwamba Kinjekitile Ngwale siyo kiongozi wa Vita ya Majimaji na kiongozi wa Vita ya Majimaji ni Sikwako Mbonde na majemedari wake Ngumbalio Mandai, Lindimio Machela, Ngumbe-kumbe Mwiru na wengine. Serikali iko tayari sasa kufanya utafiti wa kihistoria ili basi kuwaeleza Watanzania ukweli wa jambo hili? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa misingi hiyo ya kuchanganya historia ya Vita ya Majimaji, sherehe za kumbukumbu za Mashujaa wa Vita ya Majimaji kila mwaka zinafanywa Majimaji Songea badala ya kufanywa Nandete Kipatimu. Serikali iko tayari kuhamisha sherehe zile kutoka Majimaji Songea kwenda Nandete Kipatimu ambako ndiko chanzo cha Vita ya Majimaji? *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Haya! Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Kicheko)*

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane naye kuhusu ushauri anaoutoa kwamba Tanzania ikajifunze kutoka Kenya kwa sababu Wakenya waliweza kudai fidia ya Vita vya Maumau na waliweza kupata fidia hiyo, tunakubaliana naye na tutafanya hivyo ili tuweze kujua wenzetu wanafanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kufanya utafiti wa kihistoria ili kupata ukweli wa vita hii na uongozi wake na kadhalika nao ni ushauri mzuri, tunaupokea tutafanya kazi hiyo. Sasa ni hapo baada ya kupata ukweli huo, ndiyo hilo swali lake la tatu litaweza kupata jibu muafaka. Kwa sababu siwezi kulijibu sasa mpaka pale historia itakapopatikana na ukweli ukajulikana ndipo tutaweza kulizungumza hilo swali lake la tatu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tuanze na yeye ana taarifa nyingi asaidie basi au aandike kitabu. Mheshimiwa Riziki.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *actually* swali langu lilikuwa ni nyongeza kwa hapo kwamba katika hiyo historia kinachogombewa zaidi katika kumbukumbu ni ile orodha sahihi ya majina ya mashujaa wetu wale ili waenziwe kwa namna inavyostahiki. Kwa hiyo, nyongeza yangu ilikuwa, je, Serikali katika huo utafiti wake itatuletea pia orodha sahihi ya mashujaa hawa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumeshakiri kwamba tuko tayari sasa kufanya utafiti wa historia, kwa hivyo, orodha kamili itakayopatikana italetwa kama Mheshimiwa Mbunge anavyotaka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa ambalo liliathirika sana na Vita vya Majimaji ni Mahenge ambako takribani Watanzania wakati ule Watanganyika 30,000 waliuawa kwa njaa kwa sababu wanajeshi wa Ujerumani walichoma chakula cha Watanzania ili wasiweze kuishi na kufa jambo ambalo kwa tafsiri za kivita ni sawasawa na *genocide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tayari Serikali ya Ujerumani imeomba radhi na kulipa fidia kwenye Vita ya Namaqua na Herero Namibia, Serikali sasa katika mapendekezo ambayo

imeyakubali kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge itapeleka kwa Serikali ya Ujerumani pamoja na ombi la kuomba radhi rasmi kwa mauaji ambayo wanajeshi wake waliyafanya Tanzania? (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kwamba mifano ya nchi zilizoomba fidia kwa vita vilivyotokea kipindi cha ukoloni ni mingi, hapa tumetajiwa Kenya, lakini sasa tunaambiwa Namibia. Kwa hivyo, nitawaomba wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wakati wanataka kuanza rasmi taratibu hizi ili tuweze kupata hiyo fidia basi wawasiliane na nchi hizi ili kujua wameanzaje na hatimaye tuweze kupeleka hilo ombi rasmi. Wakati huohuo nataka nikubaliane na Mheshimiwa Zitto kwamba, pamoja na fidia, kama itathibitika kwamba kulikuwa kuna mambo yaliyofanyika ambayo yanaashiria *genocide*, basi Serikali hiyo iweze kuomba msamaha vilevile. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali la Mheshimiwa Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini.

Na. 89

**Chuo cha Ualimu Korogwe Kupelekewa
Wanachuo 827 Toka UDOM**

MHE. MARY P. CHATANDA aliuliza:-

Mwaka 2014 katika Chuo cha Ualimu Korogwe yalifanyika mabadiliko ya udahili, udhibiti ubora na tunu yaliyofanywa na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa – *NACTE* lakini chuo kimekuwa kikipata wanachuo wachache kuliko miundombinu na rasilimali watu waliopo; na kwa kuwa chuo hiki kwa sasa kimepelekewa wanachuo wapatao 827 kutoka Chuo Kikuu *UDOM* kwa mafunzo ya Stashahada ya Kawaida ya Elimu:-

Je, Serikali itaendelea kuwapeleka wanachuo wa kutosha ili kuendana na miundombinu na rasilimali watu waliopo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ualimu Korogwe kina uwezo wa kudahili wanachuo 1,200 kwa wakati mmoja na ndiyo sababu wanachuo wapatao 827 kutoka Chuo Kikuu *UDOM* walidahiliwa kwa mafunzo ya Stashahada ya Kawaida ya Elimu. Hata hivyo, chuo hicho kimekuwa kinadahili wanachuo wachache kuliko uwezo wake hususan mwaka 2015/2016 kilidahili wanachuo 234 kutokana na kuhuishwa sifa za kujiunga kuwa ufaulu wa daraja la I - III na kuwepo kwa ushindani wa wahitimu wa kidato cha IV kuwa na fursa nyingine za kujiunga na kidato cha V na wahitimu wa kidato cha VI kujiunga na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa dhamira ya kuwapokea wanachuo wa kutosha katika Chuo cha Ualimu Korogwe ili kuendana na miundombinu na rasilimali watu waliopo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kama ambavyo Naibu Waziri amesema kwamba chuo kile kina uwezo wa kudahili wanachuo 1,200 na ameeleza mwenyewe kwamba 2015/2016 kilidahili wanachuo 234. Kutokana na miundombinu na rasilimali iliyopo pale, kuwa na wanafunzi 234 kati ya 1,200 hatuoni kwamba hatukitendei haki chuo hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna utaratibu ule wa kuwadahili kupitia mtandao na huko vijijini hakuna mitandao kwa nini isirejee utaratibu wa kuandika barua pamoja na kutumia hizo *internet* kwa wenzetu walioko mijini ili watoto wa wanavijiji na wenyewe waweze kupata hizi nafasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, zamani utaratibu ulikuwepo wanafunzi ambao wako shuleni walikuwa wakiomba nafasi za ualimu wakiwa shuleni. Je, kwa nini wasirudishe utaratibu huo mtu aweze kuomba akiwa shuleni ili tuweze kupata wanachuo wa kutosha kuliko kuwa na chuo ambacho kinataka wanafunzi 1,200 halafu wanadahili wanachuo 234?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baada ya kuboreka kwa miundombinu hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba chuo hicho kinachukua wanafunzi wanaostahili kuwepo. leleweke kwamba baada ya kubadilisha hizo sifa kwanza hali ya ufaulu wa wanafunzi katika shule zetu ulikuwa uko chini lakini pia kutokana na mambo ambayo yalikuwa yanachangiwa humu Bungeni juu ya sifa za Mwalimu, kwa sababu ilikuwa inaonekana kwamba ualimu anapelekwa mtu mwenye sifa hafifu, kwa hiyo, Wizara ilifanya marekebisha na kuona kwamba sasa sifa ziwe mwisho ni daraja la III.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, kwa mwaka wa kwanza tulikuwa na wachache lakini kwa sasa hali ya ufaulu imeboreka kutoka katika shule zetu za Serikali na zisizo za Serikali kwa hiyo, tunao wanafunzi wengi ambao wanaweza kupelekwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika niseme tu kwamba katika suala la udahili tunaliangalia na Kamati yetu ya Huduma ya Jamii imelizungumza sana. Tunaangalia namna bora ya kudahili bila kupoteza dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa ubora unalindwa. Kwa hiyo, tutafikia maamuzi baada ya tafiti zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwapeleka wanafunzi moja kwa moja kutoka shuleni ni kwamba wanafunzi hao ni mpaka wawe wameshafanya mitihani na wengine wanachukuliwa kutoka katika ngazi mbalimbali za uombaji, kwa hiyo, matokeo yao ndiyo yanayowapeleka huko siyo tu ilimradi yuko pale shuleni na aanze kujaza. Kwa hiyo, suala ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaopelekwa katika Chuo cha Korogwe na vyuo vingine vyote ni wale wenye vigezo vya ubora unaohitajika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kifupi tu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nitaongea kwa kifupi. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na napenda tu kuongezea jambo dogo kwamba, suala hili la vyuo vya ualimu kuwa na wanafunzi wachache kuliko uwezo wake lilitokana na uamuzi wa kuwapeleka wanafunzi UDOM ambapo ilisababisha mlundikano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu yale mambo yaliyokuwa yanasemwa kwamba Serikali iliwaondoa wanafunzi UDOM ili ipate nafasi siyo kweli kwa sababu iliona ni vizuri, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Vyuo vya Ualimu vichukue wanafunzi kulingana na uwezo wake. Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Martha Umbulla atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa suala la rasilimali watu katika Wizara ya Elimu hasa kwenye vyuo vyetu na hata shule za sekondari bado ni changamoto kubwa na kwa kuwa hali hii inasababisha pia baadhi ya Waratibu wa Elimu kupangiwa masomo ya kufundisha sawasawa na Walimu wengine hali inayopelekea kuona kwamba ni kazi iliyopo nje ya *job discription* zao. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kufikiria kwa kuwa hiyo ni kazi ya ziada basi waweze kupewa posho ya ziada hawa Waratibu wa Elimu kuliko hali ya sasa ambayo wanafundisha kama Walimu wengine lakini hawana nyongeza ya mishahara? (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulitambua hilo ndiyo maana sasa hivi Serikali imeamua kuweka posho ya madaraka ambayo mwanzoni haikuwepo. Kwa kipindi kilichopita tumelipa takribani shilingi bilioni 15 kwa ajili ya posho ya madaraka. Kwa hiyo, jambo hili Serikali tumelizingatia, tunalifanyia kazi na hivi sasa watumishi wale kutokana na jukumu hilo wana posho maalum kila mwezi, kuanzia Walimu Wakuu wa Shule za Msingi, Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari halikadhalika Waratibu wa Elimu wa Kata katika maeneo yetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nataka kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na elimu Mkoa wa Katavi. Ukosefu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Mkoa wa Katavi umeleta usumbufu kwa wananchi wa Katavi. Serikali ilitenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Kilimo lakini chuo hicho kimeyeyuka. Ni nini mkakati wa Serikali kufuatilia zile pesa zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Kilimo Mkoa wa Katavi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Chuo kikuu kilichokuwa kinategemewa cha Mkoa wa Katavi kilikuwa kinadhamiriwa kujengwa kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Mpanda pamoja na wawekezaji ambao walikuwa ameingia nao ubia. Kwanza katika taratibu zilizokuwa zinaendelea kulikuwa na suala la mbia kutaka kupewa dhamana ya Serikali katika kujenga chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tuliona kwamba, kama mtu anahitaji kujenga chuo, wakati yeye tunategemea kwamba ni mwekezaji kwa maana kwamba atakuja kuwekeza katika kile chuo, dhamana ya Serikali inaweza ikasababisha mtu kuchukua deni mahali na kukimbia na kazi isiwe imefanyika. Ni vema mwekezaji awe ni mwekezaji wa kweli na awekeze kadri inavyotakiwa. Hata hivyo, kwa fedha zilizotolewa Halmashauri ya Mpanda inafahamu juu ya mambo yake na hivyo kwa kutumia Baraza lao wafuatilie na kuona kwamba fedha zao hazipotei.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 90

**Mwanafunzi Anayekatizwa Masomo
kwa Sababu ya Mimba**

MHE. ZAYNAB M. VULLU aliuliza:-

Serikali imeona umuhimu wa kuchukua hatua kali zaidi kwa mwanaume anayempa mimba mwanafunzi wa shule kwamba apatiwe kifungo cha miaka 30:-

Je, Serikali itamhakikishiaje mwanafunzi aliyepewa mimba kuwa ataweza kuendelea na masomo baada ya kujifungua?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 pamoja na mambo mengine, imeweka mkazo juu ya kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa wote. Aidha, sera inatamka wazi kuwa Serikali itaondoa vikwazo vinavyozuia fursa ya wanafunzi kuendelea na masomo na hivyo kukamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika na kwamba itahakikisha kuwa usawa wa kijinsia katika elimu na mafunzo unazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya utekelezaji wa sera hiyo, Serikali imeandaa Rasimu ya Mwongozo utakaofuatwa na wadau mbalimbali ili kuwawezesha wasichana waliopata ujauzito kurudi shuleni na kuendelea na masomo yao baada ya kujifungua. Mwongozo huu pia, baadhi ya mambo yaliyowekwa ni utaratibu utakaofuatwa kwa wasichana waliojifungua kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia ya Serikali kuondoa vikwazo kwa mtoto wa kike ili kuendelea na masomo, wito unatolewa kwa wadau mbalimbali wakiwemo wazazi, walimu, viongozi wa elimu pamoja na dini na jamii kwa ujumla kwa pamoja kuchukua hatua za makusudi za kuzuia na kudhibiti tatizo la mimba shuleni na katika umri mdogo kwani kwa kiwango kikubwa inamvunjia heshima mwanafunzi mwenyewe na kuwa chanzo cha upotevu wa maadili na pengine kupoteza dira yake ya mafanikio katika maisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Vullu.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza niseme nilitarajia angeniambia Mwongozo huo utaanza lini ukizingatia Wizara inaongozwa na Waziri mwanamke, Naibu Waziri mwanamke na Katibu Mkuu mwanamke. Je, Sheria ile ya SOSPA haoni kwamba inakinzana na sera ambayo wanaleta na vipi mtawasaidia hao watoto waweze kuendelea na utaratibu ambao mmeuweka? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mtoto wa kike na wanawake wote kibaiolojia kuna siku ambazo lazima tuzitumikie. Watoto wa shule wengi wanaacha kwenda

shule kati ya siku sita mpaka saba, ukipiga kwa mwaka mmoja mtoto wa kike anapoteza zaidi ya siku 60 au 70. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuweza kupeleka mataulo ya kuweza kuwasaidia na kutenga chumba maalum kwa ajili ya wao kuweza kujihifadhi wakati wanapohitaji? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikiri kwamba ni heshima kubwa sana Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupewa sisi wanawake kuiongoza ambao tuko jirani sana na mahitaji au matatizo ya wanawake na ndiyo maana tunasema kwamba mwongozo tayari umeshaandaliwa. Kama mazungumzo yote tunayoendelea kuyafuatilia yatakuwa yamekamili, tunatarajia tarehe Mosi, Machi, 2017 mwongozo huo uwe umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanawake ni mtambuka. Tunapozungumzia kuwawezesha vijana katika demokrasia na katika kushiriki shughuli mbalimbali za kiuongozi, tunachozungumzia ni kwamba lazima watoto wa kike wasiachwe nyuma. Kutokuwa na sehemu za kujihifadhi wanapokuwa shuleni ni tatizo. Mwongozo ulishatolewa kwamba kila shule lazima itenge chumba maalum kwa ajili ya wanafunzi hao kujihifadhi wakati maalum lakini hali kadhalika tunasema kwamba hata hizi fedha za elimu bure zinazotolewa ni vema ikatengwa sehemu ndogo kwa ajili ya kuwasaidia hawa watoto wa kike pale inapotokea mambo yametokea kwa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema bila kuficha wapate pedi zao kwa sababu tumekuwa tukificha mambo haya ya wanawake, matokeo yake hata kwenye bajeti hayawekwi. Tuseme wazi kwamba mahitaji ya mwanamke ikiwemo pedi ziwekwe kwenye bajeti ili hawa watoto wa kike waweze kusaidiwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waziri wa Viwanda? Haya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. *(Kicheko)*

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee jibu zuri la Naibu Waziri. Napenda nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba imekuja teknolojia ambapo taalo nzuri za bei nafuu zitatengenezwa. Zaidi nitoe taarifa kwamba kuna Wabunge wawili wamejasiria, tunawaongoza kusudi watengeneze viwanda hivyo.

MWENYEKITI: Haya, ahsante na kila la kheri. Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami niulize swali la nyongeza kutokana na swali la msingi la Mheshimiwa Zaynab Vullu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imalize tatizo la watoto wanaopata mimba kuendelea na masomo. Tunajisikia vibaya sisi Watanzania wanawake, kwa mfano, chukua Zanzibar, Zanzibar mtoto wa kike akipata ujauzito wanaruhusu anaendelea na masomo. Zambia, Kenya, sisi ndiyo tumebaki peke yetu wa mwisho kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa, kwa kifupi tu, taarifa zinatolewa kila siku watoto 30 wamepata mimba, watoto 20 wamepata mimba, hivi mnaona ninyi raha kutangaza kila siku na wasababishaji mnawajua ninyi wenyewe? Iliyobaki hawa watoto waruhusiwa wakasome, hakuna mjadala hapa. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lolote lile linapoteklezwa ili litekelezwe kikamilifu ni vema wadau wote wakawa pamoja. Sisi wanawake pamoja na hao wanafunzi wa kike hatuishi kwenye jamii peke yetu. Katika utekelezaji wa suala hili si tu kwamba maadam tukisema wanafunzi warudi shuleni basi unakuwa unasema umesema wakati hujui utekelezaji utakuwaje. Ndiyo maana tumewashirikisha...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Tulieni. Kama majibu ninayo mimi basi sikilizeni. Nasema hivi suala hili linahitaji Wabunge wote kuwa on board kwa misingi kwamba...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Huyu mwanafunzi anapokuwa ...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Na msisahau sisi wenyewe tulitunga sheria ya kuhakikisha kwamba yule anayetoa ujauzito kwa mtoto wa shule achukuliwe hatua.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Sasa kama ndivyo tumetunga hiyo sheria bila kuwa na ushirikishwaji na utaratibu maalum wa kuwapata hao wanaoendelea kutoa ujauzito kwa watoto wa shule, utaratibu vipi? Ndiyo maana tunataka sekta zetu zote, wadau wote, tuwe na uratibu wa kuweza kukabiliana na mambo yote mawili.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Kwa hali hiyo, wanafunzi watarudi shuleni lakini wakati huo huo lazima taratibu zetu za msingi za kufanya uratibu katika maeneo yote ikiwemo utoaji wa adhabu hasa wale akinababa ambao wanawanyemelea watoto wa shule uweze kuendelea. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Taarifa, taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, suala hili linavuta hisia nyingi sana.

MHE. ALLY M. KEISSY: Watoto wa mitaani watakuwa wengi sana.

MWENYEKITI: Bunge la bajeti halipo mbali.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MWENYEKITI: Serikali inataka izingatie misingi ya sheria na taratibu tulizojiwekea basi.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Na. 91

Ongezeko la Maduka ya Kucheza Kamari

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA aliuliza:-

Kuna ongezeko kubwa la maduka ya kucheza kamari yanayotaitwa *Jack Pot* katika miji nchini ikiwemo Dodoma; maduka hayo huchezesha kamari mchana na usiku na wateja wengi ni vijana ambao hutumia mbinu mbalimbali kupata fedha ndani ya familia ili wakacheze kamari hali ambayo husababisha uvunjifu wa maadili:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mchezo wa kamari ambao huwakosesha amani wazazi na jamii nzima?

(b) Je, Serikali haoni kuwa kuna uvunjifu wa maadili na nguvu kazi ya vijana inapotea kwa kucheza kamari badala ya kushiriki katika uzalishaji?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo yote ya kubahatisha ikiwemo kamari inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Namba 4 ya mwaka 2003, Sura 41 pamoja na kanuni zake. Kwa mujibu wa sheria, hakuna mtu au taasisi inayoruhusiwa kuendesha biashara ya michezo ya kubahatisha bila kuwa na leseni kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha pamoja na vibali vingine vinavyotolewa na mamlaka zingine za biashara. Pia, sheria inakataza watoto wenye umri chini ya miaka 18 kushiriki, kuingia, kukaa au kuzururazurura karibu na maeneo ya michezo ya kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote atakayeruhusu mtoto chini ya miaka 18 kushiriki, kuingia au kukaa karibu na eneo la mchezo wa kubahatisha anahesabika kufanya kosa na anastahili kulipa faini ya sh. 500,000 au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote kwa pamoja. Aidha, endapo kosa hili litafanywa na mwendesha mchezo wa kubahatisha, Bodi ina mamlaka kisheria ya kumfutia leseni. Hivyo basi, wajibu wa Serikali ni kuzuia watoto na vijana walio chini ya miaka 18 kucheza michezo ya kubahatisha. Hata hivyo, natoa rai kwa wazazi na walezi kuwazuia vijana wao kucheza michezo ya kubahatisha pale wanapoona kuwa uchezaji wao unakuwa na matokeo hasi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ya kubahatisha ni moja ya shughuli za kiuchumi inayoendeshwa kwa mujibu wa sheria kama shughuli nyingine zozote. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa, wote wanaoendesha michezo ya kubahatisha wanazingatia sheria na kanuni zilizowekwa. Pili, ni wajibu wetu kama wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuhakikisha kuwa vijana wetu wanazingatia mila na desturi zinazolinda maadili ya Kitanzania pindi wanapokuwa wanajishughulisha na shughuli halali za kiuchumi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mashaka ya vijana wetu yamekuwa yakizidi siku kwa siku, vijana wanajihusisha katika michezo hii ambapo muda mwingi unapotea hata muda wa masomo, muda wa kufanya kazi ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Maadili yamepotea, kuna masuala ya *betting* ambayo yanachukua muda mwingi wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waziri kuniambia kwamba kuna Sheria Namba 4 inayoruhusu mambo hayo lakini udhibiti wake ukoje? Je, mpaka sasa ni wafanyabiashara wangapi wamekamatwa na maduka yao kufungwa ambao hawakuzingatia taratibu za kuzuia vijana wenye umri mdogo kuingia sehemu hizo na je, wamepelekwa kwenye vyombo husika na kuchukuliwa hatua? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili...

MWENYEKITI: Umeuliza maswali mawili tayari.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Naam!

MWENYEKITI: Umeuliza maswali mawili tayari.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja.

MWENYEKITI: Hapana, mawili.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unanionea. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza aliuliza udhibiti wake ukoje, kama nilivyosema sheria yetu imeweka wazi na Bodi ya Michezo ya

Kubahatisha iko makini kusimamia michezo hii yote ndani ya nchi yetu ili kuhakikisha sheria hii iliyotungwa na Bunge letu Tukufu inafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ni watu wangapi na maduka mangapi yamefungwa, naomba nilichukue swali hili tuweze kulifanyia kazi kwa sababu linahitaji data mahsusili ili tuweze kumjulisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msabaha.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda na mimi nimuulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hii michezo ya kamari imekuwa ikichezwa kwenye stendi kubwa na sehemu za starehe na kupelekea watu kufilisika na wengine kufikia hatua hata ya kujiua. Je, hamwoni sasa ni wakati muafaka wa kukataza michezo hii isichezwe na wale wanaocheza michezo hii wachukuliwe hatua?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema michezo hii ipo kisheria, sisi kama Wizara hatuwezi kuisitisha. Tutafanya utafiti ili tuone kama inahitajika kuleta sheria mpya Bungeni ili tufanye hivyo. Hata hivyo, tusingahau kama nilivyosema michezo hii ni sawa na michezo mingine pale inaposimamiwa vizuri na sisi tuna uhakika inasimamiwa vizuri. Kwa mfano, kwa mwaka jana 2016 mchezo huu ulichangia zaidi ya shilingi bilioni 2.1 katika mapato yetu. Hivyo, niombe tu kama jamii na kama Taifa tuweze kuwasimamia vizuri vijana wetu ili yale madhara hasi yasiweze kupatikana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kwa niaba yake Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 92

**Mradi Mkubwa wa Maji ya Tambarare
Mwanga na Same**

MHE. SHALLY J. RAYMOND (K. n. y MHE. DKT. DAVID M. DAVID) aliuliza:-

Je, mradi wa maji tambarare ya Mwanga na Same hadi Korogwe umefikia hatua gani na wananchi wategemeo utakamilika lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa kupeleka maji katika Miji ya Mwanga na Same pamoja na Vijiji vya Wilaya ya Mwanga, Same na Korogwe vilivyopo kandokando ya bomba kuu. Mradi huu utakapokamilika unatarajia kuhudumia watu 456,931. Ujenzi wa mradi huo umegawanywa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, mitambo ya kusafisha maji na miundombinu ya kusafirisha na kusambaza maji katika miji ya Mwanga na Same. Awamu ya pili inahusisha ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji katika vijiji 38 vilivyo kandokando ya bomba kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza imepangwa katika loti tatu. Utekelezaji wa loti ya kwanza unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji na kulaza bomba la urefu wa kilomita 12.8 kutoka kwenye chanzo hadi kwenye matanki ya kituo cha kusukuma maji Kisangara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, loti ya pili inahusu ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji katika Mji wa Mwanga ambao upo katika hatua ya manunuzi. Tayari zabuni zimetangazwa ili kumpata mkandarasi mwenye sifa. Aidha, fungu la tatu la ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji katika Mji wa Same utekelezaji wake unaendelea na mkandarasi yupo katika hatua ya maandalizi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mradi wa Same - Mwanga - Korogwe awamu ya kwanza unatarajiwa kukamilika Disemba, 2019. Ujenzi wa awamu ya pili ambayo inahusisha kupeleka maji katika vijiji vilivyo kandokando ya bomba kuu haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha. Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa awamu hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya hatua husika za mradi huu, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kuhusu awamu ya kwanza inayotarajiwa kukamilika Disemba, 2019. Je, huo ndiyo wakati ambapo mabomba ya Same yatafungua maji hayo na kuona maji yakitiririka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Same haiko vizuri kifedha kuwasaidia watu wa Same ambao mpaka sasa hawana maji safi na salama zikiwepo Kata za Njoro, Same Mjini, Makanya na Hedaru. Je, Serikali iko tayari sasa kuwapatia fedha za kuchimba visima virefu ili watu hao wapate maji safi na salama wakati wakisubiri kukamilika kwa mradi huo mwaka 2019? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu la msingi limezungumzia mradi wa Same-Mwanga-Korogwe kwamba ifikapo mwaka 2019 utakuwa umekamilika kwa maana kwamba maji tayari yatakuwa yamefika Mwanga na yatakuwa yamefika Same, yatafunguliwa wananchi wanaanza kupata maji na miradi hiyo inaendelea vizuri na fedha zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili kuhusu Same, katika bajeti hii tuliyonayo kwa sasa na ninyi Waheshimiwa Wabunge mliipitisha, tulihakikisha kila Halmashauri tumeipatia fedha ili Waheshimiwa Wabunge na Madiwani katika Halmashauri zao wapange miradi kutokana na hiyo fedha ambayo tumeituma kwenye Halmashauri. Kwa bahati nzuri Halmashauri ya Same ilipewa Sh. 663,847,000 kwa ajili ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni matarajio yangu kwamba Halmashauri hizi sasa zinao uwezo, zitekeleze miradi kutokana na fedha hii kwa kuchimba visima au maji ya mtiririko kutokana na hali ya mazingira ya Halmashauri husika ili kuhakikisha wananchi wanapata maji. Mwaka huu wa fedha unaokuja tutaendelea kutenga fedha kwenye Halmashauri ili wao wenyewe waweze kutekeleza miradi ya kuwapeleka maji wananchi wao.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngonyani.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mradi huu wa maji wa Same-Korogwe ni wa muda mrefu kutoka enzi ya Profesa Mwandosya, akaja Profesa Maghembe na sasa hivi kaja Injinia Lwenge...

MWENYEKITI: Swali, swali.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mradi huu unagusa hasa sehemu za tambarare peke yake, ni lini sehemu za milimani kama vile Suji, Mkomazi, Manga Mtindilo, Mikocheni na Bwiko mradi huu nao utatekelezwa huko kwa sababu wakati wa mwanzo tuliambiwa hela zipo na mradi unaanza? Naomba kujua ni lini sehemu zile za milimani na zenyewe zitapata maji? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo vitapewa maji katika mradi huu wa Same-Mwanga ni Bwiko, Mkomazi, Nanyongie, Manga Mtindilo na Manga Mikocheni, hii ndiyo ipo kwenye mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mradi umechukua muda mrefu na sababu kubwa ni kwamba mradi huu unategemea ufadhili wa nchi za Kiarabu. Sasa fedha ambazo unategemea mtu mpaka akupe huwa inachukua muda mrefu. Hata hivyo, Serikali tumeamua katika mwaka wa fedha unaokuja ule upungufu wa bajeti ambao upo tutaweka kwenye fedha zetu za ndani. Kwa hiyo, nitaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuweke fedha za kutosha kwenye fedha za ndani ili mradi huu tuweze kuukamilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kaliua na Jimbo la Kaliua wana adha kubwa ya maji na ardhi ya Tabora nzima ikiwepo na Kaliua visima vikichimbwa vinatoa maji kidogo sana. Namna pekee ya kusaidia wananchi wa Kaliua na Wilaya nyingine ni kuweza kupata maji kutoka mto mkubwa wa Malagarasi. Je, ni lini mradi mkubwa wa kutoa maji Malagarasi kwenda Kaliua mpaka Urambo utaanza na utakamilika lini? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imekamilisha mradi wa upembuzi yakinifu wa kutoa maji kutoka Mto Malagarasi kupeleka Kaliua na Urambo. Sasa hivi mkandarasi anaendelea na usanifu wa kina wa mradi huo. Baada ya kukamilisha usanifu wa kina Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya mradi huo kukamilika sasa tutakuwa na chanzo cha uhakika kutoka Malagarasi kuleta maji Kaliua, Urambo na hatimaye kupeleka Tabora. Ni kweli kabisa ulichosema chini ya ardhi katika Mkoa wa Tabora maji ni kidogo sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 93

Tatizo la Maji Safi na Salama Mkoa wa Singida

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE aliuliza:-

Mkoa wa Singida ni miongoni mwa mikoa yenye ukame hapa nchini; ukame huo unasababisha changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa maeneo mengi Mkoani Singida:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa Singida inapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili kuwasaidia wananchi hususan wanawake kushiriki kwenye shughuli nyingine za uzalishaji mali?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida ni kati ya mikoa iliyo chini ya wastani wa kitaifa wa utoaji huduma ya maji. Hadi kufikia mwezi Juni, 2016 wananchi waliokuwa wanapata huduma ya maji katika mkoa huo ni asilimia 51.2 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 71.3 kwa maeneo ya mijini. Katika Mkoa huo hakuna mito inayotiririsha maji kwa mwaka mzima. Vyanzo vingine vya maji juu ya ardhi kama maziwa na mabwawa ya asili maji yake yana chumvi nyingi isiyofaa kwa matumizi ya binadamu. Kwa msingi huo, vyanzo vinavyotegemewa kwa huduma ya maji safi ni maji ya ardhi kupitia visima virefu na visima vifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa Mkoa wa Singida inapatiwa ufumbuzi, Serikali imekamilisha kujenga mradi wa maji safi katika Manispaa ya Singida ambapo kwa sasa huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama imeongezeka. Aidha, mkakati wa Serikali ni kuendelea kupanua mtandao wa maji na kufunga pampu katika visima vya ziada ambavyo vilichimbwa kwenye mradi huo uliokamilika.

Vilevile kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika Mji wa Manyoni na Kiomboi ambapo hadi sasa zabuni za ujenzi zimetangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji vijijini, Serikali inatekeleza miradi ya maji katika vijiji 66. Kati ya hivyo, vijiji 47 vimekamilika na vijiji vingine vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 6,750 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri zote za Mkoa wa Singida zikiwemo Halmashauri za Manyoni na Singida Vijijini. Aidha, katika juhudi za kukabiliana na hali ya ukame, Wizara imetoa agizo katika Ofisi ya Mkoa kuhakikisha kila

Halmashauri inaainisha maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa madogo na kutenga fedha katika bajeti zao za ndani kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Matembe, swali la nyongeza.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wengi wa Wilaya ya Singida Vijijini wanataabika sana kutokana na shida kubwa ya maji na matumaini yao waliweka katika ukarabati wa miundombinu ya maji ya visima inayogharamiwa na chanzo cha fedha cha LCDG ambapo fedha hizo hazijaletwa hata senti moja kwa muda wa miaka mitatu mfululizo sasa, miradi hiyo inahusisha Vijiji vya Mughamo, Sagara, Kinyeto, Mkimbii, Kihunadi, Mwanyonye... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Hauli, Mwakiti...

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: ...Ndugwira,

MWENYEKITI: Uliza swali tu.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Kijota na Semfunga: Swali; je, Serikali itapeleka lini fedha hizo ambazo ni zaidi ya shilingi milioni 300 ili kuvikarabati visima hivyo na kuondolea kero wananchi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Mji wa Itigi ni miongoni mwa miji midogo inayokua kwa kasi sana na ni Makao Makuu ya Jimbo la Manyoni Magharibi, lakini mji huu hauna kabisa mtandao wa maji: Je, sasa Serikali ipo tayari kutenga fedha za kutosha kwa mwaka ujao wa fedha, 2017/2018 ili kuwawezesha wananchi wengi kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto kubwa ya maji katika Wilaya ya Manyoni, ni ombi...

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Ni ombi, ombi Mwenyekiti. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, hebu...

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Waheshimiwa Wabunge, naomba maswali yawe mafupi tu, tusihubirie Bunge.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Matembe, hoja yake anayoizungumza katika Bunge siyo hapa tu; ananifuata ofisini, tukikutana huko mtaani, anazungumzia kuhusu

maji Singida. Tumshaongea kuhusu mikakati yote itakayohakikisha kwamba Mkoa wa Singida sasa matatizo ya maji tunayakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza awali, ni kwamba Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji tuliamua kuhakikisha kila Wilaya tunaipatia fedha ili pamoja na miradi mikubwa ambayo inatekelezwa moja kwa moja na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Halmashauri pia ziweze kutekeleza miradi kwa kujipangia wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu Itigi; napo tumefanya utaratibu huo huo, lakini pamoja na hilo, Itigi tumekamilisha ujenzi wa Bwawa la Itagata ambalo litahudumia kilimo, lakini pia Halmashauri inaweza ikaona uwezekano kama maji yanatosha, basi yaweze kusambazwa kupelekwa na kwa matumizi ya majumbani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kaunje.

MHE. HASSAN S. KAUNJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri wa Maji, tulifanya ziara ya kukagua vyanzo vya maji katika eneo la Manispaa ya Lindi na kuna mradi mkubwa wa maji wa Ng'apa, Lindi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia mradi ule utakamilika lini na wananchi wa Lindi wakaweza kupata maji ya kunywa? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa kifupi tu. Lini mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na nyaraka za kimkataba na utekelezaji unaoendelea, tunategemea mwezi Aprili mwaka huu wa 2017, mradi huo utaanza kutoa maji kwa ajili ya wananchi wa Lindi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Pamoja na kuwepo kwa changamoto kubwa ya uhaba wa maji katika Mji wa Singida, lakini pia kuna changamoto kubwa ya miundombinu mibovu kwa maana miundombinu yake ni ya muda mrefu sana. Ni lini sasa Serikali itatatua changamoto hii kwa sababu ni ya muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, lini mtatatua hilo tatizo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunatakiwa kutenga fedha za *maintenance*. Mnapoleta bajeti Waheshimiwa Wabunge kupitia kwenye Halmashauri zenu kama ambavyo wamefanya watu wa Rungwe, tunatakiwa pia kutenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ili hii miundombinu ifike mahali kwamba isichakae kabla hatujafanya ukarabati. Pia sasa hivi kama miundombinu imeshachakaa, basi tunaomba muainishe kwenye Halmashauri mtuletee ili tutenge fedha kwa ajili ya ukarabati.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali letu la mwisho kwa siku ya leo. Linaulizwa na Mheshimiwa Farida Bakar kwa niaba ya Mheshimiwa Maida Hamad.

Na. 94

Aina za Gesi Zilizogundulika Nchini

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR (K.n.y. MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH) aliuliza:-

Mafuta na gesi ni rasilimali zinazotegemewa kuwa na mchango mkubwa kwa Taifa letu:-

Je, ni aina ngapi za gesi zilizogundulika na faida iliyopatikana tangu ugunduzi huo ulivyotokea?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, lililoulizwa na Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Chakechake, Pemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), lilianza utafiti wa masuala ya mafuta na gesi asilia nchini mwaka 1950 ikihusisha utafiti katika maeneo ya baharini ya kina kirefu, maziwa na nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi asilia iliyogunduliwa katika maeneo ya bahari ya kina kirefu ni futi za ujazo trilioni 47.08 na katika nchi kavu ni futi za ujazo trilioni 10.17, hivyo kuwa na jumla ya futi za ujazo trilioni 57.25 ya gesi asilia nchini. Gesi asilia iliyogunduliwa ni ya aina moja ya *sweet gas*, yaani gesi ya kiwango cha juu sana ambayo ina kiwango cha chini sana cha *sulfur*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida kubwa iliyopatikana kutokana na ugunduzi wa matumizi ya gesi asilia nchini ni uzalishaji wa umeme wa bei nafuu kwa matumizi ya gesi asilia ikilinganishwa na mafuta. Uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi asilia umeongezeka kutoka *unit* 2,714.25 kwa mwaka 2014 hadi kufikia *unit* 4,119 mwaka 2016. Hii ni sawa na asilimia 54.66 ya ongezeko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya umeme imeshuka kutoka wastani wa sh. 188.56 kwa *unit* mwaka 2014 hadi wastani wa sh. 125.85 kwa *unit* kwa mwaka 2016, sawa na punguzo la asilimia 33.26. Mbali na punguzo kubwa la umeme, gharama za maombi ya *service charge* ziliondolewa tangu tarehe mosi Aprili, mwaka 2016, lengo likiwa ni kupunguza gharama za umeme kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Helium One* imefanya ugunduzi wa gesi ya *helium* katika maeneo ya Ziwa Rukwa katika bonde la ufa. Kiasi kilichogundulika kinakadiriwa kufikia futi za ujazo bilioni 54. Gesi ya *helium* hutumika katika matumizi ya mashine za *MRI Scanners* na vinu vya *nuclear* katika matumizi ya baluni kwa matumizi ya ndege, hasa kuruka na ndege hewani.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Faida Bakar.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumrekebisha Mheshimiwa Naibu Waziri kidogo, mimi siyo Mbunge wa Viti Maalum Chakechake. Ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini Pemba ikiwemo Chakechake na Mkoani. Ahsante. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama kawaida yake, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ukataji wa miti kwa ajili ya kuchoma mkaa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania yanaleta uharibifu wa mazingira katika nchi yetu; na kwa kuwa gesi ipo lakini haifikishwi hasa kule vijijini ambako hiyo miti ndiyo inakatwa na kufanywa mikaa: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasambazia wananchi gesi hasa za majumbani kwa ajili ya matumizi na waachane na tabia ya kukata miti na kutengeneza mkaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa watu wengi wana hamu kubwa sana ya kutumia hii gesi hasa ya majumbani lakini wanaogopa, wanasikia kwamba gesi inaua; hawana elimu hiyo: Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kutoa elimu ya kuwaelimisha wananchi hasa vijijini na mijini ili kuweza kutumia gesi hiyo kwa manufaa ya wananchi wote hasa vijijini na mijini kwa ajili ya matumizi ya kupikia majumbani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Faida kwa jinsi anavyohangaika na kushughulika na kupambana na uharibifu wa mazingira hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ambayo Serikali imechukua katika kuhakikisha kwamba uharibifu wa mazingira unapungua kwa kiasi kikubwa ni kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia hapa nchini. La kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge, na hatua ya kwanza ambayo Serikali imeanza, TPDC imeanza sasa mradi wa kusambaza gesi majumbani na katika matumizi ya magari kwa ajili ya Dar es Salaam. Hatua ya kwanza imekamilisha usanifu ambao hivi karibuni utanza utekelezaji wake na maeneo yatakayoanziwa ni pamoja na maeneo ya Mikocheni, Tabata na Sinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waharibifu wa kwanza kabisa wa mazingira hapa nchini ni wakazi wa Dar es Salaam. Dar es Salaam na wananchi kwa ujumla ni jumla ya magunia 45,000 yanaingia kwa siku kwa Jiji la Dar es Salaam. Sasa ili kupunguza athari hiyo, hatua ya kwanza ni kupunguza matumizi ya mkaa kwa wananchi wa Dar es Salaam kwa kutekeleza mradi huu.

Awamu ya pili itaenda katika maeneo ya Tabata, maeneo ya Ukonga kwa Mheshimiwa Waitara, lakini maeneo ya Kigamboni na maeneo mengine. Utaratibu huu utanda sambamba na maeneo ya Lindi na Mtwara ambapo mradi huu pia utanza mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo utekelezaji huu wa kutumia gesi utaendelea katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma ambayo inakuja kuwa Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba matumizi ya gesi yatapunguza kwa kiasi kikubwa sana uharibifu wa mazingira. Huo ni mkakati wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa pili, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imetenga pesa, jumla ya shilingi bilioni 6.5 kwenye bajeti ya mwaka huu ili gesi iweze kusambazwa katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu; ni kweli TPDC wameanza kutoa elimu japo siyo kwa kiwango kikubwa. Elimu ya kwanza ambayo imefanyika ni katika maeneo ya minada pamoja na maeneo ya maonyesho, lakini katika Mikoa ya Lindi na Mtwara TPDC imetoa elimu mashuleni, wameanza kutoa makongamano katika maeneo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara, Mwanza, Arusha pamoja na Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, harakati za kutoa elimu ili matumizi sahihi yaende sambamba na mahitaji, yanaendelea.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Katika Sekta ya Gesi utafiti wa gesi na mafuta katika Bonde la Ziwa Tanganyika pamoja na Chepechepe na Bonde la Mto Malagarasi, tungependa kujua utafiti huo umefikia wapi? (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati na Madini. Aah, nimemwona Waziri, ahsante.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa majibu mazuri, niongezee lile swali la awali; matumizi ya gesi na mambo ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba sasa hivi Mikocheni na nyumba za TPDC 70 wanatumia gesi, wana mabomba mawili mle ndani; bomba la maji na bomba la gesi. Matumizi yake kwa mwezi hawajavuka sh. 25,000/= hata wakipika vyakula kama maharage, makongoro, ni sh. 25,000. Hiyo tumefanya. Halafu kuna viwanda 37 vinatumia gesi. Hili jana liliongelewa. Tumepata fedha dola milioni 150 kutoka *African Development Bank* kwa ajili ya kusambaza gesi Dar es Salaam, Lindi na Mtwara.

Waheshimiwa Wabunge, maana ya uchumi wa gesi ni kwamba hii gesi ni lazima tujenge mabomba mengi. Sasa hivi bomba kubwa la Mtwara – Dar es Salaam liko kwenye asilimia 10 lakini likijaa kabisa gesi, ni mita za ujazo milioni 784 (*784 million cubic feet of natural gas*) ndiyo inapaswa kupita mle kwa siku. Sasa hivi bado tuko *ten percent*, lakini ikishafika pale Kinyerezi, ni lazima tujenge mabomba kwenda Morogoro, Dodoma, kila mahali, mpaka Mbeya. Hiyo ndiyo maana ya uchumi wa gesi na ndiyo maana tunasema hii nchi lazima tujenge mabomba mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ya matumizi ni kwamba elimu itakayotolewa Mheshimiwa Mbunge, nadhani siyo muhimu. Gesi ya zamani ndiyo ilikuwa inalipuka, lakini gesi ya kisasa hailipuki. Hii gesi ni *CNG (Compressed Natural Gas)*. Kwa hiyo, ukweli ni kwamba huenda hata elimu haihitajiki, ni kununua unakwenda kutumia tu na ndiyo inaingia kwenye magari. Kwa hiyo, hatuwezi kuweka gesi kwenye gari halafu tena inalipuka. Kituo cha kwanza cha gesi kiko pale Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye swali lako Mheshimiwa Nsanzugwanko, ni kwamba mkutano wa kwanza, tena nilikuwa sijamweleza Naibu Waziri, naye itabidi aniwakilishe, mzee niwakilishe; kikao cha kwanza kitafanyika Kalemee wiki ijayo cha *exploration* kwenye Ziwa Tanganyika. Ni kwamba Congo, Tanzania, Burundi na Zambia ni lazima tukae chini; tunajua kwamba kuna gesi na mafuta. Hiyo tunaweza kujua kwa sababu ya ugunduzi kule kaskazini *Lake Kivu*. Kabla hatujaanza kuzozana, ni afadhali tuanze majadiliano kwamba gesi na mafuta yakipatikana tutakuja kugawana kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *exploration* ile tunaifanya pamoja na Mto Malagarasi, tunajua dalili kwamba kuna ama gesi au mafuta, lakini huku gesi tumeshaiona huku Kipili kusini mwa Ziwa Tanganyika huku, ipo. Sasa tunataka kujua ni kiasi gani na ni mafuta kiasi gani. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo mwisho wa kipindi cha maswali kwa siku ya leo. Bado naendelea kuomba, naona Serikali inajitahidi sana kwamba Wizara nyingi majibu ni mafupi sana, lakini sasa maswali ya nyongeza bado ni marefu. Tujitahidi kwa kifupi tu unamuuliza Waziri, atajibu, atakuelewa tu.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo. Kwanza Wageni walioko Bungeni, jukwaa la Spika, ni Mgeni wa Spika wa Bunge ambaye ni Balozi Tuvwako Manongi. Balozi Manongi mtakavyokumbuka, alikuwa Mwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, Mjini New York-Marekani na sasa amemaliza muda wake na ameambatana na mke wake, Mrs Upendo Manongi. Balozi na mke wako karibu sana. Tunathamini sana mchango wako kwa Taifa hili. Tunafurahi kukuona wewe na mke wako hapa Dodoma. (Makofi)

Wageni wengine waliotembelea Bunge ni wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni walioalikwa kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo hapa Bungeni. Karibuni sana popote mlipo. Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo wako wapi tuwaone? Ahsanteni sana. Mjitahidi kuelewa mifumo yetu ya Kibunge wakati mpo hapa. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine; Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) wapo hapa Bungeni kwa ajili ya utoaji huduma ya kuwasajili Waheshimiwa Wabunge ambao hawajasajiliwa ili kupata vitambulisho vya Taifa, pamoja na kugawa vitambulisho vya Taifa kwa Waheshimiwa Wabunge ambao hawajachukua vitambulisho vyao. Huduma ya usajili itahusisha kujaza fomu za maombi ya vitambulisho, kupigwa picha, kuchukuliwa saini ya kielekroniki na kuchukuliwa alama za vidole. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge ambao hamjajiandikisha, mnaombwa kuandaa nakala ya nyaraka zifuatazo:-

Cheti cha kuzaliwa, *passport*, vyeti vya shule; eeh! Vyeti vya shule ya msingi! Heee! Kitambulisho cha mpiga kura, leseni ya udereva, *TIN number*, kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kadi ya Bima ya Afya na kadi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Waheshimiwa Wabunge, nayasoma kama yalivyo. Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbushwa zoezi hili ni muhimu na ni muhimu kwa kila Mheshimiwa Mbunge kuwa na kitambulisho cha Taifa. Usajili unafanyika kwenye Ukumbi wa Zahanati ya zamani Jengo la Ukumbi wa Msekwa kule nyuma tukatekeleze wajibu wetu huo.

Tangazo la tatu, hii imetoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu. Inawataarifu kwamba Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Kampuni ya *Ivory Tower Limited* inayohusika na shughuli za uendeshaji makazi na majengo ya biashara nchini watakuwa na maonesho ya shughuli zao za uendelezaji wa makazi na majengo ya biashara katika Jiji la Dar es Salaam, mradi ujulikanao kama *Power Village Project*. Maonesho hayo yatafanyika nyuma ya jengo la utawala kuelekea jengo la habari leo tarehe 8 Februari, 2017. Mnaalikwa wote mtembelee pale mwone waliyonayo.

Tangazo la nne, naomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati kuu ya Chama cha Wabunge cha Masuala ya Idadi ya Watu na Maendeleo (TPAPD) kuwa leo tarehe 8 mwezi wa Pili saa 7.00 mchana katika chumba namba 230 kutakuwepo na kikao. Ghorofa ya pili pale jengo la utawala, kutakuwa na kikao.

Tangazo la tano; Katibu wa Wabunge wanawake wa CCM anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanawake wa CCM kuwa leo tarehe 8 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Viongozi Wakuu wa UWT na viongozi wenu wa UWT Ukumbi wa *White House* pale Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi. Mnaombwa kuhudhuria bila kukosa. Hayo ndiyo matangazo niliyoletewa hapa mezani.

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika! Huku nyuma.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Ngoja nichukue kalamu na Makatibu wanisaidie. Mwongozo huku, hamna.

MBUNGE FULANI: Mpe kalamu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche.

MBUNGE FULANI: Aahh subiri kwanza.

MWENYEKITI: Ngoja, nachukua tu majina. Mheshimiwa Sugu na Mheshimiwa Waitara. Jamani Waheshimiwa Wabunge, muda! Unafahamu tunapochukua Wabunge wengi wa mwongozo, tunakula muda wa shughuli za Bunge.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mimi nilikuwa wa kwanza kusimama Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga. Mheshimiwa nani mwingine?

MHE. OSCAR R. MUKASA: Oscar Mukasa.

MWENYEKITI: Eeh!

MHE. OSCAR R. MUKASA: Oscar.

MWENYEKITI: Nani?

MWENYEKITI: Nianze na huyu wa mwisho, Mheshimiwa...

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Oscar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) inayozungumzia habari ya jambo linalotokea, lakini sambamba na kanuni ya 46 kuhusu majibu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikijibu swali namba 88 asubuhi ya leo, wameongelea uwezekano wa kufanya utafiti upya kuhusiana na ni nani hasa aliyeongoza Vita vya Maji Maji? Kwa kuzingatia kwamba sisi wote hapa tumesoma historia Darasa la Kwanza na wengine wameendelea mpaka viwango vya juu vya *degree*, tulishafundishwa kwamba ni Kinjekitile. Sasa kwa sababu matokeo ya utafiti yanaweza kuwa ama yakaidhinisha tulichofundishwa ama yakabatilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wasiwasi wangu ni kwamba endapo yatabatilisha mustakabali wa wote tuliosoma hivyo kwa miaka 50 na wengine wana *degree* zenye mchepuo huo, naomba mwongozo wako kuhusu uwezekano wa Serikali kutoa majibu kwa ufafanuzi zaidi kwamba endapo itatokea majibu yakawa kinyume na sisi tulichosoma na wengine wana shahada hapa, tutafanyaje? Nakushukuru. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona na ninasimama kwa kanuni ya 68(7), lakini pia napenda kusimamia kanuni ya 46(1) ambayo inawataka Waheshimiwa Mawaziri kujibu maswali kikamilifu na hapa nilikuwa narejea wakati majibu yanatolewa kwa swali namba 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba 90 linagusa hisia za watu wengi hasa sisi watetezi wa watoto wa kike kwa maana kwamba tunahitaji mtoto wa kike katika Taifa hili awe na *security* ya kupata elimu kwa kadri atakavyoweza bila kuzuiwa na hizi changamoto ndogo ndogo kama ya kupata ujauzito. Hata hivyo, majibu yaliyotolewa na Serikali hapa, hayaoneshi kuguswa na hili jambo; na Mheshimiwa Waziri wakati anajibu maswali hapa anasema kwamba mpaka akakae na wadau ndiyo aweze kujiridhisha kwamba hili jambo ni nyeti. Hivi kuna mdau gani wa mtoto kike zaidi ya Wabunge wa Kike na Wabunge wa Kiume? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako uone kama kanuni hii ya 46 hasa wakati swali hili linajibiwa ilitendewa haki. Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Sugu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nasimama kwa kanuni ya 68(7) tuokoe muda. Naomba mwongozo wako ili kuokoa Jiji la Mbeya dhidi ya mlipuko wa kipindupindu. Nasimama kwa sababu nilisimama kwenye swali namba 93 lakini nikakosa swali la nyongeza, lakini Mbeya hali ni mbaya sana, sasa kwa wiki ya pili maji hayajatoka kabisa hata tone.

MBUNGE FULANI: Wiki ya nne!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Wiki ya nne sasa. Kuanzia Uyole, Mwakibete, Sae, Mama John; Jiji lote la Mbeya maji hakuna hata tone. Juzi *weekend* nilikuwa Mbeya, Mbunge Jumapili nimeenda Kanisani bila kuoga. Sasa wananchi wa kawaida siwezi kuelewa hali iko vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niliwahi kushauri kwamba tuchukue hatua sasa twende kwenye *source* ya maji ya Ziwa Nyasa ambapo maji yale yatapita Kyela Mjini, yatakuja Tukuyu, yatapita Mbeya Mjini, Mbalizi na yatakwenda mpaka Tunduma na maeneo mengine kama ilivyofanyika Ziwa Victoria kutumika kama *source* ya maji kwenye maeneo ya Shinyanga, hivyo hivyo nilishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, tufanye nini ili Jiji la Mbeya maji yatoke *immediately* kwa sababu mradi mkubwa sana wa mabilioni ulishafanywa na Rais Kikwete akaenda kuzindua, lakini bado haujasaidia kitu? Kwa hiyo, tunafanya nini? Naomba mwongozo wako ili kuokoa kipindupindu kisilipuke Mbeya.

MWENYEKITI: Tunaendelea. Anafuata Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Nasimama kwa kanuni ya 68(7) lakini najielekeza kwenye kanuni ya 50 na 51 zote kwa pamoja. Naomba mwongozo wako kwamba maelezo haya ambayo nimemwandikia Spika na nakukupa nakala wewe, niitoe sasa hivi au niitoe baadaye?

MWENYEKITI: Hebu rudia nikupate.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema, nimesimama kwa kanuni ya 68(7), lakini najielekeza kwenye kanuni ya 50 na 51 ambayo nataka nitoe maelezo binafsi hapa. Sasa naomba mwongozo wako kama unataka nitoe maelezo hayo sasa hivi au utanipa nafasi baadaye? (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za hivi karibuni tumesikia kuna Mtanzania anaitwa Ben Sanane amepotea, haijulikani alipo...

MWENYEKITI: Hiyo ni Kanuni gani?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kanuni ya 68(7). Mtanzania mwenzetu anayejulikana kwa jina la Ben Sanane amepotea, haijulikani aliko, lakini wakati huo huo Serikali yetu...

MBUNGE FULANI: Hilo jambo halijatokea Bungeni Bwana Mwenyekiti, aah!

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo Serikali yetu tumesikia kwa muda mrefu sana ikimtafuta Faru John kwa kutumia fedha nyingi sana ambazo ni kodi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti nataka nijue, hivi kati ya Faru John na Ben Sanane ni kipi kina thamani? Ni shilingi ngapi ambazo tumetumia hadi sasa kumtafuta Faru John tukimwacha binadamu mwenzetu amepotea na Waziri wa Mambo ya Ndani hajawahi kuzungumza lolote na Serikali iko kimya. Naomba mwongozo wako kama hili suala linaruhusiwa au haliruhusiwi, kutafuta mnyama badala ya binadamu? Ahsante sana.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Kazi ya Mwenyekiti wa Mtaa hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche utaona kwamba nimekuacha makusudi kwa sababu wewe unaangukia kwenye kanuni ambayo inasimama peke yake. Tujifunze kanuni hizi. Kwanza nakushukuru sana kwamba umezingatia kanuni ipasavyo kwamba umeijulisha meza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kanuni ya 51 ukiisoma vizuri, inakutaka umjulishwe Spika mapema, lakini pia useme ni nini unachotaka kusema kwamba ni haki ipi ambayo unadhani imekiukwa. Kwa hiyo, naona yako mezani hapa, hilo limetokelezw. Nitakupatia nafasi baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mukasa ameomba mwongozo wangu unaotokana na jibu lililotolewa na Serikali kwenye swali namba 88 kuhusiana na suala la Vita vya Maji Maji na majibu ya Serikali. Wasiwasi wake anasema; "kwakuwa wote tuliosoma shule hadi hapa leo swali hili linaulizwa, tumejulishwa (na mimi pia, ndiyo, tulijulishwa) Vita ya Maji Maji, viongozi wake walikuwa akina nani; na wengine." Amesema mengi mazuri tu. Sasa anauliza, iwapo matokeo ya tathmini au tafiti itakayofanywa na Serikali utabadilisha hali hiyo, hali itakuwaje?

Mwongozo wangu kwa hili, umejiridhisha kwamba jibu limekidhi hoja ya swali la msingi. Sasa Serikali nilivyoelewa kwenye jibu lake inasema kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki watalifikisha suala hili huko ili tuone kama yaliyooombwa (*reparations*) fidia kama inaweza ikalipwa. Sasa suala litakalotokana na utafiti huo kama ni Kinjekitile na wengine hawakuwepo, basi mwongozo wangu ni kwamba itabidi historia ya Tanzania kwenye eneo hilo iandikwe upya tena. (*Kicheko/Makofi*)

Siamini kwamba historia ya nchi hii utafiti uliofanywa haukuwa wa kina kiasi cha kusema leo tutakuja kubadilisha hayo yaliyotokea. Tusubiri hayo ambayo yataletwa na Serikali, tusiwahishe mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mtolea amesema swali namba 90 lina hisia sana na kweli wakati linajibiwa hapa, majibu ya Serikali unaweza kuona walioomba maswali ya nyongeza karibu nyumba yote ilisimama. Mheshimiwa Margaret Sitta yeye alitoa ushauri wa haraka sana, lakini na Serikali nayo imesimama ikasema kwamba sheria iliyopo tumeitunga sisi wenyewe. Kama tunataka sasa tufike kwa matarajio ya wengi, basi itabidi tena sheria hiyo irejeshwe Bungeni ili tuifanyie marekebisho.

Mwongozo wangu kwa hili, pamoja na hisia zote hizo na lengo zuri tu kwamba binti huyu wa kike tunataka asome mpaka ukomo wa uwezo wake wa akili, lakini tuzingatie basi kama kuna sheria ambayo imeweka masharti fulani fulani tuishughulikie kwanza. Nilivyoielewa Serikali, ndiyo hoja yao. Sasa kama na wenyewe wanaliona hilo sasa, ni wao kujipanga haraka iwezekanavyo kama hoja hii itadhibiti waweze kuleta marekebisho ya Sheria hiyo Bungeni.

Mheshimiwa Sugu, nadhani ulikuwa unataka kusikika tu, siku nyingi hujasimama. Umesikika. Mheshimiwa Sugu umesikika! Maana kanuni ya 68(7) wewe unasema, lazima jambo hilo limetokea hapa Bungeni mapema na nilitolee mwongozo kama linaruhusiwa au haliruhusiwi. Sasa Jumapili umeenda kusali, ni kitu kizuri sana japo hukuoga, bahati mbaya sana, samahani. (*Kicheko*)

Kwa hali hiyo uliyoisemea kwa uchungu sana kuhusu suala la maji na leo maswali mawili hayo ya maji yameibua hisia za Wabunge wote. Unapokaa hapa unaona kila kona. Sasa hilo unaweza ukatumia njia mbalimbali kulifikisha hapa Bungeni, ikiwa ni swali, maelezo binafsi, *adjoinment motion* inayotaka mjadala au inayotaka maelezo ya Serikali; yote haya Waheshimiwa Wabunge kanuni hizi zinawapeni nafasi na uwanja mpana wa kuweza kuyafanya hayo. Kwa hiyo, mwongozo wangu kwa hilo, halijatokea hapa Bungeni. Kwa hiyo, siwezi kulisemea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waitara ameniuliza, ninapotaka kutoa maelezo binafsi nitoe lini? Wote tunajifunza kila siku. Kanuni ya 50 ya Kanuni zetu fasili ya (1) inasema hivi: "Mbunge yeyote anaweza kwa idhini ya Spika kutoa maelezo binafsi Bungeni yanayolenga kufafanua kuhusu jambo lolote linalomhusu na lililoifikia jamii. (2) Mbunge anayekusudia kutoa maelezo binafsi atapaswa kuwasilisha maelezo hayo mapema kwa Spika na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi 15 na maelezo hayo hayatakuwa na mjadala kuhusu jambo hilo."

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli za Bunge zinaongozwa na mpangilio ambao lazima uzingatiwe kwenye Kanuni ya 30 fasili ya (4), Shughuli za Bunge zitaendeshwa kwa mpangilio ufuatao: "Kuapishwa kwa Wabunge wapya, Taarifa ya Rais; (huu ndiyo mpangilio), Taarifa ya Spika; kuwasilisha maombi (*petitions*) kutoka kwa wananchi; Hati za Kuwasilisha Bungeni kupitia Kanuni ya 37; Maswali kwa Waziri Mkuu, Maswali ambayo Taarifa yake imetolewa; Hoja za Kuahirisha Shughuli ili kujadili mambo muhimu ya dharura; Kauli za Mawaziri;

Maelezo Binafsi ya Mbunge; ndiyo yanaangukia hapo, halafu nyingine zinafuata. Kwa hiyo, la haki na lenyewe linafuata chini ya hapa - unaweza ukapewa.

Waheshimiwa Wabunge, nianze kama nilivyosema mapema. Wewe umesimama kupitia Kanuni ya 68 (7) kuhusu mwongozo, lakini uka-link na hii ya 50. Hii ya 50 inasimama peke yake. Sasa kwa sababu unapaswa umwandikie Spika kumjulisha kwamba unataka kutoa maelezo binafsi, utaeleza yanahusu nini kwa yaliyokufika. Akishaipokea sasa, ndiyo ataiweka katika mpangilio huu, atakutambua wakati atakapona sasa inafaa utoe maelezo yako. Kwa sasa hivi siwezi kutoa mwongozo kwa sababu sijapata mapema kusudio lako la kutoa maelezo binafsi.

Mheshimiwa Haonga, nadhani na wewe ulikuwa na nia tu ya kusikika humu. Kwanza huyo Sanane sisi hatumjui ni nani. Hoja ya msingi hapa, kifungu cha 68(7) lazima ihusu jambo ambalo limetokea humu Bungeni mapema. Sasa Faru John, Sanane, sijui ni kitu gani, havituhusu sisi hapa kwa wakati huu. Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba halijakaa vizuri kupewa mwongozo. (Kicheko/Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya kusema hayo, kama nilivyosema, kwa vile meza ina taarifa kutoka kwa Mheshimiwa John Heche ya kusudio la kuwasilisha hoja kuhusu Haki za Bunge kupitia Kanuni ya 51 fasili ya (1), basi nakupa fursa hiyo, ile hatua ya kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo kujifunza tu, katika hatua hii, hata kama ungelikuja kwenye dharura, unaanza na hatua ya kwanza, unaleta ombi. Unasema kwa kifupi hicho ambacho umeruhusiwa ukiseme.

Katika hatua hiyo, hakuna haja ya kutoa hoja, kwa sababu Spika au Kiti hakijakubaliana *whether* uendeleo. Unaporuhusiwa kuendelea, sasa ndiyo unapewa ule muda, dakika 15 ufafanue sasa, hiyo unayodai ni Haki ya Bunge au la. Ukikataliwa pale mwanzoni, ndiyo mwisho wa hiyo. Kwa hiyo, napenda nikupe tu hiyo hatua ya kwanza useme nijiridhishe kama inakidhi kupewa sasa uitoe rasmi na iungwe mkono. Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHÉ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niseme kama ambavyo nimekuandikia leo asubuhi kwa Kanuni ya 51 ambayo sina sababu yoyote ya kuikariri hapa kwamba, Bunge ni chombo ambacho duniani kote kina heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge ndiyo chombo ambacho kinatunga Sheria, kinapitisha bajeti ya Serikali na duniani kote Bunge lina heshima yake. Kwa mujibu wa kitu ambacho nataka kusema, heshima ya Bunge inaanza kupotea pale Mbunge mmoja mmoja anapotezewa heshima na baadaye Bunge zima kwa umoja wake linakuwa halina heshima tena. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *trend* ambayo tumekuwa tunaiona kwa siku za hivi karibuni ambayo sasa kwa mujibu wa Kanuni hii na maelekezo yako nitatoa ufafanuzi kama utaniruhusu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge wengi sana kuhusu kunyanyaswa, kukamatwa hovy hovy bila kiti chako na Bunge lenyewe kuwa *notified*; lakini pia hata kutoka Wilayani, Wabunge wote hapa kwa umoja wetu wamelalamika vitendo wanavyofanyiwa na ma-DC huko Wilayani hata kwenye barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ajili ya kulinda hadhi na heshima ya Bunge. Sasa naomba uniruhusu niweze kuendelea na jambo hili na naomba kujadili ili Wabunge wenzangu tuone kama wataniunga mkono tulisemee kidogo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, nakushukuru kwa maelezo yako. Hujawa *very specific*, umesema ya jumla tu, lakini nimejaribu kukuelewa unakotaka kwenda katika hatua ya pili, labda ndiyo ungeweza kufafanua huko.

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi wangu, kwa sababu suala hili lilianza jana na limetolewa mwongozo, nashauri tubaki hapo hapo na uamuzi uliotolewa jana na Mheshimiwa Naibu Spika, maana ni sahihi sana kisheria. Ukiisoma Sheria ya Haki, Madaraka na Kinga za Bunge ile sehemu ya pili, mkipata nafasi isomeni tu, sitaki kurudia sababu muda umeenda sana alilieleza vizuri na huo ndiyo msimamo wa sheria yetu hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kutumia busara na hekima tu, nashauri suala hili, ili tuwe na mahusiano mazuri, maana vyombo viwili hivi; Serikali na Bunge, siyo vizuri vikafanya kazi ya kukinzana. Ushauri wangu kwa masuala ambayo yanawahusu Waheshimiwa Wabunge, tofauti na pale ambapo mtu anasema nimefanyiwa hiki, mnapima. Je, ni kanuni za Bunge zimekiukwa au inakiuka haki za Mbunge?

Sasa haya kwa sababu tunaongea na tuna Kamati mahsusi kabisa kwa masuala haya ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, nashauri Mheshimiwa Heche, ungelimwandikia Katibu wa Bunge *exhaustively* ukayaeleza haya na pendekezo lako mahsusi kwamba suala hili lililotokea kuhusiana na Mheshimiwa Chenge au Mheshimiwa 'X', haya yanayofanyika na hayo ambayo yanaweza kufanyika kesho, ifikishe kwenye Kamati ya Haki, Madaraka na Kinga ya Bunge *and then* unakuwa na kitu mahsusi ambacho Kamati itakuwa *ceased off* na kuweza kulifanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, likishafika katika hatua hiyo, kuna njia mbili; uongozi wa Bunge unaweza na wenyewe kwa busara tu ukasema hebu tulichukue suala hili na sisi tuone tuwe na majadiliano na Serikali kuhusiana na masuala kama haya yanapotokea wakati Bunge liko *in session*.

Nadhani tukienda hivyo itakuwa ni vizuri tu. Maana unaangalia, kesho kutwa tunamaliza Bunge hili, hata mimi ningepata matatizo kama siyo kutaka kupindua nchi au nimeua mtu, makosa mengine haya ni ya kawaida tu, yana dhamana. Unaweza ukasema sisi huyu tunamhitaji. Polisi huwezi ukawafundisha kazi yao. Wanajua sana na ninyi mfahamu Polisi wanajua mahali ambapo kila mmoja wetu anakaa. Wanaweza wakakusubiri huko, wakaenda.

Waheshimiwa Wabunge, nasema, naelewa ni suala zito, lakini tuzingatie tu utaratibu ambao nimeutoa kuhusiana na maombi ya Mheshimiwa Heche. Nami kwa nafasi yangu nitalifikisha pia kwa Mheshimiwa Spika. Huo ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi)*

Katibu.

MBUNGE FULANI: Hoja ya kuahirisha mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuahirisha mjadala.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kwa Kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaanza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya viwanda, Biashara na mazingira. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. *(Makofi)*

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2016, kwa niaba ya Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira naomba kuwasilisha taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imezifanya katika kipindi cha kuanzia Januari, 2016 mpaka Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao waliteuliwa kwa mujibu wa kanuni ya 116 (1) na Mheshimiwa Spika, majina yao yameorodheshwa hapa. Kwa sababu ya muda, sitayasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inasimamia shughuli zinazotekelezwa na Wizara mbili; ambazo ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017 Kamati ilihudhuria mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilitekeleza shughuli za kupokea taarifa za utendaji wa Wizara hizo; Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilikagua na kutembelea na kushauriana na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Katika Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya mwaka 2016/2017 inayotekelezwa sasa, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti katika miradi ya maendeleo kwa asilimia 16. Jambo la kusikitisha ni kwamba Serikali imeshindwa kutoa fedha hizo zilizopitishwa na Bunge kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inaidumaza azma ya Serikali ya kufikia nchi ya viwanda. Hadi kufikia Januari, 2017 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilikuwa imepokea asilimia 7.6 tu. Hali hii siyo nzuri na inaashiria Serikali kushindwa kutekeleza azma yake ya kuipeleka nchi hii kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea na kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na yenyewe hali siyo tofauti sana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Hadi Januari, 2017, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikuwa haijapokea fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hali hii inaathiri sana kiwango kikubwa cha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, napenda sasa nisome uchambuzi, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoeleza kwenye taarifa ambayo mtakuwa mmeipokea Waheshimiwa Wabunge, Kamati imetekeleza majukumu yake ya Kikanuni kwa kuzisimamia Wizara hizo na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba uniruhusu niwasilishe maoni na mapendekezo ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na kuliomba Bunge lako liazimie kuwa yawe maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la nchi kuwa ya viwanda ifikapo 2025 ni suala la kufa na kupona, ninayo imani kwamba maazimio haya ya Bunge ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati nyingine yatafuatiliwa utekelezaji wake ili kuhakikisha Taifa linasonga mbele kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kamati inaona ni jambo la msingi Bunge kuwa na kamati maalum ya kufuatilia maazimio haya tunayoyapitisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na ilibaini kwamba Wizara iliandaa mkakati wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa ambao Kamati iliona haujitoshelezi, kwa sababu haukuonesha hata bajeti ya kutekeleza jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huo pia haukuonesha namna ya kviendeleza viwanda hivyo. Pia, kasi ya utekelezaji wa mkakati huo ni ndogo, Waheshimiwa Wabunge wenyewe mnaona, kwani kwa mwaka mmoja Wizara ilituambia iliweza kutwaa kiwanda kimoja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huo pia unaonesha kuwa Serikali imejikita zaidi katika kujaribu kufufua viwanda kwa kuandaa utaratibu wa kuvitwaa na kviendesha ama kwa ubia ama peke yake, badala ya kujenga mazingira bora ya uwekezaji ili kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza na kuvifufua viwanda hivi na pia kujenga viwanda vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu, utekelezaji wa Sera ya Viwanda Nchini unaonekana kuwa ni wa kinadharia zaidi na hivyo kupelekea sekta binafsi kukosa kabisa hamasa ya kuwekeza katika kufufua viwanda na uanzishwaji wa viwanda vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania inadhamiria kuwa nchi ya viwanda, ifikapo mwaka 2025; na kwa kuwa wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi ni muhimu sana kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda; na kwa kuwa wawekezaji wanahitaji mazingira ya uwekezaji yanayotabirika, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba Serikali iandae na kutekeleza mkakati unaoweka mazingira rafiki ya uwekezaji nchini *(Ease of doing business)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa elimu na ufundi stadi ni muhimu katika ukuaji wa viwanda, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa Serikali iandae utaratibu wa kviendeleza vyo ambavyo vinatoa elimu ya ufundi ili kuhakikisha vinatoa elimu stahiki ili kupata wafanyakazi na wajasiriamali wenye taaluma ya viwanda vikubwa na vidogo. VETA na vyo vingine vya kati viandae mikakati ya kufundisha kwa mazingira na mahitaji yaliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara haipewi fedha za kutosha na kwa wakati za kutekeleza miradi ya maendeleo na hasa ile ya kimkakati, ambayo ikitekelezwa itahamasisha ujenzi wa viwanda nchini, miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Mchuchuma Liganga wa

kuchimba makaa ya mawe na kuzalisha umeme na kuchimba chuma kwa ajili ya kupata chuma na kuendeleza viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kifungu namba 2(11)(4) cha mpango wa Taifa wa miaka mitano kwa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 kinahimiza utekelezaji wa haraka wa miradi hii ya kimkakati ili kuharakisha ufufuaji wa viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa: moja, Serikali iharakishe utekelezaji wa kutoa vivutio kama vilivyokuwa kwenye makubaliano ya awali kwa kampuni ya ubia ya Tanzania, China *International Mineral Resources Company* ili iweze kuendelea na ujenzi wa mgodi. Utekelezaji huu ukamilike katika kipindi cha bajeti tuliyonayo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ilipe fidia mara moja kwa wananchi wa Ludewa ili wasiendelee kulalamikia Serikali yao kwamba imewatelekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, TANESCO ikamilishe mkataba wa kuuziana umeme na Kampuni ya *TCIMRL* ili uchimbaji wa makaa ya mawe na mradi wa kuzalisha umeme wa *Megawatt 600*, uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali ijenge barabara muhimu kwenda kwenye eneo la mradi kama ilivyokuwa imeainishwa kwenye bajeti ya 2016/2017. Ujenzi huu ukamilike kwenye kipindi cha bajeti ya mwaka Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchambua taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamati ilibaini kuwa ofisi hii haikupewa fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoendelea. Hadi kufikia tarehe 30 Januari, ofisi hii ilikuwa haijapokea kiasi chochote kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hali hii inaathiri sana utekelezaji wa majukumu ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa Serikali iipatie fedha zinazopangiwa Ofisi ya Makamu wa Rais katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ili iweze kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni muhimu kulinda viwanda vya ndani ili kukuza ajira ya Watanzania, Bunge lako Tukufu liazimie viwanda vya ndani vyenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya soko, ni vyema Serikali ikatengeneza mazingira ya kulinda viwanda hivyo. Aidha, manunuzi ya umma nayo yapendeleo viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili viwanda vya ubia kati ya Serikali na nchi nyingine au ubia kati ya kampuni, zina changamoto nyingi. Tunaiomba Serikali iongeze fedha, iongeze ubia ili iwe na maamuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi nyingi zinazosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais kama vile *TBS, TEMDO, SIDO, WMA, FCC, NEMC* na nyinginezo zilikaguliwa na kusikilizwa na zina changamoto zinazofanana. Taasisi hizo hazipewi fedha za kutosha kuweza kujiendesha, taasisi za udhibiti kama *TBS* na *WAMA, WMA* na taasisi za utafiti, *TEMDO, SIDO* na nyingine hazina maabara ya kutosha na zenye ustadi wa kutoa huduma bora. Aidha, taasisi hizi hazina watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu wa taasisi hizi katika kufufua uchumi, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie yafuatayo:-

Moja, Serikali ihakikishe inatoa fedha za kutosha kwa taasisi hizi; pili, taasisi zinazotoa huduma za utafiti na udhibiti zipatiwe fedha za kutosha badala ya kutegemea tozo za huduma za leseni. Hali hii inapelekea kuongeza gharama za uendeshaji na biashara kwa walaji; tatu, taasisi zisizoweza kujitegemea kutokana na shughuli zake kwa kuwa zinatoa huduma na siyo za kufanya biashara, zipewe OC katika bajeti ya mwaka 2018 ili ziweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi na mamlaka za udhibiti kama TBS, TIRDO na TEMDO ambazo zipo kwa ajili ya kutoa huduma, zisitozwe kodi ya VAT on capital goods zinapoagiza vifaa na vitu vya kutumia kwenye kazi zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, taasisi kama TBS na FCC (Fair Competition Commission) ambazo zina jukumu kubwa katika kulinda afya ya mlaji, Serikali itoe vibali vya kuajiri watumishi mapema iwezekanavyo ili kuongeza ufanisi wa taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zinazosimamia mazingira bora na rahisi ya kufanya kazi (ease of doing business) kama TIC, EPZA, BRELA na nyingine zikiwemo Wizara na Idara za Serikali kama Uhamiaji, Ardhi, Nishati na Madini; na Kilimo, hazina mawasiliano ya kutosha hivyo kuwepo kwa mlolongo mkubwa wa kutafuta vibali, leseni, ardhi ya kufanyia kazi na kujenga viwanda au migodi na hivyo mara nyingi kukatisha tamaa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taasisi hizi ni muhimu sana katika juhudi za kujenga viwanda na biashara kwa ujumla, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu, kuwa TIC ikishirikiana na mamlaka za udhibiti na Idara za Serikali zinazosimamia uwekezaji ziweke sehemu moja yenye maamuzi ya kuwapokelea wawekezaji wa ndani na nje (one stop center) ili kupunguza milolongo ya wawekezaji kutafuta huduma kwenye taasisi mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga maeneo ya uwekezaji nchini chini ya EPZA na SEZ lakini haitengi fedha za kutosha katika bajeti ya Wizara kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo hayo. Hivyo kufuatia kusuasua kwa ulipaji wa fidia, madeni yamekuwa yakiongezeka kutoka shilingi bilioni 60 yakaenda shilingi bilioni 191 na sasa hivi sijui yako kiasi gani. Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa Serikali katika bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa shughuli za Kamati za kukutana na kushauriana na wadau wa viwanda, biashara na uwekezaji ulibaini mambo yafuatayo: Serikali kwa ujumla imefunga milango ya mashauriano na wadau. Wadau wa uwekezaji wa viwanda, migodi, wafanyabiashara wa ndani na nje wamekata tamaa kwa sababu Serikali katika shughuli zake za usimamizi inawasumbua sana na kuwaona kama ni wakwepa kodi na hivyo wezi wa rasilimali za Taifa. Hali hii imesababisha wawekezaji wengi kuchagua nchi nyingine kwenda kuwekeza na kusababisha kupungua kwa kasi ya uwekezaji nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji hasa wa Sekta ya Uziduaji (extractive industries) wanayo hofu kubwa juu ya Serikali kuwafutia vibali na leseni kwenye miradi ambayo wamekwisha kufanya upembuzi yakinifu. Kwa kuwekeza fedha nyingi. Hali hii inaifanya nchi ipoteze taswira yake mbele ya wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya mara kwa mara, vivutio na kodi kwa wawekezaji, wafanyabiashara na wengine wote, unafanya nchi isitabirike katika uwekezaji. Kwa mfano, mabadiliko ya ushuru wa forodha yaliyowekwa katika sheria ya mwaka 2016. Mfano mwingine ni kuwalazimisha watafutaji wa mafuta, gesi na madini kulipa kodi. Tulifanya mabadiliko hayo mwaka 2016 wakati hawajaanza hata kuzalisha au kupata faida; na kuwekwa

kwa VAT kwenye *capital goods*. Mabadiliko hayo yamekatisha tamaa wawekezaji waliopo nchini na wale wanaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekii, uwepo wa wingi wa kodi za tozo, zinachelewesha sana ufufuaji wa viwanda na uanzishwaji wa viwanda vipya. Tanzania imeazimia kuwa nchi ya viwanda; na kwa kuwa masuala ya kuvutia mtaji kutoka nje (*FDI*) ni mhimili mmojawapo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda; na kwa kuwa wawekezaji wanahitaji mazingira mazuri ya uwekezaji, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie yafuatayo:-

Kwanza, Serikali ifungue milango ya mawasiliano kati yake na wadau wake mbalimbali kwa kuweka utaratibu wa kukutana na wadau hao mara kwa mara, ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, watoa huduma wawapokee wadau wenye biashara, viwanda kwa upole kama wadau wa maendeleo, badala ya kuwaona kama maadui na wahalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wake wa kusimamia ujenzi wa uchumi na kuhudumia wananchi wake, ili kujenga uchumi wao binafsi, Serikali izingatie sheria zilizopo kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali izipitie upya tozo na kodi zinazosababisha mazingira ya uwekezaji yasitabirike. Tozo hizo ni pamoja na VAT kwenye vifaa vya *capital goods*; lakini VAT nyingine nyingi ambazo mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge tulizipitisha ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa bajeti kama ilivyoielezwa, Kamati iliweza kutembelea na kukagua miradi michache sana, hususan minne. Mradi wa kufufua Kiwanda cha *General Tyre*, Mradi wa Viuadudu Kibaha, Mradi wa Kuhifadhi Mazingira Ufukwe wa Bahari ya Dar es Salaam na mradi wa *EPZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iligundua na kuainisha kuwa mradi wa maendeleo wa kufufua viwanda wa matairi ulikuwa haujapatiwa fedha za kuutekeleza, japokuwa Serikali imeeleza kuwa imeunda timu ya wataalam kuchambua na kupata mwelekeo mpya.

Kwa kuwa ni azma ya Serikali kufufua viwanda vilivyobinafsishwa na kufa; na kwa kuwa mradi wa kiwanda cha *General Tyre* ni miongoni wa viwanda muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi, Bunge liazimie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itekeleze mradi huu kwa haraka sana. Taarifa ya tathmini ya wataalam iwasilishwe kwenye Kamati katika kipindi cha wiki mbili kama ilivyokuwa imeahidiwa kwenye Bunge lililopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea viwanda binafsi mbalimbali kuona mafanikio na changamoto zinavyovikabili viwanda hivyo. Viwanda hivi vinatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini na kuuza mazao yaliyoongezwa thamani hapa nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vina changamoto na upungufu unaofanana, zikiwemo uhaba wa umeme wa kutosha na kuaminika. Gharama kubwa ya malighafi ya

viwanda kiasi cha kulazimika kuagiza kutoka nje na baadhi ya viwanda kukosa soko la ndani na migodi kuwa na ajira ya wafanyakazi wenye ujira mdogo na mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukuza viwanda vya ndani ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ikiwa ni pamoja na kulinda ajira kwa wananchi ni la msingi sana. Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie yafuatayo:-

Moja, Serikali iimarishe miundombinu ya umeme, maji, barabara ili kuvipa viwanda uwezo wa kuzalisha bidhaa kwa gharama nafuu; *(Makofi)*

Pili, Serikali ihakikishe inalinda bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ya nchi, kwa kuweka kodi kwenye bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi au kupiga marufuku uagizaji wa bidhaa zinazozalishwa na kutosheleza soko hapa nchini. Tatu, Serikali iimarishe taaluma mbalimbali wa kuanzisha mafunzo ya taaluma stadi zinazohitajika. Nne, Serikali isimamie ajira na haki za wafanyakazi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Bandari ya Dar es Salaam na kukutana na wadau wa Bandari ya Dar es Salaam, TRA na TPA na kushuhudia shughuli za huduma bandarini hapo. Kamati pamoja na kushuhudia upungufu wa shughuli za bandari ilielezwa na TPA na TRA kwamba kupungua kwa shehena bandarini kulitokana na mdodoro wa uchumi ulioathiri nchi ya China na dunia; kuwepo kwa uchaguzi wa nchini Zambia na kupungua kwa uchimbaji wa madini ya shaba DRC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa wadau, wao walieleza kwamba hali hiyo imesababishwa pia na kupandishwa kwa ghafla kwa tozo za huduma za bidhaa bandarini; kuanzishwa kwa kodi ya ongezeko la thamani kwa huduma zinazotolewa kwa mizigo ya bidhaa inayopita bandarini; VAT on auxiliary services on transit kwenda Rwanda, Zambia na kadhalika; na kuanza kutumika kwa utaratibu wa himaya moja ya ushuru wa forodha kati ya DRC na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bandari hii ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Taifa letu; na kwa kuwa Serikali imeazimia kufufua uchumi wa Taifa la Tanzania ni muhimu sana kuikua bandari ili itoe huduma bora. Kamati inaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudi zake za kufufua tena shughuli za Bandari ya Dar es Salaam kwa kufanya mashauriano na wadau, wafanyabishara wa nchi ya Kongo na Zambia wakiwemo Waheshimiwa Maraisi wa nchi hizo. Hii imeifanya Bandari ya Dar es Salaam ianze kufanya vizuri tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa, Serikali iendelee kufungua milango ya mawasiliano na mashauriano kati yake na wadau wake mbalimbali wafanyabiashara na watumiaji wa bandari ya Dar es Salaam, wawekezaji wengine wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali iangalie upya madhara ya kutozwa kwa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mizigo inayopita. Tatu, Serikali izishawishi nchi nyingine hususan Jamhuri ya Kenya yenye bandari shindani ya Mombasa ianze kutumia utaratibu wa *single custom territory*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ili kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam na kupunguza kero za mamlaka za udhibiti, ni vyema Serikali ikaanzisha *one stop center* kuwahudumia watumiaji wa bandari. Mwisho, Serikali ichambue upya faida na hasara za tozo na kodi nyingine zilizoongezeka kwenye huduma ya Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutembelea viwanda na shughuli za uhifadhi wa mazingira na kupokea taarifa ya shughuli hizo, Kamati ilichambua uhalisia wa shughuli hizo. Kamati ilibaini kuwa jamii haina uelewa wa kutosha juu ya athari za mazingira jambo linalowapelekea kuharibu mazingira bila kujali. Aidha, matumizi ya mkaa ni makubwa sana na ndiyo chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi na viwanda vingi nchini havitunzi mazingira ipasavyo, lakini pia miradi mingi ya maendeleo nchini, chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais haitekelezwi kwa weledi na kwa wakati kwa sababu haipewi fedha ya kutosha. Pia mradi wa Ziwa Victoria unamalizika Desemba, 2017, lakini siyo endelevu kwa kuwa hautakuwa umeleta matokeo tarajiwa ya kulilinda ziwa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua mipango ya Serikali ya kuwasaidia wachimbaji wadogo, wananchi wa maeneo ya migodi kwa kuwapa masalia ya mawe yajulikanayo kama magwangala, lakini wachimbaji hawa...

(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kukaribia kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Kengele ya kwanza hiyo...

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia haijatambua umuhimu wa kutekeleza miradi ya uhifadhi wa mazingira kwani hata bajeti iliyotengwa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mazingira ni suala mtambuka; na kwa kuwa mipango mingi inayopangwa kutekelezwa sasa ya ujenzi wa viwanda inahusisha mazingira; naomba Bunge lako Tukufu liazimie yafuatayo:-

Moja, Serikali iongeze juhudi za kuhifadhi na kutunza mazingira; tozo na kodi za mazingira kwenye Mfuko wa Mazingira nchini ulioanzishwa katika bajeti ya mwaka wa 2016/2017 zipelekwe kwenye mfuko huo;

Pili, Bunge liazimie pia kwamba kutekeleza mkakati wa utunzaji wa mazingira nchini kwa kuanzisha miradi ya utunzaji visiki hai, upandaji miti na utunzaji wa Ziwa Victoria ufanywe kwa nguvu ya tofauti.

Tatu, Bunge liazimie kubuni utekelezaji kwa umahiri na weledi wa kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutekeleza mradi wa namba 5301 wa *climate change*.

Nne, Serikali ikutane na wadau wa plastiki na kufanya mazungumzo ili kupata muafaka wa namna ya kusitisha utengenezaji wa bidhaa hiyo. La sivyo, tutaharibu ajira nyingi sana katika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hitimisho kwa kusema, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, kwa uongozi wake wa kuisaidia Kamati; na pia nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha taarifa hii. Pia nachukua nafasi hii kuwashukuru Mawaziri wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa January Makamba na Naibu Waziri, Mheshimiwa Luhaga Mpina kwa ushirikiano wao wa kuisadia Kamati yetu. Nawashukuru pia Makatibu Wakuu na Watendaji kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Kashiillah na Watendaji wengine wote kwa kuisaidia Kamati yetu. Mwisho, nawashukuru Makatibu wa Bunge wakiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto; Katibu, Ndugu Zainab na mwisho Ndugu Pauline. Ahsanteni sana kwa kuisaidia Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Nawaona wote huko. Ahsante sana.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA
MAZINGIRA KUANZAIA JANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2016, kwa niaba ya Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imezifanya katika kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (5) ambazo katika sehemu ya kwanza inaelezea maelezo ya jumla, sehemu ya pili shughuli zilizotekelezwa na Kamati, sehemu ya tatu inahusu Uchambuzi na matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati, sehemu ya nne imebainisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati na sehemu ya tano ni Hitimisho la taarifa hii.

1.1 WAJUMBE WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira uliowateua kwa mujibu wa kanuni ya 116 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la 2016 ni hawa wafuatao:-

- | | | |
|----|----------------------------------|-------------|
| 1. | Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Vicky Passcal Kamata, Mb | M/wenyekiti |
| 3. | Mhe. Salim Hassan Turkey, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb | Mjumbe |

6.	Mhe. Khatib Said Haji, Mb	Mjumbe
7.	Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb	Mjumbe
8.	Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb	Mjumbe
9.	Mhe. Anthony Calist Komu, Mb	Mjumbe
10.	Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
11.	Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mb	Mjumbe
12.	Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb	Mjumbe
13.	Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
14.	Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb	Mjumbe
15.	Mhe. Jesca David Kishoa, Mb	Mjumbe
16.	Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb	Mjumbe
17.	Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb	Mjumbe
18.	Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb	Mjumbe
19.	Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb	Mjumbe
20.	Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb	Mjumbe
21.	Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb	Mjumbe
22.	Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb	Mjumbe
23.	Mhe. Dkt. Raphael M.M. Chegeni, Mb	Mjumbe
24.	Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb	Mjumbe
25.	Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb	Mjumbe
26.	Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb	Mjumbe
27.	Mhe. Joyce John Mukya, Mb	Mjumbe

1.2 MUUNDO NA MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira imepewa majukumu yafuatayo:

- (i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;
- (ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo;
- (iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- (iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016, mbali ya majukumu ya msingi ya Kamati kama yalivyo ainishwa hapo juu Kamati yoyote inaweza kupendekeza kwa Spika kupewa majukumu ya nyongeza, pia Spika anaweza kukabidhi jambo lolote jingine kwa Kamati yoyote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo.

1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitumia njia mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utendaji kutoka kwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambazo ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira pamoja na Taasisi zilizo chini yake;

(ii) Kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utendaji wa Taasisi ambazo utendaji wake unahusiana na utendaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;

(iii) Kukutana na wadau wa Sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira kwa ajili ya kusikiliza maoni na changamoto zao;

(iv) Kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati, ile iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pia ambayo haikutengewa Fedha kwa ajili ya kubaini umuhimu wake ili kuweza kuishauri Serikali kuipatia fedha ili iweze kutekelezwa;

(v) Kutembelea Viwanda ambavyo vinachakata malighafi zinazozalishwa hapa nchini; na

(vi) Kupatiwa Semina mbalimbali kwa lengo la kujengea Kamati uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZILIZOFANYA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inasimamia shughuli zinazotekelezwa na Wizara mbili (2), ambazo ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Kamati katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017 ilihudhuria mafunzo na kutekeleza shughuli za kupokea taarifa za utendaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na taasisi chini ya Wizara hizi na zile ambazo shughuli zake zinahusiana na shughuli za Sekta ya Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilikagua Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira.

2.1 MAFUNZO NA SEMINA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipatiwa Semina mbalimbali kuhusu masuala yanayohusu Sekta zilizo chini ya Wizara inazosisimamia kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati, Semina hizo zilifanyika katika kipindi cha Bunge la Aprili, Septemba na Novemba, 2016 Februari, 2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata Semina ya Uchambuzi wa Bajeti iliyoendeshwa na *Legislative Support Program* chini ya Ofisi ya Bunge. Katika Semina hiyo Kamati ilijengewa uwezo juu ya Bunge na Kamati zake na majukumu ya Mbunge katika Kamati. Pia walijengewa uelewa katika masuala ya uchambuzi wa Bajeti na Miswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipewa Semina kuhusu Fursa za Mtangamano wa Afrika Mashariki. Semina hii iliendeshwa na Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki ambapo Kamati ilipata kuzifahamu fursa zinazopatikana katika Mtangamano huu.

Mheshimiwa Spika, Semina nyingine ilikuwa Semina ya Mazingira Kuhusu Visiki Hai. Semina hii iliendeshwa na Taasisi ya *LEAD Foundation*, ambapo Kamati ilijengewa uelewa kuhusu masuala ya mazingira hususani katika Mradi wa upandaji miti ukikusisha Visiki Hai ambao ni utaratibu wa kutnza maeneo yenye visiki hai vya miti ili vikue kuwa miti na misitu tena. Mradi wa Visiki hupunguza ili kupunguza gharama za upandaji miti upya. Visiki hai; kwa kuwa tayari vipo vinao uwezo wa kukabiliana na hali ya hewa kama vitatuzwa tu na ni rahisi kustawi tena kwa gharama ndogo badala ya kupanda miti upya.

Mheshimiwa Spika, aidha, Semina ya Soko la Bidhaa iliitolewa kwa Wajumbe wa Kamati. Semina iliendeshwa na watu wa *Capital Market and Security Authority* ambapo lengo lilikuwa ni kuwapatia Wajumbe uelewa juu ya masoko ya bidhaa na uanzishwaji wa soko la biadhaa hapa Tanzania na fursa zitakazopatikana pindi Soko hilo litakapo anzishwa hapa Tanzania.

2.2 KUPOKEA TAARIFA ZA UTENDAJI WA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI PAMOJA NA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira pamoja na Taasisi zilizopo chini Wizara hizi na zile zinazohusika na usimamizi wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Mazingira lakini hazipo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati.

2.2.1 Taarifa za Wizara Ya Viwanda, Biashara Na Uwekezaji

A. Mkakati wa Serikali wa Kurudisha Viwanda Vilivyobinafsishwa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu Mkakati wa Serikali katika kuvirudisha viwanda vilivyobinafsishwa ambayo kwa sasa havifanyi kazi. Taarifa hiyo ilitoa historia fupi ya jinsi ubinafsishaji ulivyofanyika, taratibu zilizotumiwa kubinafsisha viwanda hivyo, hatua walizofuata katika kutaka kutekeleza zoezi la kuvirudisha viwanda hivyo na changamoto katika kutekeleza zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa hii na kubaini mambo muhimu matatu. Kwanza, Serikali haikuwa na Mkakati unaojitosheleza wa kutekeleza mpango huu kwani hakukuwa hata na bajeti iliyoainishwa na iliyotengwa kwa ajili utekezaji. Mkakati huo pia haukuonyesha namna ya kviendeleza Viwanda hivyo. Pili, kasi ya Serikali katika kutekeleza Mkakati huo ni ndogo sana kwani kwa mwaka mmoja na nusu sasa imefanikiwa kutwaa kiwanda kimoja tu.

Mheshimiwa Spika, Jambo la tatu ni ni kwamba Serikali imejikita zaidi katika kujaribu kufufua viwanda kwa kuandaa utaratibu wa kuvitwaa na kviendesha aidha kwa ubia au peke yake badala ya kujenga mazingira bora na ya rafiki ya uwekezaji (*ease of doing business*) ili kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika Viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri na kupendekeza kwa Seikali mambo yafuatayo:-

(i) Serikali iongenze nguvu za kuwavutia Wawekezaji wapya na kuwapa mazingira rafiki ya kuwekeza kwemye Viwanda vilivyobinafsiwa na kujenga viwanda vipya;

(ii) Serikali iongeze nguvu na kasi katika kuwavutia wawekezaji wapya kwa kutafuta maeneo ambayo yatakuwa maalumu kwa viwanda na kuyajengea miundombinu muhimu ili kujenga Viwanda vipya;

(iii) Serikali iandae mazingira mazuri kwa wawekezaji ili waweze kuzalisha kwa gharama nafuu na kuuza bidhaa zao kwa bei nafuu. Hatua hii itaongeza ushindani na bidhaa zinazolingia kutoka nje ya nchi; na

(iv) Katika kutekeleza Azma ya Serikali ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Uchumi wa kati ambao msingi wake ni Viwanda ni lazima Serikali ijipange kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Aidha, fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya Wizara hii zitolewe kwa wakati.

2.2.2 Bajeti za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka Fedha 2015/2016 pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati iliishauri Serikali kujitahidi kuzingatia na kutekeleza ushauri wa Kamati. Kamati inaendelea kusisitiza utekelezaji wa Mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti inayotekelezwa sasa ya mwaka wa fedha **2016/2017** Kamati iliipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti katika Miradi ya Maendeleo kutoka sh **35,387,381,000/=** mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka sh **42,159,950,000/=** mwaka wa fedha **2016/2017**. Ongezeko lililokuwa sawa na asilimia **16.06** ya Bajeti ya mwaka **2015/2016**. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba Serikali imeshindwa kutoa fedha zilizopitishwa na Bunge kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa wakati. Kwa namna hii azma ya Serikali ya kufikia nchi ya Viwanda ifikapo mwaka 20125 inaweza kuwa ndoto.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia robo ya pili ya Mwaka wa Fedha **2016/2017**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilikuwa haijapokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, hadi kufikia mwezi **Januari, 2017** imepokea kiasi cha Sh Billioni **7.6** tu sawa na asilimia **18.6** ya Fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hali hii siyo nzuri na inaashiria Serikali kushindwa kutekeleza Azma yake ya kutekeleza miradi mingi ya Maendeleo kama ilivyokuwa imepanga.

2.2.3 Taarifa za Utendaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira

A. Taarifa kuhusu Mustakabali wa Bidhaa za Plastiki na Viwanda vya Plastiki Nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Ofisa ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Mustakabali wa bidhaa za Plastiki na Viwanda vya Plastiki nchini. Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau wa plastiki kusikiliza hoja zao kuhusu kusudio la Serikali la kupiga marufuku baadhi ya bidhaa za plastiki. Wadau wa viwanda vya plastiki waliomba Serikali iwaongeze

muda ili waweze kujipanga kwa ajili ya mabadiliko hayo. Kamati ilishauri kuwa kabla ya kuzuia uzalishaji wa ndani wa mifuko ya Plastiki, Serikali uingizaji haramu wa mifuko ya plastiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano kati ya Kamati, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Wadau wa plastiki Kamati ilibaini kuwa; Wazalishaji wa ndani wanachangia kiasi kidogo sana cha uharibifu wa mazingira kwa kuwa mifuko mingi ya Plastiki inaingizwa kutoka nje ya nchi kwa njia zisizo za halali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya maamuzi haya kwa kufanya utafiti katika nchi kama Rwanda ambayo ni nchi ndogo na ni rahisi kudhibiti mipaka yake katika uingizaji wa bidhaa haramu. Aidha, wakati nchi ya Rwanda inapiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchi hiyo haikuwa na hata kiwanda kimoja kinachozalisha plastiki. Serikali inatakiwa kujifunza kwa kuangalia nchi kubwa kama India ambayo ilijaribu kutekeleza utaratibu wa kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki lakini walishindwa.

Mheshimiwa Spika, kuna athari kubwa sana za kiuchumi kwa wazalishaji hawa wa ndani kwa kutekeleza uamuzi huu haraka kwani wadau wa plastiki wamewekeza fedha nyingi katika Viwanda hivi, pia wana mikopo katika mablenki hivyo kufungwa kwa viwanda hivi kutaleta athari pia kwenye mablenki na kuondoa ajira zipatazo 60,000 kwa watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali itekeleze mpango huo kwa kutoa muda wa kubadilisha biashara (*grace period*) isiyozidi miaka 3 ili Wazalishaji waweze kuendelea na uzalishaji kwa muda kidogo huku wakifanya utaratibu wa kuhamia katika teknolojia rafiki kwa mazingira au kubadilisha biashara.

B. Taarifa Kuhusu Kupitiwa Upya kwa Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliwasilisha Rasimu ya Sera Mpya ya Mazingira; Sera inayoandaliwa kuchukua nafasi ya Sera ya sasa iliyoandaliwa mwaka 1997 takribani miaka 19 iliyopita. Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997 imepitwa na wakati kwa kuwa haikuwa imehusisha changamoto zilizopo katika mazingira ya sasa kama mabadiliko ya Tanbianchi. Hivyo Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa kuona umuhimu wa kuipitia na kuifanyia maboresho ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa.

C. Taarifa ya maendeleo ya Mradi wa Upandaji Miti nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipatiwa uelewa juu ya Mradi wa Upandaji miti nchini. Mradi huu ulielezwa kwenye Mkakati wa Upandaji Miti ulioandaliwa kutokana na kiasi kikubwa cha uharibifu wa misitu nchini unaosababisha kupotea kwa misitu na kusababisha uharibifu wa makazi na bioanuai. Mkakati huu unalenga kupunguza kasi hii kwa njia ya kupanda na kutunza miti na kuhakikisha kwamba nchi nzima inakuwa ya kijani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa pamoja na mambo mengine Mkakati uliolenga kurekebisha changamoto zilizojitokeza za utegemezi wa wafadhili katika kufadhili miradi ya namna hii na kutoshirikisha wananchi/wadau katika kutekeleza miradi hii. Mradi huu utazingatia changamoto za awali ili kupata matokeo chanya ya Mradi. Ilielezwa pia kuwa Mkakati ulihusisha kuanzishwa kwa Mfuko wa Mazingira Nchini uliotengewa **Sh. Bilioni 2.1** katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, ilibainika pia kuwa kuna matumizi makubwa ya nishati ya mkaa ambapo asilimia 70 ya uharibifu wa misitu unachangiwa na mahitaji ya nishati ya mkaa. Kwa mfano Jiji la Dar es Salaam pekee linatumia magunia 200,000 hadi 300,000 kwa mwezi, yenge

wastani wa kilo 50 kwa kila gunia. Hali ya Mazingira nchini ni mbaya inakisiwa kwamba uvunaji wa misitu usiozingatia taratibu za utunzani wa mazingira ni hekta 372,000 kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kuwa Mkakati wa Upandaji Miti na Uhifadhi wa maeneo ya Hifadhi ni lazima uende kwa kasi kubwa Zaidi kuliko ilivyo sasa.

D. Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha **2015/2016** na kuchambua Makadirio ya mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha **2016/2017**. Katika mapitio hayo kamati ilibaini kwamba Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha **2015/2016** ilikuwa ni asilimia **11** tu ya Bajeti yote ya Ofisi ya Makamu wa Raisi, na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ulikuwa ni asilimia **1** tu ya Bajeti yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti unayotekelezwa sasa ya **2016/2017** pamoja na Serikali kuongeza bajeti ya maendeleo kutoka Sh, **3,868,847,000** kwa Mwaka wa Fedha **2015/2016** hadi sh, **10,973,083,448** kwa Mwaka wa Fedha **2016/2017** ongezeko hili ni sawa na asilimia **64.7** lakini mpaka kufikia tarehe **30 Januari, 2017** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilikuwa haijapokea kiasi chochote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka HAZINA. Hali hii inaathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa majukumu ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira.

2.2.1 Taarifa za Utendaji wa Taasisi Chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

A. Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Taasisi hii inahusika na usajili wa makampuni chini ya Sheria ya Makampuni ya sheria za nchi; usajili wa majina ya biashara chini ya Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara; usajili wa alama za biashara na huduma chini ya Sheria ya Alama za Biashara na Huduma; na usajili wa leseni za viwanda kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto inazokabiliana nazo BRELA ni pamoja na uelewa mdogo wa wadau wengi katika uendeshaji wa makampuni na biashara kwa ujumla; wadau wengi kutotaka kutumia wataalamu wakati wa usajili na uendeshaji wa makampuni; na uelewa mdogo na ukosefu wa miundombinu ya TEHAMA kwa wadau walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa ushauri kwa taasisi ya BRELA kuwa kutokana na uelewa mdogo wa baadhi ya wamiliki wa Makampuni juu ya umuhimu wa shughuli zake ni vema BRELA ikapeleka shughuli zake karibu na wananchi katika ngazi ya mkoa na wilaya ili kupunguza mawakala matapeli. Aidha, Kamati iliipongeza Mamlaka hiyo kwa kuingia kwenye mfumo wa kujisajili wa kielekroniki, na kuishauri kuupitia upya mfumo huo na kuraahisisha kidogo ili uweze kutumika kirahisi Zaidi na wadau walio wengi.

B. Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya hali ya uwekezaji nchini kutoka kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), walielezewa huduma zinazotolewa na kituo, majukumu ya kituo na mafanikio na changamoto katika uendeshaji wa kituo.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya taasisi ya TIC ni pamoja na kubuni mbinu za kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kuwekeza kwenye biashara, Viwanda, Migodi na Shughuli nyingine za kukuza uchumi; kusaidia wawekezaji kupata vibali mbalimbali na hati za biashara kisheria; na kuandaa na kusambaza taarifa sahihi kuhusu fursa za utekelezaji pamoja na upatikanaji wa mitaji na wabia wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine ya TIC ni kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta muhimu zitakazokuza uchumi kwa haraka; na kushirikiana na serikali kutafuta maeneo ya uwekezaji na kuyatayarisha ili wawekezaji wapate urahisi wa kuanza uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu hayo TIC inakabiliana na changamoto kadhaa zikiwemo mlolongo mrefu wa uhawilishaji wa ardhi kutoka ardhi ya jumla na kupewa mwekezaji; ukosefu wa maeneo kwa ajili ya uwekezaji; upatikanaji duni wa mitaji kwa ajili ya wawekezaji wa ndani; na migogoro ya ardhi baina ya wawekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, urasimu katika baadhi ya taasisi na Idara za Serikali katika kuwahudumia wawekezaji katika kutoa huduma bora na ya haraka ikiwa ni pamoja na kuchelewa kuwapa ardhi, huduma za nishati (kama umeme) na kuchelewa kutoa leseni na vibali mbalimbali ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri kuwa TIC ikishirikiana na Mamlaka za udhibiti na Idara za Serikali iweke *One Stop Center* ili kupunguza mlolongo wa wawekezaji kutafuta huduma kwenye Taasisi na idara nyingi za Serikali. Aidha TIC ikishirikiana na na Mamlaka za Miji, Halmashauri za Miji, na Taasisi ya EPZA watoe na kutenga maeneo ya uwekezaji nje kidogo ya miji na makazi ili kuepuka migogoro ya ardhi. Nje ya miji kuna maeneo mengi tena yasiyo na migogoro ya ardhi kama maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Spika, TIC ijitangaze zaidi na kuhakikisha shuhuli zao zinafahamika vizuri kwa wananchi na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje.

C. Shirika la Udhibiti wa Viwango Nchini (TBS)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuelewa shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa viwango nchini (TBS). Ilikezwa kuwa majukumu ya Shirika ni pamoja na kutayarisha na kutangaza viwango vya ubora wa bidhaa za Tanzania kwenye sekta zote nchini; kutekeleza viwango vya ubora vilivyotangazwa kwa kutumia mifumo mbalimbali ya udhibiti; kupima sampuli zilizokusanywa na wakaguzi wa TBS; na kutoa mafunzo kwa wenye viwanda na biashara juu ya uzalishaji na utoaji huduma bora kwa kuzingatia viwango.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linakabiliana na changamoto kadhaa zikiwemo uelewa mdogo wa umma na jumuiya ya wafanyabishara juu ya umuhimu wa viwango katika kulinda afya na usalama wa mlaji na kuongeza uwezo wa kuuza bidhaa zetu nje ya nchi; ufinyu wa nafasi katika maabara zake wakati ufanyaji wa kazi wa shirika unategemea sana matokeo ya kimaabara. Maabara zilizopo sasa zinauwezo wa kuhudumia sampuli chache wakati mahitaji ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni uhaba wa wafanyakazi katika shirika, ili shirika ililiweze kufanya kazi kwa ufanisi linahitaji wafanyakazi 750 na kwa sasa linao wafanyakazi 366 tu. Jambo hili linapelekea Shirika kufanya kazi nusu ya zile zinatarajiwa kufanyika na kusababisha tatizo la uwepo wa bidhaa zisizo na viwango nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Shirika halipati bajeti kwa ajili ya maendeleo na wakati huo huo shirika linapoagiza vifaa kwa ajili ya matumizi ya maabara zake zinatozwa kodi, Kamati inashauri Serikali ifute kodi kwenye vifaa hivi ili kupunguza gharama kwa Shirika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kulipa shirika hili fedha ya kutosha kujiendesha badala ya kutegemea tozo za uduma, lakini pia shirika lisaidiwe kuajiri watumishi wa kutosha na kuwa na maabara za kutosheleza kazi zake za msingi.

D. Wakala wa Vipimo Nchini (WMA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Wakala wa Usimamiza na Udhhibiti wa Vipimo Nchini (WMA) na kujifunza kuhusu majukumu ya Wakala huu. Majukumu ya Wakala ni pamoja na kuhakiki na kudhibiti usahihi wa vipimo mbalimbali vvinavyotumika katika biashara nchini; kumlinda mlaji kwa kuhakiki na kudhibiti usahihi wa vipimo mbalimbali vinavyotumika kwenye biashara, afya na usalama wa mazingira; kutoa taarifa na maelezo ya kitaalamu kuhusu masuala ya vipimo; na Kufuatilia usahihi wa vipimo.

Mheshimiwa Spika, changamoto za Wakala wa Vipimo nchini (WMA) ni pamoja na uchakavu wa vifaa vya kiufundi; gharama kubwa za ununuzi wa vifaa vya kitaalamu; uhaba wa watumishi katika soko hususani wa Kada ya Maafisa Vipimo; na wakala wa vipimo kutumia sheria za vipimo zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utendaji kazi wa Tasisi ya WMA Kamati inaishauri Serikali kuipa Taasisi ya WMA fedha za kutosheleza mahitaji yake ya kujiendesha badala ya kuitaka Tasisi kukusanya fedha kutokana na tozo za kutoa huduma; kwani mamlaka hii ipo kwa ajili ya kutoa huduma na si kwa ajili ya kufanya biashara. Hali hii inailazimu Taasisi hii kuongeza bei ya huduma zake na kuongeza gharama kwa mlaji.

E. Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Mamlaka ya Biashara Tanzania (TanTrade) kuhusu ushindani katika Sekta ya Biashara Nchini, Kikanda na Kimataifa. Katika kutekeleza majukumu yake taasisi inashughulika na kufanya tafiti za kuendeleza bidhaa na kupata masoko; kujenga uwezo wa Sekta ndogo na za kati ili kujiendeleza na kujiimarisha kiushindani; kutangaza bidhaa kwa masoko ya ndani na nje; kutoa ushauri wa sera za Biashara na Uwekezaji; na kusimamia maonyesho ya Kimataifa nchini kama maonyesho ya Kimataifa ya Biashara (sabasaba).

Mheshimiwa Spika, changamoto za Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE) ni pamoja na wafanyabiashara wengi wa ndani kuendelea kuuza mazao au bidhaa nje ya nchi zikiwa ghafi badala ya kuchakata malighafi ili kuuza bidhaa iliyoongezwa thamani; wafanyabiashara kuendelea kufanya biashara nje ya nchi kwa kupitisha bidhaa mipakani kwa njia za panya bila kufuata taratibu.

F. Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

Mheshimiwa Spika, kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kuhusu Shughuli za Uendeshaji wa Shirika na Mikakati yake ya kupelekea Tanzania kuwa ya Viwanda. Taarifa ya NDC iliwasilisha maelezo ya Mradi wa Mchuchuma-Liganga ambao pia ipo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

(2016/2017 – 2020/2021). NDC ilieleza pia miradi mingine miwili ambayo ni Miradi ya Kimkakati kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja 2016/2017. IMiradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Magadi soda wa Engaruka Mkoani Arusha, Mradi ya Makaa ya Mawe Ngaka na Mradi wa Viuadudu Wilayani Kibaha. Miradi hii inaelezwa kwenye aya zifuatazo hapa chini.

i) Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga

Mheshimiwa Spika, Mradi huu wa Kimkakati ulianza kutekelezwa mwaka 2011 ambao unatekelezwa na kampuni ya *Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL)* ambayo ni ubia kati ya NDC na kampuni ya *Sichuan Hongda* ya China. Mradi huu unahusisha kuanzishwa kwa mgodi wa makaa ya mawe unaotarajiwa kuzalisha makaa si chini ya tani milioni 3 kwa mwaka, kituo cha kufua umeme *Megawatt 600*, wenye msongo wa umeme swa *Kilo Volt 220*; na mgodi wa Chuma Liganga unaoweza kuzalisha chuma ghafi kadiri ya tani milioni million 1 kwa mwaka. Uwekezaji wa mradi huu unakadiriwa kuwa Dola za Kimarekeni Bilioni 3 na uzalishaji unatarajiwa kuanzia mwaka 2018/19.

Mheshimiwa Spika, Utekezaji wa mradi ni pamoja na kutolewa kwa leseni ya uchimbaji madini; kukamilika kwa uchorongaji wa kubaini kiasi cha malighafi ya chuma iliyopo; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kubaini kuwa mradi unaweza kutekelezwa kwa faida.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa uthaminishaji wa mali za wananchi walio ndani ya maeneo ya mradi ili kulipa fidia stahiki. Majadiliano yanayoendelea kati ya kampuni ya ubia ya Tanzania China International Mineral Resources Limited na TANESCO juu ya mkataba wa kununua umeme PPA yaliyotarajiwa kukamilika Agosti, 2016 lakini hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Mchuchuma-Liganga tangu mwanzo ulipewa hadhi ya uwekezaji wa kimkakati lakini mpaka sasa *Government Notice (GN)* kuidhinisha vivutio vilivyotolewa haijatangazwa na hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kuanza kwa utekezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa miundombinu ya barabara na madaraja kuelekea maeneo ya miradi, jambo ambalo linakwamisha shughuli za mradi kwani itahitajika kusafirishwa vifaa na mashine nzito kwa ajili ya mradi na baadaye kusafirisha malighafi ya chuma kwenda Viwandani na kwenye masoko. Changamoto nyingine ni kutokuunganishwa kwa Wilaya ya Ludewa kwenye Gridi ya Taifa ili iweze kubebe umeme usiopungua megawati 600 utakaozalishwa na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuchelewesha kutoa fidia kwa wananchi waliopo kwenye maeneo ya mradi kunawanyima haki wananchi wa Wilaya ya Ludewa kupata manufaa ya mradi wanayoyatarajia. Aidha, kuchelewa kwa makubaliano kati ya TCIMRL na TANESCO kuhusu PPA na kutotolewa kwa GN kuhusu vivutio vinakwamisha utekezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashindwa kuelewa kwa ni Serikali haifanyi uamuzi wa haraka wa mambo ambayo awali Serikali ilikubaliana na Mbia kutoa vivutio kwenye mradi huu wa Kimkakati na Mkataba wa kuuziana Umeme *Power Purchase Agreement (PPA)* kati ya TANESCO na Mbia huyu. Aidha Serikali inasuaua kulipa fidia kwa wananchi pamoja na kwamba Mbia alishatoa shillingi Bilioni 2 kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iharakishe utekezaji wa Mradi huu wa Kimkakati kwa: kutoa vivutio kama yalivyokuwa makubalianao ya awali; kulipa maramoja fidia kwa wananchi wa Ludewa ili wasiendeleo kulalamikia Serikali kwa

kuwatelekeza; TANESCO iingie Mkataba wa kuuziana Umeme (PPA) na kampuni ya TCIMRL ili mradi wa kuzalisha umeme wa MW 600 uweze kuanza; na mwisho Serikali ijenga barabara muhimu kwenda kwenye eneo la Mradi.

Mheshimiwa Spika, NDC pia iliieleza Kamati maendeleo ya utekelezaji wa Miradi mingine mitatu ambayo si ya Kimkakati. Miradi hiyo ni; Mradi wa Magadi soda wa Engaruka Wilayani Monduli; Mradi wa Makaa ya Mawe Ngaka Mkoani Ruvuma; na Mradi wa Viuwadudu Wilayani Kibaha.

ii) Mradi wa Magadi Soda wa Bonde la Engaruka

Mheshimiwa Spika, Mradi wa magadi soda uliopo wilayani Monduli, mkoani Arusha, wenye lengo la kuanzisha uchimbaji wa magadi na kuanzisha kiwanda cha kuzalisha magadi si chini ya tani milioni 1 kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya kemikali nchini na kuuza nje. Mradi huu unatekelezwa na NDC kwa niaba ya Serikali na lengo la mradi ni kupata mbia wa kujenga kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi unahusisha uchorongaji ili kubaini wingi na ubora wa magadi umekamilika na kiasi cha takribani mita za ujazo bilioni 4.7 za magadi ya maji (brine) kwa ajili ya kuzalisha magadi soda zimegunduliwa. Utafiti wa njia bora za uvunaji magadi magadi umefanyika, NDC imeainisha mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kiwanda na maombi rasmi yameshapelekwa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya Monduli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo ya mradi kufikia bado unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo Kukosekana kwa fedha za kufanya tafiti za msingi (Techno-Economic na ESIA); hadi leo hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu; uwepo wa miundombinu hafifu ya barabara, reli, umeme na Bandari ya Tanga; na gharama kubwa ya kupata maji safi kwa matumizi ya kawaida kujenga miundombinu ya kusambaza maji safi.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ukitekelezwa unazo faida nyingi sana ambazo ni pamoja na kuondoa utegemezi wa kuagiza magadi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya viwanda vyetu vya kemikali, kupata fedha za kigeni kwa kuuza magadi nje ya nchi, kuchochea uendelezaji wa Viwanda vya kemikali nchini pamoja na viwanda vingine vitumiavyo magadi kama malighafi na mwisho itachochea ujenzi wa miundombinu kuelekea katika maeneo ya mradi.

iii) Mradi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unahusisha mgodi wa makaa ya mawe wenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 2.5 kwa mwaka katika eneo la Ngaka na kituo cha kufua umeme wa Megawati 400 ambao utaunganishwa katika Gridi ya Taifa. Upembuzi yakinifu uliofanyika mwaka 2010/2011 umebaini uwepo wa tani milioni 423 za makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unamilikiwa kwa pamoja kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) yenye hisa asilimia 30 na Kampuni ya Tancoal Energy Limited ya Australia yenye hisa asilimia 70. Mradi huu ukikamilika utaweza kuliingizia Taifa mapato ya Dola za Kimarekani milioni 197.3 kwa mwaka na kutoa ajira kwa watu 3,250.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mradi huu unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa Miundombinu ya msongo wa umeme katika eneo la mradi, ukimilishaji wa Mkataba wa kuuza umeme na miundombinu ya usafirishaji wa makaa ya mawe ni dhaifu. Aidha, Mradi huu

umeanza kuchimba makaa yam awe kwa lengo la uwauzia watumiaji wa nishati hii wakiwemo Viwanda vya saruji.

Mheshimiwa Spika, Mgodini wa Makaa ya mawe wa Ngaka ulipewa zabuni ya kupeleka makaa ya mawe kwenye Kiwanda cha Saruji cha Dangote kiasi cha tani laki moja na nusu kwa mwezi lakini kilishindwa kukidhi mahitaji ya kiwanda hicho kwani kiliweza kupeleka tani elfu 25 tu kwa mwezi hali iliyokisumbua sana kiwanda hicho baada ya Waziri anayehusika na Nishati kuzuia uingizaji makaa ya mawe kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali ambayo ni Mbia katika Mgodini hu kuingezea Uwekezaji ili kuinua uzalishaji wa makaa ya Mawe ili kutosheleza soko la ndani.

iv) Mradi wa Kiwanda cha Viadudu Kibaha

Mheshimiwa Spika, mradi wa kiwanda cha viadudu ni kiwanda cha kuzalisha vimelea vya kibiolojia kwa ajili kuua viluilui wa mbu ili kukabiliana na kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni miongoni mwa miradi ambayo ilitembelewa na Kamati katika kipindi cha ukaguzi wa miradi mwezi Machi, 2016. Katika kipindi cha ziara Kiwanda kilikuwa katika hatua za kufanya uzalishaji wa majaribio, Kamati ilijulishwa kuwa Kiwanda kimefanya uzalishaji wa majaribio wamepata kama lita milioni kumi na tatu (13). Uzalishaji kwa ajili ya biashara ulikuwa haujaanza kutokana na changamoto ya mtaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepata taarifa kutoka NDC kuwa mradi huu ulipata fedha kutoka Serikalini kwa ajili kuwalipa mkandarasi Shilingi Bilioni 2.1 na fedha kwa ajili ya kuanza uzalishaji mradi Shilingi Bilioni 4.6 imekopwa kutoka NSSF, hivyo basi mradi umeanza uzalishaji kwa ajili ya biashara. Kwa sasa Kiwanda kinazalisha lita 96,000 kwa mwezi na kimeanza kupokea oda kutoka ndani na nje ya nchi, mfano nchi ya Niger imeweka oda ya lita 100,000.

G. Bodi ya Leseni ya Maghala (TWLB)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Bodi ya Leseni ya Maghala (TWLB) kuhusu namna Bodi ilivyojipanga kukabiliana na Urasimu wa Mfumo wa Stakabadhi Maghalani katika kuelekea kuanzishwa kwa Soko la Bidhaa ambalo utendaji wake unategemea sana Mfumo huo. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mfumo huu ni kukuza juhudi za Serikali kurasimisha mifumo ya masoko iliyopo kwa lengo la kupunguza vipingamizi mbalimbali vinavyokwaza mwenendo mzima wa masoko ya kilimo ambapo wakulima wameonekana kuonewa kwa kiasi kikubwa na wanunuzi wakaguzi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unafanyakazi kwa kujenga maghala na kukusanya mazao ya wakulima kwenye maghala na kuwapa wakulima stakabadhi yenye thamani sawa na mazao yake. Mfumo huu unamhakikishia mkulima soko zuri la mazao yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa mfumo huu kwa mkulima, mfumo wa mazao ghalani unachangamoto nyingi sana zikiwemo upotevu wa mazao ghalani kutokana na baadhi ya wamiliki wa maghala kutokuwa waaminifu; ukosefu wa uelewa kwa wadau na upotoshaji wa makusudi. Uhaba wa watendaji na vitendea kazi; uchakavu wa maghala na miundombinu yake; gharama kubwa za uendeshaji wa maghala; na ukiritimba wa vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na urasimu uliopo katika Mfumo wa Stakabadhi Maghalani Bodi inaunganisha mifumo ya utoaji taarifa (kati ya Bodi, soko la bidhaa, taasisi

husika na wadau) ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi tena kwa wakati. Aidha, Bodi inasimamia kwa makini Jukwaa la kuuzia mazao ya wakulima kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na wadau wengine na kuwachukulia hatua wahujumu na wabadhirifu waliopo ndani ya mfumo.

H. Shirika la Uhandisi wa Mitambo ya Viwanda Tanzania (TEMDO)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa taarifa juu ya shirika la Uhandisi na Mitambo ya Viwanda Tanzania. Kamati ilipata uelewa juu ya shughuli za Shirika hilo. TEMDO inajishughulisha na utafiti, ubunifu ili kuendeleza na kuunda mitambo, teknolojia, mashine na vifaaa mbalimbali na kuhamasisha utengenezaji wake kibishara; TEMDO pia inatoa huduma za kihandisi kwenye viwanda vikubwa na vya kati kwa lengo la kuongeza ufanisi na matumiza bora ya rasilimali; na linatoa mafunzo kwa wahandisi na mafundi mchundo viwandani na taasisi nyingine ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Shirika linazo changamoto katika kutekeleza majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na kutokusambazwa kwa mashine na teknolojia zilizobuniwa na kuendelezwa na TEMDO katika kiwango cha kuwafikia watumiaji wengi katika sehemu mbalimbali; kutokutosheleza kwa vitendea kazi na mazingira duni ya uendelezaji wa shughuli za ubunifu na kukuza teknolojia; na

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni ukosefu wa fedha za kuboresha maabara na kuwa na vifaa vya kisasa; na ukosefu wa mafunzo juu ya utafiti na kukosekana kwa motisha kwa wafanyakazi na ufinyu wa bajeti unakwamisha shughuli za shirika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, shirika la TEMDO likihudumiwa vizuri ni nyenzo muhimu na mahususi ya uendelezaji wa Viwanda nchini. Kamati inaiomba Serikali ilisaidie shirika hili kusimama. Kamati iliishauri TEMDO kujikita katika kufanya tafiti chache kwa kuzingatia ufinyu wa Bajeti yao. Tafiti hizi zizingatie kupata mitambo ambayo itawafikia na kuwanufaisha watu wengi zaidi. Mfano mitambo itakayosaidia kuongeza thamani mazao yetu ya kilimo ili tuweze kuongeza thamani bidhaa (*final products*) nyingi kutoka nchini badala ya kuuza malighafi tu.

I. Baraza la Ushindani (FCT)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipatiwa Taarifa ya Utendaji wa Baraza la Ushindani (FCT), Baraza la Ushindani linajishughulisha na: kusikiliza mashauri ya rufaa kutoka tume ya Ushindani na mamlaka za udhibiti; kudhibiti, kutengua au kubadilisha uamuzi au amri ya Tume ya Ushindani (FCC) au mamlaka ya udhibiti husika; na kurudisha shauri kwenye tume ya Ushindani au mamlaka ya udhibiti na kuwaamuru kutafuta ushahidi upya.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake baraza linakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti, ushiriki hafifu wa Baraza katika mikutano muhimu ya kimataifa, upungufu wa vitendea kazi, Baraza kutojulikana kwa wadau, Baraza kutokuwa na wawakilishi nje ya Dar es salaam na ushindani wa kibiashara kuwa jambo lisiloeleweka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Baraza la Ushindani Kamati ilielezwa kuwa Bajeti ya Baraza inachangiwa na taasisi (EWURA, TCRA, SUMATRA na TCAA) wakiwa wadau wa Shirika. Hali hii inajenga mazingira kuwa wanapoingia kwenye mgogoro na mtu, Baraza wakati wa kutoa hukumu inaweza isiwe ya haki/halali kwa kuhofika kama wakimuhukumu mdau wao wanaweza kukosa fedha. Kamati inashauri Serikali iangalie upya jambo hili kama inataka wadau wengine kuwa na imani na Shirika.

J. Tume ya Ushindani- Fair Competition Commission (FCC)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipatiwa Taarifa ya Utendaji wa Tume ya Ushindani (FCC), Tume ya Ushindani inajishuhulisha na: kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ushindani ili kuhamasisha ushindani na pia maslahi ya mlaji; kuchunguza na kutafiti juu ya masuala yanayohusu ushindani na kulinda maslahi ya mlaji; kuchunguza vikwazo katika ushindani pamoja na vizuizi katika kuanzisha na kufungua makampuni katika uchumi na sekta kwa ujumla; na kushauriana na asasi za walaji, mamlaka za Udhhibiti na asasi za biashara na watu wengine wenye maslahi ili kuhakikisha wanamlinda mlaji.

Mheshimiwa Spika, Tume katika kutekeleza majukumu yake inakabiliana na mbalimbali ikiwa ni pamoja na idadi ndogo ya watumishi kulinganisha na mahitaji ya makubwa ya Tume ya kutoa huduma kwa mlaji; uelewa mdogo wa wadau kuhusu Sera na Sheria ya ushindani na faida zake kwa jamii na uchumi; Tume kutopata nafasi ya kushiriki kutoa maoni katika rasimu za Sera na sheria kabla ya Sheria hizo kupitishwa rasmi na Bungeni; uhaba wa vitendea kazi; kutokuwepo kwa sera madhubuti ya kumlinda mlaji; na Bodi za Mazao kuwa na uwezo wa kisheria wa kupanga bei na viwango vya ubora wa mazao badala ya kuiachia nguvu ya soko. Mfano ni Bodi za Tumbaku, Pamba na Korosho zinapanga bei za kuwakandamiza wakulima.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliitaka Serikali kuhakikisha inaipatia Tume vibali vya kuajiri ili kuongeza rasilimali watu katika Tume hivyo na kuiwezesha kuwafikia wadau wengi. Bajeti ya Tume inachangiwa asilimia 45 na taasisi ya SUMATRA, EWURA, TCAA na TCRA hivyo Kamati ilishauri Serikali kusimamia kwa karibu Mamlaka hizi kuhakikisha zinaipatia Tume fedha hizo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Aidha, migogoro mingi kati ya Tume na wadau inatokana na uelewa mdogo juu ya Sheria ya Ushindani, Kamati iliishauri Tume kujitangaza na kuhakikisha wadau wake wanauielewa wa kutosha juu ya Sheria hizo.

K. Baraza la Utetezi wa Mlaji (NCAC)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Baraza la Utetezi wa Mlaji (NCAC), Kamati ilibaini kuwa Baraza halijawahi kufanyakazi tangu 2011. Kutokufanya kazi kwa NCAC tangu 2011 kunaashiria kuwa Shirika hili siyo muhimu kuwepo au majukumu yake yanaweza kutekelezwa na taasisi nyingine. Kamati ilitoa ushauri kuwa Serikali iangalie majukumu ya Taasisi zake na kama yanafanana au hazina umuhimu ziunganishwa na kupewa nguvu ili ziweze kufanyakazi kwa tija.

L. Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda Tanzania (CTI) na Wafanyabiashara

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kukutana wawakilishi wa wenye Viwanda nchini kwa lengo la kusikiliza changamoto za ukuaji wa Sekta ya Viwanda na Uwekezaji. Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda Tanzania (CTI) iliwasilisha changamoto inazokumbana nazo na ushauri wake kwa Serikali kuhusu namna bora ya kukuza sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, CTI pamoja na wafanyabiashara mmoja mmoja walitoa maelezo ya changamoto wanazokabiliana nazo na kutoa mapendekezo ya utatuzi. Baadhi ya changamoto walizoziwasilisha ni pamoja na uduni wa huduma za kifedha ambapo Serikali kupitia Benki Kuu inazikopesha Benki za Biashara kwa riba ya juu hivyo kulazimu benki hizo pia kukopesha kwa riba kubwa na kusababisha wafanyabiashara wengi kushindwa kumudu kukopa. Aidha, Uingizaji holele wa bidhaa kutoka nje ambazo zinaweza kuzalishwa na viwanda vyetu vya ndani imeongeza ushindani katika soko na unadhohofisha viwanda vya ndani. Mfano TANESCO wanapoagiza transfoma wakati TANELEC wanazalisha bidhaa hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kubwa kwa wadau wa biashara na Viwanda ni pamoja na tozo nyingi za mamlaka za uthibiti, kwa mfano TBS, TFDA, OSHA, FIRE, NEMC, Mkemia Mkuu, SUMATRA n.k. Ipo pia changamoto ya kodi kubwa katika kuingiza malighafi nchini ambazo uingizaji wa malighafi unatozwa kodi sawa na bidhaa iliyoongezwa thamani; kwa mfano malighafi ya kutengenezea dawa ya meno ya *whitedent* ni sawa na tozo yakuingiza dawa ya meno iliyo kamili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukutana na wadau wa Viwanda na Biashara Kamati ilishauriana na Serikali (Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wadau wengine) kuhusu changamoto za ukuaji wa Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji, na mikakati ya kufikia Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa nne kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na wadau kuhusu Mkakati wa kufikia Tanzania ya Viwanda. Taarifa hizo ni taarifa ya CTI na taarifa ya TPSF, taarifa ya muelekeo na muafaka wa kufikia Tanzania ya Viwanda iliyotolewa na NEMC na Taarifa ya Mkakatiwa Serikali kufikia nchi ya Viwanda ifikapo 2025.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano hayo yafuatayo yalidhihirika:-

(i) Upatikanaji wa mitaji ni changamoto miongoni mwa wadau wengi. Mwekezaji akitaka kuanzisha kiwanda kikubwa au biashara kubwa ni vigumu sana kupata mtaji mkubwa kutoka mabanki;

(ii) Upatikanaji wa vibali vya kuanzisha kiwanda una mlolongo mrefu sana na unapitia taasisi nyingi sana kabla ya kupata kibali hicho; na

(iii) Maabara za Taasisi au mamalaka za udhibiti hazina vifaa vya kutosha kufanya uchunguzi wenye kukidhi masharti ya kimataifa hivyo kuzikwamisha bidhaa zizalishwazo nchini na kushindwa kuingia katika masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali iziwezeshe Taasisi zake kifedha, vitendea kazi na maabara ili kuhakikisha zinakidhi vigezo vya kimataifa; na ni lazima Serikali ifanye utafiti kamilifu kuhusu faida za kiushindani tulizonazo ili kufanya maamuzi sahihi.

2.2.4 Kutembelea na Kupokea Taarifa za Utendaji wa Taasisi ambazo Utendaji wake Unaathiri Shughuli za Viwanda, Biashara na Uwekezaji

A. Kupokea maoni ya wafanyabiashara watumiaji wa Bandari ya Dar es Salaam pamoja na Ziara ya Kamati katika Bandari ya Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitembelea Bandari ya Dar es Salaam ili kujionea hali halisi ya Biashara na utendaji katika bandari hiyo. Kabla ya ziara Kamati ilifanya kikao na Wadau wa Bandari ili kupata changamoto wanazokabiliana nazo. Katika kikao hicho pamoja na Kamati kufanya ziara kwenye Bandarini ya Dar es Salaam changamoto zifuatazo zilibainika:-

(i) Uwepo wa mfumo wa Himaya moja ya Ushuru wa Forodha kwa Nchi za Afrika ya Mashariki (*Singe Custom Territory*) unatumika kati ya nchi ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) tu. Mfumo huu unataka bidhaa zinazolingia nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kulipiwa kodi mara moja kwenye Bandari ya nchi itakayoingilia. Hata hivyo, kutumika kwa utaratibu huu kwa Tanzania pekee katika nchi za Afrika Mashariki kumefanya

baadhi ya wafanyabiashara wa DRC kuihama Bandari ya Dar es Salaam kwa madai kwamba unaongeza gharama. Wafanyabiashara hao wamehamia katika Bandari nyingine hususani Bandari ya Mombasa, Nakara na Beila ambazo hazitumii utaratibu huu;

(ii) Kutozwa kwa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye huduma inayotolewa kwenye mizigo ya bidhaa zinazopita katika Bandari ya Dar es Salaam (*VAT on auxiliary service on transit goods*) ni kikwazo kwa wafanyabiashara na kuwafanya wahamie katika Bandari ambazo hazitozi VAT ya aina hiyo. Bandari ya Dar es Salaam ndiyo pekee inayotoza VAT katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika kwenye huduma zitolewazo kwenye bidhaa zinazopita. Kutoza VAT kwenye huduma zinazotolewa kwenye bidhaa zinazopita imetafsiriwa kuwa ni kutoza VAT kwenye bidhaa zinazoenda nje ya nchi utaratibu huu ni kinyume na sheria za kimataifa ambapo bidhaa za *export* au *transit* hazitozwi VAT;

(iii) Uwepo wa Mamlaka na Taasisi za Udhhibiti nyingi na kutoka Wizara tofauti katika Bandarini. Taasisi hizo ni pamoja na TRA, TBS, TFDA, NEMC, FCC, OSHA, SUMATRA, Mkemia Mkuu, Fire n.k. Utaratibu huu unawalazimu watumiaji wa Bandari kuwa na mlolongo mrefu sana na kutumia muda mwingi kutoa mizigo Bandarini;

(iv) Kupanda kwa ghafla kwa gharama nyingi za leseni ni changamoto kubwa sana kwa watumiaji wa Bandari. Baadhi ya mifano ya gharama hizo zinajumuisha zifuatazo:-

§ Malipo ya leseni ya *transit* kutoka Dola 12 mpaka Dola 200 kwa kila gari. Wadau walieleza kuwa mabadiliko haya yalifanywa na Serikali bila kuwashirikisha wadau, na wadau waliona tangazo tu kwenye Gazeri la Serikali.

§ Bei ya vibandiko vya SUMATRA imepanda kutoka Tsh. 7,000 mpaka Tsh. 120,000 sawa na asilimia zaidi ya 1,000 jambo linalowaumiza wafanyabiashara ya usafirishaji; na

§ Kuanzishwa Kwa Tozo ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kwenye Mbolea inayoagizwa Kutoka nje ya Nchi au kupitia Bandari ya Dar es Salaam kutoka Dola 1 hadi 2 kwa *metric* tani moja ya kemikali kulingana na aina ya kemikali. Tozo hii ni kubwa sana na inatozwa katika Bandari ya Dar es Salaam pekee, katika nchi nyingine kama Afrika ya Kusini hutoza Dola 100 tu kwa *Bill of Lading*. Hatua hii inaongeza gharama za kutumia Bandari ya Dar es Salaam na kusababisha wafanyabiashara wanaopitisha mbolea katika Bandari ya Dar es Salaam kuamua kutumia Bandari za nchi jirani kama vile Durban nchini Afrika Kusini na Beira na Nakara nchini Msumbiji;

(v) Uamuzi wa Serikali kuwahamasisha wawekezaji kuwekeza katika Biashara ya Bandari Kavu (ICDs na CIDATs) ili kupunguza msongamano wa Bandari ya Dar es Salaam iliojitokeza kuanzia mwaka 2008. Wawekezaji waliitikia wito na kuwekeza kuipunguzia msongamano Bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, kila Bandari Kavu moja iliwekeza wastani wa Dola za Kimarekani milioni 10 kwa ajili ya kununua ardhi na kuwekeza kwenye miundombinu. Lakini tangu shughuli za biashara ilipopungua Bandarini, Serikali haijachukua hatua mahsusi ya kukabiliana na tatizo hilo na wawekezaji wengi wamekabiliwa na matatizo ya kibiashara kwa vile wengi walikopa Benki ili kuwekeza. Uamuzi wa Serikali kwamba ICDs na CIDAT zote ziondoke katikati ya Jiji na ziwe kilomita 30 kutoka Bandarini, una athari kubwa kwa wawekezaji hawa kwani gharama za uwekezaji huo hazijarejeshwa. Utekelezaji wa agizo hili utawalazimu wawekezaji kufanya uwekezaji mpya wakati wanadaiwa mikopo na wengi wameshindwa kulipa kutokana na kupungua kwa shehena Bandarini. Aidha, ni vyema kutambua kuwa wafanyabiashara hawa walihamasishwa na Serikali kusaidia ujenzi wa ICDs ili kusaidia kuunguza mizigo kwenye Bandari ya Dar es Salaam iliyokuwa imezidiwa na mizigo wakati ule. Walichukua

mikopo katika mabenki ili kufanya uwekezaji huu hivyo agizo hili linaathari kubwa sana kwa wadau hawa na pia kwa mabenki.

(vi) Hatua ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuongeza bei (*uplifting*) kwenye bidhaa zinazolingia nchi hususani magari imekuwa kikwazo kikuwa na chanzo cha kupungua kwa shughuli kwenye Bandari ya Dar es Salaam kwani vigezo vinavyotumika havipo wazi. Wafanyabiashara wengi hupata katika minada na magulio kwa bei nafuu lakini wakifika Bandari ya Dar es Salaam mzigo hiyo hupandishwa bei (*uplifting*) bila kuwasikiliza wenye mizigo wala kuangalia nyaraka zilizoambatana na mzigo au bidhaa hiyo. Jambo hili linaongeza gharama na kuwafanya wadau wengi kuhama Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika; kutokana na mambo hayo yaliyojitokeza Kamati ilipotembelea Bandari ya Dar Es Salaam na kukutana na TRA, TPA na wadau wa Bandari ya Dar Es Salaam, Kamati iliishauri Serikali mambo yafuatayo:-

(i) Serikali kufungua milango ya mawasiliano kati yake na wadau wake mbalimbali (wafanyabiashara na watumiaji wa Bandari ya Dar es Salaam na wawekezaji wengine) wa ndani na Nje ya nchi, badala ya kuwaona kuwa wote ni wakwepa kodi na wezi;

(ii) Serikali kuwasiliana na Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; Malawi, Zambia, Burundi, Rwanda na nchi zingine watumiaji wakubwa wa Bandari ya Dar es Salaam ili kutoa elimu sahihi juu ya uzuri wa bandari ya Dar es Salaam ili nchi hizo ziwashawishi wafanyabiashara na watumiaji wa Bandari ya Dar Es salaam kwenye nchi zao kurudi tena kuitumia Bandari ya Dar es Salaam;

(iii) Serikali kuangalia upya madhara ya kutozwa kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma zinazotolewa katika mizigo au bidhaa inayopitia bandari hiyo kwenda nchi za jirani (*VAT on auxiliary services on transit goods*) za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda na Uganda. Hususan ni tafsiri iliyojengeka kwa wenye mizigo na bidhaa ambao ni watu wa nje kuwa wanatozwa kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa au mizigo yao kinyume na sheria za kimataifa kwa vile wanaolipa kodi hiyo ni ni wao na wala siyo watoa huduma na kama kuna ukweli yafanyike marekebisho ya sheria mwezi Januari au mwaka wa Fedha 2017/18 baada ya kupata chanzo kingine cha mapato.

(iv) Serikali kushawishi nchi zingine hususan Kenya yenye Bandari shindani ya Mombasa ianze kutumia pia utaratibu wa Himaya moja ya Ushuru wa Forodha (*Single Custom Territory - SCT*), ili kuondoa hisia hasi kuhusu gharama za kutumia Bandari ya Dar es Salaam eti kutokana na kuanza kutumika kwa Mfumo wa SCT na kuleta utangamano wa kiuchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(v) Muda wa kutunza mizigo ya mafuta (*Liquid Cargo*) Bandarini ni mdogo uongezwe kutoka siku 30 mpaka 90 kufanana na Bandari zingine kama Mombasa na Nakara ili kuleta ushindani ulio sawa.

B. Uendelezaji wa Jotoardhi Nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya Taasisi ya *Tanzania Geothermal Development Corporation* (TGDC) kuhusu ya shughuli za uendelezaji wa chanzo cha nishati ya Jotoardhi (*Geothermal Energy*) na uhusiano wake katika utunzaji mazingira kwa lengo la kupata uelewa kuhusu nishati mbadala ambazo pia ni rafiki wa mazingira. Kamati pia ilipata uelewa juu ya vyanzo vingine vya nishati vitakavyo saidia kuongeza nishati hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa majukumu ya kampuni, maeneo ambayo mradi umeshaanza kutekelezwa, ambako ni maeneo yenye viashiria vya uwepo wa jotoardhi hapa nchini. Maelezo pia yalitolewa kuhusu changamoto inazokumbana nazo katika kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, maelezo yalitolewa pia kuwa nishati itokanayo na Jotoardhi hupatikana kwa gharama nafuu na kwa uhakika kwa kuwa haitegemei hali ya hewa. Utumiaji wa nishati hiyo hauna athari katika mazingira kwa kuwa hutoa nishati safi na kwa kutumia eneo dogo la ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mradi huu ni mpya unatekelezwa kwa mara ya kwanza nchini, hivyo hakuna wataalamu wa kutosha wenye ujuzi wa fani hii. Na hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuwa kwa kushirikiana na VETA ianzishe kozi ya Jotoardhi kwa ngazi ya VETA, Cheti na Diploma ili kupata wataalamu wazawa; na

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali mambo yafuatayo:-

- i) Kutunga Sheria ya Jotoardhi na kuingia Mkataba Mikataba inayozingatia maslahi ya pande zote mbili yaani Serikali na Mwekezaji.
- ii) Kuipatia ruzuku za kutosha TGDC ili iweze kununua vifaa vya kitaalamu vya kutosha na kukamilisha upatikanaji wa Niashati ya Jotoardhi kuanza kusambazwa kwa ajili ya matumizi kwa gharama nafuu.

2.3 UKAGUZI WA MIRADI NA TAASISI ZILIOPO CHINI YA WIZARA ZINAZOSIMAMIWA NA KAMATI

2.3.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 na ile ambayo haikutengewa fedha.

A. Mradi wa NDC-Revive of General Tyre

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo, Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu 44.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa NDC-Revive of General Tyre unatekelezwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ambao ni mradi wa ukarabati na ufufuaji kiwanda cha Matairi cha General Tyre kilichopo katika jiji la Arusha ambacho kilisimamisha uzalishaji wake tangu mwaka 2009. Katika Bajeti ya 2015/2016 Mradi huu ulitengewa shilingi **Bilioni 2.15** kwa ajili ya kukamilisha awamu ya tatu ya ukarabati wa mfumo wa umeme na mitambo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba hadi kufikia tarehe 31 Juni, 2016 mradi huu ulikuwa haujapelekewa fedha yoyote hali iliyosababisha mradi huu kutokutekelezwa. Ucheleweshaji wa kupeleka fedha kwenye mradi huu umepelekea kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huu kwa muda mrefu na kusababisha ongezeko la gharama za ufufuaji wa kiwanda kutoka **Bilioni 45** mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka **Bilioni 60** mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa maelezo ya Serikali; fedha hiyo itahitajika kwa ajili kukamilisha ukarabati wa awamu ya tatu na kufanya majaribio ya uzalishaji kabla ya kuanza uzalishaji kamili.

Mheshimiwa Spika, hali ya utekelezaji wa mradi huu sio ya kuridhisha. Kamati haioni nia ya dhati ya Serikali katika kufufua kiwanda hiki. Juhudi zilizofanyika za kufufua kiwanda hicho hadi sasa hazitoshi kwani mitambo iliyopo imechakaa na hata kama itafanyiwa ukarabati

haitaweza kuzalisha kwa uwezo unaostahiki kwa sababu ya kupitwa na wakati wa teknolojia ya kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuchelewa kwa utekelezaji wa muda mrefu wa kufufua kiwanda hiki iliamuriwa kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 kiwanda kilipangiwa shilingi **Milioni 150** tu kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu ili kuona ni namna gani kiwanda hiki kinaweza kufufuliwa kwa kuangalia ununzi wa teknolojia mpya badala ya kufufua mitambo iliyopo ambayo imepitwa na wakati kabisa.

Mheshimiwa Spika, nusu ya mwaka wa Fedha wa 2016/2017 kamati ilitaka kujua hatua ya Mradi huu ilipofikia ambapo aliomba Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu hatua za Utekelezaji wa mradi huu. Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa hakuna hatua nzuri iliyofikiwa kwani serikali ilikuwa haijafanya upembuzi wowote ambao ungeshirikisha wataalamu mbalimbali waliobobea kwenye tasnia ya matairi ili kupata namana nzuri ya kifufua kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, Baada ya Taarifa kuwasilishwa, Kamati iliagiza kupatiwa Taarifa ya upembuzi huo utakapokamilika mapema iwezekanavyo ili iweze kushiriki kutoa ushauri stahiki kwa Serikali ikiwa na uelewa wa kutosha. Aidha, Kamati ilihamngazwa na uwepo wa NSSF katika kundi la wataalamu wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa kiwanda cha General Tyre kwani Shirika la NSSF tayari ni Mbia katika kiwanda. Hivyo taarifa ya upembuzi yakinifu inaweza kuwa haina weledi kwa vile inaweza kumpendelea Mbia huyo.

B. Mradi wa Benjamin William Mkapa – Economic Processing Zones Agency (EPZA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Wakala wa EPZA pamoja na Mradi wa Benjamin William Mkapa - EPZ, ili pamoja na mambo mengine kujionea baadhi ya Viwanda vilivyopo katika eneo hili. Kamati ilipata maelezo juu ya Uwekezaji unaofanyika na Vivutio vilivyopo chini ya mradi huo. Maelezo yalitolewa pia juu ya masoko ya nje kwa ajili ya Viwanda hivyo na faida inayopatikana kutokana na uendeshaji wa Mradi huu wa EPZA.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa EPZA hutenga na kusimamia maeneo maalum ya uwekezaji ya ya *Economic Processing Zones (EPZ)* na *Special Economic Zones (SEZ)*; maeneo yaliyowekwa maalumu kwa ajili ya kuanzisha viwanda ili kupata bidhaa kwa ajili ya masoko ya nje nani je ya nchi. Katika kutembelea Taasisi ya hii (EPZA) na Mradi wa Benjamin William Mkapa Kamati ilibaini mambo ifuatavyo:-

i) Vivutio vilivyopo chini ya Mradi huu ni vizuri sana lakini vinatumiwa sana na Wawekezaji kutoka nje sababu Wawekezaji wazawa hawana uelewana pia uwezo wa kifedha juu ya miradi hii;

ii) Maeneo yanatengwa chini ya Mradi huu lakini Serikali haitengi Bajeti kwa ajili ya kulipa fidia za maeneo hayo. Hali hii hupelekea kuongezeka kwa ghara ma ya fidia. Mfano Katika mwaka wa fedha 2015/2016 fidia hiyo ilikuwa **bilioni 60**. Wakati Kamati inatembelea mradi huu Mwezi Machi, 2016 deni lilikuwa limefikia **bilini 191**. Ongezeko hili linatokana na riba ya ucheleweshaji; na

iii) Taasisi zinazosimamia uwekezaji kama TIC, TBS, TRA, BRELA, n.k. hazitoi ushirikiano wa kutosha kwa EPZ na SEZ katika utendaji wake wa kazi na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa wawekezaji kwa kutumia muda mrefu kufuatilia viabali kuwekeza chini ya Miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali mambo yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa bidhaa nyingi zinazozalisha chini ya EPZ na SEZ zinazuzwa nje ya nchi. Kamati ilipendekeza kuwa Serikali itoe vivutio (*incentives*) kwa wawekezaji chini ya miradi hii zitakazowawezesha pia kuuza baadhi ya bidhaa hapa nchini na sio bidhaa zote kusafirishwa kwenye masoko ya nje ya nchi tu;

(ii) Ili kuwezesha upatikanaji wa haraka wa maeneo ya uwekezaji, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuwalipa fidia kwa haraka wenye maeneo yanayotwaliwa ili kupunguza malalamiko la kupanda kwa fidia; na

(iii) Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga maeneo ya uwekezaji chini ya EPZ na SEZ lakini haijatenga fedha ya kutosha katika Bajeti ya Wizara kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo hayo, hivyo kuongeza gharama za fidia na hivyo kuwafanya wananchi wa maeneo hayo kushindwa kujiendeleza, Serikali itenge fedha za kutosha kulipa fidia kwenye maeneo haya. Kamati inatambua kuwa maeneo maalumu ya Kurasini na Bagamoyo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji hayakuwa yamefidiwa. Kamati inashauri Serikali iharakishe kuwafidia wananchi wa maeneo haya ili kuharakisha uwekezaji nchini.

C. Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TIRDO)

Mheshimiwa spika, Kamati ilitembelea taasisi ya TIRDO, inahusika na utafiti wa shughuli za Viwanda, na ina umuhimu wa mkubwa katika kipindi hiki tunapo elekea kwenye Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa spika, pamoja na umuhimu wa taasisi ya TIRDO Serikali haitoi ruzuka ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi na badala yake kuitaka taasisi kutegemea mapato yake kwa ajili ya kujiendesha. Ni maoni ya Kamati kuwa Taasisi za udhibiti zipo kwa jaili ya kutoa huduma na si kwa ajili ya kufanya biashara, hivyo basi kutaka Taasisi ijitegemee kimapato ni kukwamisha juhudi za utafiti wa Viwanda;

Mheshimiwa spika, ilidhihirika kuwa hakuna sheria yoyote inayoelekeza Viwanda kutumia huduma ya TIRDO hivyo kuifanya taasisi hii kukosa uhalali wa kufanya kazi hizo, hali hii inapelekea Viwanda kutoka nje kutumia mashirika na makampuni ya nje yanayotambulika kimataifa kufanyiwa utafiti badala ya TIRDO na kuifanya TIRDO kukosa uhalali wa kufanya kazi hizo; na

Mheshimiwa spika, Taasisi ya TIRDO inazo changamoto kubwa ya uchakavu ya maabara na vifaa vya kitaalamu vinavyotumika kufanya tafiti. Kamati imetambua mchango mkubwa wa taasisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza ruzuku kwa taasisi, ili ipate uwezo wa kutoa huduma nzuri.

D. Karakana ya Viwanda Vidogovidogo (SIDO)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi kutembelea karakana ya Viwanda Vidogo vidogo (SIDO) na kupatiwa taarifa ya maendeleo ya Viwanda vidogovidogo nchini. Majukumu ya Taasisi ni pamoja kutoa huduma za kiufundi na kiteknolojia kwa wajasiriamali ili kuweza kuendeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji; kutoa ushauri na huduma ya ugani katika nyanja za uchumi ufundi, uongozi, masoko, ubora wa bidhaa na teknolojia; kufanya utafiti na kuwashauri wajasiriamali juu ya upatikanaji wa masoko; utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali; na uanzishaji wa miradi ya viwanda vidogo vidogo vijijini kupitia mkakati wa wilaya moja bidhaa moja. Na kutekeleza mradi wa kuendeleza ujasiriamali vijijini (MUVI).

Mheshimiwa Spika, SIDO inakabiliana na Changamoto kuwa, wakati SIDO inaendelea kukua na mahitaji yameendelea kuongezeka, Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo kwenye bajeti yake kwa ajili ya taasisi hivyo hivyo kuathiri utendaji wake. Changamoto nyingine ni Sheria ya SIDO ambayo ni ya zamani imepitwa na wakati hivyo kushindwa kukidhi mahitaji katika mazingira ya sasa. Aidha, mtazamo wa wadau wengine kuhusu ujasiriamali na huduma za ugani kwa wajasiriamali zipo chini ya Halimashauri kwa ajili ya kuwaongoza wananchi wao lakini Halmashauri hazioni shughuli za SIDO kama ni sehemu ya majukumu yake. Changamoto nyingine ni kwamba wajasilimali waliofundishwa na SIDO wanao ujuzi wa kutosha lakini wameshindwa kupata mitaji kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuongeza Bajeti kwa Taasisi hii ili kuongeza tija ya huduma inayotolewa na Taasisi ya SIDO na kuhakikisha inawafikia na kuwanufaisha wajasiriamali wengi.

E. Mradi wa *Climate Change Adaptation Programme*

Mheshimiwa Spika, Mradi namba 5301 wa *Climate Change Adaptation Programme* ni mradi wa Ujenzi wa ukuta katika Ukanda wa Pwani ya dar Es Salaam, Tanga na Zanzibar kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la usawa wa bahari linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Maeneo ya mradi huu ni Ocean Road, Kigamboni, Pangani, Kisiwa Panza (Pemba) na Kilimani Unguja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea eneo la *Ocean Road* ili pamoja na mambo mengine, kujionea sehemu ya utekelezaji wa mradi huu, katika kipindi cha ziara, utekelezaji ulikuwa katika hatua za mwanzo, ambapo Upembuzi Yakunifu ulikuwa umeshafanyika, Upembuzi huo ulihusisha tathmini ya miamba, gharama za ujenzi, mchoro wa ujenzi na tenda ya kupata mkandarasi imekwishakutangazwa na mradi ulikuwa unatarajia kuanza Aprili, 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepata taarifa zisizo rasmi kuwa utekelezaji wa mradi umeanza, mradi umepata fedha za wafadhili kutoka wa *Adaptation Fund*, kwa eneo la Ocean Road mita 250 za awali zinakaribia kukamilika na maeneo mengine kama eneo la Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere na ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Bahari linalozunguka chuo hicho umeanza. Kamati inapongeza hatua iliyofikia katika mradi huu kwani utasaidia kukabiliana na kupungua kwa kina cha Bahari yetu.

F. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea mradi namba 6507 ambao ni mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi za Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC katika maeneo ya Mikocheni, Mradi huu haukutengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Lengo la Kamati kutembelea mradi huu ilikuwa ni kujionea namna utekelezaji unaweza kufanyika na kuishauri Serikali kuupatia fedha mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa NEMC inatumia Jengo dogo ambalo halitoshelezi mahitaji yao ya kuweka vitendea kazi na rasilimali watu ili kuongeza ufanisi. Eneo la mradi lina fursa kubwa ya kufanya uwekezaji wa majengo (*Real Estate*), mpango wa NEMC ni kujenga Jengo lenye urefu wa ghorofa **21**, ambapo baadhi ya ghorofa zitatumika kama Ofisi za NEMC na nyingine zitatumika kama kitega uchumi na hivyo kuliongezea mapato na kulipunguzia Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) uhitaji wa ruzuku toka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iongeze juhudi za kutekeleza mradi huu kwa kutafuta fedha za Serikali lakini pia Wafadhili na Wawekezaji ili kujenga jengo hili na kuongeza uwezo wa NEMC kutenda kazi zake za uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa ufanisi.

2.3.2 Ukaguzi wa Shughuli za Viwanda, Biashara na Uwekezaji Binafsi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea baadhi ya Viwanda binafsi ambavyo vinachakata malighafi zinazozalishwa hapa nchini, lengo likiwa kuona michango ya viwanda hivi katika uchumi wa Taifa na kubaini mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo katika utendaji wao.

A. Kiwanda cha Nguo cha URAFIKI

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea kiwanda cha *URAFIKI* ambacho ni kiwanda Ushirika kati ya Serikali ya watu wa China na Tanzania. Madhumuni ya ziara hii yalikuwa ni kujifunza na kujua ni namna gani Serikali ya Tanzania inanufaika na Ushirika huu katika kiwanda hiki. Katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa Kiwanda kimetelekezwa na Serikali ya Tanzania. Serikali haijui kitu chochote kinachoendelea katika kiwanda; jambo linalowapelekea wabia ambao ni Serikali ya watu wa China kuamua kugeuza baadhi ya majengo ya kiwanda kuwa magodauni. Kamati iligundua kuwa wabia hao wanao mpango hata wa kuligeuza eneo hilo kuwa *Business Park*. Kiwanda hiki kinazalisha chini ya kiwango hivyo kuwepo mpango wa kubadilisha matumizi ya kiwanda.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *URAFIKI* kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa wafanyakazi unaosababisha mfanyakazi mmoja kuendesha kati ya Machine moja mpaka nane. Aidha, Mishahara midogo kwa wafanyakazi, hali hii inapunguza ari yawafanyakazi kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa kwa viwanda vya ushirika kati ya Serikali na Nchi nyingine, ilikuepusha changamoto ya wabia kujiamulia mambo bila kuishirikisha Serikali, ni vema Serikali iongeze hisa katika viwanda vya namna hiyo ili kuwa na maamuzi. Mfano kiwanda cha Urafiki iongeze hisa kutoka 49 za sasa mpaka zaidi ya 50 ili kuwa na maamuzi. Aidha, kiwanda kina uwezo mkubwa wa kuzalisha na kukidhi soko la ndani na nje ni vema Serikali ikakisaidia kwa kukipatia wafanyakazi wa kutosha na umeme wa uhakika.

B. Kiwanda cha Bia TBL, Kiwanda cha Unga cha Bakheresa na Kiwanda cha Ngozi cha Saki na Kiwanda cha Mafuta cha Maunt Meru

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea viwanda tajwa na katika ziara hizo Wajumbe walibaini changamoto za kukatikakatika kwa umeme bila taarifa yoyote na kuathiri uzalishaji na hivyo kuvifanya Viwanda kushindwa kufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mara kwa mara ya Sera na Sheria za Uwekezaji, yalibainika kuaathiri sana wawekezaji na hasa kwa wawekezaji wenye mitaji mikubwa wamepata changamoto sana ya kushindwa kurudisha gharama za mradi kwa wakati kwani huchukua muda mrefu zaidi. Kwa mfano mabadiliko ya Sheria yaliyoweka ulazima wa kulipa VAT kwenye *Capital Goods* zinazolingizwa nchini kwa ajili ya uwekezaji imewafanya wawekezaji wengi waamue kwenda nyingine ambazo hazina kodi ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ugumu wa kupatikana maeneo ya Viwanda katika maeneo mengi nchini, kutokana na ukweli kwamba katika Mipango miji ya miji mingi hakuna maeneo rasmi

ambayo yametengwa kwa ajili ya Viwanda na kuwekewa miundombinu kama maji, barabara na umeme ni changamoto inayochelewesha na kuzuia uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa Kiwanda cha Ngozi cha Saki kilichopo mjini Arusha licha ya kuwa na mazingira yasiyofaa kwa wafanyakazi kilikuwa pia na Mazingira machafu. Kamati ilipendekeza kwa Serikali kufuatilia kiwanda hiki ili kuboresha mazingira ya ajira ya wafanyakazi kwa ujira wao na mazingira ya kufanyia kazi. Pia kiwanda kiweze kufuata taratibu za utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa kiwanda cha TBL ukubwa wa kodi inayotozwa katika *mault* (shayiri iliyochakatwa kwa ajili ya kutengeneza bia) inayozalishwa ndani ya nchi unaathiri sana kiwanda hiki. Kodi hii ambayo ni asilimia 30 inaifanya *mault* ya ndani ya nchi kuwa yenye gharama kubwa kuliko ile inayoingia kutoka nje. Hali hii inawakatisha tamaa wakulima wanaolima shayiri hapa nchini kwani shayiri yao inakosa soko.

C. Kiwanda cha Plastiki cha Falcon Packaging LTD

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Kiwanda cha Falcon Parking LTD cha mjini Mwanza, Kiwanda hiki kinatengeneza makasha ya EPS na Polythene yanazotumika kwa ajili ya kuhifadhi samaki wanaosafirishwa nje ya nchi. Aidha, kiwanda kinatengeneza mbao za plastiki iitwayo *greenwood*. Mbao hizi hutengenezwa kwa kutumia takataka za mifuko na chupa za plastiki. Kiwanda hiki ni rafiki wa mazingira kwa kuwa hukusanya taka za plastikina kuzichakata kupata bidhaa hii. Endapo matumizi ya *green wood* yatahamasishwa hii itapunguza kasi ya ukataji miti kwa ajili ya kutengeneza mbao za samani.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda kina changamoto ya kuwa hakitambuliki vizuri kwenye jamii na kwa Serekali pia, hali hii inapelekea kukosa soko la bidhaa zake. Uongozi wa kiwanda waliomba Kamati ya Bunge kusaidia kukitambulisha kiwanda hiki. Mradi huu ukitambulika vizuri na kupata soko la bidhaa zake, nchi inaweza kumaliza tataizo la taka za plastiki mitaani kwani malighafi hii itahitajika kwa wingi sana kwenye kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuwekeza katika miradi ya namna hii kwani ni miradi rafiki kwa mazingira, kwanza inatumia taka za plastiki zilizozagaa mitaani kutengeneza bidhaa zake na pia itapunguza tatizo la kukata miti kwa ajili ya kutengeneza mbao.

D. Viwanda vya Samaki vya Tanzania Fish Processors na Victoria Perch

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara pia katika Viwanda vya Samaki vya Tanzania Fish Processors LTD Victoria Perch vya mjini Mwanza, vinavyochakata minofu ya samaki aina ya sangara kwa ajili ya kuuza kwenye soko la Ulaya, Japani na China.

Mheshimiwa Spika, Viwanda hivi vinakabiliwa na Changamoto ya upungufu wa samaki ambao unasababishwa na uvuvi haramu uliokithiri katika Ziwa Victoria na mabadilliko ya tabianchi, jambo linalopelekea viwanda hivi kuzalisha chini ya uwezo wake. Kiwanda cha Tanzania Fish Processors kilikuwa kinazalisha tani 120 kwa siku na sasa kinazalisha tani 25 kwa siku, wakati kiwanda cha Victoria Perch kilikuwa kinazalisha tani 40 na sasa kinazalisha tani 32 kwa siku. Kukatika katika kwa Umeme tena mara kwa mara bila taarifa yoyote, kunasababisha uharibifu wa baadhi ya mitambo na kuharibu minofu ya samaki. Viwanda vya samaki vinahitaji umeme wa kutosha katika uhifadhi wa bidhaa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri viwanda hivi kuwa ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa malighafi inayosababishwa na uvuvi haramu, ni vema Viwanda hivi vikashiriki

katika miradi mbalimbali ya kuikwamua jamii inayovizunguka kichumi. Kushiriki katika miradi ya kiuchumi na jamii itaifanya jamii kuachana na suala la uvuvi usio na tija na kuvisaidia viwanda kupata malighafi ya uhakika.

2.3.3 Ukaguzi wa Shughuli za Mazingira na Uwekezaji.

A. Mgodu wa Almasi wa Mwadui na Mgodu wa Dhahabu wa Geita Gold Mine.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Migodi hii miwili (Mgodu wa Almasi wa Mwadui na Mgodu wa Dhahabu wa Geita) kwa lengo la kujionea hali ya utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi na changamoto za uwekezaji kwenye migodi hiyo.

i) Mgodu wa almasi Mwadui (WDL)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea mgodi wa Mwadui ambao wa ubia kati ya Serikali ya Tanzania (25%) na Petra Diamond (75%) kupitia kampuni ya ubia ya Williamson Diamond Limited (WDL). Kamati ilipata maelezo ya juhudi za kuuboresha mgodi huu ili uweze kupata faida na kulipa kodi ya mapato ifikapo mwaka 2019. Kwa sasa mgodi unalipa kodi nyingine zikiwemo PAYE, SDL, WHT, Service levy na zingine kwa kiwango cha dola za Marekani **Milioni 11.6** ambazo ni takribani shilingi za kitanzania **Bilioni 23.2** kwa mwaka. Mgodu wa WDL ulieleza Kamati kuwa unayochangamoto moja ya kutorejeshewa VAT na Serikali ya kiasi cha Dola za Marekani zipatazo **Milioni 12** tangu 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishuhudia hali ya utunzaji mazingira kuwa ni ya kuridhisha licha ya kuwa shughuli za migodi huathiri sana Mazingira. Mgodu huu unadhibiti vizuri taka za maji kwa kuzisafisha na kuyatumia tena maji hayo (*water recycling*). Mgodu unayo miradi ya kuhifadhi Mazingira kwa kutunza miti na pia kupanda miti. Lakini pia huwaruhusu wananchi wanaozunguka mgodi kuvuna miti hiyo kwa kukata matawi tu bila kuikata na kutumia kama nishati ya kuni. Mgodu huu pia unatoa elimu kuhusu Mazingira kwa wananchi na kuwapa miche ya kupanda kutoka kwenye vitalu vyake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipongeza Mgodu huu kwa kutoa ajira nyingi kwa watanzania, na kuitaka uongozi wa Mgodu kufanya jitihada za kuhakikisha katika nafasi ya uongozi kunakuwa na wanawake wa kutosha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kurudisha VAT kiasi cha Dola za kimarekani **Milioni 12** inayodaiwa na Mgodu huu na migodi mingine ili iweze kuongeza uwekezaji wake.

ii) Mgodu wa Dhahabu wa Geita (GGM)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ilitolewa kwa Kamati kuwa mgodi wa dhahabu wa Geita unaomilikiwa kwa asilimia 100 na kampuni ya AnglogoldAshanti ya Afrika Kusini kampuni hii pia inayo migodi mingine sita katika nchi za Afrika ikiwemo Ghana, Afrika Kusini, Mali na DRC.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa mgodi hu umewekeza kiasi cha Dola za Mazekani **Milioni 600** katika kipindi cha miaka 5. Mgodu huu unalipa Kodi ya Mapato kiashi cha Dola za Marekani **Milioni 31.3** kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Mgodu ulilipa kodi zingine kiasi cha Dola za Marekani **Milioni 53.79** kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utunzaji wa Mazingira Kamati ilijionea juhudi za Mgodu katika kutunza taka za sumu kwenye Bwawa la taka za sumu *Tailing Storage Facility* (TSF) ukifanyika vizuri. Aidha, utunzaji wa taka ngumu za mawe yasiyo na dhahabu nao ulikuwa wa kuridhisha. Kamati pia ilishuhudia utunzwaji wa Misititu unaofanyawa na mgodi wa GGM ambapo misititu

kwenye eneo lake ni mizuri sana. Kamati ilitembelea pia uchimbaji wa dhahabu chini ya ardhi (*Underground*) na kujionea changamoto za wafanyakazi chini ya Mgodu kuhusu usalama wao. Kiongozi wa chama cha wafanyakazi migodini (TAMICO) aliiomba Kamati iishauri Serikali kuruhusu wafanyakazi hao kujitoa kwenye Mfuko wa Mafao (Fao la Kujitoa) endapo wataacha kazi, kwani siyo rahisi Mfanyakazi kufanya kazi katika mazingira hayo kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea Mradi wa kuwasaidia wachimbaji wadogo (wananchi wa maeneo ya Mgodu) wa kuwapa masalia ya mawe yajulikanayo kama Magwangala na kukuta mawe hayajachukuliwa. Hali hii inakaribisha uharibifu wa mazingira iwapo mawe hayo hayatachukuliwa. Kamati ilishauri Serikali pamoja na Mgodu kuwa endapo mawe haya hayatachukuliwa ni vema mradi huo ukasitishwa na kutafuta maeneo stahiki kuwapa wachimbaji wadogo waweze kuchimba kwa faida ili kuepuka uwezekano wa uchafuzi wa mazingira kwenye eneo hilo. Uchafuzi wa mazingira unaweza kutokea kwa sababu eneo lanalowekewa "magwangala" hayo halijafanyiwa tathimini ya mazingira (*Environment Impact Assesment -EIA*) na wala kuwekewa mpango wa utunzaji mazingira (*Environment Management Plan - EMP*) ya kulitunza eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mgodu ulieleza Kamati baadhi ya changamoto inazokutana nazo ikiwa ni pamoja na uchimbaji mdogo wa dhahabu usio ruhuswa katika maeneo yaliyo kwenye leseni ya migodi hii. Uchimbaji huu pia hutumia kemikali ya mercury kuchenjua dhahabu, kemikali ambayo huishia kuchanganyika kwenye maji na kusababisha madhara kwa watumiaji wa maji hayo. Changamoto nyingine ni ukataji haramu wa Miti katika maeneo ya hifadhi ya misitu; uchomaji wa moto hovyoto katika maeneo yaliyoboreshwa na Mgodu.

B. Mradi wa Mazingira wa Ziwa Victoria

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa utunzaji wa Mazingira wa Ziwa Victoria. Mradi huu ulianzishwa ili kupunguza tatatizo ya uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya ndani yanayozunguka Ziwa Victoria. Mradi unatekelezwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya Commission ya Umoja wa Afrika Mashariki. Kwa upande wa Tanzania unatekelezwa chini ya Wizara ya Maji kwa ufadhili ya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekeleza miradi midogomidogo chini yake, miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa ukarabati wa Machinjio ya Nyama njini Mwanza; Mradi wa uzalishaji wa Mbawakavu (wadudu waharibifu wa magugumaji) kwa ajili ya utekelezaji wa magugumaji; Mradi wa ufugaji wa nyuki na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa kushirikiana na jamii inayozunguka ziwa, mradi wa uopoaji na uvunaji wa magugu maji; na mradi wa utunzaji wa kingo za mto Simiyu.

Mheshimiwa Spika, Mradi unazo changamoto kadha katika uendeshaji wake, changamoto hizo ni pamoja na mabadiliko ya Tabianchi; Kupungua kwa ubora wa maji unaosababishwa na mito inayoingiza maji ziwani kupunguza wingi wa maji badala yake kuingiza tope na mawe; Magugumaji, kupungua kwa kina cha maji; na haribifu wa mazingira unaofanywa jamii inalolizunguka ziwa.

Baada ya kupata taarifa ya Mradi na kutembelea mradi Kamati ilibaini mambo yafuatayo:

- i) Awamu ya pili ya mradi inaishia mwaka huu wa 2017 lakini utekelezaji wa mradi hauna tija kwa sababu miradi unayotekelezwa ni mingi na midogo midogo;

- ii) Mradi unatekelezwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini baadhi ya nchi hazitekelezi mradi huu kikamilifu;
- iii) Mradi huu ni wakimkakati lakini manunuzi ya vifaa vinavyotumika kutekeleza mradi huu vinatozwa kodi ya VAT wakati wa kuviingiza nchini, kiasi cha kusababisha kupanda kwa gharama za utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufuta kodi kwenye vifaa vinanyoingizwa nchini ili kutumika kwenye miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa kutunza Ziwa Viktoria unamalizika Disemba, 2017 lakini siyo endelevu kwa kuwa hautakuwa umeleta matokeo tarajiwa ya kulitunza Ziwa Viktoria. kamati inaishauri Serikali ibuni mradi mkubwa zaidi utakao shughulika pamoja na mambo mengine utunzaji wa vyanzo vya mito kagera, Mara na Simiyu ili kuhakikisha maji mengi yanayoingia ziwani ili kuongeza kina cha maji.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

3.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza awali kwenye taarifa hii, katika kipindi cha kuanzia Januari 2016 - Januari 2017 Kamati ilitekeleza Majukumu yake ya Kikanuni kwa kuzisimamia Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo, pia Kamati ilikutana na Wadau wa Sekta za Viwanda, Biashara Uwekezaji na Mazingira na kujadiliana mambo mbalimbali. Sasa naomba uniruhusu niwasilishe Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na niliombe Bunge lako Tukufu liazimie kuwa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninayo imani kwamba Maazimio haya ya Bunge kwa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati zingine yatafuatiliwa utekelezaji wake ili kuhakikisha Taifa linasonga mbele kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kamati inaona ni jambo la msingi Bunge kuwa na Kamati Maalumu ya kufuatilia maazimio haya.

3.2 WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda Biashara ya Uwekezaji na ilibaini kwamba Wizara iliandaa Mkakati wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa usiojitosheleza; kwani haukuonesha hata bajeti kwa ajili utekelezaji. Mkakati huo pia haukuonyesha namna ya kuviendeleza Viwanda hivyo. Lakini pia kasi ya utekelezaji wa Mkakati huo ni ndogo sana kwani kwa mwaka mmoja na nusu sasa imefanikiwa kutwaa kiwanda kimoja tu. Mkakati huo pia unaonesha kuwa Serikali imejikita zaidi katika kujaribu kufufua viwanda kwa kuandaa utaratibu wa kuvitwaa na kuviendesha ama kwa ubia au peke yake, badala ya kujenga mazingira bora ya uwekezaji ili kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza na kuvifufua Viwanda hivyo na hata kujenga viwanda vipya katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu. Utekelezaji wa Sera ya Viwanda nchini unaonekana kuwa ni wa kinadharia na hivyo kupelekea sekta binafsi kukosa hamasa ya kuwekeza katika uazishwaji wa Viwanda vipya.

Mheshimiwa Spika, Kwa Kuwa Tanzania inadhamiria kuwa nchi ya Viwanda ifikapo 2025 na **Kwa Kuwa** wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi ni muhimu sana kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, na **Kwa kuwa** Wawekezaji wanahitaji mazingira ya uwekezaji yanayotabirika; **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba**; Serikali iandae na kutekeleza Mkakati unaoweka mazingira rafiki ya uwekezaji nchini (*ease of doing business*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa elimu na ufundistadi ni muhimu katika ukuaji wa Viwanda, **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa** Serikali iandae utaratibu wa kuviendeleza Vyuho ambavyo vinatoa elimu ya ufundi ili kuhakikisha vinatoa elimu stahiki ili tuweze kupata wafanyakazi na wajasiriamali wenye taaluma ya Viwanda vikubwa na vidogo vidogo. Mfano kwa kushirikiana na VETA iandae mitaala ya kufundishia kwa kuzingatia na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, Kwa Kuwa Wizara haipewi fedha za kutosha na kwa wakati za kutekeleza Miradi ya Maendeleo na hasa ile ya kimkakati ambayo ikitekelezwa itahamasisha ujenzi wa Viwanda nchini. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Mchuchuma–Liganga wa kuchimba makaa ya mawe na kuzalisha umeme; na kuchimba chuma kwa ajili ya kupata chuma na kuendeleza viwanda vya chuma nchini. **Na Kwa kuwa**, Kifungu Na. 2.11.4 cha Mpango wa Taifa wa Miaka 5 wa mwaka 2016/2017 – 2010/2021 kinahimiza utekelezaji wa haraka wa Miradi wa Mchuchuma na Liganga ili kuharakisha ufufuaji wa viwanda nchini, **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-**

(i) Serikali iharakishe utekelezaji wa kutoa vuvutio kama yalivyokuwa makubalianao ya awali kwa Kampuni ya Ubia ya *Tanzania China International Mineral Resources Company Limited* (TCIMRL) ili iweze kuendelea na ujenzi wa Mgodini. Utekelezaji huu ukamilike katika Kipindi cha Bajeti tuliyonayo ya Mwaka 2016/2017;

(ii) Serikali ilipe mara moja fidia kwa wananchi wa Ludewa ili wasiendelee kulalamikia Serikali yao kwa kuwatelekeza;

(iii) TANESCO ikamilishe Mkataba wa kuuziana Umeme (PPA) na kampuni ya TCIMRL ili mradi wa kuzalisha umeme wa MW 600 uweze kuanza; na

(iv) Serikali ijenge barabara muhimu kwenda kwenye eneo la Mradi kama ilivyokuwa imeainishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2016/2017. Ujenzi huu ukamilike kwenye kipindi hiki cha Bajeti inayoishia Juni 2017.

Mheshimiwa Spika, Katika kuchambua Taarifa za Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira Kamati ilibaini kuwa Ofisi hii haikupewa fedha ya kutosha kutekeleza Miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoendelea kwani kufikia tarehe 30 Januari, 2017 Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilikuwa haijapokea kiasi chochote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka HAZINA. **Kwa Kuwa** hali hii inaathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa majukumu ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa** Serikali iipatie fedha ilizopangiwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017 ili iweze kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kwa Kuwa ni muhimu kulinda Viwanda vya ndani ili kukuza ajira ya watanzania. **Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-**

i) Viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha na vinauwezo wa kukidhi mahitaji ya soko ni vema Serikali ikatengeneza mazingira ya kuvilinda Viwanda hivyo. Aidha, manunuzi ya

umma (*Public procurement*) yatoe kipaumbele kwa viwanda vya ndani na Serikali ifanye marekebisho kwenye Sheria ya manunuzi.

ii) Viwanda vya Ubia kati ya Serikali na Nchi nyingine au kampuni ya nje, ilikuepusha changamoto ya wabia kujiamulia mambo bila kuishirikisha Serikali, ni vema Serikali iongeze hisa katika kiwanda vya namna hiyo. Mfano kiwanda cha Urafiki iongeze hisa kutoka 49 za sasa mpaka zaidi ya 50 ili kuwa na maamuzi.

3.3 TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingi zinazosimamiwa na Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira zikiwemo TBS, TEMDO, SIDO, WMA, FCC, TanTRADE, TWLB, TIC, NDC na NEMC zilikaguliwa na kusikilizwa na zina changamoto zinazofanana. Tasisi hizo hazipewi fedha za kutosha ya kuweza kujiendesha; Taasisi za Udhhibiti kama TBS na WMA na Taasisi za utafiti kama TEMDO, SIDO na TIRDO hazina maabara za kutosha na zenye ustadi na ubora unaotakiwa. Aidha Tasisi hizi hazina watumishi wa kutosha kumudu kazi za kutoa huduma kwa wateja ambao ni wawekezaji, wenye viwanda na wananchi kwa ujumla. **Kwa Kuwa** Serikali inatambua umuhimu wa Taasisi hizi katika kufufua uchumi wa nchi, **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-**

(i) Serikali ihakikishe inatoa fedha za kutosha kwa Taasisi hizi kuweza kufanya shughuli zake za udhibiti na uhamasishaji wa uwekezaji nchini;

(ii) Taasisi zinazotoa huduma za utafiti na udhibiti zipatiwe fedha za kutosha badala ya kutegemea tozo za huduma na leseni; hali inayopelekea kuongeza gharama za uendeshaji wa biashara au kiwanda na kuongeza gharama kwa mlaji pia;

(iii) Taasisi zisizoweza kujitegemea kutokana na shughuli zake kuwa za kutoa huduma siyo kufanya biashara zipewe OC kwenye mwaka wa fedha wa 2017/2018 ili ziweze kujiendesha;

(iv) Taasisi na mamlaka za udhibiti kama TBS, TIRDO, TEMDO n.k ambazo zipo kwa ajili ya kutoa huduma zisitozwe kodi ya VAT on Capital Good zinapoagiza mitambo na vifaa vya maabara ili kupunguza gharama; na

(v) Taasisi kama TBS na FCC ambazo zina jukumu kubwa katika kulinda afya ya mlaji, Serikali itoe vibali vya kuajiri watumishi mapema iwezekanavyo ili kuongeza ufanisi wa Taasisi hizi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zinazosimamia mazingira bora na rahisi ya kufanyia kazi (*ease of doing business*) kama TIC, EPZA, BRELA, Wizara na Idara za Serikali kama Uhamiaji, Ardhi, Nishati na Madini, Kilimo n.k hazina mawasiliano ya kutosha hivyo kuwepo kwa mlolongo mkubwa wa kutafuta na kupata vibali, leseni na maeneo (ardhi) ya kufanyiakazi na kujenga viwanda au migodi na hivyo mara nyingi kukatisha tamaa wawekezaji. **Kwa Kuwa** Tasisi hizi ni muhimu sana katika juhudi za kujenga viwanda na biashara kwa ujumla, **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa** TIC ikishirikiana na Mamlaka za udhibiti na Idara za Serikali zinazosimamia uwekezaji na biashara ziweke sehemu moja yenye maamuzi ya kuwapokelea wawekezaji wa ndani na nje (*One Stop Center*) ili kupunguza mlolongo wa wawekezaji kutafuta huduma kwenye Taasisi na idara nyingi za Serikali.

Mheshimia Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga maeneo ya uwekezaji chini ya EPZ na SEZ lakini haitengi fedha ya kutosha katika Bajeti ya Wizara kwa ajili ya kulipa fidia kwa

maeneo hayo. Hivyo kufuatia kusuasua kwa ulipaji wa fidia katika maeneo hayo deni limeendelea kupanda kutoka **Bilioni 60** katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 hadi kufikia **Bilioni 191** Mwaka wa Fedha 2015/2016 Kamati ilipotembelea mradi huu. Hivyo basi **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa** Serikali katika Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 itenge fedha ya kutosha kwa ajili ya kulipa deni hili lote.

3.4 MIKUTANO NA WADAU WA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa shughuli za Kamati za kukutana na kushauriana na Wadau wa Viwanda Biashara na Uwekezaji ulibaini pamoja na mambo mengine mambo yafuatayo:-

(i) Serikali kwa ujumla imefunga milango ya mashauriano na Wadau. Wadau (wawekezaji wenye Viwanda, Migodi na Wafanyabiashara) wa ndani na nje wamekata tamaa kwa sababu Serikali katika shughuli zake za usimamizi inawasumbua sana na kuwaona kana kwamba ni wakwepa kodi na hivyo wezi wa rasilimali ya Taifa. Hali hii imesababisha wawekezaji wengi kuchagua nchi zingine kwenda kuwekeza na kusababisha kupungua kwa kasi ya uwekezaji nchini;

(ii) Wawekezaji hasa wa Sekta ya uzinduaji (*Extractive Industry*) wanayo hofu kubwa juu ya Serikali kuwafutia vibali na leseni kwenye miradi ambayo wamekwisha kamilisha Upembuzi Yakiniifu kwa kuwekeza fedha nyingi. Hali hii inaifanya nchi ipoteze taswira yake mbele ya wawekezaji (*attractiveness*);

(iii) Mabadiliko ya mara kwa mara ya vivutio na kodi (*Unpredictability*) kwa wawekezaji, wafanyabiashara, wenye viwanda na wenye migodi, unaifanya nchi isitabirike katika uwekezaji. Kwa mfano mabadiliko ya Ushuru wa Forodha yaliyowekwa katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kulazimisha watafutaji wa mafuta, gesi na madini kulipa kodi ya mapato ya asilimia 30% wakati hawajaanza kuzalisha na kupata faida; na kuwekwa kwa VAT kwenye *Capital Goods* mabadiliko haya yamekatisha tamaa wawekezaji waliopo nchini kuendelea kuwekeza (*reinvest*) na wale waliotaka kuja wameamua kutokuja kabisa; na

(iv) Uwepo wa wingi wa kodi na tozo zinachelewesha ufufuaji wa viwanda na uanzishwaji wa viwanda vipya.

Mheshimiwa Spika, Kwa Kuwa Tanzania imeazimia kuwa nchi ya Viwanda na **Kwa Kuwa** wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi ni muhimili mmojawapo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, na **Kwa Kuwa** Wawekezaji wanahitaji mazingira mazuri ya uwekezaji, **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu** liazimie kuwa:

(i) Serikali ifungue milango ya mawasiliano kati yake na wadau wake mbalimbali kwa kuweka utaratibu wa kukutana na wadau hao mara kwa mara wa ndani na nje ya Nchi. Aidha, watoa huduma wawapokee wadau wenye viwanda, wafanyabiashara na wawekezaji mbalimbali kwa upole kama wadau wa maendeleo badala ya kuwaona kama maadui na wahalifu;

(ii) Katika utekelezaji wake wa kusimamia ujenzi wa uchumi na kuhudumia wananchi wake ili kujenga uchumi wao binafsi, Serikali izingatie Sheria zilizopo kwenye sekta mbalimbali; na

(iii) Serikali izipitie upya tozo na kodi zinazosababisha mazingira ya uwekezaji yasiyotabirika (*Unpredictable*). Tozo na kodi hizo ni: VAT kwenye mitambo ya uwekezaji yani

(VAT on Capital Goods); VAT kwenye huduma za mizigo nayopita yani (VAT on auxiliary services on transit goods) na tozo zingine zilizoainishwa kwenye taarifa hii.

3.5 ZIARA ZA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Kamati iliweza kutembelea, kukagua na kuchambua miradi ya maendeleo inayoismamia ipatayo minne tu ikiwa ni Mradi wa Kufufua Kiwanda cha General Tyre cha Arusha; Mradi wa Viuadudu wa Kibaha; Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ufukwe wa Bahari ya Dar es Salaam; na Mradi wa EPZ wa Benjamin William Mkapa wa Ubungo. Kamati iligundua na kuainisha kuwa Mradi wa maendeleo wa kufufua Kiwanda cha Matiri cha *General Tyre* ulikuwa haujapatiwa fedha ya kuutekeleza, japokuwa Serikali ilieleza kuwa imeunda Timu ya Wataalamu kuchambua na kupata mwelekeo mpya wa kufufua kiwanda hiki lakini mradi haujatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa ni azma ya Serikali kufufua viwanda vilivyobinafishwa na kufa, na **Kwa kuwa** Mradi wa Kiwanda cha General Tyre ni miongoni mwa Viwanda muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi, **Bunge lako Tukufu liazimie kuwa** Serikali itekeleze Mradi huu kwa haraka sana, taarifa ya tathmini ya wataalamu iwasilishwe kwenye Kamati katika kipindi cha wiki mbili kama ilivyo ahidi kuwasilisha kwenye Bunge hili na hatua zichukwe ipasavyo.

3.6 ZIARA KUTEMBELEA VIWANDA BINAFSI.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Viwanda binafsi mbalimbali kuona mafanikio na changamoto zinazokabiliana navyo ili kuzalisha bidhaa na kulinda ajira ya wataanzania. Viwanda hivi vinatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini na kuuza mazao yaliyoongezwa thamani hapa ndani au nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Viwanda hivi vina changamoto na mapungufu yanayofanana zikiwemo: uhaba wa Umeme wa kutosha na wakuaminika; gharama kubwa ya malighafi ya kiwanda kiasi cha kulazimika kuagiza kutoka nje; na baadhi ya Viwanda kukosa soko la ndani na Viwanda na Migodi kuwa na ajira za wafanyakazi wenye ujira mdogo na mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la kukuza Viwanda vya ndani ili kuongeza kazi ya ukuaji wa uchumi ikiwa ni pamoja na kulinda ajira za wananchi ni la msingi sana, **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-**

- i) Serikali iimarisha miundombinu ya umeme, maji na barabara ili kuvipa Viwanda viweze kuzalisha bidhaa kwa gharama nafuu;
- ii) Serikali ihakikishe inalinda bidhaa zinazozalishwa na Viwanda vya ndani ya nchi kwa kuweka Kodi kwenye Bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi au kupiga marufuku uingizaji wa wa bidhaa zinazo zalishwa na kutosheleza soko hapa nchini;
- iii) Serikali iimarisha taaluma mbalimbali kwa kuanzisha a kuendeleza mafunzo ya taaluma na stadi kwa Viwanda hivyo ili kukidhi soko la rasilimali watu nchini; na
- iv) Serikali isimamie ajira na haki za wafanyakazi viwandani ili kulinda haki za wafanyakazi kwani mazingira yao ya kazi ni duni na hatarishi kwa maisha yao.

3.7 UTENDAJI NA UFANISI WA BANDARI YA DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Bandari ya Dar es Salaam pia na kukukata na Wadau wa Bandari, TRA na TPA na kushuhudia shughuli za huduma Badarini hapo. Kamati

pamoja na kushuhudia kupungua kwa shughuli Bandarini iliezwa na TPA na TRA kwamba kupungua shehena Bandari ya Dar es Salaam kulitokana na mdodoro wa uchumi uliyoiathiri nchi ya China na Dunia; kuwepo kwa uchaguzi wa nchini Zambia na kupungua kwa uchimbaji wa madini ya shaba nchini DRC.

Aidha, kwa upande wa wadau wao, waliieleza kamati kuwa hali hiyo imesababishwa pia na kupandishwa kwa ghafla kwa tozo za huduma na bidhaa bandarini; kuanzishwa kwa kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma zinazotolewa katika mizigo au bidhaa inayopitia bandari hiyo kwenda nchi za jirani (*VAT on auxiliary services on transit goods*) za DRC, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda; Uganda; na kuanza kutumika kwa utaratibu wa Himaya moja ya Ushuru wa Forodha (*Single Custom Territory - SCT*), kati ya DRC na Tanzania wakati nchi zingine za Afrika Mashariki hazitumii mfumo huo na kusababisha huduma za utoaji wa mizigo Bandari ya Dar es salaam kupanda ukilinganisha na Bandari ya Mombasa; na TPA na TRA (Serikali) kufunga milango ya mashauriano na wadau wake.

Mheshimiwa Spika, **Kwa Kuwa** Bandari ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Taifa lolote, na **kwa kuwa** Serikali imeazimia kufufua uchumi wa Taifa la Tanzania ni muhimu kuikua Bandari ili itoe huduma bora zaidi. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudi zake za kufufua tena shughuli za Bandari ya Dar Es Salaam kwa kufanya mashauriano na Wadau (wafanyabiashara) wa nchi za Kongo na Zambia wakiwemo Weheshimiwa Marais wa Nchi hizo. Hii imefanya Bandari ya Dar Es Salaam ianze kufanya vizuri tena. **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu** liazimie kuwa:-

(i) Serikali iendeleo kufungua milango ya mawasiliano na mashauriano kati yake na wadau wake mbalimbali (wafanyabiashara na watumiaji wa Bandari ya Dar es Salaam na wawekezaji wengine) wa ndani ya nchi, kwa kuwa ni wadau wa maendeleo; badala ya kuwaona kuwa wote ni wakwepa kodi na wezi;

(ii) Serikali iangalie upya madhara ya kutozwa kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma zinazotolewa katika mizigo au bidhaa inayopitia bandari hiyo kwenda nchi za jirani (*VAT on auxiliary services on transit goods*) za Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda na Uganda. Hususan ni tafsiri iliyojengeka kwa wenye mizigo na bidhaa ambao ni za watu wa nje kuwa wanatozwa kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa au mizigo yao kinyume na sheria za kimataifa kwa vile wanaolipa kodi hiyo ni wao wageni na wala siyo watoa huduma. Kama kuna ukweli kwenye suala hilo basi tufanye marekebisho ya sheria mwaka wa Fedha 2017/18 baada ya kupata chanzo kingine cha mapato;

(iii) Serikali izishawishi nchi zingine hususa ni Jamuhuri ya Kenya yenye Bandari shindani ya Mombasa ianze kutumia utaratibu wa Himaya Moja ya Ushuru wa Forodha (*Single Custom Territory - SCT*), ili kuondoa hisia zilizojengeka kuwa; kutumika kwa Mfumo wa SCT kwa Tanzania tu kunaongeza gharama kwa watumiaji wa wanaopitisha mizigo kwenye Bandari ya Dar es Salaam ukilinganisha na Mombasa ambako mfumo huo haujaanza kutumika;

(iv) Ili kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam na kupunguza kero za Mamlaka za Udhhibiti ni vema Serikali ikaweka Mamlaka moja ambayo itafanya ukaguzi wote. Aidha, kodi za matumizi ya Bandari ziunganishwe na kuwe na mamlaka moja ambayo itazikusanya kwani fedha zote zinaingia katika mfuko moja; na

(v) Serikali ichambue upya faida na hasara ya tozo na kodi nyingine zilizoongezeka kwenye huduma na Bandari ya Dar es Salaam na kufanya marekebisho kama yatahitajika.

3.8 UHIFADHI NA UTUNZANJI WA MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Viwanda, na shughuli za uhifadhi wa mazingira na kupokea taarifa za shughuli hizo lakini pia ilichambua hali halisi ya shughuli hizo na Kamati ilibaini kuwa jamii haina uelewa wa kutosha juu ya athari ya uharibifu wa mazingira jambo ninalowapelekea kuharibu mazingira bila kujali. Aidha, matumizi ya mkaa ni makubwa sana na ndiyo chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, migodi na viwanda vingi nchini havitunzi mazingira iipasavyo; lakini pia Miradi mingi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira haitekelezwi kwa weledi na kwa wakati; na Mradi wa Ziwa Viktoria unamalizika Disemba, 2017 lakini siyo endelevu kwa kuwa hautakuwa umelefa matokeo tarajiwa ya kulitunza Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua mipango ya Serikali ya kuwasaidia wachimbaji wadogo (wananchi wa maeneo ya Mgodi) kwa kuwapa masalia ya mawe yajulikanayo kama Magwangala. Lakini wachimbaji hawa hawayachukui mawe haya baada ya kugundua kuwa hayana dhahabu jambo linalopelekea kukaribisha uharibifu wa mazingira katika eneo yalipowekwa. Uchafuzi wa mazingira unaweza kutokea kwa sababu eneo lanalowekeka "magwangala" hayo halijafanyiwa tathimini ya mazingira *Environment Impact Assesment* (EIA) na wala halina *Environment Management Plan* (EMP) ya kulitunza eneo hilo. Kamati ilishauri Serikali pamoja na Mgodi kutafuta maeneo stahiki na kuwapa wachimbaji wadogo waweze kuchimba kwa faida ili kuepuka uwezekano wa uchafuzi wa mazingira kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali pia haijatambua umuhimu wa kutekeleza miradi ya uhifadhi wa mazingira kwani hata bajeti inayotengwa kwa ajili ya miradi ya mazingira haitoshi na fedha hazipelekwi kwa wakati. Kwa Mfano Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira mpaka kufikia tarehe 30 Januari, 2017 ilikuwa hajiapokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa mazingira ni suala mtambuka na linahusisha uhai; na **Kwa Kuwa** mipango mingi inayopangwa kutekelezwa hivi sasa kama Ujenzi wa Viwanda na kukuza kilimo utekelezaji wake unategemea sana uhifadhi wa mazingira; **Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu** liazimie kwamba:

(i) Serikali iongeze juhudi za uhifadhi na utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuelekeza kodi na tozo za mazingira kwenye Mfuko wa Mazingira Nchini ulioanzishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2016/2017 ili kupata fedha za kutosha kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira nchini;

(ii) kutekeleza Mkakati wa Utunzaji wa Mazingira Nchini kwa kuanzisha miradi ya utunzaji Visiki Hai na upandaji miti nchini na Mradi wa Utunzaji wa Ziwa Victoria utakapomalizika Desemba 2017 uhuishwe upya ili ushughulikie pamoja na mambo mengine utunzaji wa vyanzo vya mito Kagera, Mara na Simiyu ili kuhakikisha maji mengi yanayoingia ziwani na kuongeza kina cha maji;

(iii) Serikali ibuni na itekeleze kwa umahili na weledi Miradi ya kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni pamoja na Mradi namba 5301 wa *Climate Change Adaptation Programme* wa Ujenzi wa ukuta katika Ukanda wa Pwani ya Dar Es Salaam, Tanga na Zanzibar kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la usawa wa bahari linalosababishwa na Mabadiliko ya Tabianchi;

(iv) Serikali ikutane na wadau wa plastiki na kufanya mazungumzo ili kupata muafaka wa namna ya kusitisha utengenezaji wa bidhaa za plastiki bila kuathiri ajira na

uwekezaji uliofanyika. Namna bora inaweza kuwa ni kutoa muda wa kutosha kwa wadau kubadilisha teknolojia au kubadili biashara;

(v) Ofisi ya Makamu wa Raisi-Mazingira katika kutekeleza miradi yake ya upandaji miti izingatie maeneo ambayo yameathirika na ukame kwa kiwango kikubwa na Serikali iweke vivutio kwa viwanda vinavyo tumia taka za plastiki katika kutengeneza bidhaa mbalimbali. Mfano kiwanda cha Falcon Packaging LTD kilichopo mjini Mwanza; na

(vi) Serikali isimamie kikamilifu uvunaji wa rasilimali ya misitu kama chanzo cha Mapato ya nchi na wananchi kwa uendelevu na pia kutafuta vyanzo vya Nishati mbadala yenye gharama nafuu kama Jotoardhi (*Geothermal*), Nuruja (*Solar*) n.k ili kupunguza matumizi ya mkaa.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa uongozi wako na kuisaidia Kamati kutekeleza Majukumu yake. Na pia nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa ushirikiano wao Mawaziri wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rai-Mazingira Mhe. January Makamba na Naibu wake Mhe. Luhaga Mpina. Nawashukuru pia Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kasilillah, kwa ushirikiano ambao amekuwa akitoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati, Ndg. Wilfred Magova na Ndg. Zainab Mkamba pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Dkt. Dalaly Peter Kafumu, (Mb)

MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA
8 FEBRUARI, 2017

MWENYEKITI: Tunaendelea na hoja inayofuata, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Karibu Mwenyekiti.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa mwaka 2016 na kuliomba Bunge lako Tukufu kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa sababu ya muda nitasoma baadhi ya maeneo ya taarifa hii, hivyo naomba taarifa yote ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo sitayasoma yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni Kamati mpya katika Bunge la Kumi na Moja. Katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017 Kamati imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji na utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa. Kamati inaamini ni kutokana na kutambua umuhimu wa uwekezaji katika maendeleo ya Taifa ndiyo maana Mheshimiwa Spika, aliamua kuanzisha Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inayo majukumu yafuatayo:-

Moja, kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa Umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na sheria na miongozo mujarabu ya biashara;

Pili, kuchambua na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa;

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongozwa na Kanuni za Kudumu za Bunge katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati pia imefanya kazi zake kwa kuzingatia miongozo mingine kama ifuatavyo:-

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;
- Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004;
- Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001;
- Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370; na
- Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka mmoja, yaani Januari, 2016 na Januari, 2017, Kamati imetekeleza majukumu yake kwa njia ya semina. Kamati imeshirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kuratibu mafunzo mbalimbali kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo Wajumbe katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni Kujadili Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu Uwekezaji na Utendaji wa Mashirika ya Umma. Kati ya Mashirika 264 yaliyo chini ya Msajili wa Hazina, hadi tarehe 30 Juni, 2016, Kamati imepitia utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma 41. Orodha ya Taasisi na Mashirika hayo 264 imeambatanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika kipindi cha Januari, 2017, Kamati ilifanya Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji iliyotekelezwa katika Mashirika ya Umma katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ili kuiwezesha Kamati kujiridhisha na ufanisi wa uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma na matokeo yake. Taarifa ya Msajili wa Hazina ambayo ndio msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati inaonesha kwamba, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 Serikali ilifanya uwekezaji wenye jumla ya shilingi trilioni 22.35 katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Aidha, faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji huo, kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2016, kwa njia ya kukusanya mapato yasiyo ya kodi (*non-tax revenue*), jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 204.64 ziliweza kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imewekeza pia katika Kampuni mbalimbali ndani ya nchi kwa ubia na wawekezaji kutoka sekta binafsi. Thamani ya Uwekezaji huo ni jumla ya thamani ya shilingi bilioni 558.85. Aidha, Serikali imepata faida kutokana na uwekezaji huo kwa njia ya gawio na mauzo ya hisa yenye jumla ya shilingi bilioni 218.33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hicho cha gawio kimepatikana kutoka mashirika ya kibiashara na makampuni 13 kati ya mashirika na makampuni 64 yaliyopaswa kutoa gawio kwa Serikali. Orodha kamili ya mchanganuo wa mashirika na makampuni hayo imeambatishwa kwenye vitabu vilivyogawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa zilizokaguliwa za mwaka 2015, Serikali imewekeza kiasi cha shilingi bilioni 471 katika Taasisi tisa zilizo nje ya nchi. Katika uwekezaji uliofanywa na Serikali katika taasisi za nje, Serikali imepata faida kwa njia ya gawio ya kiasi cha shilingi milioni 183.37.

Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mwenendo wa uwekezaji kwa kipindi cha miaka mitano ya nyuma, mwaka 2011/2012 – 2015/2016. Mwaka 2011/2012 uwekezaji ulikuwa wa thamani ya shilingi trilioni 12.21 na mwaka 2015/2016 uwekezaji umefikia thamani ya shilingi trilioni 23. Mwenendo huo unaonekana katika Jedwali Na. 1 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2016 naomba thamani ya uwekezaji isomeke shilingi trilioni 12.21 badala ya shilingi trilioni 14.03 kama ilivyoonekana katika taarifa ya Kamati. Kamati imefanya uchambuzi wa kina na taarifa ziliwasilishwa na Taasisi na Mashirika ya Umma ili kubaini tija ya uwekezaji. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni sura ya mitaji. Kamati imechambua mizania ya Mashirika ya Umma mbalimbali ili kubaini sura ya mitaji katika uwekezaji. Katika mashirika yaliyofanyiwa uchunguzi, baadhi ya mashirika yamebainika kuwa na tatizo la uwiano usio mzuri kati ya mtaji wa ndani na mtaji wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika mengi ya Umma yamekosa uwezo wa kulipa madeni yake ya muda mrefu na muda mfupi kutokana na kutoongezeka kwa mitaji yake (*equity growth*) na hivyo malengo ya taasisi kutofikiwa. Aidha, taasisi kutokuwa na uwezo wa kulipa madeni yake kunaleta viashiria vya hatari kwani zinaweza kushtakiwa na wadeni wake pamoja na kufilisiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa Taasisi ya Umma yenye madeni mengi kupita mtaji ni Kampuni ya Mbolea Tanzania (*TFC*). Kamati imebaini kuwa, Kampuni hii imekuwa ikipata hasara mwaka hadi mwaka kutokana na kupungua kwa mapato ilihali matumizi yamekuwa yakiongezeka. Hali hii imesababisha mtaji wa Kampuni wa shilingi bilioni 17.9 kuisha na kuisababishia kuwa na nakisi (*negative equity*) ya shilingi bilioni 12.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi umeonesha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu, madeni ya kampuni yameongezeka kwa asilimia 6.6 kutoka shilingi bilioni 33.9 mwaka 2013 hadi shilingi bilioni 36 mwaka 2015. Tafsiri ya takwimu hizi ni kuwa *TFC* imekuwa mzigo mkubwa kwa umma kwa kiwango cha thamani yake na kuzidi. Thamani ya mali za kampuni hiyo ni shilingi bilioni 23.8 na madeni ni shilingi bilioni 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma; katika uchambuzi wake Kamati ilibaini uwepo wa baadhi ya taasisi zenye mikataba mibovu inayohusu uwekezaji ambayo imekuwa ikiisababishia Serikali pamoja na taasisi hizo hasara kubwa. Mikataba hiyo hailinufaishi Taifa letu na badala yake inawanufaisha wawekezaji ambao wanatumia rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Kamati, baadhi ya mashirika yalibainika kuingia mikataba ya uwekezaji ambayo haina tija kwa Taifa yakiwemo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shirika la Ugavi la *TANESCO* na Shirika la Simu la *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuingia kwenye uchambuzi, nafikiri uchambuzi uko pale, nawaomba mpitie Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la tathmini ya uwekezaji katika ardhi na Soko la Hisa, Kamati imebaini kuwa, Taasisi nyingi za Umma zimeingia katika uwekezaji wa majengo na makazi ya kibiashara ambao unatumia fedha nyingi, huku mapato yanayopatikana (*return on investment*) ni kidogo jambo linalosababisha kuchukua kipindi kirefu kurudisha gharama (*payback period*). Hali hii imesababisha taasisi hizo kutopata faida inayostahili ikilinganishwa na uwekezaji uliofanyika, gharama na muda uliotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine, uwekezaji mwingine ambao Kamati imebaini hauna tija, uliofanywa na Mfuko wa *GEPF*, kwa kununua hisa katika Kampuni ya *NICOL*; *GEPF* ilinunua hisa za Kampuni ya *NICOL* katika Soko la Hisa Dar es Salaam zenye thamani ya shilingi milioni 600. Baadaye kampuni hii iliondolewa kwenye orodha ya makampuni yaliyosajiliwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa kutotimiza baadhi ya masharti ya usajili. Hali hii imesababisha mfuko kushindwa kurejesha fedha zilizowekezwa katika Kampuni ya *NICOL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwiano kati ya uwezo wa kulipa madeni na mali zilizopo; Kamati ilipitia na kuichambua Taarifa ya Utendaji wa Taasisi za Umma ambapo ilibaini kuwa mashirika yamekuwa na uwezo mdogo wa kulipa madeni kutokana na taasisi hizo kupata hasara kwa miaka mingi mfululizo na kusababisha mtaji wote wa taasisi kuliwa na madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la kifedha limejitokea pia katika Shirika la Taifa la *NDC* ambapo, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya 2015 inaonesha kuwa madeni ya muda mfupi (*current liability*) yanazidi mali ya muda mfupi (*current asset*) kwa shilingi bilioni 30.2 ambapo uwiano kati ya madeni na mali ya muda mfupi (*current ratio*) upo chini 0.20:1 ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika ambacho ni 2:1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nafasi ya Bodi za Wakurugenzi katika Utawala kwenye Uwekezaji wa Mitaji ya Umma; baada ya kujadili na kuchambua Taarifa ya Msajili wa Hazina, baadhi ya mashirika yalibainika kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi pamoja na Bodi za Wadhamini. Kukosekana kwa bodi hizo kumeathiri utendaji na utekelezaji wa shughuli za taasisi hizo, kwani bodi ndizo zenye dhamana ya kufanya maamuzi mbalimbali kwa ajili ya utendaji na uendeshaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kukosekana kwa bodi kumesababisha Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu kuchelewa kuthibitishwa katika nyadhifa zao jambo linaloathiri baadhi ya maamuzi ambayo yanahitaji watu wenye mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa maamuzi ya bodi kumeathiri utendaji wa baadhi ya mashirika pamoja na kusababisha hasara. Mfano, kutokuwa na bodi kumeisababishia Serikali kukosa shilingi bilioni 10 kwa mwaka kama tozo kutoka kwenye Sekta ya Hoteli za Kitalii zilizojengwa ndani ya Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ilitoa hukumu tarehe 12 Septemba, 2014 chini ya Jaji S. E. Mugasha wa Mahakama ya Kanda ya Kaskazini Arusha kuwa, wawekezaji wote walio ndani ya hifadhi walipe tozo na kuipa mamlaka Bodi kupanga kiwango cha tozo ili zianze kulipwa. Hata hivyo, TANAPA mpaka inawasilisha taarifa kwenye Kamati tarehe 12 Aprili, 2016, Bodi ya TANAPA ilikuwa haijaundwa na hivyo kuwafanya wawekezaji hao waendeleo kunufaika kwa kutolipa tozo na Serikali kuendelea kukosa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Kibiashara; Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura Na. 370 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebisha mwaka 2010, inaipa majukumu Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia uwekezaji unaofanywa na Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni yote ambayo Serikali ina hisa. Hata hivyo, Sheria hii haigusi Mifuko ya Hifadhi za Jamii, ambayo kimsingi ni Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzingatiaji wa Sera ya Taasisi kuhusu Uwekezaji; kwa kuwa Sera ya Uwekezaji ya Taasisi ndiyo inayotoa mwongozo wa aina ya kiwango cha uwekezaji unaoweza kufanyika katika Taasisi za Umma. Kamati inataka kujiridhisha kuhusu uwepo wa sera hiyo kwa kila taasisi na namna inavyozingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha kuwa, kati ya taasisi 41 zilizowasilisha taarifa zake kwa ajili ya uchambuzi wa Kamati, taasisi 15 tu ndizo zenye Sera ya Uwekezaji. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 36.6 ya sampuli ya mashirika na taasisi zilizofanyiwa kazi na Kamati. Hali hii inahatarisha uwezo wa taasisi kufanya uwekezaji wenye tija na wenye manufaa kwa Taifa na kinyume na utaratibu bora wa uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la uendeshaji na utendaji wa Taasisi zinazofanya uwekezaji uliangalia maeneo mbalimbali. Moja, tuliangalia uhusiano kati ya matumizi na uwekezaji. Taasisi nyingi zimekuwa zikitumia fedha nyingi katika matumizi ya kawaida ikilinganishwa na mapato. Mfano, Taasisi ya NSSF katika kipindi cha mwaka 2015/2016, ilitumia shilingi bilioni 113.47 ikiwa ni 17.8% ya michango ya wanachama kwa mwaka kwa ajili ya kukimu kugharamia gharama za kiutawala na uendeshaji. Gharama hizi ni kubwa ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 10 inayopendekezwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano mingine Waheshimiwa Wajumbe, mtapitia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa, Taasisi nyingi za Umma zimekuwa zikijiendesha kwa hasara kwa muda mrefu na kushindwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mifano ya Taasisi hizo ni Kampuni ya Mbolea, Kampuni ya Magazeti, Shirika la Madini la Taifa, kama ilivyo kwenye ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika utendaji wa majukumu yake, imekumbana na changamoto kadhaa ambazo kwa kiasi fulani zimeathiri utendaji wa Kamati. Baadhi ya

changamoto hizo ni muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya Kamati kupitia Taarifa za Mashirika na Taasisi za Umma; Wajumbe kutopata semina iliyoweza kuwashibisha mpaka kuweza kuelewa mashirika ya ndani na nje; na muda mchache wa ziara na kutopatikana kwa nyaraka za kisheria za Mashirika na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye mapendekezo ya Kamati. Kwa kuzingatia uchambuzi kuhusiana na uwekezaji wa mitaji ya umma, Kamati inapenda kutoa maoni ya jumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ambayo inatokana na uwekezaji wa mitaji ya umma bado ni ndogo ikilinganishwa na kiasi kilichowekezwa. Hadi tarehe 30 Juni, 2016 Serikali ilikuwa imewekeza mitaji yenye thamani ya shilingi trilioni 23, lakini faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji huo kwa mwaka 2015/2016 ilikuwa ni bilioni 422 tu, ambayo ni asilimia 1.83. Kamati inatambua dhamira njema ya Serikali kwamba, sehemu ya uwekezaji uliofanyika inalenga kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado Kamati inaamini kwamba, iwapo uwekezaji huo utatekelezwa kwa ufanisi, unaweza kuleta faida zaidi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali na kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maoni ya Kamati kutokana na uchambuzi na uwekezaji wa mitaji ya umma, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba ya Uwekezaji Isiyo na Tija:-

KWA KUWA imebainika kuwa, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekumbwa na tatizo la uendeshaji kutokana na mikataba isiyofaa, mibovu na isiyo na tija, kwa Taifa.

NA KWA KUWA, hali hiyo imeongeza mzigo kwa Serikali na kusababisha matumizi ya rasilimali za umma kwenye uwekezaji huo kutokuwa na tija.

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa:-

(i) Serikali isimamie mapitio ya vipengele vyote vyenye utata na visivyo na manufaa kwa Taifa ili virekebishwe muda wa kupitia upya Mikataba hiyo utakapowadia;

(ii) Serikali iwekeze katika utafiti na kuwajengea uwezo (*Capacity Building*) Wataalam wa Taasisi zake kuhusiana na mikataba na upembuzi yakinifu ili waweze kusimamia kikamilifu miradi ambayo taasisi hizo zinaingia na wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Faida inayopatikana kutoka katika Uwekezaji:-

KWA KUWA, Serikali inapata faida kidogo kutoka katika taasisi na Mashirika ya Umma kutokana na taasisi hizo kujiendesha kwa lengo la kutoa huduma na faida ya kutosha kutoka katika makampuni ambayo yana hisa chache yanayojiendesha kibiashara;

NA KWA KUWA, hali hiyo ya Mashirika mengi ya Umma kujiendesha kwa lengo la kutoa huduma inasababisha Serikali kukosa gawio na mchango mdogo katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa:-

- (i) Serikali iangalie namna bora ya kuboresha utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ambapo kuna uwekezaji wa Serikali.
- (ii) Serikali iondokane na dhana ya kutoa huduma pekee kwa taasisi zake na badala yake ziweze kujiendesha kibiashara ili ziweze kupata faida na kutoa gawio pamoja na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.
- (iii) Serikali iongeze uwekezaji katika Makampuni ambayo yanazalisha faida kubwa ili Serikali ipate gawio kubwa.

KWA KUWA, kukosekana kwa Bodi za Wakurugenzi; licha ya umuhimu wa Bodi za Wakurugenzi katika usimamizi na uamuzi wa kimkakati kwenye uwekezaji, zipo Taasisi na Mashirika ya Umma yasiyokuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa muda mrefu.

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa:-

Serikali ihakikishe kwamba zoezi la uteuzi wa Bodi hizo ufanyike kwa haraka na umakini ili kuongeza ufanisi katika Taasisi na Mashirika yanayofanya uwekezaji wa mitaji ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Bodi uzingatie sifa na weledi kwa Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi pamoja na kufuata ushauri wa Msajili wa Hazina kwa kuwa ndiye msimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali.

KWA KUWA, mgongano wa kisheria; Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, inaelekezwa na Sheria zilizoanzisha mifuko hiyo kuwasilisha Taarifa za uwekezaji na utendaji wa mashirika kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Benki Kuu ya Tanzania jambo ambalo haliendani na masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, inayotaka taasisi zote za umma kuwasilisha Taarifa zake za uwekezaji na utendaji;

NA KWA KUWA, mgongano huo wa kisheria, unasababisha Msajili wa Hazina ashindwe kufuatilia ipasavyo utendaji na uwekezaji unaofanywa na mifuko hiyo;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali iangalie uwezekano wa kuzifanyia marekebisho Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ili ziweze kumtambua Msajili wa Hazina (TR) kama Msimamizi Mkuu wa Taasisi za Umma ambazo Serikali ina hisa. *(Makofi)*

KWA KUWA, uzalishaji wa umeme kwa gharama za juu; imebainika kuwa kampuni ya uzalishaji umeme ya IPTL na AGGREKO yanaendesha mitambo yake kwa kutumia mafuta jambo linalosababisha umeme unaozalishwa kuuzwa kwa bei kubwa ikilinganishwa na vyanzo vingine kama maji na gesi;

NA KWA KUWA, TANESCO inalazimika kugharamia umeme huo, hivyo kuwa na gharama kubwa za uendeshaji jambo linalosababisha hasara;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali iangalie njia bora ya kuliwezesha Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO) kuongeza umeme kwa kutumia vyanzo vingine vya nishati kama vile Gesi asilia, Upepo, Jotoaridhi, Jua, Makaa ya Mawe, na kadhalika. (Makofi)

KWA KUWA, uwekezaji katika Bodi ya Mazao kutokana na faida ya wakulima; licha ya dhamira nzuri ya kuwekeza kwenye bodi nyingi za mazao, hakuna faida inayopatikana kutokana na uwekezaji huo na wakulima hawawezeshwi kupata kwa wakati pembejeo bora, kwa bei nafuu na masoko ya uhakika kwa mazao yao;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa faida itokanayo na uwekezaji kwenye bodi nyingi za mazao ni kinyume na matarajio ya azma ya kuanzisha bodi hizo ambazo ni nyingi kwa idadi;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali iangalie upya muundo na malengo ya kuanzishwa kwa bodi za mazao ili uwekezaji katika bodi hizo uwe na faida pamoja na kuchangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao.

KWA KUWA, uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na Shirika la Nyumba; Jukumu la msingi la Shirika la Nyumba la Taifa ni kuwekeza katika majengo kwa lengo la kuboresha hali ya makazi nchini na kupata faida kulingana na hali ya soko bila kuathiri azma ya kuboresha makazi kwa wananchi,

NA KWA KUWA, utekelezaji wa jukumu hilo, umefanyika kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba ambapo Shirika hilo limegharamia miundombinu iliyopaswa kugharamiwa na taasisi nyingine za umma, jambo linalopandisha gharama za nyumba hizo na kusababisha bei yake kuwa kubwa ikilinganisha na uwezo wa Watanzania wa kawaida katika soko;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali ihakikishe kuwa kabla ya Shirika la Nyumba kufanya uwekezaji wake, taasisi mbalimbali zinazohusika na ujenzi wa miundombinu zitekeleze ipasavyo majukumu yake. Taasisi zinazofanya uwekezaji ziwe na Sera ya Uwekezaji ya taasisi. (Makofi)

KWA KUWA, Sera ya Uwekezaji ya Taasisi ndiyo inayotoa mwongozo wa aina na kiwango cha uwekezaji unaoweza kufanyika katika Taasisi za Umma, lakini uchambuzi umeonesha kuwepo kwa taasisi na mashirika mengi yanayofanya uwekezaji bila kuwa na sera ya uwekezaji;

NA KWA KUWA, ukosefu wa sera ya uwekezaji kwa taasisi na mashirika yanayowekeza una hatari ya kukosa ufanisi, tija na faida kwa taasisi na Serikali;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali izitake Taasisi zote zinazowekeza kwa kutumia mitaji ya umma, ziwe na Sera ya Uwekezaji wa Taasisi. (Makofi)

Bado dakika ngapi?

MWENYEKITI: Tano.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Tano, sawa.

KWA KUWA, utoaji wa mitaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma; Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa na changamoto ya kutokuwa na mitaji ya kutosha (*undercapitalized*);

NA KWA KUWA, kukosekana kwa mitaji hiyo kumekosesha Taasisi na Mashirika hayo ya Umma kushindwa kujiendesha vyema na kushindwa kulipa gawio kwa Serikali;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali iweke mitaji ya kutosha katika Taasisi za Umma, kama Benki ya Wanawake, Twiga Bancorp, TIB, TPB, TADB na mashirika mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwekezaji katika Mto Ruvu:

KWA KUWA, imebainika kuwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kwa ununuzi wa mitambo iliyopo Ruvu juu unakabiliwa na hatari ya kutorejsha fedha kutokana na uwezekano wa kuzimwa kwa mitambo utakaosababishwa na kukosekana kwa maji;

NA KWA KUWA, hali hiyo itasababisha mitambo iliyonunuliwa kwa fedha nyingi za umma kutofanya kazi na kuwa hasara kwa Serikali;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali iandae mikakati madhubuti utakaosaidia kupatikana kwa njia mbadala kama vile utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili kuifanya mitambo hiyo ifanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu makini uliowezesha Kamati na taarifa hii kufika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Profesa Oswald Mashindano kwa kuteuliwa kuwa Msajili wa Hazina na kwa ushirikiano wake alioutoa kwa Kamati toka kuteuliwa kwake. Aidha, napenda kumshukuru Ndugu Lawrence Mafuru aliyekuwa Msajili wa Hazina pamoja na wafanyakazi wote wa ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano waliouonesha kwa wakati wote na kwa muda mfupi tulioupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kasilillah na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge ndugu Athumani na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael pamoja na makatibu wa Kamati Amina Salum na Suzan Ngole, pamoja na msaidizi wao Elias Kyando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashukuru watumishi kutoka katika Ofisi ya Mshauri wa Mambo wa Kisheria wa Bunge ndugu Serafine Tamba, ndugu Everlyn Shibandiko na ndugu Stephan Mbutu pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii imefafanua matokeo ya uchambuzi kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, maoni ya Kamati na Mapendekezo yaliyotokana na matokeo ya uchambuzi, kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na kuijadili ikiwa na Maoni na Mapendekezo ili hatimaye Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante Mwenyekiti wa Kamati kwa wasilisho lako.

TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa mwaka 2016 na kuliomba Bunge lako tukufu kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni Kamati mpya katika Bunge la Kumi na Moja. Katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017 Kamati imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji na utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa. Kamati ina amini ni kutokana na kutambua umuhimu wa uwekezaji katika maendeleo ya Taifa ndiyo maana Mheshimiwa Spika, aliamua kuanzisha Kamati hii. Mtazamo huu unashabihiana kabisa na mtazamo wa Rais wa Rwanda, Paulo Kagame, ambaye anaamini biashara na uwekezaji ndiyo nguzo za maendeleo, na siyo kutegemea misaada.

Katika kitabu chake kiitwacho **Grappling with Change in Africa “The Dream of Prosperity using African Wisdoms”** Mwandishi Emmanuel Danstan Chinumba, ananukuu maneno yafuatayo kutoka kwa Rais wa Rwanda, Paul Kagame; **“In Africa today, we recognise that trade and investment, and not aid, are pillars of development”**.

Kwa tafsiri isiyo rasmi anachosema Mwandishi hapa ni kwamba, **“Leo katika Afrika tunatambua kwamba, biashara na uwekezaji, ndizo nguzo za maendeleo, na siyo misaada”**

Majukumu ya kikanuni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 12 Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ina majukumu yafuatayo:-

- i) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na Sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na
- ii) Kuchambua na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongozwa na Kanuni za Kudumu za Bunge katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati pia imefanya kazi zake kwa kuzingatia miongozo mingine kama ifuatavyo:-

- i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;
- ii) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004,
- iii) Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001,
- iv) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370 na;
- v) Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992.

Shughuli zilizotekelezwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja yaani Januari, 2016 /Januari, 2017, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao kwa kujadili Taarifa za Msajili wa Hazina na kupata semina mbalimbali zinazohusu Uwekezaji. Pamoja na ukaguzi wa miradi ya uwekezaji katika Mashirika mbalimbali ya Umma ili kujiridhisha juu ya Uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Mashirika hayo.

Semina za Mafunzo

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikishirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuratibu Mafunzo mbalimbali kwa dhumuni la kuwajengea uwezo wajumbe katika kutekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yalihusu mambo yafuatayo:-

- i) Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa lengo la kupata uelewa kuhusu dhima ya Msajili wa Hazina katika uangalizi (*Custodianship*) wa Uwekezaji unaofanywa na Serikali,
- ii) Usimamizi wa uendeshaji wa Mashirika na Taasisi zinazofanya uwekezaji,
- iii) Muundo na majukumu ya Kamati,
- iv) Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa shughuli za Kamati na,
- v) Uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Mashirika ya Umma.

Kujadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu Uwekezaji na Utendaji wa Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, Kati ya Mashirika 264 yaliyochini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina hadi tarehe 30 Juni, 2016, Kamati ilipitia Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma Arobaini na Moja (41). Orodha ya Taasisi na Mashirika hayo 264 imeambatishwa¹.

¹ Kiambatisho Na. 01: Orodha ya Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyochini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina hadi tarehe 30 Juni, 2016

Mheshimiwa Spika, Mashirika na Taasisi Arobaini zilizowasilisha Taarifa zake mbele ya Kamati ni zifuatazo:

- 1) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT)
- 2) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)
- 3) Mfuko Wa Pensheni Kwa Watumishi Wa Serikali Za Mitaa (LAPF)
- 4) Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)
- 5) Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Mashirika ya Umma (PPF)
- 6) Mfuko wa Pensheni wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)
- 7) Mfuko wa Pensheni wa Wastaafu wa GEFP
- 8) Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO)
- 9) Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC)
- 10) Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
- 11) Wakala wa Umeme Vijijini (REA)
- 12) Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)
- 13) Bodi ya Pamba
- 14) Bodi ya Korosho
- 15) Bodi ya Kahawa
- 16) Bodi ya Tumbaku
- 17) Bodi ya Sukari
- 18) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)
- 19) Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL)
- 20) Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)
- 21) Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)
- 22) Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA)
- 23) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA)
- 24) Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)
- 25) Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC)
- 26) Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA)
- 27) Shirika la Reli Tanzania (TRL)
- 28) Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB)
- 29) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)
- 30) Kampuni ya Huduma ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASCO)
- 31) Kampuni Hodhi ya Mali za Serikali (RAHCO)
- 32) Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC)
- 33) Shirika la Bima la Taifa (NIC)
- 34) Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC)
- 35) Benki ya Posta Tanzania (TPB)
- 36) Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)
- 37) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji na Huduma kwa Wawekezaji (UTT - AMIS)
- 38) Kampuni ya kuibua na kutekeleza miradi (UTT - PID)
- 39) Kampuni kwa ajili ya utoaji mikopo midogo midogo (UTT –Microfinance Public Ltd co)
- 40) Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)
- 41) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Ziara za ukaguzi wa Miradi ya uwekezaji

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2017 Kamati ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji inayotekelezwa na Mashirika ya Umma katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ili kuiwezesha kamati kujiridhisha na ufanisi wa uwekezaji.

Miradi iliyotembelewa ni hii ifuatayo.

- i) Mradi wa Ujenzi wa Terminal III katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere unaosimamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA);
- ii) Miradi ya Ujenzi wa Nyumba za kisasa inayosimamiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC);
- iii) Miradi ya Majengo Pacha na Nyumba za gharama nafuu inayosimamiwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF);
- iv) Miradi ya Maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini inayosimamiwa na Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO); na
- v) Mradi wa Kiwanda cha kutengeneza Dawa ya kuuu viluilui vinavyozalisha mbu na Mradi wa kuendeleza eneo la viwanda TAMCO Kibaha inayosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC).

Muhtasari wa matokeo ya Uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua uwekezaji wa mitaji ya umma kwa lengo la kubaini iwapo uwekezaji huo una tija na iwapo umezingatia, Sheria na miongozo mujarabu ya biashara. Na matokeo ya uchambuzi yameonesha haya yafuatavyo:-

- i) Yapo baadhi ya Mashirika ya umma yanayofanya uwekezaji wa mitaji ya umma bila kuzingatia sheria, taratibu na miongozo mujarabu ya biashara;
- ii) Baadhi ya mashirika yanayowekeza yamekosa uwezo wa kulipa madeni kutokana na kutoongezeka kwa mitaji yake;
- iii) Uwekezaji wa mitaji ya umma katika baadhi ya mashirika na taasisi umeshindwa kuwa na tija kutokana na mikataba isiyoridhisha;
- iv) Baadhi ya taasisi zimewekeza kwa namna isiyokuwa na ufanisi,
- v) Msajili wa Hazina kutokupata hesabu zilizokaguliwa za mashirika na taasisi zinazofanya uwekezaji kutokana na kukosekana kwa bodi,
- vi) Kutofungamana kwa Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370 na Sheria zilizoanzisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, na
- vii) Baadhi ya taasisi zinazowekeza kuwa na gharama za uendeshaji zinazozidi ukomo uliowekwa kwa mujibu wa sheria na miongozo mingine ya uwekezaji.

Maoni ya jumla kuhusu matokeo ya uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya uchambuzi wa mitaji ya umma, maoni ya jumla ya kamati ni kwamba:-

- i) Mikataba mibovu na isiyo na tija kwa Taifa, imechangia kuwepo kwa matatizo ya kiuendeshaji katika baadhi ya Mashirika ya Umma na kuiongezea mzigo serikali,
- ii) Kutokana na Taasisi na Mashirika mengi ya umma kujiendesha kwa lengo la kutoa huduma pekee, Serikali inakosa gawio kutoka taasisi hizo,
- iii) Kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi, kukaimiwa kwa nafasi za juu kulipelekea kuathiri uendeshaji na uwekezaji.
- iv) Mgongano kati ya Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370 na Sheria zilizoanzisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, unasababisha Msajili wa Hazina kukosa nguvu ya kuisimamia na kufuatilia uwekezaji unaofanywa na Mifuko hiyo. Hali hii inatokana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutowasilisha Taarifa zake za Uwekezaji na Utendaji kwa Msajili wa Hazina kwa kuwa Sheria zilizoanzisha Mifuko hiyo inaelekeza Taarifa hizo ziwasilishwe kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Benki Kuu ya Tanzania.
- v) Hasara inayopatikana katika Shirika la Ugavi la Umeme (TANESCO) inachangiwa na gharama kubwa za umeme unaonunuliwa kutoka Makampuni ya uzalishaji umeme ya IPTL na AGGREKO yanayoendesha mitambo yake kwa kutumia mafuta.

- vi) Kukosekana kwa faida itokanayo na uwekezaji kwenye bodi nyingi za mazao ni kinyume na matarajio ya azma ya kuanzisha bodi hizo ambazo ni nyingi kwa idadi. Kwa mfano, uwekezaji katika bodi hizo hausaidii kuwawezesha wakulima kupata kwa wakati, pembejeo bora kwa bei nafuu na masoko ya uhakika kwa mazao yao.
- vii) Utekelezaji wa Jukumu la msingi la Shirika la Nyumba la Taifa kwa kuwekeza ujenzi wa nyumba na kugharamia miundombinu iliyopaswa kugharamiwa na taasisi nyingine za umma, umechangia kuongeza gharama za nyumba hizo na kusababisha bei yake kuwa kubwa ikilinganisha na uwezo wa Watanzania wa kawaida katika soko.
- viii) Ukosefu wa Sera ya Uwekezaji kwa taasisi na mashirika yanayowekeza unaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi, tija na faida kwa taasisi na Serikali.
- ix) Kukosekana kwa mitaji ya kutosha kwa ajili ya Taasisi na Mashirika ya Umma kumechangia Taasisi na Mashirika hayo ya Umma kushindwa kujiendesha vyema na kutokutoa gawio kwa Serikali.
- x) Ukiukaji wa Mikataba uliofanywa na Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni 51 kati ya 64 kwa kutokutoa gawio kwa Serikali katika Mwaka wa Fedha ulioishia 30 Juni, 2016 sio tu kwamba unavunja Mikataba lakini pia unapunguza mapato kwa Serikali na kuongeza hasara katika uwekezaji ambao Serikali imefanya. Ni maoni ya Kamati kwamba jambo hili litazamwe kwa kina.
- xi) Kwa Taasisi nyingi za Umma kutozingatia masharti ya *Sheria ya Msajili wa Hazina* (Sura 370), inayozitaka kutokuwa na Gharama za Uendeshaji zinazozidi asilimia 60 ya Mapato Ghafi (*Gross Revenue*), ni kinyume na utaratibu bora wa uwekezaji wa mitaji ya umma na pia inaathiri kiwango cha fedha kinachoweza kutumika kutoa gawio serikalini.
- xii) Hatari inayoukabili uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kwa ununuzi wa mitambo iliyopo Ruvu juu, kutokana na uwezekano wa kuzimwa kwa mitambo utakaosababishwa na kukosekana kwa maji, inahitaji kukabiliwa ili kunusuru dhamira ya ununuzi wa mitambo hiyo.
- xiii) Utendaji usio ridhisha kwa Taasisi nyingi za Umma umechangia Taasisi hizo kujiendesha kwa hasara na kuiongezea Serikali mzigo kwa kuwa na utegemezi mkubwa, jambo linalopaswa kufanyiwa kazi ili kuboresha hali hiyo.

SEHEMU YA PILI

UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA NA MATOKEO YAKE

Maelezo ya jumla kuhusu uwekezaji

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni jukumu la msingi la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC). Jukumu hilo linatokana na dhamira ya Bunge la kumi na moja kujipanga kwa ajili ya kutekeleza dhana ya Usimamizi wa Kibunge katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*Parliamentary Oversight over Public Investment*).

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Msajili wa Hazina ambayo ndio msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati inaonesha kwamba, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 Serikali ilifanya uwekezaji wenye jumla ya **Shilingi Tirion 22.50** katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Taasisi na Mashirika hayo ni yale ambayo Serikali ina umiliki wa kuanzia asilimia 51 mpaka 100. Aidha, Faida iliyopatikana kutokana na Uwekezaji huo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia 30 Juni, 2016 ni kwa njia ya kukusanya mapato yasiyo ya kodi (non-tax revenue). Jumla ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 204.64** zilikusanywa kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

- i) Gawio (Dividends) – **Shilingi Bilioni 80.86**
- ii) Mchango wa asilimia 15 ya Mapato ghafi **Shilingi Bilioni 105.37**
- iii) Mapato kutoka kwenye Mfumo wa Kusimamia na Kuratibu Mawasiliano ya Simu Nchini (TCRA- TTMS) **Shilingi Bilioni 18.41**

Mheshimiwa Spika, Serikali imewekeza pia katika Kampuni mbalimbali ndani ya nchi kwa ubia na wawekezaji kutoka sekta binafsi ambapo umiliki wake ni asilimia 50 au chini ya asilimia 50. Thamani ya uwekezaji huo ni **Shilingi Bilioni 558.85**

Aidha, Serikali imepata faida kutokana na uwekezaji huo kwa njia ya gawio na mauzo ya hisa yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 218.33** kwa Mwaka wa Fedha ulioishia 30 Juni, 2016. Mchanganuo wa mapato kutoka kwenye makampuni hayo ni kama ifuatavyo;

- i) Gawio (Dividends) – Shilingi Bilioni 38.34
- ii) Mauzo ya Hisa za Kampuni ya Sigara (TCC) – Shilingi Bilioni 4.26
- iii) Mauzo ya Hisa za Kampuni ya Bia (TBL) – Shilingi Bilioni 175.73

Mheshimiwa Spika, Kiasi hicho cha Gawio (*Dividends*) kimepatikana kutoka mashirika ya kibiashara na makampuni 13 kati ya Mashirika na Makampuni 64 yaliyopaswa kutoa gawio kwa serikali. Orodha kamili ya mchanganuo wa mashirika na makampuni hayo imeambatishwa.²

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa zilizokaguliwa za mwaka 2015, Serikali imewekeza kiasi cha **Shilingi Bilioni 471.09** katika Taasisi Tisa zilizo nje ya nchi. Katika Uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Taasisi za nje, Serikali ilipata faida kwa njia ya gawio ya kiasi cha **Shilingi Milioni 183.37** kutoka katika Kampuni ya African Re-Insurance Corporation pekee katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016.

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 Msajili wa Hazina alikuwa amepokea Taarifa za Uwekezaji kutoka katika Taasisi Mia Mbili Arobaini na Tatu (243), kati ya Mia Mbili Sifini na Nne (264) zilizopo.

Kati ya Taasisi 243 zilizowasilisha Taarifa zake, 180 zinatoa huduma kama vile Elimu, Afya, Kilimo, Maji, Mifugo, Utafiti na Hifadhi ya Jamii. Kati ya Taasisi hizi 180 ni 10 tu (Mamlaka za Udhubiti) ndizo zinazochangia Asilimia 15 ya mapato ghafi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Aidha, Taasisi 21 zilizosalia ambazo bado hazijaingizwa kwenye Taarifa ya uwekezaji ya Msajili wa Hazina ni mpya na hesabu hazijakaguliwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza dhima ya ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mwenendo wa uwekezaji kwa kipindi cha miaka mitano ya nyuma, 2011/2012 hadi 2015/2016. Mwaka 2011/2012 Uwekezaji ulikuwa wa thamani ya **Shilingi Tirioni 14.03** na mwaka 2015/2016 uwekezaji ulifikia thamani ya **Shilingi Tirioni 23.06** Mwenendo huo unaonekana katika Jedwali Na. 01.

² Kiambatisho Na. 02: Orodha ya Mashirika na Makampuni ya Kibishara yanayopaswa kutoa Gawio.


Jedwali Na. 01: Mwenendo wa Uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa

**Chanzo:
Taarifa
ya TR
2015/2
016**

MWAKA	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
Idadi ya taasisi	213	215	215	216	243
Uwekezaji (bilioni)	12,215.1	14,031.5	17,320.6	20,238.4	23,062.7
Ongezeko la Mtaji kwa asilimia	17.9	14.9	23.4	16.1	13.9
Faida iliyopatikana	208,132,532,126	61,552,740,840	100,596,208,942	161,038,578,686	422,968,027,083.68
Faida kwa asilimia	1.70	0.44	0.58	0.80	1.83
Makisio ya michango katika Mfuko Mkuu wa Serikali	303,437,179,586	156,545,404,000	195,154,240,025	185,259,413,830	237,440,513,207

Mheshimiwa Spika, Jedwali la hapo juu linaonesha tofauti kubwa kati ya makisio na makusanyo. Sababu ya tofauti hizo ni kutokana na ufanisi mdogo katika utendaji wa Taasisi, mabadiliko ya Sheria na hasara katika baadhi ya makampuni ambayo Serikali imewezeza. Aidha mwenendo wa ukuaji wa uwekezaji wa mitaji pamoja na faida iliyopatikana umeoneshwa katika Mchoro Namba 1

Mchoro(Bar Graph) Na 01: Ongezeko la thamani ya uwekezaji ikilinganishwa na Faida kwa Mwaka 2011/12 hadi 2015/16



Chanzo: Jedwali no 1

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2010/11 hadi 2015/16 Uwekezaji wa Serikali ulikuwa ukiongezeka. Sababu za ongezeko la uwekezaji ni pamoja na:-

- i) Sehemu kubwa ya mashirika ya umma yamewasilisha hesabu zilizokaguliwa zinazotoa sura ya thamani halisi ya hisa na mitaji kwa sasa
- ii) Kuongezeka kwa hisa za baadhi ya taasisi za kibiashara na mitaji ya baadhi ya taasisi zisizo za kibiashara
- iii) Ongezeko kubwa la fedha za hisa linalitokana na tathmini mpya ya hisa na mtaji.

Mheshimiwa Spika, Hadi Tarehe 30 Juni, 2016, Serikali ilikuwa imewekeza katika Mashirika, Taasisi za Umma na Makampuni 243 kwa mchanganuo wa umilikii wa Hisa za Serikali kama ifuatavyo:


Jedwali Na. 02: Mchanganuo wa umiliki wa hisa za Serikali katika Mashirika, Taasisi na Makampuni 243 ambayo yamewasilisha Hesabu zake kwa TR

Kiasi cha umiliki kwa asilimia (%)	Idadi ya Taasisi
Asilimia 100	202
Asilimia 50 na zaidi	4
Asilimia 50	4
Asilimia 49 au pungufu	33
Jumla	243

Chanzo: Taarifa ya TR 2015/2016

Picha halisi ya mchanganuo uliopo kwenye Jedwali Na. 02 inaonekana katika kupitia Chati Duara Na. 01 ya Taarifa hii.

Chati Na. 01: Picha halisi ya Mchanganuo wa umiliki wa Hisa za Serikali katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni.



Uchambuzi wa Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Taarifa zilizowasilishwa za Taasisi na Mashirika ya umma ili kubaini tija ya uwekezaji. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitumia njia mbalimbali zifuatazo:-

- i) Kupitia Taarifa za Uwekezaji na Utendaji wa Mashirika na Taasisi za umma zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya umma.
- ii) Kupitia sheria zilizoanzisha Mashirika na Taasisi za Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji umezingatia taratibu, sheria na miongozo mujarabu ya biashara;
- iii) Kupokea na kujadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu Uchambuzi wa Utendaji na Uwekezaji wa Mashirika na Taasisi za Umma. Lengo ni kupokea maoni ya Msimamizi wa Mashirika na Taasisi zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya umma;
- iv) Kufanya mahojiano na Wenyeviti wa Bodi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifuatilia uwekezaji, kwa kufanya uchambuzi wa mambo yafuatayo:-

- i) Sura ya Mitaji katika uwekezaji,
- ii) Mfumo wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma,
- iii) Tathmini ya Uwekezaji katika Ardhi na Soko la Hisa
- iv) Uwiano kati ya uwezo wa kulipa madeni na mali zilizopo,
- v) Nafasi ya Bodi za Wakurugenzi katika Utawala kwenye uwekezaji wa Mitaji ya Umma,
- vi) Uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kibiashara,
- vii) Uzingatiaji wa Sera ya Taasisi kuhusu Uwekezaji
- viii) Uendeshaji na utendaji wa Taasisi zinazofanya uwekezaji wa Mitaji ya Umma nchini,
- ix) Masuala mengine ya msisitizo kuhusu uwekezaji wa Mitaji ya Umma, na
- x) Changamoto za Ujumla.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

Sura ya Mitaji katika Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua mizania ya Mashirika ya Umma mbalimbali ili kubaini sura ya mitaji katika uwekezaji. katika Mashirika yaliyofanyiwa uchambuzi, baadhi ya Mashirika yalibainika kuwa na tatizo la uwiano usio mzuri kati ya Mtaji wa ndani na mtaji toka nje.

Mheshimiwa Spika, Mashirika mengi ya Umma yamekosa uwezo wa kulipa madeni yake ya muda mrefu na muda mfupi kutokana na kutoongezeka kwa mitaji yake (equity growth) na hivyo malengo ya Taasisi kutofikiwa. Aidha, Taasisi kutokuwa na uwezo wa kulipa madeni yake kunaleta viashiria vya hatari kwani zinaweza kushitakiwa na wadeni wake pamoja na kufilisiwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uwiano usio mzuri katika Taasisi za Umma zinazofanya uwekezaji kwani Taasisi nyingi hazina ubunifu na zimekuwa zikitegemea kuwezeshwa na Serikali pasipo kutegemea mikopo kutoka taasisi za kifedha kwa ajili ya uendeshaji wa Taasisi na kurejesha mikopo hiyo. Hali hii imefanya Mashirika ya Umma kubweteka na kushindwa kuwajibika ipasavyo (accountability).

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Mashirika ya Umma yalichukua mikopo mikubwa na kufanya uwiano wa madeni na mali kuwa mbaya ikilinganishwa na kiwango cha uendeshaji (Debt Equity Ratio Standards) kisichoziwa wastani wa 0.5 – 2. Hali hiyo imesababisha madeni hayo kulipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa Taasisi ya Umma yenye madeni mengi kupita mtaji ni Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC). Kamati imebaini kuwa, Kampuni hii imekuwa ikipata hasara mwaka hadi mwaka kutokana na kupungua kwa mapato ilihali matumizi yamekuwa yakiongezeka. Hali hii imesababisha mtaji wa Kampuni wa **Shilingi Bilioni 17.9** kuisha na kuisababishia kuwa na nakisi (negative equity) ya **Shilingi Bilioni 12.3**.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, katika kipindi cha miaka mitatu, madeni ya Kampuni yameongezeka kwa asilimia 6.6 kutoka **Shilingi Bilioni 33.9** (Mwaka 2013) hadi **Shilingi Bilioni 36** (Mwaka 2015). Tafsiri ya takwimu hizo ni kuwa, ili kulipa madeni yote ya Kamapuni hiyo fedha zinazohitajika ni sawa na thamani ya mali yote ya Kampuni ikiongezwa zaidi ya nusu ya thamani ya mali. Kwa maneno mengine, TFC imekuwa mzigo mkubwa kwa umma kwa kiwango cha thamani yake na kuzidi. Thamani ya mali za Kampuni hiyo ni **Shilingi Bilioni 23.8** na madeni ni **Shilingi Bilioni 36**.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya Mbolea imekuwa ikitumia mikopo zaidi kwa ajili ya kujiendesha. Kwa mfano, TFC ilichukua Mkopo wa **Shilingi Bilioni 17** kutoka Benki za CRDB, na mkopo wa **Shilingi Bilioni 20** kutoka Benki ya ABC pamoja na *bank overdraft facilities* ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 5** kutoka benki ya Exim.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, mnamo Tarehe 19 Disemba, 2011, Kikao cha Baraza la Mawaziri kiliridhia kuwa madeni ya Benki za CRDB na ABC yanayofikia **Shilingi Bilioni 44.43** ambayo Kampuni ya Mbolea inadaiwa, yalipwe na Serikali. Hata hivyo, urejeshaji wa mikopo hiyo umekuwa ni wa kusuasua na Serikali

ilikuwa imelipa kwa kiasi kidogo jambo linalosababisha kuongezeka kwa gharama za mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Matatizo mengine yaliyosababisha kuwa na sura mbaya ya mtaji katika Mashirika na Taasisi za Umma ni pamoja na Miradi ya muda mrefu kama vile miradi ya ujenzi wa nyumba kufadhiliwa na madeni ya muda mfupi, kukosa uwezo wa kulipa gawio kwa Serikali pamoja na kushindwa kulipa kodi.

Aidha, Mashirika mengi ya Umma hayafanyi uchambuzi mahususi (financing analysis appraisal) kwa lengo la kuweka kigezo cha sura ya mtaji wa Taasisi husika ili kuweka uwiano mzuri. Hali hiyo inasababisha kuweka Mkakati wa kuangalia kiwango cha juu cha ongezeko la faida (Marginal Profit) ikilinganishwa na kiwango cha ongezeko la gharama (Marginal cost).

Mfumo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili Taarifa ya Msajili wa Hazina (*The Treasury Statement*) inayobainisha kwa kina Uwekezaji wa Serikali, Dhamana za Serikali, Mikopo ya Serikali na Mapato yatokanayo na Uwekezaji husika.

Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini uwepo wa baadhi ya Taasisi zenye mikataba mibovu inayohusu uwekezaji ambayo imekuwa ikiisababishia Serikali pamoja na Taasisi hizo hasara kubwa. Mikataba hiyo hailinufaishi taifa letu na badala yake inawanufaisha Wawekezaji ambao wanatumia rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Kamati, baadhi ya Mashirika yalibainika kuingia mikataba ya uwekezaji ambayo haina tija kwa Taifa yakiwemo, Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Shirika la Ugavi la Umeme (TANESCO) na Kampuni ya Simu za Mkononi Tanzania (TTCL).

Mheshimiwa Spika, Chuo kikuu cha Dar es salaam kiliingia mkataba na Kampuni ya Mlimani GH kutoka Botswana kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa eneo la biashara la Mlimani City. Katika Mkataba huo, Chuo kimetoa ardhi yake kwa mwekezaji kwa mkataba wa miaka hamsini (50) ambapo Chuo kinapata asilimia kumi tu (10%) ya mapato yanayotokana na uwekezaji uliofanyika. Mradi huu umewekwa katika mfumo wa B.O.T (Build, Operate and Transfer). Mfumo huu ni aina ya mpangilio ambapo, sekta binafsi inajenga miundombinu ya mradi, inaifanyia kazi (operates) na baadae kuhamisha umiliki wa mradi Serikalini.

Kamati inaona kuwa kipindi cha Mkataba ni kirefu sana na hakuna uhakika juu ya thamani halisi ya uwekezaji na ubora wa majengo hayo wakati mkataba utakapomalizika na mradi kukabidhiwa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mkataba mwingine ni baina ya Shirika la Ugavi wa Umeme Tanesco na Makampuni ya uzalishaji umeme ya IPTL na AGGREKO. Makampuni haya yanaendesha mitambo yake kwa kutumia mafuta mazito hivyo kusababisha umeme unaozalishwa kuwa ghali sana ikilinganishwa na vyanzo vingine kama vya maji na gesi. Mikataba hii haina tija kwakuwa inafanya gharama za umeme unaopelekwa TANESCO kuwa wa gharama ya juu.

Ingawa Wawekezaji hawa hawakuja na Mtaji bado Serikali iliingia nao mkataba na kuwalipa Capacity Charge, hata pale ambapo hawazalishi umeme na kutozingatia

kigezo cha kulipa *capacity charge* kinachohitaji mwekezaji alipwe anapokuja na mtaji. Kupitia Mkataba huo, Serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa kwa kila mwezi kwa kuwalipa makampuni ya AGGREKO na IPTL kama gharama za *capacity charges*.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) ilikuwa katika mgogoro na Kampuni ya Bharti Airtel, kutokana na kutopata malipo yoyote tangu ilipoingia mkataba na Kampuni hiyo. Mkataba huo ambao haukuinufaisha TTCL kwa namna yoyote ile, ulianza Februari 23, 2001, mara baada ya Serikali kuibinafsisha Kampuni hiyo kwa Kampuni ya MSI ya Uholanzi.

Uwiano wa umiliki wa hisa kati ya Serikali na Mbia mwenza ulikuwa ni asilimia 65 kwa asilimia 35 sawia. Umiliki wa Mbia mwenza ulibadilika mara nne kutoka MSI/Derecon kwenda Celtel, kutoka Celtel kwenda Zain, na kutoka Zain kwenda Bharti Airtel Tanzania B.V.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imechukua jukumu la kumaliza mgogoro uliopo TTCL kwa kumlipa mbia hisa zake na hivyo, TTCL kwa sasa inamilikiwa na Serikali kwa Asilimia 100. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua. Ni mategemeo ya Kamati kuwa, TTCL itaimarika na kuleta tija zaidi kwa ustawi wa uchumi wa nchi na maendeleo kwa ujumla.

Tathmini ya Uwekezaji katika Ardhi na Soko la Hisa

Mheshimiwa Spika, katika kujadili na kuchambua Taarifa ya Msajili wa Hazina, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Taasisi ambazo Serikali ina hisa zimeshindwa kutoa gawio Serikalini kama Sheria inavyohitaji. Kutokana na hali hii, Serikali imekuwa ikikosa mapato ambayo yangesaidia katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na utoaji wa Huduma kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Katika eneo hili Kamati imebaini kuwa, Taasisi nyingi za Umma zimeingia katika uwekezaji wa majengo ya makazi na kibiashara ambao unatumia fedha nyingi, huku mapato yanayopatikana (*return on investment*) ni kidogo jambo linalosababisha kuchukua kipindi kirefu kurudisha gharama (*payback period*). Hali hii imesababisha Taasisi hizo kutopata faida inayostahiki ikilinganishwa na Uwekezaji uliofanyika, gharama na muda uliotumika.

Aidha, Taasisi nyingi zimekuwa zikiwekeza katika eneo moja na kumlenga mteja mmoja hivyo kusababisha majengo mengi kukosa wapangaji. Mfano wa taasisi hizo ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya PPF, PSPF, NSSF, LAPF na GEPF ambayo imekuwa ikitumia michango ya Wanachama wao katika uwekezaji huo. Hali hii inahatarisha usalama wa fedha za Wanachama wao pindi zitakapohitajika kwa wahusika na kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pia imewekeza katika ununuzi wa Ardhi katika maeneo mbalimbali kwa gharama kubwa sana ambapo maeneo hayo yangeweza kununuziwa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa mahali viwanja vilipo na gharama za ununuzi wake ni kama ifuatavyo:-

NAKALA YA MTANDAO- (ONLINE DOCUMENT)

S/N	MFUKO		MAHALI KIWANJA KILIPO	BEI YA KUNUNULIA	UKUBWA WA KIWANJA(MITA ZA MRABA)	BEI YA MITA YA MRABA
1	PPF	a)	Ubungo Kinondoni	362,617,508.25	3,598	100,783.07
2	GEFF	a)	Ilemela -Mwanza	2,000,000,000.00	8,191	244,170.43
		b)	Raha Leo - Mtwara	225,000,000.00	1,428	157,563.02
		c)	Raha Leo - Mtwara	225,000,000.00	1,424	158,005.61
3	NSSF	a)	Tazara -Dar es Salaam	4,242,000,000.00	8,825	480,679.88
		b)	Kunduchi -Dar es Salaam	1,595,000,000.00	4,888	326,309.32
		c)	Kunduchi -Dar es Salaam	3,727,000,000.00	25,036	148,865.63
		d)	Bahari Ufukwe wa barabara ya Bagamoyo - Mbuyuni -Dar es Salaam	1,600,000,000.00	5,553	288,132.54
4	PSPF	a)	City Centre - Arusha	2,000,000,000.00	3,901	512,689.05
		b)	Ibadakuli - Shinyanga	65,603,640.00	150	437,357.60
		c)	Usule - Tabora	84,000,000.00	210	400,000.00
5	LAPF	a)	Sisimba - Mbeya Mc	401,000,000.00	2,383	168,275.28

S/N	MFUKO		MAHALI KIWANJA KILIPO	BEI YA KUNUNULIA	UKUBWA WA KIWANJA(MITA ZA MRABA)	BEI YA MITA YA MRABA
		b)	Sisimba - Mbeya Mc	380,000,000.00	1,977	192,210.42
		c)	Nunge Beach - Bagamoyo	4,053,562,500.00	34,240	118,386.76
		d)	Ngarenaro - Arusha	1,800,000,000.00	2,414	745,650.37

Chanzo cha Taarifa: Taarifa ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji mwingine ambao Kamati imebaini hauna tija ni uliofanywa na Mfuko wa Mafao ya Kustaafu wa GEPF, kwa kununua hisa katika Kampuni ya NICOL. GEPF ilinunua hisa za kampuni ya NICOL katika soko la hisa Dar es salaam zenye thamani ya **Shilingi milioni 600**. Baadae Kampuni hii iliondolewa kwenye orodha ya Makampuni yaliyosajiliwa na Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE), kwa kutotimiza baadhi ya masharti ya usajili. Hali hiyo imesababisha Mfuko kushindwa kurejesha fedha zilizowekezwa katika Kampuni ya NICOL. Kamati inaona kwamba, Mfuko wa GEPF haukufanya utafiti wa kina kabla ya kuamua kufanya uwekezaji huu ili kubaini viashiria vya hatari na kuepuka hasara inayoweza kutokea kwakuwa, fedha zilizopelekwa katika uwekezaji huo ni michango ya wanachama.

Uwiano kati ya uwezo wa kulipa madeni na mali zilizopo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa za utendaji za Taasisi za Umma ambapo ilibainika kuwa, Mashirika yamekuwa na uwezo mdogo wa kulipa madeni kutokana na Taasisi hizo kupata hasara kwa miaka mingi mfululizo na kusababisha mtaji wote wa Taasisi kuliwa na madeni.

Mheshimiwa Spika, Mfano uwezo wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) kulipa madeni yake ya muda mfupi unapimwa na uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi ya Kampuni (Current Ratio). Uchambuzi wa hesabu za TFC unaonesha kuwa madeni ya muda mfupi ya Kampuni (current liabilities) yanazidi mali za muda mfupi (current asset) kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.6** na hivyo kufanya uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi (current ratio) kuwa **0.60:1**. Uwiano huu upo chini sana ukilinganishwa na kiwango elekezi (ideal ratio) cha 2:1.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la kifedha limejitokeza pia katika Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ambapo, Taarifa ya Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2015 ilionesha kuwa, madeni ya muda mfupi (current liabilities) yanazidi mali ya muda mfupi (current asset) kwa **Tsh Bilioni 30.2** ambapo Uwiano kati ya mali na madeni ya muda mfupi (current ratio) upo chini kwa **0.20:1** ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika ambacho ni **2:1**, Aidha, viwango vingine navyo ni vidogo (Return on Asset ni 0.05%, Return on Equity ni 0.07% na Return on Sales ni 4.54%)

Nafasi ya Bodi za Wakurugenzi katika Utawala kwenye Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili na kuchambua Taarifa ya Msajili wa Hazina, baadhi ya Mashirika yalibainika kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi pamoja na Bodi za Wadhamini. Kukosekana kwa Bodi hizo kumeathiri utendaji na utekelezaji wa shughuli za Taasisi hizo kwani Bodi ndizo zenye dhamana ya kufanya maamuzi mbalimbali kwa ajili ya utendaji na uendeshaji wenye tija.

Aidha, kukosekana kwa Bodi, kumesababisha Wakuu wa Idara/Vitengo wanaokaimu kuchelewa kuthibitishwa katika nyadhifa zao, jambo linaloathiri baadhi ya maamuzi ambayo yanahitaji watu wenye Mamlaka kamili. Vile vile, kukosekana kwa Bodi kumesababisha Taarifa za Ukaguzi kutowasilishwa kwa Msajili wa Hazina (TR) kutokana na kutothibitishwa na Bodi. Hali hii inasababisha Taasisi hizo kushindwa kuwasilisha Taarifa zinazohusu Utendaji mbele ya Kamati.

Kukosekana kwa maamuzi ya Bodi kumeathiri utendaji wa baadhi ya Mashirika pamoja na kusababisha hasara. Mfano, kutokuwa na Bodi kumeisababishia Serikali kukosa kiasi cha **shilingi Bilioni 10** kwa Mwaka kama tozo kutoka kwenye Sekta ya Hoteli za kitalii zilizoengwa ndani ya Hifadhi za Taifa (TANAPA)

Mheshimiwa Spika, Mahakama ilitoa hukumu **Tarehe 12/09/2014** chini ya **Jaji S.E. Mugasha** wa Mahakama ya Kanda ya Kaskazini Arusha kuwa, wawekezaji wote walio ndani ya Hifadhi walipe tozo na kuipa Mamlaka Bodi kupanga kiwango cha tozo hizo ili zianze kulipwa. Hata hivyo, hadi TANAPA inawasilisha Taarifa zake mbele ya Kamati Tarehe 12 Aprili, 2016, Bodi ya TANAPA ilikuwa haijaundwa na hivyo kuwafanya wawekezaji hao waendeleo kunufaika kwa kutolipa tozo na Serikali kuendelea kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, taratibu zinazitaka Mamlaka husika kuanza mchakato wa kuunda Bodi Mpya angalau miezi Sita kabla ya Bodi zilizopo madarakani kumaliza muda wake.

Aidha, Kamati imebaini kuwa, Sheria nyingi za Mashirika ya Umma hazielezei juu ya kuwa na muendelezo wa Uongozi (Succession Plan) katika mfumo wa uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi. Mashirika yenye Sheria zenye maelekezo hayo ni za Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji (EWURA) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Kukosekana kwa maelezo hayo, kunafanya kusiwepo na uratibu wa kutosha Kisheria na kutozingatiwa kwa vigezo muhimu wakati wa uundwaji wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, Mashirika 13 kati ya 41 ambayo hadi yanakutana na Kamati hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi na Bodi za Wadhamini ni haya yafuatayo;

- i) Mfuko wa Pensheni wa Hifadhi ya Jamii (NSSF),
- ii) Bodi ya Pamba,
- iii) Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO),
- iv) Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA),
- v) Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA),
- vi) Bodi ya Kahawa,
- vii) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).
- viii) Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC)
- ix) Kampuni ya Reli Tanzania (TRL),
- x) Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO),
- xi) Kampuni ya kuibua na kutekeleza miradi (UTT Project and Infrastructure Development - UTT PID),
- xii) Kampuni kwa ajili ya utoaji mikopo midogo midogo (UTT Microfinance),

- xiii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji na Huduma Kwa Wawekezaji (UTT Asset Management and Investor Services (UTT AMIS)).

Uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, taratibu na Miongozo ya Kibiashara

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, baadhi ya Mashirika na Taasisi zimekuwa zikikiuka taratibu kwa kutowasilisha Taarifa zao kwa Msajili wa Hazina kama Sheria ya Msajili wa Hazina inavyohitaji.

Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370 ya Mwaka 2002 kama ilivyorekebisha Mwaka 2010, inaipa majukumu Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia uwekezaji unaofanywa na Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni yote ambayo Serikali ina hisa. Hata hivyo, Sheria hii haigusi mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ambayo nayo kimsingi ni Taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hazina Masharti yanayohusu kutambua mamlaka ya Msajili wa Hazina. Aidha, uwepo wa Mamlaka nyingi za Usimamizi wa Mashirika katika ngazi tofauti za kiutendaji, unasababisha mkanganyiko wa kiutendaji ambao unamkosha Msajili wa Hazina nguvu ya kufuatilia miradi ya uwekezaji kuanzia ngazi ya awali (ubunifu wa mradi) hadi katika hatua ya utekelezaji na utendaji. Mfano Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inasimamiwa na Mamlaka zifuatazo: Wizara husika, Benki kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) na Sheria inamtaka Msajili wa Hazina kufanya hivyo.

Taasisi zote zilizo chini ya msajili wa Hazina zinatakiwa kufanya mambo yafuatayo:-

- i) Kupata idhini ya Msajili wa Hazina ya posho zinazolipwa na taasisi kwa Bodi na watumishi,
- ii) Kupata kibali cha Msajili wa Hazina cha Sera ya uwekezaji,
- iii) Mpango wa uwekezaji wa taasisi uidhinishwe na Msajili wa Hazina,
- iv) Kama taasisi imechukua mkopo kwa ajili ya uwekezaji kwa kutumia dhamana ya mali za taasisi inatakiwa ipate idhini ya Msajili wa Hazina, na
- v) Taasisi inatakiwa kuwasilisha Mpango wa Biashara (Business Plan) kwa Msajili wa Hazina kwa Uchambuzi na idhini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mashirika na makampuni ambayo yanafanya uwekezaji bila ya kuzingatia masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina ni pamoja na NSSF, PSPF, LAPF, PPF na GEPP.

Kamati pia imebaini kuwa baadhi ya mashirika wanafanya uwekezaji bila kuzingatia masharti ya Sheria zilizoanzisha mashirika hayo, mfano Taasisi nyingi zinawekeza kwenye majengo kwa lengo la kupata faida kutokana na uwekezaji huo. Mfano Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) katika taarifa zao wameonekana kuvutiwa na mradi wa ujenzi wa majengo ya makazi na kuboresha Hospitali shughuli ambazo hazikuwa mojawapo ya malengo mahususi (core functions) ya uanzishwaji wa Shirika hilo.

Changamoto ambayo kamati imebaini ni mapungufu ya Sheria ya Manunuzi ya umma, Taasisi nyingi zinazowekeza mitaji ya umma kwenye miradi mbalimbali hususani kwenye majengo zimelalamikia Sheria ya Manunuzi ya Umma kuwa masharti ya mchakato wa uwekezaji unasababisha ucheleweshwaji wa kukamilika kwa baadhi ya miradi na kufanya uwekezaji huo kuwa wa ghali sana na hivyo kurefusha muda wa urejeshwaji wa mitaji iliyowekezwa (*pay back period*) ya miradi ya uwekezaji wa mitaji ya Umma.

Uzingatiaji wa Sera ya taasisi kuhusu Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Sera ya Uwekezaji ya Taasisi ndiyo inayotoa mwongozo wa aina na kiwango cha uwekezaji unaoweza kufanyika katika Taasisi za Umma, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu uwepo wa sera hiyo kwa kila taasisi na namna inavyozingatwa. Uchambuzi ulionyesha kuwa kati ya Taasisi 41 zilizowasilisha taarifa zake kwa ajili ya uchambuzi wa Kamati, Taasisi 15 tu ndizo zenye Sera ya uwekezaji. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 36.6 ya sampuli ya mashirika/taasisi zilizofanyiwa kazi na Kamati³. Hali hii inahatarisha uwezo wa Taasisi kufanya uwekezaji wenye tija na wenye manufaa kwa Taifa na ni kinyume na utaratibu bora wa uwekezaji wa mitaji ya umma.

Uendeshaji na utendaji wa Taasisi zinazofanya uwekezaji wa Mitaji ya Umma nchini

Mheshimiwa Spika, katika eneo la uendeshaji na utendaji Kamati imeangalia maeneo mbalimbali ikiwemo uhusiano kati ya Matumizi na uwekezaji, Taasisi za Umma kujiendesha kahasara pamoja na utegemezi kwa ruzuku za serikali. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati imebaini kama ifuatavyo:-

a) Uhusiano kati ya Matumizi na uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingi zimekuwa zikitumia fedha nyingi katika matumizi ya kawaida ikilinganishwa na mapato yao. Hata hivyo matumizi hayo ambayo yanasababisha Taasisi kupata hasara hayahusiani na uwekezaji. Mfano wa Taasisi zenye matumizi makubwa ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambao katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, ulitumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 113.47** ikiwa ni sawa na **Asilimia 17.8** ya michango ya wanachama kwa mwaka kwa ajili ya kukimu gharama za kiutawala na uendeshaji. Gharama hizi ni kubwa ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 10 kama inavyoelekezwa na Mdhambi wa Uendeshaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa pili ni Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) ambacho kina matumizi makubwa yasiyowiana na mapato yake. Hii inathibitishwa na Uwiano wa Matumizi ya Uendeshaji na Mapato (Operating Expenditure to Income Ratio) ambapo katika mwaka wa fedha 2010/11 ilikuwa asilimia 90, 2011/12 asilimia 88, 2012/13 asilimia 92, 2013/14 asilimia 105, na 2014/15 asilimia 87. Tafsiri ya maelezo hayo ni kuwa sehemu kubwa ya mapato ya AICC yanatumiwa na Shirika na hivyo kubaki na ziada ndogo au hasara.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikizisitiza Taasisi za Umma kutekeleza matakwa ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Sura 370) kama ilivyorekebishwa katika Kifungu cha 46 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 kwa kuhakikisha kwamba Gharama za Uendeshaji hazizidi asilimia 60 ya Mapato Ghafi (*Gross Revenue*).

b) Taasisi za Umma kujiendesha kwa hasara

Mheshimiwa Spika, katika upande mwingine wa uendeshaji wa Taasisi za Umma, Kamati imebaini kuwa, Taasisi nyingi za Umma zimekuwa zikijiendesha kwa hasara kwa muda mrefu na kushindwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mifano ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

³ Tazama Kiambatisho Na. 03: Orodha ya Taasisi/ Mashirika ambazo Taarifa zake zimechambuliwa na Kamati

Kwanza ni Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), ambayo imekuwa ikipata hasara mfululizo ambapo mpaka kufikia Juni, 2015, Kampuni hii ilipata hasara iliyofikia kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.2**. kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2011/12 hadi 2014/15 limbikizo la hasara lilifikia kiasi cha **Shilingi Bilioni 30.2**. Hali hii mbaya ya kifedha inatokana na Kampuni kutokuwa na mikakati thabiti ya kujikinga na athari za kibiashara (*Business Risk and Uncertainties Strategy*) ambazo hazitabiriki. Aidha, kutokuwepo kwa udhibiti wa matumizi kumechangia kuporomoka kwa ufanisi wa kifedha wa Kampuni (*Financial Performance*);

Pili ni Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imekuwa na utendaji usioridhisha. Kampuni ilianza kufanya vibaya na kutengeneza hasara kuanzia mwaka 2013. Mpaka sasa Kampuni imeendelea kupata hasara kila mwaka. Hivyo, Uongozi wa TSN unatakiwa kuandaa mkakati wa kubadilisha hali hiyo (Turn-around Strategy) ili Kampuni ianze kupata faida na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali; na

Tatu ni Shirika la Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) imeshindwa kujiendesha kwa faida kutokana na kasoro za kimuundo na utendaji usioridhisha ambao unachangiwa Watendaji kushindwa kufanya maamuzi kutokana na kukaimu nafasi zao pamoja ukosefu wa ubunifu katika kuendesha Shirika.

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingine zinazojiendesha kwa hasara ni Bodi za Mazao nchini. Katika kufuatilia mwenendo wa uwekezaji wa Bodi za mazao, Kamati ilichambua taarifa za bodi tano za mazao. Bodi hizo ni: Bodi ya Pamba, Bodi ya Korosho, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Tumbaku na Bodi ya Sukari. Uchambuzi ulionesha kuwa Bodi hizo zimekuwa zikijiendesha kwa hasara kwa muda mrefu kutokana na dosari mbalimbali katika Uongozi na uendeshaji wake. Baadhi ya dosari hizo ni:-

- i) Kutotilia mkazo eneo la uzalishaji kwa wakulima,
- ii) kuacha jukumu la msingi la kusimamia (regulator) na kufanya kazi ya uzalishaji na biashara, hali inayosababisha kuua mazao ya wakulima,
- iii) Kutokuwa na juhudi za makusudi katika kukuza mfuko wa maendeleo ya mazao na kusambaza pembejeo kwa wakulima,
- iv) Bodi kutumiwa na kuwanufaisha Wawekezaji (wafanyabiashara) pekee na kuwasahau Wakulima,
- v) Kuwa na matumizi makubwa ikilinganishwa na mapato japo Serikali imekuwa haipeleki ruzuku kikamilifu na kwa wakati au kutopeleka kabisa, na
- vi) Kushindwa kubaini vyanzo vipya vya mapato.

c) Utegemezi kwa ruzuku za Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Mashirika/Taasisi nyingi za Umma zimekuwa zikijiendesha kwa kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Hali hii inasababishwa na ubunifu mdogo kwa waliopewa dhamana ya kuongoza Taasisi hizi na usimamizi wa rasilimali usiojali maslahi ya Taifa. Iwapo Taasisi hizo zitaendeshwa kwa weledi pamoja na kutazama upya Mitaji yake na kupitia uwiano wa mapato na matumizi, kuna uwezekano mkubwa zikajitegemea na kuachana na utegemezi wa Ruzuku ya Serikali.

Kwa mfano; Taasisi za Elimu zinaweza kuboresha vitengo vya huduma za ushauri (*consultancy services*) na kuvitumia kujiongezea mapato. Vilevile, Bodi za Mazao kama Pamba, Kahawa na Korosho zinaweza kubuni njia mbadala za kujiongezea kipato na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini. Aidha, Shirika la madini la Taifa (STAMICO) limeshindwa kujiendesha kutokana na kutopatiwa mtaji na Serikali. Hali hiyo imesababisha shirika liendeleo kutegemea ruzuku ya Serikali na hivyo kushindwa kutoa gawio kwa Serikali.

Masuala mengine ya msisitizo kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Kamati imejadili na kuchambua masuala mbalimbali kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Katika uchambuzi wake imebaini mapungufu na matatizo mbalimbali ambayo yamekuwa yakisabaishwa na Serikali kama ifuatavyo:-

a) Madeni Makubwa ambayo Serikali inadaiwa na Mashirika na Taasisi zake

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu utendaji wa Taasisi mbalimbali za Umma na kubaini madeni makubwa ambayo Serikali inadaiwa na Taasisi hizo. kwa ujumla uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Serikali imekuwa na tabia ya kutumia huduma au kukopa kutoka katika Taasisi zake bila kufanya malipo. Mfano katika Kampuni ya Magazeti ya Serikali, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Shirika la Ugavi la Umeme Tanesco na Kampuni za Huduma ya Maji safi na Maji Taka Dar es Salaam. Serikali imekuwa ikidaiwa fedha nyingi, na madeni hayo yamekuwa yakilimbikizwa mwaka hadi mwaka. Hali hii inadidimiza ukuaji wa Taasisi hizo na kuzisababishia hasara kubwa katika utendaji wao hivyo basi, Serikali ijenge utamaduni wa kulipia huduma inazopata katika Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya uwekezaji na utendaji wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF) na kubaini madeni mengi ambayo Serikali inadaiwa na Mfuko huo. Baada ya uchambuzi wa Taarifa hiyo, Kamati ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kujua msimamo wa Serikali juu ya ulipaji wa madeni hayo. Wakati wa kikao baina ya Wizara na Kamati, Wizara iliwasilisha Taarifa yake kuhusu ulipaji wa deni wanalodaiwa na Mfuko huo ambao umegawanyika katika sehemu Tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kundi la Kwanza ni madeni yanayotokana na dhima ya mafao ya Watumishi wa Serikali ambao walirithiwa na Mfuko wa PSPF kipindi ulipoanzishwa Mwaka 1999 (Pre- 99), katika kundi hili, Wizara ya Fedha na Mipango ilibainisha deni ambalo Serikali inadaiwa na Mfuko hadi kufikia Juni, 2015, ambalo ni **Shilingi Tirioni 1.97** Aidha, kiasi hicho kilicholipwa na PSPF kwa Wastaafu hao kimezaa riba ya **Shilingi Bilioni 698** na kusababisha deni lifikie jumla ya **Shilingi Tirioni 2.67**

Taarifa zilizowasilishwa na Mfuko wa PSPF, zilibainisha kwamba, uwezo wa Mfuko kulipa mafao kwa Wanachama wake utategemeana na namna Serikali itakavyolipa michango yake kwa wakati pamoja na kulipa deni la Wanachama kwa kipindi cha utumishi wa kabla ya Julai, 1999.

Mheshimiwa Spika, Kundi la Pili ni madeni yanayotokana na Uwekezaji wa PSPF katika miradi mbalimbali ya Serikali. Katika kundi hili Kamati imebaini kukinzana baina ya Serikali na Mfuko wa PSPF. Wakati Serikali inadai deni inalodaiwa ni shilingi **Bilioni 290**, Mfuko wa PSPF unadai deni halisi ni shilingi **Bilioni 533**. Hata hivyo, licha ya Serikali kudai hilo ndilo deni inalodaiwa bado imeshindwa kutekeleza ahadi yake ya kutoa **Hati Fungani** zenye thamani ya Shilingi **Bilioni 290** kwa ajili ya kulipa deni hilo.

Kamati imebaini kwamba, tofauti ya tafsiri ya kiwango cha deni baina ya Serikali na Mfuko inatokana na kutokuwepo kwa makubaliano baina ya pande mbili hizi kunatokana na tafsiri ya mikataba juu ya utozaji wa riba na tozo, pale Serikali inaposhindwa kulipa madeni kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kundi la Tatu ni madeni ya malimbikizo ya Mchango wa Mwajiri (15% Serikali) wa kila mwezi. Deni lililotokana na malimbikizo hayo ni shilingi

Bilioni 253.78 ambalo ni la kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi februari, 2016. Wizara ilidai kwamba, ingewasilisha kiasi chote kinachodaiwa na Mfuko hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilichambua Taarifa ya Uwekezaji na Utendaji wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa (LAPF) na kubaini madeni makubwa ambayo Serikali inadaiwa na Mfuko huo. Madeni ambayo Serikali inadaiwa na LAPF yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ikiwa ni Mchango wa asilimia 15 kutoka Serikalini na Madeni yatokanayo na Taasisi za Serikali (Wajajiri) kutowasilisha Michango ya Watumishi wao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango imeonekana kutotimiza wajibu wake wa kuchangia 15% kwenye Mfuko wa LAPF, ambayo ni Michango ya Watumishi kwa upande wa Serikali kama Sheria inavyotaka. Hali hiyo imesababisha deni ambalo LAPF inaidai Wizara kukua na kufikia **Shilingi Bilioni 47.24** ambazo ni sawa na 76.29% ya deni lote ambalo Mfuko unadai. Vile vile, Katika madeni yatokanayo na Taasisi za Serikali, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, jumla ya Taasisi za Serikali 365 zinadaiwa na Mfuko wa LAPF, kiasi cha **Shilingi Bilioni 11.20** ambacho ni sawa na **18.09%** ya deni lote ambalo Mfuko unadai. Aidha, katika orodha hiyo, uchambuzi umebaini kuwa Taasisi 61 ni zile ambazo kila moja inadaiwa zaidi ya **Milioni Hamsini (50)** huku Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ikiongoza kwa kuwa na deni kubwa zaidi linalofikia **Shilingi Milioni 626.75**

b) Usimamizi wa Madeni

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya Uwekezaji na Utendaji wa Benki ya Maendeleo Tanzania (TIB) na kubaini kuwa imebebehsa mzigo mkubwa wa usimamizi wa madeni ya Taasisi nyingine na Serikali hali inayosabaisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na kusababisha benki kushindwa kujikita katika jukumu lake la Msingi.

Mheshimiwa Spika, Benki ya TIB iliteuliwa na Serikali kukusanya madeni ya mikopo iliyokuwa imetolewa kupitia Wizara ya Fedha kwa ajili ya uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi (Japanese Commodity Import Support – CIS). Hadi kufikia Juni 2016, kiasi kilichokusanywa na Benki ni **Shilingi Bilioni 7.5** kati ya **Bilioni 16.8** ikiwa ni **asilimia 45** ya madeni yote yaliyopokelewa na Benki ya TIB.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kufungwa kwa iliyokuwa Benki ya Nyumba Tanzania (THB) mwaka 1995, Benki ya TIB iliteuliwa kuwa wakala wa mfilisi wa THB. TIB imeendelea kutekeleza wajibu huo pamoja na kukusanya madeni, kusimamia kesi mahakamani, kutoa hati kwa wale ambao madeni yao yamelipwa kikamilifu na kuendelea kutunza kumbukumbu na nyaraka za wadaiwa. Tangu kuanza kwa zoezi hili, kiasi cha **Shilingi milioni 755.45** tu kimekusanywa ikilinganishwa na matumizi makubwa zaidi ya **Shilingi Bilioni 2**. Aidha, gharama za pango, kesi, matangazo na mishahara zimeendelea kuwa changamoto kubwa kwa benki.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini changamoto kubwa katika usimamizi wa madeni katika kiwanda cha kusindika nyama cha SAAFI. Mnamo Mwaka 2004, Kampuni ya SAAFI ilipatiwa mkopo wa **Shilingi Bilioni 6.2** na Benki ya Standard Chartered kwa ajili ya mitambo na ujenzi wa Kiwanda cha nyama. Mkopo huo ulipata dhamana (Guaranteed) ya Serikali chini ya *BOT Credit Guarantee Scheme*. Mradi uliposhindwa kulipa deni la Standard Chartered, Serikali kutokana na kuweka

dhamana hiyo ililazimika kulipa mkopo wote pamoja na riba kwa Benki ya Standard Chartered kiasi cha **Shilingi Bilioni 10.097**.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine Serikali iliongeza mkopo wa **Shilingi Bilioni 4.852** kwa Kiwanda cha SAAFI hivyo, kufanya jumla ya mkopo kufikia **Shilingi Bilioni 14.949**. Mkopo huu baadae ulihamishiwa TIB kwa ajili ya usimamizi (Agency Agreement) uliosainiwa tarehe 14 Aprili 2008. Mkopo ulipewa masharti nafuu ikiwa ni pamoja na riba nafuu ya asilimia 6.18 ambapo chini ya mkataba wa uwakala, TIB ilipewa majukumu ya kusimamia mkopo uliokwishatolewa na kuletwa TIB, kuhakikisha deni la Serikali linalipwa pamoja na riba, kuwasilisha fedha za mkopo kwa Serikali baada ya kulipwa na kutoa taarifa ya maendeleo ya mradi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Katika mkakati wa kuisaidia Kampuni ya SAAFI iweze kujiendesha vizuri na kurejesha mikopo ya awali, Benki ya TIB nayo ilitoa mkopo wa kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.5** kama mtaji wa uendeshaji (Working Capital) kwa kiwanda cha SAAFI ambazo pia hazijarejeshwa. Hadi kufikia mwezi Juni 2016, Kampuni ya SAAFI ilikuwa ikidaiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 20.37**.

c) Tathmini ya Uwezo wa Mashirika ya Umma kwenye kuingia Mikataba ya Uwekezaji **Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati imebainika kuwa, Taasisi za Umma zinazosimamia Miradi mbalimbali ya Uwekezaji na kuingia mikataba na wawekezaji kutoka nje ya nchi zimekuwa na mapungufu kadhaa. Mapungufu hayo ni pamoja na kushindwa kufanya tathmini ya miradi kabla ya kuingia katika uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya uwekezaji na utendaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) imebanisha kuwa, Shirika limekuwa likitekeleza Miradi yake kwa kuingia ubia na sekta binafsi kwa niaba ya Serikali. Kutokana na ufinyu wa bajeti toka Serikalini, mitaji mingi ya kutekeleza miradi hutoka katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Maendeleo ni Taasisi muhimu ambayo imekuwepo kwa muda mrefu, Shirika lina dhamana kubwa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Shirika linasimamia miradi mingi ambayo mpaka sasa haijafikia mwisho. Mwenendo huu wa utendaji wa Shirika hauoneshi kama NDC itafikia malengo yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipata hisa kidogo katika miradi mingi ya ubia kutokana na sehemu kubwa ya utafiti kufanywa na mbia na kukosa usimamizi wa karibu wa mwakilishi wa nchi ili kubaini thamani halisi ya mradi na faida itakayopatikana. Aidha, gharama za utafiti ni kubwa mno kiasi cha kusababisha kiasi cha hisa kwa upande wa Serikali kuwa kidogo. Hali hiyo imesababishwa na Serikali kutowekeza katika utafiti na katika makubaliano ya mikataba. Aidha, utaratibu unaotumika katika ugawaji wa hisa unategemeana na bajeti ya Serikali iliyotumika katika utafiti. Kamati ina maoni kuwa utaratibu huo si mzuri kwa kuwa nchi imekuwa ikipoteza rasilimali nyingi. Mfano wa Miradi inayotekelezwa kwa mbia kufanya utafiti ni kama ifuatavyo:-

i) Miradi ya Mchuchuma na Liganga.

Mradi huu una thamani ya **Dola za Kimarekani Bilioni 3.0** ambapo mradi ni wa ubia kati ya NDC na SHCL kwa umiliki wa Asilimia 20 kwa 80 mtawalia. Mradi unatekelezwa na Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources Limited.

ii) Mradi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka.

Mradi huu una thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 800 ambapo mradi ni wa ubia kati na NDC na Kampuni ya Intra Energy Corporation kwa umiliki wa Asilimia 30 kwa 70 mtawalia. Mradi unatekelezwa na Kampuni ya Tancoal Energy Limited.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ya utendaji wa Shirika inachangiwa na Serikali kutojipanga wakati wa kuingia mikataba na kukosekana kwa ushirikishwaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Changamoto za Ujumla

Mheshimiwa Spika, Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake imekumbana na changamoto kadhaa ambazo kwa kiasi fulani zinaathiri utendaji wa Kamati. Baadhi ya changamoto ni kama zifuatazo:-

Muda uliotengwa kwa ajili ya Kamati kupitia Taarifa za Mashirika na Taasisi za Umma

Mheshimiwa Spika, Kamati inajukumu la kuchambua Uwekezaji na utendaji wa jumla ya Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa Mia Mbili Sitini na Nne (264). Kutokana na Ufinyu wa muda Kamati imeshindwa kuyafikia Mashirika mengi ili kujiridhisha na Uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na Taasisi hizo.

Wajumbe kutopata Semina ya Kujengewa uwezo

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati wanatakiwa kupata fursa ya kujengewa uwezo ili kuchambua na kubaini kama uwekezaji wa mitaji ya umma unazingatia sheria, taratibu na miongozo ya uwekezaji. Aidha Kamati inatakiwa kujifunza kwa Nchi ambazo Taasisi zake zimefanikiwa katika uwekezaji ili kufahamu njia zilizotumika ili kufanikisha uwekezaji huo.

Ziara za Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, Kamati imekosa nafasi ya kufanya ziara za ukaguzi katika Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo yamewasilisha Taarifa zake za uwekezaji mbele ya Kamati. Mfano katika Kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017 Kamati iliweza kufanya ukaguzi katika Taasisi Tano (5) kati ya Arobaini na Moja (41) zilizofika mbele ya Kamati.

Upatikanaji wa Nyaraka za Kisheria

Mheshimiwa Spika, Kamati inafanya kazi kwa karibu na Washauri wa Mambo ya Kisheria kutoka Ofisi ya Bunge ili kuchambua Sheria zilizoanzisha Taasisi mbalimbali za Umma na kubaini iwapo Sheria hizo zinafuatwa katika hatua mbalimbali za Uwekezaji. Aidha Uchambuzi hufanyika ili kubaini iwapo Mikataba ya Uwekezaji ambayo Taasisi za Umma zimeingia zimefuata Sheria na Miongozo ya Uwekezaji. Hata hivyo, Taasisi nyingi zimekua zikishindwa kuwasilisha nyaraka hizo muhimu kwa Wataalamu wa Sheria ili waweze kuishauri Kamati.

SEHEMU YA TATU

MAONI NA MAPENDEKEZO

Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi kuhusiana na uwekezaji wa mitaji ya Umma, Kamati inapenda kutoa maoni ya jumla yafuatayo:-

Faida ambayo inatokana na uwekezaji wa mitaji ya umma bado ni ndogo ikilinganishwa na kiasi kilichowekezwa. Hadi tarehe 30 Juni, 2016 Serikali ilikuwa imewekeza mitaji yenye thamani ya shilingi trilioni 23, lakini faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji huo kwa mwaka 2015/16 ilikuwa ni shilingi bilioni 422 tu, ambayo ni sawa na asilimia 1.83.

Kamati inatambua dhamira njema ya Serikali kwamba, sehemu ya uwekezaji uliofanyika inalenga kutoa huduma kwa jamii. Hata hivyo, bado Kamati inaamini kwamba, iwapo uwekezaji huo utatekelezwa kwa ufanisi, unaweza kuleta faida zaidi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali na kuboresha utoaji wa huduma.

Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maoni ya Kamati kutokana na uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mikataba ya Uwekezaji isiyo na Tija

Kwa kuwa, imebainika kuwa, baadhi ya Taasisi na mashirika ya umma yamekumbwa na tatizo la uendeshaji kutokana na mikataba isiyofaa, mibovu na isiyo na tija, kwa Taifa,

Na Kwa kuwa, hali hiyo inaongeza mzigo kwa Serikali na kusababisha matumizi ya rasilimali za umma kwenye uwekezaji huo kutokuwa na tija.

Kwa hiyo Basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa:

- i) Serikali isimamie mapitio ya vipengele vyote vyenye utata na visivyo na manufaa kwa Taifa ili virekebishwe muda wa kupitia upya Mikataba hiyo utakapowadia,
- ii) Serikali iwekeze katika utafiti na kuwajengea uwezo (Capacity Building) wataalamu wa Taasisi zake kuhusiana na Mikataba, upembuzi yakinifu ili waweze kusimamia kikamilifu miradi ambayo Taasisi hizo zinaingia na wawekezaji wa nje.

Faida inayopatikana kutoka katika Uwekezaji

Kwa Kuwa, Serikali inapata faida kidogo kutoka katika taasisi na Mashirika ya Umma kutokana na Taasisi hizo kujiendesha kwa lengo la kutoa huduma, na faida ya kutosha kutoka katika makampuni ambapo ina hisa chache yanayojiendesha kibiashara,

Na Kwa kuwa, Hali hiyo ya Mashirika mengi ya Umma kujiendesha kwa lengo la kutoa huduma inasababisha Serikali kukosa gawio na mchango mdogo katika Mfuko Mkuu wa Serikali,

Kwa hiyo Basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa:-

- i) Serikali iangalie namna bora ya kuboresha utendaji wa Taasisi na Mshirika ya Umma ambapo kuna uwekezaji wa Serikali.
- ii) Serikali iondokane na dhana ya kutoa huduma pekee kwa Taasisi zake na badala yake ziweze kujiendesha kibiashara ili ziweze kupata faida na kutoa gawio pamoja na kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali,
- iii) Serikali iongeze uwekezaji katika Makampuni ambayo yanazalisha faida kubwa ili Serikali ipate gawio kubwa.

Kukosekana kwa Bodi za Wakurugenzi

Kwa kuwa, licha ya umuhimu wa Bodi za Wakurugenzi katika usimamizi na uamuzi wa kinkakati kwenye uwekezaji, zipo Taasisi na Mashirika ya Umma yasiyokuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa muda mrefu,

Na Kwa kuwa, Kukosekana kwa Bodi za Wakurugenzi ni jambo linaloathiri maamuzi ya kinkakati, usimamizi thabiti na utendaji kwa ujumla,

Kwa hiyo Basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa:-

- i) Serikali ifanye zoezi la uteuzi wa Bodi hizo lifanyike kwa haraka na umakini ili kuongeza ufanisi katika Taasisi na Mashirika yanayofanya uwekezaji wa mitaji ya umma,
- ii) Serikali ihakikishe kuwa uteuzi wa Bodi uzingatie sifa na weledi kwa Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi pamoja na kufuata ushauri wa Msajili wa Hazina kwakuwa ndiye msimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali.

Mgongano wa Kisheria

Kwa Kuwa, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, inaelekezwa na Sheria zilizoanzisha mifuko hiyo kuwasilisha Taarifa za uwekezaji na Utendaji kwa Mamlaka ya Udhidhi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Benki Kuu ya Tanzania jambo ambalo haliendani na masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, inayotaka taasisi zote za Umma kuwasilisha Taarifa zake za uwekezaji na Utendaji,

Na kwa kuwa, mgongano huo wa kisheria, unasababisha Msajili wa Hazina ashindwe kufuatilia ipasavyo utendaji na uwekezaji unaofanywa na mifuko hiyo,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali iangalie uwezekano wa kuzifanyia marekebisho Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ili ziweze kumtambua Msajili wa Hazina (TR) kama Msimamizi Mkuu wa Taasisi za Umma ambazo Serikali ina hisa.

Uzalishaji wa Umeme kwa gharama za juu

Kwa kuwa, imebainika kuwa Makampuni ya uzalishaji umeme ya IPTL na AGGREKO yanaendesha mitambo yake kwa kutumia mafuta jambo linalosababisha umeme unaozalishwa kuuzwa kwa bei kubwa ikilinganishwa na vyanzo vingine kama maji na gesi,

Na kwa kuwa, TANESCO inalazimika kugharamia umeme huo, hivyo kuwa na gharama kubwa za uendeshaji jambo linalosababisha hasara,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali iangalie njia bora ya kuliwezesha Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO) kuongeza umeme kwa kutumia vyanzo vingine vya nishati kama vile Gesi asilia, Upepo, Jotoaridhi, Jua, Makaa ya Mawe, na kadhalika. Kuongezeka kwa umeme kutaliwezesha shirika hilo kuepuka kununua umeme unaozalishwa kutokana na nishati ya mafuta ambao ni ghali, na unamuumiza mlaji wa mwisho.

Uwekezaji katika Bodi za Mazao kutokuwa na faida kwa wakulima

Kwa kuwa, licha ya dhamira nzuri ya kuwekeza kwenye Bodi nyingi za mazao, hakuna faida inayopatikana kutokana na Uwekezaji huo, na wakulima hawawezeshwi kupata kwa wakati pembejeo bora, kwa bei nafuu na masoko ya uhakika kwa mazao yao,

Na kwa kuwa, kukosekana kwa faida itokanayo na uwekezaji kwenye bodi nyingi za mazao ni kinyume na matarajio ya azma ya kuanzisha bodi hizo ambazo ni nyingi kwa idadi,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali iangalie upya muundo na malengo ya kuanzishwa kwa bodi za mazao ili uwekezaji katika bodi hizo uwe na faida pamoja na kuchangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao.

Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa

Kwa Kuwa, Jukumu la msingi la Shirika la Nyumba la Taifa ni kuwekeza katika Majengo kwa lengo la kuboresha hali ya makazi nchini na kupata faida kulingana na hali ya soko bila kuathiri azma ya kuboresha makazi kwa wananchi,

Na Kwa Kuwa, utekelezaji wa jukumu hilo, umefanyika kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba ambapo Shirika hilo limegharamia miundombinu iliyopaswa kugharamiwa na taasisi nyingine za umma, jambo linalopandisha gharama za nyumba hizo na kusababisha bei yake kuwa kubwa ikilinganisha na uwezo wa Watanzania wa kawaida katika soko,

Kwa hiyo Basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali ihakikishe kuwa kabla ya Shirika la nyumba kufanya uwekezaji wake, taasisi mbalimbali zinazohusika na ujenzi wa miundombinu zinatekeleza ipasavyo majukumu yake.

Taasisi zinazofanya uwekezaji ziwe na Sera ya Uwekezaji ya Taasisi

Kwa kuwa, Sera ya Uwekezaji ya Taasisi ndiyo inayotoa mwongozo wa aina na kiwango cha uwekezaji unaoweza kufanyika katika Taasisi za Umma, lakini uchambuzi umeonesha kuwepo kwa Taasisi na mashirika mengi yanayofanya uwekezaji bila kuwa na Sera yake ya uwekezaji,

Na kwa kuwa, ukosefu wa sera ya uwekezaji kwa taasisi na mashirika yanaowekeza una hatari ya kukosa ufanisi, tija na faida kwa taasisi na Serikali,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali izitake Taasisi zote zinazowekeza kwa kutumia mitaji ya umma, ziwe na Sera ya Uwekezaji ya Taasisi.

Utoaji wa Mitaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma

Kwa kuwa, Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa na changamoto ya kutokuwa na mitaji ya kutosha (*undercapitalized*),

Na Kwa kuwa, kukosekana kwa mitaji hiyo kumesababisha Taasisi na Mashirika hayo ya Umma kushindwa kujiendesha vyema na kushindwa kulipa gawio kwa Serikali,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali iweke mitaji ya kutosha katika Taasisi za Umma, hasa katika Benki ya Wanawake (TWB), Twiga Bancorp, TIB Development Bank, TIB Corporate Bank, Benki ya Posta Tanzania (TPB) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili Taasisi hizi ziweze kujiendesha kwa tija zaidi na kutoa gawio Serikalini.

Taasisi za Umma zinazofanya Biashara kutozingatia utoaji wa Gawio kwa Serikali

Kwa Kuwa, licha ya Mikataba ya uwekezaji kuzitaka Taasisi, Mashirika ya Umma na makampuni ambapo Serikali ina hisa kutoa gawio kwa Serikali, Taasisi, mashirika na makampuni 51 kati 64 hazijafanya hivyo,

Na Kwa kuwa, hatua ya kutokutoa gawio kwa Serikali kama kunakiuka makubaliano ya kimkataba na kuikoshesha serikali mapato kwa kiwango kikubwa,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali ichukue hatua stahiki za kisheria dhidi ya Kampuni na Taasisi ambazo hazijatoa gawio na kuzitaka zizingatie makubaliano yaliyopo kwenye mikataba.

Taasisi za Umma kutozingatia Sheria ya Msajili wa Hazina ya kutozidi matumizi ya Asilimia 60

Kwa kuwa, Taasisi nyingi za Umma hazizingatii masharti ya *Sheria ya Msajili wa Hazina* (Sura 370) inayozitaka kutokuwa na Gharama za Uendeshaji zinazozidi asilimia 60 ya Mapato Ghafi (*Gross Revenue*),

Na Kwa kuwa, kutokuzingatia masharti ya *Sheria ya Msajili wa Hazina* (Sura 370) ni kinyume na utaratibu bora wa uwekezaji wa mitaji ya umma na pia inaathiri kiwango cha fedha kinachoweza kutumika kutoa gawio serikalini,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa Serikali isimamie ipasavyo utekelezaji wa *Sheria* na kuzichukulia hatua Taasisi za Umma zinazovuka kiwango cha matumizi cha asilimia 60 ya mapato ghafi.

Uwekezaji katika Mitambo ya Mto Ruvu

Kwa kuwa, Imebainika kuwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kwa ununuzi wa mitambo iliyopo Ruvu juu unakabiliwa na hatari ya kutorejesha fedha kutokana na uwezekano wa kuzimwa kwa mitambo utakaosababishwa na kukosekana kwa maji,

Na Kwa Kuwa, Hali hiyo itasababisha mitambo iliyonunuliwa kwa fedha nyingi za umma kutofanya kazi na kuwa hasara kwa serikali,

Kwa hiyo Basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali iandae mkakati madhubuti utakaosaidia kupatikana kwa njia mbadala kama vile utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa bwawa la Kidunda ili kuifanya mitambo hiyo ifanye kazi.

Utendaji usio ridhisha wa Mashirika ya Umma

Kwa kuwa, Taasisi nyingi za Umma zimebainika kuwa na utendaji usio ridhisha na kusababisha Taasisi hizo kujiendesha kiasara,

Na kwa kuwa, hasara inayotokana na Taasisi za Umma inaongeza mzigo kwa kuwa tegemezi kwa Serikali na Taifa kwa ujumla,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kuwa, Serikali imtaka Msajili wa Hazina aharakishe kufanya mapitio ya mfumo na utendaji wa mashirika yote ya Umma yenye utendaji usioridhisha na kufanya maboresho yanayostahili.

HITIMISHO

Shukurani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu makini ambao umeniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, maelekezo ya kiti chako yameiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo na wakati wote Kamati imepata msaada pale ilipohitaji.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Prof. Oswald Mashindano kwa kuteuliwa kuwa Msajili wa Hazina na kwa ushirikiano wake aliutoa kwa Kamati toka kuteuliwa kwake. Aidha, napenda kumshukuru Ndugu Lawrence Mafuru aliyekuwa Msajili wa Hazina pamoja na wafanyakazi wote wa ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa Kamati wakati wote ilipokutana na Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Umma. Ofisi ya Msajili wa Hazina ni kitendea kazi muhimu kwa Kamati kwani ndiyo yenye dhamana ya kusimamia uwekezaji katika Taasisi na Mashirika yote ya Umma ambayo Serikali ina hisa, na kuhakikisha ufanisi katika utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb		–	Mwenyekiti
2.	Mhe. Lolesia Jeremia Bukwimba, Mb	–		M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb	–		Mjumbe
4.	Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb	–		Mjumbe
5.	Mhe. Elias John Kwandikwa, Mb	–		Mjumbe
6.	Mhe. Fatuma Hassan Toufiq, Mb	–		Mjumbe
7.	Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb	–		Mjumbe
8.	Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	–		Mjumbe
9.	Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb	–		Mjumbe
10.	Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	–		Mjumbe
11.	Mhe. Juma Othman Hija, Mb	–		Mjumbe
12.	Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	–		Mjumbe
13.	Mhe. Maftah Abdallah Nachuma, Mb	–		Mjumbe
14.	Mhe. Othman Omar Haji, Mb	–		Mjumbe
15.	Mhe. Riziki Saidi Lulida, Mb	–		Mjumbe
16.	Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb	–		Mjumbe
17.	Mhe. Sannda Edwin Mgante, Mb	–		Mjumbe
18.	Mhe. Sophia Mattayo Simba, Mb	–		Mjumbe
19.	Mhe. Stephen Hilary Ngonyani, Mb	–		Mjumbe
20.	Mhe. Zainab Athuman Katimba, Mb	–		Mjumbe
21.	Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb	–		Mjumbe
22.	Mhe. Muhammed Amour Muhammed, Mb	–		Mjumbe
23.	Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb	–		Mjumbe
24.	Mhe. Zaynab Matitu Vulu, Mb	–		Mjumbe
25.	Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb	–		Mjumbe
26.	Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb	–		Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashillilah, kwa ushauri wake kwa Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg Michael Chikokoto na Katibu wa Kamati, Ndugu Amina Salumu na Ndugu Susan Ngole na msaidizi wa Katibu Ndugu Elias Kyando. Pia tunawashukuru Watumishi kutoka Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Seraphin Tamba, Ndugu Evelyn Shibandiko na Ndugu Stephano Mbutu, pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

Hoja

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imefafanua matokeo ya uchambuzi kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, maoni ya Kamati na Mapendekezo yanayotokana na matokeo ya uchambuzi, kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, na kujadili ikiwa na Maoni na Mapendekezo ili hatimaye Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa Hoja.

.....
Mhe. Albert O. Ntabaliba, Mb

Mwenyekiti

Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

08 Februari, 2017

MWENYEKITI: Sasa Waheshimiwa Wabunge hoja mbili hizi tutazijadili kwa pamoja kama tulivyofanya kwa hoja zingine lakini wakati wa kuhitimisha mtaamua kila moja peke yake. Sasa tuna nusu hapa tunaweza tukaitumia vizuri tu, nina orodha ya wachangiaji ; kwanza tunaanza na Mheshimiwa Juma Nkamia atafuatia na Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ajiandae. Huwa napenda kuwa tunachanganya Bunge hili najua uwiano wa vyama lakini inapendeza kama tunachanganya ili tuwe na *balanced debate*. Tunaanza na Mheshimiwa Nkamia. *(Makofi)*

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi hii nichangie kidogo kwenye taarifa hii, lakini nitajikita zaidi kwenye taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na nimpungeze sana Mwenyekiti na Kamati yake hiyo, niseme Kamati zote mbili kwa kazi nzuri walioifanya ya kutuchambulia yale ambayo Kamati hizi zinatakiwa kufanya kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema Sera hii ya Viwanda ni jambo zuri sana kinadharia lakini utekelezaji wake ndio changamoto kubwa sana. Nadhani hata Mheshimiwa Rais mwenyewe anapata shida pia kwenye utekelezaji wake kwa sababu kaikuta tu kwenye ilani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ambalo siku zote najiuliza na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda yupo hapa ni vizuri akasikiliza. Tunapozungumza uchumi wa viwanda leo, hivi tulikuwa na viwanda vingapi; tumejiuliza kwa nini viwanda vile vilikufa? Kwa nini viwanda vile vilikufa *this is the basic question* ambayo lazima tujulize na tuje na *concrete research*; kutoka pale tunaweza kuanza kufikiria kujenga viwanda vipya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini tukisema tu nakuletea kiwanda leo, kesho, keshokutwa hatuwezi kwenda hivyo. Sidhani hata nchi zilizoendelea kiviwanda zinaenda katika *style* hiyo; tulikuwa na viwanda vingi MWATEX, MOTEX, lakini viwanda vimekufa; bila kujua aliyeya viwanda hivi tutaimba wimbo huu wa kuwa na Taifa la viwanda leo, kesho na hata milele. Leo tunazungumza kiwanda cha *General Tyre* utakifufuaje mpira huna? Uta-*import* mpira kutoka nje utatengeneza gurudumu utamuuzia nani na kwa bei gani? Haya ni maswali ambayo lazima tufike mahali tukae chini tujulize, tuje na majibu ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sera yetu tunasema tunajenga viwanda; nani anajenga Serikali au watu binafsi? Mfumo wa uchumi duniani sasa hivi, mimi sio mchumi lakini mfumo wa uchumi duniani sasa hivi unazilazimisha *third world countries* kupiga makofi kwa yale yanayoamuliwa na wakubwa. Leo tunasema watu wafanye *investment* Tanzania ya viwanda; tuna viwanda karibu 30 vya pamba lakini *raw material* zinazolingia kwenye viwanda vile hazitoshi. Tuna-*import* karibu asilimia 51 ya mafuta ya kula kutoka nje, viwanda vya mbegu za pamba ambavyo vingeweza kutoa mafuta havipati *material* ya kutosha kwa sababu uzalishaji wa pamba wenyewe umeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwenye mawese na alizeti; viwanda vipo vya kutosha, nadhani tuanze sasa pengine tuimarisha viwanda vilivyopo sasa badala ya kuanza kufikiria kujenga vingine. Kwa sababu wasiwasi wangu tukiendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda kwa kiwango kikubwa hata hivi ambavyo vipo tena navyo vitakufa. Kwa sababu mfumo wa soko duniani sasa hivi ni *competitive* lakini *how can you compete with a giant* katika uchumi. Hayo ni mambo ambayo lazima tuyaangalie sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza siku moja rafiki yangu, Mjomba wangu, Waziri wa Viwanda anasema amepata soko la mihogo china; sasa nikasema tunahamasisha kujenga viwanda halafu tena tunataka tuuze *raw material* nje, hivi viwanda vitafanyaje? Ni jambo la kukaa sisi kama Taifa tufanye maamuzi kwa lengo la kutoa nchi yetu hapa ilipo iende mahali. Nimetoa angalizo tu kwamba mfumo wa *globalization* duniani leo kwa *third world country* kama ya kwetu na tukawaomba hawa hawa wakubwa njooni mjenge viwanda, lazima tuwe *very careful*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu njooni na *concrete research* kwamba kwa nini viwanda hivi vilikufa; mkija nayo mkakaa mezani mka-*brainstorm* vya kutosha mtakuja na *policy* nzuri sana ya kuleta viwanda ambavyo kweli tunavihitaji. Leo ukimuuliza Mwijage hata ukikutana nae hapo mlangoni anakwambia nakuletea kiwanda, ukikutana nae *canteen* pale anakwambia nakuletea kiwanda; sasa hata bajeti yenyewe hivi viwanda anasema anakuletea hana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hapa imetuambia leo kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya hili zoezi haijatoka; lakini Waziri wa Viwanda yupo tayari kukuletea kiwanda. Sasa *I have been asking* kwamba hivi viwanda mnavyo kwenye mifuko ya makoti? Tusipowaambia ukweli tutakuwa tunadanganyana na sisi bila kusema ukweli hatuwezi kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unaweza kulalamikiwa hivi kwamba ukaonekana huyu jamaa mbona anasema sema vibaya, *no* lazima tuseme ukweli kwa lengo la kusaidia Taifa letu, lakini tukisema tu kwa sababu ya kufurahishana tutakuwa hatuendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu ilani ya uchaguzi ya Chama chetu imeweka mambo mengi sana nafikiri, samahani kwa siku zijazo hata vyama vya siasa ni vizuri mgombea Urais akapatikana kabla ilani hazijaandikwa. Kwa sababu matokeo yake hata Rais huyu amekuta ilani ina ahadi 148; hata ule utekelezaji ule wa milioni 50 kila Kijiji mpaka wakati mwingine namuonea huruma Rais; kwa sababu unakuta umeandikiwa vitu walioandika watu wengine wewe unaambiwa nenda katekeleze. Nadhani tufike mahali tuseme ukweli kwa lengo la kulisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la viwanda tunawashukuru sana Kamati mmefanya kazi nzuri sana lakini pia tuache siasa kwenye viwanda. Ukianza kusema nakuletea kiwanda huna kiwanda mfukoni, *don't do that*; mtapiga *sound* hapa *wee 20 years* inakaribia kuisha, kesho tutasema jiulizeni tu. Niombe Mheshimiwa Mwijage wewe baba mkwe sijui nani sielewi vizuri lakini tusaidie tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanye stadi nzuri ya mfumo wa uchumi duniani ulivyo sasa. Mkifanya utafiti wa kutosha kwamba mfumo wa uchumi duniani ukoje *then* unaweza kuja na hii *concrete idea* ukafika mahali ukasema tunachofanya hiki, ni hiki na hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho tu kwa mfano, viwanda vya kuchambua pamba, tuviimarisha vile ili mafuta haya yazalishwe hapa nchini, lakini pia tuwasaidie wakulima bila kuboresha kilimo tutaimba wimbo wa viwanda leo, kesho na kesho kutwa. Kila Kijiji leo tuna *extension officers* lakini wanasaidia wananchi wetu kwenye kilimo vipi? Bado wananchi wanamwaga mbegu na hawa ni waajiriwa wa Serikali na wanalipwa; kila mwisho wa mwezi kuna *extension officer* anapata mshahara, ana kazi gani zaidi ya kupima ng'ombe na anachukua maini, *they have nothing to do*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuboresha kilimo mfumo huu tunaouzungumza wa viwanda utatusumbua sana wazee wangu. Tukae chini tutafakari nchi yetu iweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nawashukuru kwa mara nyingine tena niwapongeze sana Timu ya Taifa ya Vijana Serengeti Boys kwa kufuzu kwa michezo ya *under seventeen* ya Afrika, hongera sana Mheshimiwa Nape na timu yako yote; sasa tujipange basi kuiandaa timu yetu kwa sababu hiyo nayo pia ni sehemu ya viwanda. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa. Tunaendelea Mheshimiwa Hawa Ghasia atafuatiwa na Mheshimiwa...

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika taarifa za Kamati hizi mbili. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa ajili ya kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kwanza wa miaka mitano wa maendeleo ulikuwa na lengo la kutoa vikwazo vya kimaendeleo ambavyo vilikuwepo kipindi kile ikiwa ni pamoja kuongeza upatikanaji wa umeme, kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli na barabara pamoja ya kuboresha bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Pili ambao tunao ambao una lengo la kuhakikisha kwamba tunakuwa na uchumi wa viwanda. Naliunga mkono sana hilo lakini wasiwasi wangu nahisi tunaweza tusifike mbali kwa sababu bado vile vikwazo ambavyo vilikuwepo katika mpango wa kwanza vinaelekea kwamba bado tunaendelea kuwa navyo na vingine si kwamba vikwazo halisi vipo lakini baadhi tu ya watu wanaamua kuvifanya viwe vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri wa Viwanda na Biashara, vile viwanda wanavyosema anatembea navyo mfukoni kwangu kwa kweli amenisaidia sana na tumefikia hatua nzuri. Nilimwomba kiwanda kwa ajili ya *sulphur* kwa sababu sisi kule ni wakulima wa korosho na *sulphur* kwa kiasi kikubwa tunaagiza kutoka nje, basi tuliomba angalau hata kufunga waje waifungie kule kwetu lakini pia tunaweza kutengeneza kwa sababu tunayo gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mwekezaji amekuja, Mtwara amekwenda, ardhi tumempatia sasa hivi yuko hatua za mwisho na nina imani kabisa huko *TIC* atamaliza lakini wasiwasi wangu ni upande wa nishati, upande wa upatikanaji wa gesi na upande wa umeme, ndiyo maana nikasema kwamba vile vikwazo bado vipo. Gesi inatoka Mtwara lakini mpaka tunapozungumza hapa tunavyo viwanda zaidi ya viwili, vingine vinashindwa kujengwa; bado Wizara haina nia ya dhati ya kusaidia wawekezaji kuwapatia gesi au kuwapatia umeme wale ambao wanataka kuwekeza Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu; mwakani tutakapokuwa tunajadili Kamati ya Viwanda na Biashara iunganishwe na Nishati na Madini kwa sababu tulikutoka tulikuwa na changamoto sana ya ardhi kwa wawekezaji wetu kwenye viwanda. Sasa hivi hatuna tatizo kwenye ardhi, hatuna tatizo na Wizara ya Viwanda na Biashara, tatizo kubwa lililopo ni upande wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara tunavyozungumza sasa hivi umeme ni wa shida, mitambo inakufa kila mara, megawati 18 zinazozalishwa mahitaji zimeshazidi megawati 18 na hatuoni mipango ya uhakika ya kuhakikisha tatizo hilo linakufa. Tunacho kiwanda cha mbolea, tayari wamekuja Wizara ya Viwanda na Biashara imewasaidia imetoa eneo lake la *EPZA*, Wizara ya Miundombinu wamejenga barabara ya lami mpaka katika hilo eneo, lakini mpaka sasa hivi watu wa Wizara ya Nishati hawajaonesha nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba kiwanda kile kinakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndani ya Serikali kwa mtazamo wangu, wenyewe kwa wenyewe wanakwamishana na kwa kiasi kikubwa nahisi hata vile viwanda tunavyovihisi kwamba viko mfukoni si ajabu vinakwama kwenye nishati. Kwa hiyo, tuseme bila kigugumizi kwamba Wizara ya Nishati isaidie Wizara nyingine katika kuhakikisha kwamba viwanda, kama uchumi wetu ni wa viwanda, nishati kwa kiasi kikubwa itatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini kwamba Mtwara ile mpaka sasa hivi hawajamuingizia umeme hata mtu mmoja, hawajamuingizia gesi hata mtu mmoja na wala hawana mpango. Pia nimuombe Waziri wa Viwanda na Biashara atuelezee mpango mkakati wa kuendeleza viwanda katika Mji wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo ardhi, eneo la EPZA, wengine wanalia fidia sisi fidia ilishatolewa tangu mwaka 2000, eneo lipo kuzunguka bandari, hakuna matatizo ya fidia wala nini, wanasubiriwa wawekezaji. Eneo ambalo Dangote amejenga kiwanda ni hekta 17,000, yeye amepewa 4,000 tu nyingine zipo za kumwaga hazihitaji fidia, hazihitaji kitu chochote, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara atuelezee na Waziri wa Nishati na Madini mikakati yao ya kuhakikisha gesi inatumika katika viwanda katika Mji wa Mtwara. Ni haki yetu watu wa Mtwara na sisi kupata maendeleo ya nchi hii na wala hatuombi *favour*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka nizingumzie, kama nilivyotangulia kusema eneo la EPZA Mtwara tunalo fidia ilishalipwa tangu kipindi cha Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, eneo lipo wazi. Sambamba na EPZA ya Mtwara, tunayo Kurasini, tunayo pale Benjamin Mkapa na katika mikoa maeneo mbalimbali, EPZA ndiyo njia rahisi kama walivyotangulia kusema, ya kuhakikisha nchi inaendelea kwa haraka. Watu wanakuja na mitaji yao, wanakuja na teknolojia yao, sisi tunachopata pale, kwanza tunapata ajira, tunapata teknolojia mpya na pia tunapata pesa za kigeni. Hivi kwa nini tusihakikishe kwamba hii EPZA inakwenda kwa kasi, hata China tunaosema wameendelea walianzia na EPZA, kule akina Shenzhen, maeneo mengi, akina Guangzhou, kote walianzia kama EPZA, kwa nini tusiige hayo mambo mazuri na sisi tukaweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wale wanaosema kwamba viwanda vile ambavyo vilibinafsishwa vihakikishe vinafanya kazi iliyokusudiwa. Kule kwetu Mtwara viwanda vya korosho watu walipewa kwa bei ya kutupa lakini hakuna hata mtu mmoja anayebangua korosho, wengi kazi yao wamefanya maghala wanayakodisha kipindi cha ununuzi wa korosho wanaona inawalipa kuliko kufanya viwanda, korosho zetu zinakwenda nje zikiwa hazijabanguuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kuhakikisha kwamba viwanda vile kama watu madhumuni waliyopewa, kwa sababu hawakupewa kwa bei ya soko, walipewa kwa bei ya kutupa, wahakikishe aidha, wafanye kazi iliyokusudiwa au wanyang'anywe wapewe watu wengine ili waweze kufanya kazi iliyokusudiwa. Haiwezekani kiwanda cha korosho leo kinageuzwa ghala la kuhifadhia korosho, kwa kweli hilo tulisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri wa Viwanda na Biashara, anahangaika katika kutafuta viwanda. Sisi kama Wabunge katika maeneo yetu lazima na sisi tumuunge mkono, amenipa mwekezaji nimekwenda naye nimeembeza katika maeneo yote

ya ardhi na akachagua eneo analolipenda na tumefikia hatua nzuri, nina uhakika kile kiwanda kitafika, lakini wasiwasi wangu Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Ardhi kwa sababu ili uweze kuwekeza vitu vikubwa muhimu ni ardhi, nishati na wenzetu hao Wizara ya Viwanda na Biashara ambao tunategemea waweke mazingira mazuri. Kwa sababu hawezi kujenga viwanda Waziri wa Viwanda na Biashara. Kazi ya Waziri wa Viwanda na Biashara ni kuweka mazingira mazuri ambayo anayaweka, Waziri wa Ardhi hana matatizo kwenye uwekezaji, ardhi, migogoro anatusaidia kutatua, lakini Nishati na Madini kwa kweli kama tunataka tuwe na uchumi wa viwanda Wizara ya Nishati na Madini kwa kweli iamke. Ndiyo tunapata umeme wa REA vijijini, lakini ule ni kuwasha tu vikoroboi badala ya vikoroboi sasa tunaleta *bulb*, tunahitaji umeme uzalishe, uinue uchumi wa nchi hii...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonist.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana...

MWENYEKITI: Aaah! Muda hautawezekana!

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu. Kwanza kabisa naomba ku-*declare interest* kwamba ni Mjumbe wa Kamati hii ya Viwanda na Biashara pamoja na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mwenyekiti wangu kwa uwasilisho wake mzuri, amewasilisha vizuri na kwa kweli aliyoyaeleza ndiyo ambayo Kamati imeyasema niko hapa tu kwa ajili ya kusisitiza kwa baadhi ya mambo fulani ambayo nadhani ni muhimu tukayasisitiza na Serikali ikajua na Bunge likatambua nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda na biashara kwanza ni suala mtambuka ambalo si kazi pekee inayomwelelea Waziri mhusika wa Viwanda na Biashara lakini ni suala mtambuka ambalo kama Serikali au nchi nzima kupitia sekta nyingine basi inabidi tushikamane bega kwa bega kuhakikisha kwamba tunaipeleka nchi yetu kwenda kwenye nchi ya viwanda kama Sera ya Chama cha Mapinduzi inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yamezungumzwa katika Kamati na katika kusisitiza, ni suala la upelekaji wa fedha za maendeleo katika Wizara zilivyopangiwa bajeti zake yaani katika Wizara husika. Kwa mfano, Wizara ya Viwanda na Biashara, pesa walizopata ni asilimia saba nukta tano tu na leo tuko *quarter* ya tatu tunakwenda kwenye *quarter* ya mwisho. Asilimia saba nukta tano Wizara ya Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais wenyewe hata sifuri, yaani hata *percent* kadhaa hawajapata wao ni sifuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kweli hii inawanyong'onyesha watendaji wetu na Serikali iangalie namna ya kupeleka pesa za maendeleo kwenye sekta husika kwa muda unaostahili ili kusudi yale yaliyopangwa yaweze kutekelezwa. Ucheleweshaji huu sijui Waziri atafanya muujiza wa namna gani, sijui watendaji watafanya miujiza ya namna gani, kazi wamepewa, pesa za mishahara wanapelekewa, pesa za mishahara wanakula lakini pesa za kufanyia kazi hawapati, ina maana kama pesa ya maendeleo haijaenda ina maana hawa wafanyakazi wanapewa mishahara ya bure. Tunataka pesa ziende kwa wakati ili waweze kutekeleza yale ambayo yamepangwa na yale ambayo yanatakiwa yatekelezwe kwa muda uliostahili au muda uliopangwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hii imeelezea kuhusu kodi, tunapiga kelele sana kuhusu kodi na tozo mbalimbali, tunaomba vyombo husika muangalie upya kuhusu hizi kodi na hasa kwenye kodi ya *capital investment*, kwenye *capital investment* kuna VAT, kuna VAT hadi kwenye vyombo vya Serikali. TBS anapokwenda kuagiza vifaa vya maabara ili aweze kukagua bidhaa mbalimbali kwa usalama wa Mtanzania, maabara zao wanapoagiza vifaa zinatozwa kodi ya VAT, haya masuala tunakwenda kwenye bajeti inayokuja wayaondoe, Serikali iondoe VAT kwenye kodi za maabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji mkubwa anayetaka kuwekeza kwenye kiwanda cha kukamua bidhaa za mkulima anapoagiza bidhaa kubwa kwa maana ya mashine za kuchakata bidhaa mbalimbali za kilimo na zenyewe ana kodi kubwa amewekewa, tunaomba hizi kodi ziondolewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya Sheria ya Manunuzi, ukienda pale TANELEC unakuta kabisa kwamba mmiliki wa TANELEC mmoja wa *shareholders* ni NDC na TANESCO ikiwemo, wana asilimia 10 mle ndani. Kutokana na Sheria hii ya Manunuzi inawafanya hawa TANELEC wakose biashara kwa TANESCO, yaani Mjumbe wa Bodi ya TANESCO ambaye ni Mkurugenzi wa TANESCO anaingia kwenye *Board of Directors* lakini biashara badala ya kuipa TANELEC ambayo yeye mwenyewe ndio mhusika mle ndani, TANESCO pamoja na REA wananunua transfoma na waya kutoka nje, wanaikosha biashara pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tumetazama katika nchi za jirani, tuliangalia *tender board* iliyotolewa kule Kenya kwenye shirika la umeme vilevile, wana-favour kampuni zao kwa kutoa tenda maalum kwamba tenda hii ijazwe na watu wanaofanya uzalishaji ndani ya nchi ile lakini sisi tunapeleka biashara nje. Sheria ya Manunuzi bado tunaendelea kuipigia kelele tuirekebishe na irekebishwe, kwa kweli inasikitisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme nilishaliongelea, umeme sio wa uhakika. *Quantity* na *quality* ya umeme wetu bado ni tatizo kubwa, hatuwezi kwenda kwenye viwanda kama umeme wetu unaendelea kukatika namna hii na uzalishaji ukawa ni wa shida na bado umeme wetu ni bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye bandari, bandari yetu ni kivutio kikubwa sana cha watu kufanya biashara na naomba niseme kwamba bandari ipo chini ya Wizara ya Miundombinu, lakini bandari utekelezaji wake kikubwa ni kufanya biashara. Biashara ndicho chanzo kikubwa cha kuwepo kwa bandari pale, lakini ufanisi wa biashara wa bandari yetu hauvutii na ndiyo maana watu wanakwenda kuwekeza au kutumia bandari nyingine za

jirani. Matatizo tumeyazungumza mengi – kuna *single customer territory*, tumeyaongea masuala ya kodi *on auxiliary goods*, yote tumekwishaongea, lakini ninachotaka kuzungumza leo, hata bandari yenyewe ndani ina matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama toka mwaka 2012 mpaka 2017 wakurugenzi wa bandari wamebadilishwa watano, alikuwepo mzee Mgawe, alikuwepo Kipande, Massawe, Matei na mpaka leo yupo Injinia Kakoko, kila siku wanabadilishwa, kwa watumiaji inatia wasiwasi. Ukimtazama hata huyu aliyepo sasa hivi Mheshimiwa *Engineer* Kakoko amefanya mabadiliko ndani ya bandari, katika ile *top management* kabadilisha watu saba, kamwondoa bwana Gawire Mkurugenzi wa Utumishi, kapiga chini, Kilian Kaimu Mkurugenzi wa TEHAMA kafukuza, Magesa Kaimu Mkurugenzi wa Utekelezaji kafukuza, bwana Masoud Kaimu Meneja wa Fedha kafukuza, bwana Muhanga Kaimu Meneja wa Bandari kafukuza, bwana Mosha Meneja Msaidizi wa Bandari kafukuza, bwana Macha Meneja wa Utumishi kafukuza. Cha ajabu kabisa badala ya kufukuza kuweka watu *competent*, kaondoa hapa Msaidizi *Operations Manager* katoa kaweka mlinzi kuwa *Operations Manager*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini, kuna siku atapakua mzigo kwenye bandari upande mmoja upande mwingine meli inazama, tuwe makini, haya mabadiliko yanatia wasiwasi, wafanyabiashara hawawezi kuja bandarini watakwenda sehemu nyingine, mtu wa *security* anakuwa *Operations Manager*, tunaomba tuwe *serious*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, meneja halipi watu *on time*. Wapakuaji wa mizigo, wanasema ile ni *casual labour*, wale wapakuaji hawana mkataba wa kupakua mizigo, sio wafanyakazi wa kudumu, wanapakua kama vibarua, wanapakua leo wapewe pesa zao leo, anayesafisha leo apewe pesa yake ya kibarua leo, Mheshimiwa huyu hawalipi wale watu alio-*outsourced*, wale watu wenye kampuni ambazo zinaendesha zile shughuli hawalipwi, wanalipwa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanamwandikia barua awalipe anachelewa kuwalipa, hapa nina barua amepokea tarehe 23, mwezi wa kwanza, wanamwomba tulipe hela. Kuna kampuni inawadai hawalipi, ina maana wale wapakuaji, huyu mwenye kampuni itafika atashindwa kupata *cash* ya kuwalipa watu *on a daily basis*, atakosa ile pesa na akikosa pesa wale wafanyakazi watagoma na wakigoma hiyo habari itatoka nje, itakwenda Congo, itakwenda na nchi nyingine kwamba wafanyakazi wa Bandari ya Dar es Salaam wamegoma hawajalipwa, *at the end of the day* watumiaji wa bandari wanakwenda Beira, watakwenda Durban, watakwenda Mombasa, haya ndiyo yanayotuletea matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Meneja wa Bandari mwingine katolewa Mhasibu kutoka TANROADS amekwenda kuwa meneja pale, *that's a professional job*, ni watu wataalam wanatakiwa wafanye zile kazi. Jana sikupata muda wa kuongea kwa watu wa miundombinu – chunguzeni hili, kuna kampuni nyingine pale zinaonewa, kuna wengine wamepewa kazi tatu, moja anapakua mizigo ya kontena wanamu-*underpay* kwa sababu ana kazi nyingine mbili, wana... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa mchana wa kwanza watakuwa hawa watatu; Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Joseph Haule na Mheshimiwa Abdallah Ulega.

Nina tangazo linatoka kwa Mheshimiwa Joseph Selasini, Mwenyekiti wa kikundi cha *St. Thomas Moore*; Waheshimiwa Wabunge Wakristo Wakatoliki leo Jumatano, tarehe 8 hii, kutakuwa na Ibada ya Misa mara tu baada ya kuahirishwa Bunge saa saba, saa hizi, katika Kanisa dogo lililopo ghorofa ya pili Ukumbi wa Msekwa, Wabunge wengine Wakristo tunakaribishwa kushiriki katika Ibada Takatifu. Aidha, kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya mara tu baada ya ibada hiyo. Kwa hiyo, ni ibada muhimu sana itakayofuatwa na tukio muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi leo saa kumi alasiri.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Wakati nasitisha shughuli za Bunge, nilikuwa nimeanza kutaja majina.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Miongozo si tulimaliza asubuhi? Eehh! Haya, Mheshimiwa ngoja tumalize niangalie sitaki kurudia rudia. Mheshimiwa Ulega.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia kanuni ya 68(7) nasimama hapa kuomba mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea leo na sisi Wabunge tumelipata kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia vyombo hivyo vya habari, iko taarifa kwamba Mkuu wetu wa Mkoa wa Dar es salaam, Mheshimiwa Paul Makonda ametoa kauli ambazo kwa namna moja ama nyingine zinaashiria na kuonesha dharau kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuko mstari wa mbele katika kuhakikisha tunapambana na kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye vita dhidi ya madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba, Sheria inayosimamia vita dhidi ya madawa ya kulevya imeundwa kwenye Bunge hili. Kama haitoshi, Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado tunayo kumbukumbu siku alipokuja kipenzi chetu, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na kutuhutubia

na tulimshangilia kwa makofi mengi sana alipotangaza rasmi kwa nguvu zake zote vita dhidi ya madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameambiwa ya kwamba hawana jambo isipokuwa wanakuja kufanya kazi ya kulala tu katika Bunge hili. Mimi ni kijana pia na ni mzalendo sana na Paul Makonda ni mdogo wangu na ni rafiki yangu pia, lakini ni lazima Bunge kama chombo huru kiendeleo kuheshimika na sisi tunadhani kwamba, mawili:- *(Makofi)*

- (i) Aidha, Kijana mwenzangu huyu hakuwa anajua anachokisema.
- (ii) Au amefanya dharau ya makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja zifuatazo ili iweze kunipa mwongozo na kuona tunakwendaje kutoka hapa tulipo ikizingatiwa kwamba sisi ndiyo nambari one wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika vita hii:-

- (i) Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Kassim Majaliwa Majaliwa akiwa kama kiongozi Mkuu wa Serikali achukue hatua za makusudi ili kutulindia heshima yetu kama Wabunge. *(Makofi)*
- (ii) Au kwa kutumia kanuni za Kibunge na sisi Bunge tunayo kanuni yetu ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge basi hatua zichukuliwe kupitia Mhimili huu ama atumie tena vyombo vilevile vya habari kusema kwamba amekosea na anaomba radhi. Naomba mwongozo huo, ahsante sana. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Toa hoja

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Huna haja ya hoja.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Ahsante sana...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa kwa heshima zote.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisikilize dakika moja tu.

MWENYEKITI: Hukuwepo lakini...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti dakika moja tu.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini nampongeza Mbunge mwenzetu ametoa hoja ya msingi sana na ningeomba kwa sababu hii hoja aliyotoa inahusu hadhi ya Bunge na ningeomba ingeenda kwenye kanuni ya 51 ili Wabunge tujadili kuhusiana na tabia ya Mkuu wa Mkoa huyu ambaye anadhailisha chombo hiki ambacho ni mhimili muhimu ambacho kinaweza ku-*balance*. Lengo ni ku-*balance* Serikali ifanye kazi, kwa hiyo ni hilo tu. Hoja aliyotoa Mbunge ni hoja ya msingi sana, naomba Wabunge tujadili kusudi hadhi ya Bunge iweze kulindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ili Wabunge waniunge mkono.

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba mketi basi. Waheshimiwa Wabunge nimepokea hili ombi la mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge wa Mkuranga na hii ambayo Mheshimiwa Msigwa ametaka kuchombeza kama hoja ya kujadili.

Mimi nitajielekeza kwenye ombi la mwongozo. Nimemwelewa Mheshimiwa Ulega maelezo yake mazuri tu sijapata bahati ya kusikiliza hayo maneno ambayo yamesemwa au yanadaiwa kusemwa na Mheshimiwa Makonda lakini kwa kiongozi kama huyu anayeomba mwongozo, kiongozi makini anayefahamu uzito wa namna ya kuongoza shughuli za Bunge na pia mihimili hii miwili au mitatu inayopaswa kufanya kazi. Niseme moja tu la jumla ambalo litasaidia na wananchi na humu namuingiza Mheshimiwa anayedaiwa kutamka hayo yaliyosemwa.

Kwa Watanzania, Mtanzania yeyote anayejisikia kwamba ameathirika na matamshi yaliyosemwa na mmoja wetu humu Bungeni au baadhi yetu kupitia kanuni hizi za Bunge, ana haki ya kuwasilisha malalamiko yake kwa Spika na suala lake linapokelewa kama tunavyolalamikiwa Wabunge na kupelekwa kwenye Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Sasa nadhani kumsaidia Mheshimiwa huyu na wengine wanaoona haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wanasema humu Bungeni, haipendezi kwenda nje na ukafytuka tu. Wewe kama unaona umeathirika muandikie Spika rasmi ukilalamika, ukieleza nini ili upate sasa angalau kusafishwa kupitia Kamati yetu na hatimaye Bunge lenyewe ndilo litakalojadili hilo.

Hilo nimeona niliseme la jumla kuwasaidia Watanzania wengine katika sura inayofanana na Mkuu wetu wa Mkoa wa Dar es salaam. Sasa kwa mwongozo ambao nimeombwa sasa, wala sitamfikisha PM (Paul Makonda) kwa hili, wala sitahitaji aombe radhi, hapana. Maana mpaka sasa hivi hayo mnayosema na ninyi mnasema mmesikia na mimi Mwenyekiti wenu nasema wala kusikia sijasikia, wala kuona, lakini kitu chochote ambacho kinakaribia au kinaonekana kudharau na kushusha hadhi ya Bunge hili hakikubaliki hata kidogo. (Makofi)

Bunge kama Taasisi na Wajumbe wake na ni mhimili miongoni mwa mihimili mitatu, lazima iendelee kuheshimiwa na mtu yeyote. Unaweza usinipende mimi lakini Taasisi hii lazima iheshimiwe na iendelee kuheshimiwa. (Makofi)

Sasa mwongozo wangu ni huu; Bunge hili katika umoja wake kama Taasisi lazima tulinde kwa wivu sana mamlaka tuliyonayo. Hata hivyo, kwa vile tumejiwekea utaratibu wetu kupitia kanuni za Bunge na tuna Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, ili sasa ikathibitike ameyasema hayo, kama ameyasema, ameyasemea wapi na lini? Pia kama yanaangukia ndani ya Sheria yetu ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, huko ndiyo ukweli wote utakapodhihirika.

Kwa hiyo, kwa suala hili naagiza; Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa taratibu zilizopo wamtake Mheshimiwa Mkuu wetu Mkoa wa Dar es Salaam atoe tu yale maelezo yake kama kweli amesema watayapokea, kama hakusema atasema hajasema ili sasa yale ambayo yatapokelewa na Katibu wa Bunge yapelekwe kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. (Makofi)

Tutakuwa tuko ndani ya taratibu zetu za kikanuni lakini pia ndani ya Sheria yenyewe ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge kwa sababu lazima ithibitike kama kweli inaangukia miongoni mwa haki za Bunge ambazo zinapaswa ziheshimike. Nadhani kwa hilo huo ndiyo mwongozo wangu Waheshimiwa Wabunge.

Narudia tena; chombo hiki lazima kiendelee kuheshimiwa na wananchi wote na sisi wenyewe kama Wajumbe wachombo hiki lazima tuishi na matendo yetu yafanane na hadhi ya Taasisi hii kama moja ya mihimili ya nchi yetu, huo ndiyo mwongozo wangu. Ahsanteni. (Makofi)

Barua ya Katibu wa Bunge ndiyo itakayosema ndani ya muda. Mimi nimeshatoa maelekezo hayo inaeleweka. Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Joseph Leonard Haule na atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Ulega. Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nichukue fursa hii kupongeza uamuzi uliouchukua, kiukweli tunaona mambo mengi yanaenda ndivyo sivyo napongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye hotuba yetu ya Kamati, kwanza, na-*declare interest* ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa hiyo mambo nitakayoyaongea hapa nayajua hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara mpaka tunavyoongea tarehe 31 Januari, 2017 tukiwa kwenye robo ya tatu, Wizara imepokea fedha ya maendeleo kutoka kwenye bajeti ya bilioni 42, imepokea bilioni 7.6 sawa na asilimia 18.6. Naongea hayo tukiwa

tumebakiza theluthi moja tu ya kumaliza mwaka, Wizara imepokea pesa ya maendeleo shilingi bilioni 7.6 nimesema hapa nimemwambia Waziri wa Viwanda mimi leo nitakutetea, una haki ya kuwa unapiga *propaganda* kwa sababu kiukweli hakuna chochote unachoweza kufanya bila kuwa na pesa, hakuna chochote unaweza kukifanya kwenye Wizara yako, kwenye idara zako bila kuwa na *fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea nini kama tunakuja hapa tena na bajeti ambayo imekuwa na ongezeko la asilimia 16. Kipindi cha mwaka 2015/2016 pesa ya maendeleo ilikuwa ni bilioni 35, Watu mmekuja hapa mnajinasibu kwa Serikali iliyopita ilikuwa imelala, sasa tunaongeza bajeti, mmeongeza bajeti kwa asilimia 16, tumeenda kwenye bilioni 42, lakini tunavyoongea leo katika robo ya tatu ni bilioni 7.6 tu zimepelekwa kwenye Wizara kama fedha za maendeleo. Swali najiuliza, *Are we still on the track?* Bado tupo kwenye mpango wetu wa kuleta maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu mtashangaa nitakachowaambia hiki. Mtukufu alivyokuwa katika ziara zake anahamasisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *Hostel* ambayo tunapongeza sana, alitoa ahadi kwamba atatoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa *hostel* za wanafunzi wa vyuo. Hatukatai, lakini tunarudi katika swali la msingi; hicho ndiyo tulichokuja Bungeni na kubajeti kwamba tunataka kufanya kama kipaumbele cha Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo *hostel* ambazo Mtukufu ameenda ametoa bilioni 10 kwa nyakati ambazo aliona zinafaa, lakini tupo tunaongelea Serikali ya viwanda, tunaongelea uchumi wa viwanda, bado wana bilioni 7.6 katika theluthi ya tatu. Tutamlaumu Waziri maskini ya Mungu, tutamsema sana lakini atafanya nini? Atasema nini? Turudi tuiulize Serikali bado tupo kwenye *track*? Bado tunataka kuendesha uchumi wa viwanda au zilikuwa ni *story* tu ambazo tulikuwa tunajinasibu kwa sababu ilikuwa Serikali mpya kwa hiyo tulitaka kuja na kitu kipya? Na kiukweli ndiyo hicho ninachokiona. Tulitaka kuja na kauli mbiu mpya japo kitu kilikuwa kile kile, *business as usual* na inaonekana katika *money value*. Tunaongelea mabadiliko yoyote, tunaongelea kutoka *stage* moja kwenda sehemu nyingine sasa tuko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo viwanda ambavyo Mheshimiwa Waziri anakuwa anafungua kila siku bahati mbaya sisi Kamati hatujui, ila kubwa zaidi ninachojua anafungua viwanda vya watu, viwanda vidogo vidogo vya watu binafsi kitu ambacho pia sio kibaya, lakini turudi kama Serikali yake sasa, Serikali inataka kufanya nini kama mkakati wa kuanzisha viwanda katika nchi yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu alikuja kwenye kamati yetu anaeleza kile kilichoitwa mkakati wa kufufua viwanda. Akatueleza katika kipindi cha mwaka mmoja mwaka ambao tupo sasa 2017...

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: kuhusu utaratibu, Kanuni ya 68.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu. Mheshimiwa, hebu keti kidogo. Kanuni ya ngapi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(1) inayozungumzia mambo yanayohusu utaratibu. Naomba isomwe kwa pamoja na Kanuni ya 64(1)(d) kwamba: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibaya ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge (d) inasema sasa hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.

MWENYEKITI: Endelea

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri anaendelea kuutoa Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Anatropia Theonest anarudia neno mtukufu mara kwa mara bila shaka akilenga kumaanisha Mheshimiwa Rais. Nadhani neno hili la "Mtukufu" kwa sababu analisema kwa muktadha wa kutaja maagizo aliyoyatoa Mheshimiwa Rais alipokuwa anazindua mradi wa ujenzi wa *hostel* pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa maana hiyo, anamaanisha kumkejeli Mheshimiwa Rais kwa kutumia neno "Mtukufu" jambo ambalo nadhani si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nimesimama kwa sababu nadhani Mheshimiwa Mbunge amevunja Kanuni hii na hivyo naomba umwelekeze ayaondoe hayo maneno ili yasiingie kwenye *Hansard*. Ahsante.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MWENYEKITI: Uamuzi wangu kwa hilo suala ni ufuatao: Mheshimiwa unayechangia, Mheshimiwa Anatropia, tumia neno Mtukufu Rais au Rais. Hayo ndiyo maelekezo yangu. Usipopenda kutumia Mtukufu Rais au Mheshimiwa Rais nitakutaka sasa ufute tu hayo utakayoanza, endelea. *(Makofi)*

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitakariri vizuri, Mtukufu Rais wakati anazindua majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliahidi atatoa bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa chuo. Sasa swali linakuja? *Track* na mchezo wetu na wimbo wetu hapa Bungeni ilikuwa ni viwanda lakini katika theluthi ya tatu ya viwanda yenyewe, Wizara husika imepewa tu, bilioni 7.6 ikiwa chini ya pesa alizotoa Mtukufu Rais alivyoshawishiwa na maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda Waziri anikumbushe vizuri, kama bado tuko kwenye wimbo ule ule au tumebadilisha kauli na sasa tuko kwenye kitu kingine kama sera yetu ya Awamu ya Tano. Nimekwenda kwenye mkakati wa viwanda aliowasilisha Katibu Mkuu kwenye Wizara yetu ni kwamba; kwa Mwaka huu wa Fedha na pesa waliyoipata wameweza kufufua kiwanda kimoja tu, kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, kwa vile bado miaka minne, tutarajie kwa pace iliyopo tutaweza kuwa na viwanda vitano tu! Hii tunasema ni Serikali ya viwanda, sasa swali, je, kauli mbiu tulizokuwa tunaziimba za nchi ya viwanda zilikuwa sahihi au tulikuwa tunawahadaa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tumeuliza juu ya Sera, ni Sera gani tuliyonayo kama nchi? Bado tuko kwenye Sera ya Ujamaa na Kujitegemea, tuko kwenye Sera ya Ubepari? Bado hata sisi wenyewe hata kauli mbiu ya nchi yetu hatuelewi tuko sehemu gani. Hilo swali tumeliuliza katika Kamati yetu. Tunakuja hapa tunasema sisi kama Serikali tunaenda kuwekeza kwenye viwanda, sisi kama Serikali tuna uwezo wa kuwekeza kwenye viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza Mbunge mwenzangu; tumejiuliza ni kwa nini viwanda vyetu vilishindwa katika Awamu zilizopita na bado tunajidanganya kwamba tuna uwezo wa kuwekeza kwenye viwanda. Tukae chini tujiulize, Sera yetu ni nini? Ujamaa na Kujitegemea au tunaacha watu binafsi wawekeze kwenye viwanda. Kama tunataka watu binafsi wawekeze kwenye viwanda tumejiandaa vipi kuondoa kero ambazo zimekuwa zinawasibu na kurudisha viwanda nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye kero mbalimbali ambazo wafanyabiashara wanapitia. Tumeandaa mazingira gani mazuri ya kuvutia wawekezaji wakati hapa nchini wafanyabiashara na wawekezaji wadogo tunawaona ni wapiga *deal* tu, leo sasa imekuja kauli mpya, wanaonekana kama ndiyo wanafanya biashara haramu. Sera zetu ni zipi kuhusu wawekezaji, hilo ndilo swali la tatu tunalopaswa kujiuliza juu ya mazingira rafiki. Nitaomba muda wangu ulindwe kwa sababu kuna mtu alitumia vibaya tena kwa makusudi! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira rafiki ya viwanda. Kuondoa tozo mbalimbali, kuweka *one stop center*. Nimeongea hapa Bungeni na narudia leo, tuwekeni *one stop center* na sio *one collection center*, kitu ambacho tunacho leo ni *one collection center*. Unaenda pale unawakuta Idara mbalimbali lakini wapo hawawezi kutoa maamuzi. Mtu yupo kama *representative* na inapokuja kwenye kufanya maamuzi anasema ngoja nimpigie bosu wangu. Sasa tunachokitaka ni *one stop center* na sio *one collection center* kama ilivyo leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi; kuna titiri mbalimbali za utozaji wa kodi. Unaenda *TBS* unaenda, *TFDA*, unaenda *OSHA* na vitu vingine ambavyo vinafanya kazi zile zile *more or less the same function* na tunasema kwenye Kamati tunataka mpango mkakati wa *ku-harmonize* hizi taasisi, hizi *regulatory authority* – tuwe na vitu vichache ambavyo vinapunguza kero kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi na inayosikitisha zaidi, *TBS* wanalalamika, *TFDA* wanalalamika, wanavyotaka kuingiza mashine za maabara wanatozwa pesa nyingi sana kama tozo ya ile mizigo inayoingia nchini na tunaomba sasa tozo zile zitolewe au zipunguzwe ili waweze kuingiza mashine za kutosha kwa ajili ya kuleta ufanisi ili kupunguza pia gharama za kupima vile vitu ambavyo wanapima kama *whatever!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni miradi ya kuchochea maendeleo. Tangu nikiwa mwanafunzi wa shule nasikia mnaongelea Liganga na Mchuchuma. Nataka Waziri atuambie, hiyo *story* mwisho lini? Hii Serikali inayotuongopea na Hapa Kazi Tu ina mipango mikakati gani ya kumaliza ujenzi wa viwanda vya Liganga na Mchuchuma kama vichochezi vya kiuchumi wa miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiona leo ni Mtukufu Rais kama mlivyosema akifanya ziara sehemu fulani akaona kuna changamoto ya barabara anaagiza barabara fulani itengenezwe kitu ambacho sisemi kama ni kibaya, lakini lazima tujikite katika kujenga miundombinu ambayo ita-link viwanda, maeneo ya uwekezaji na itawezesha ufanyaji wa biashara na mazingira mazuri kwa maana ya miundombinu katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuongezeka kwa riba ya yale maeneo ambayo yalikuwa yametengwa kama maeneo ya uwekezaji, EPZA. Tunavyozidi kuchelewa kulipa fidia ya maeneo hayo ndiyo gharama ya haya maeneo yanavyozidi kupanda. Amesema Mwenyekiti wa Kamati ilianza ikiwa bilioni 60, mwaka jana ilikuwa bilioni 191 na yeye amemaliza kusema hajui mwaka huu tutaambia ni bilioni ngapi, *who knows* pengine itakuja bilioni 300! Swali ni je, bado tuko kwenye *the same track* ya kutaka kuwekeza? Nini vipaumbele na mawazo yetu juu ya kuwekeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu anasema wanataka waanzishe EPZA, maeneo maalum ya uwekezaji. Sasa maeneo maalum ya uwekezaji yanazidi kubaki kuwa ndotoni kwa sababu uhalisia haupo, maeneo hayajalipiwa fidia, hakuna hata ndoto ya kupata pesa ya kulipia fidia halafu tunakuja hapa tunasema Serikali ya viwanda. Ni lazima tujipange upya na tuamue tunataka kufanya nini kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi hatuwezi kuwekeza kwenye viwanda, tuandae Sera, mazingira, mazuri ya watu wengine kuwekeza. Kuna watu wanaosaidia kuleta ushindani katika kuwekeza, mfano *fair competition* kuna taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na *Fair Competition Commission*. Wanakuja kutuambia wana wafanyakazi 53 tu na sio hao tu kuna TBS, kuna wafanyakazi, kuna idadi chache sana ya wafanyakazi na wale wanapaswa kufanya kazi nchi nzima. Tunategemea wale watu wafanye kazi kwa miujiza na wanachodai ni kwamba hawapati vibali vya kuajiri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, atafuatwa na Mheshimiwa Ulega.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niweze kuchangia kidogo katika hoja hii muhimu iliyokuwa mbele yetu. Kwanza na-*declare*, ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na nimeshiriki kikamilifu na nipongeze sana hotuba hii ya Kamati kwa asilimia zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya ziara kadhaa katika mashirika kadhaa ya umma lakini pia tuliweza kufanya ziara kadhaa katika makampuni hapa na pale ili kuangalia uwekezaji ambao taifa letu imefanya. Nishukuru sana Mashirika hayo aliyoonesha ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza nijikite moja kwa moja katika hoja iliyopo ambapo bado inaonekana kuna tatizo kubwa sana la kusaini mikataba ambayo taasisi zetu za umma zimekuwa zikifanya na wawekezaji mbalimbali. Mfano; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

kilisaini mkataba na kampuni kutoka Botswana inaitwa Mlimani GH na mkataba huo ni wa miaka 50 ambapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Serikali itakuwa inapata asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha jinsi gani ambavyo tumekuwa tukisaini mikataba hiyo, lakini pia inaonesha kwamba baada ya matumizi hayo na uwekezaji huo na Serikali kupata hiyo asilimia 10 baada ya miaka 50 ndiyo Serikali itakuja kunufaika na kupewa hayo majengo. Kwa mtaji huo tunarudi kule kule kwenye *business as usual* kwa sababu hakuna mtu ana *guarantee* kwamba Mlimani City kwenye miaka 50 ijayo itakuwa kwenye hali gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii inapelekea Taifa letu kukosa magawio, lakini pia imekuwa ikipata hasara kubwa na kushindwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na mwisho wa siku kuleta mzigo mzito sana kwa Watanzania. Kwa hiyo, moja kati ya Kamati ilipopitia na kuona, imeona kwamba mkataba kama huu uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam umekuwa ni mkataba ambao ni mzigo mzito sana kwa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tangu sijawa Mbunge wa Mikumi, nilikuwa nikisikia mkataba uliokuwa ukiendelea kati ya TANESCO na IPTL, tunaweza kuona kwamba mkataba huu pia umeonekana kuwa mzigo mzito na sisi tulikuwa tukisikia katika Bunge la 2014, Novemba. Bunge hili liliamua kwamba ule mkataba usitishwe na zile mali ziweze kutaifishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri atakapokuja hapa tuweze kujua mkataba huo umeishia wapi kwa sababu umeonekana kuwa mzigo mzito sana kwa Watanzania, kwa sababu Tanzania inaonekana kulipa shilingi milioni 300 kwa IPTL. Kwa hiyo, inaonekanaka milioni 300 kwa siku, ni mzigo mkubwa sana kwa Taifa letu ambalo kila siku tunasema bado liko kwenye hali ya checheme checheme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hiyo, mashirika mengi ya umma yamekuwa yakiilalamikia Serikali, imekuwa ikiyapa madeni mazito, inakopa katika masuala haya ya msingi. Mfano, katika taasisi za umma kama TANESCO, inaidai Serikali pesa nyingi, lakini pia suala la maji safi na taka inadai pesa nyingi. Vile vile mifuko ya kijamii imekuwa ikidai pia pesa nyingi sana kwa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Juni 2016 imeonekana kwamba Serikali inadaiwa trilioni mbili nukta sita na PSPF. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi gani Serikali imekuwa ikipeleka mizigo mizito sana kwa hii mifuko ya kijamii ambayo sasa ili kuweza kututumka imeanza kupeleka hili gao la mafao sasa hivi watu wanaambiwa mpaka wafikishe miaka 55. Mpaka hapa ninavyoongea nimepigiwa simu na watu wangu wa Kilombero Sugar Company wananiambia walikuwa wakitaka kusaini na PPF kwenye fomu zao lakini wameambiwa wasubiri mpaka miaka 55. Huo ni mzigo mzito sana kwa Watanzania ndugu zangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iweze kulipa madeni yake ambayo inadaiwa na taasisi zake. Hiyo nimetaja mfano tu wa PSPF lakini mifuko mingi ya kijamii inaonekana kukopwa na Serikali bila kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, tunajaribu kuangalia migongano ya Sera na Sheria. TR ndiyo msimamizi wa mashirika yote ya umma lakini inaonekana mifuko hii ya kijamii inapotaka kwenda kufanya manunuzi au inapotaka kufanya michanganuo ya kujiendesha na

kuweka uwekezaji imekuwa ikipata miongozo kutoka sehemu tofauti. Mara huku wanaambiwa na BOT, mara huku wanaitwa na SSRA miluzi mingi inampoteza mbwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko hii ya jamiii inaonekana kwamba inashindwa jinsi ya kwenda kwa sababu TR anakuwa hana taarifa rasmi za kuhusu uwekezaji unaotaka kufanyika kwa sababu viongozi wa sehemu mbalimbali wakiwemo BOT pamoja na SSRA wameonekana kuwa wakitoa miongozo tofauti kitu ambacho kinapelekea mashirika haya kwenda kununua bidhaa au kununua viwanja na ardhi kwa bei kubwa ambayo inapelekea mashirika haya yajenge nyumba kwa pesa nyingi ambazo mwisho wa siku Mtanzania maskini ndiyo anataabika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Shirika la Nyumba kama NHC linataka kujenga nyumba ambazo zitakuwa na uwezo na kumfanya mwananchi wa kawaida aweze kumudu lakini kwa gharama ambazo zipo hadi sisi Wabunge tunaanza ku-beep kwamba jinsi gani tunaweza tukanunua hizo nyumba hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo nyumba zinazosemwa za bei nafuu tumeenda kukagua juzi mradi wa NHC kule Chamazi ni hela nyingi sana ambayo kiukweli kwa maskini wa Kitanzania itakuwa ngumu sana kuweza kuchukua nyumba kama hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana pamoja na yote, lakini pia kwenye Bodi za Wakurugenzi wameonekana wakichaguliwa watu ambao hawana uwezo kiasi kwamba wanapeleka mashirika mengi kufa na mashirika mengine pia kuweza kuwa na watendaji ambao ni wabovu. Wakurugenzi wengi wanaoteuliwa wanateuliwa kirafikirafiki na wengine wanapewa ahsante ahsante, kitu ambacho kinapelekea mashirika yetu ya muhimu kwa Taifa letu kuweza kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo tunashauri upatikanaji wa Watendaji hao uweze kufanyika kwa *recruitment* ili waweze kushindanishwa na wafanyiwe *interview* ili majina matatu yaweze kupeleka kwenye mamlaka ambazo zinaweza kuteua mmoja atakayekuwa na tija na kusaidia mashirika yetu ya umma kwa ajili ya kwenda kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mambo mengine yanayosumbua ni pamoja na wanasiasa kuingilia mashirika haya ya umma ambayo mengine yanafanya biashara. Utasikia kuna miongozo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara fulani mara Naibu Waziri anasema hiki na hiki, fungu liende huku, kitu ambacho kinapelekea matatizo makubwa sana kwenye haya mashirika yetu ya umma na kufanya mengi yaweze ku-*stuck* na kushindwa kuendelea na kazi ambayo wamekuwa wakiifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nisisitize tunahitaji kuwaachia watendaji wetu wakuu ambao tumewapa madaraka na mamlaka ya kuweza kuongoza ili waweze kutupeleka kwenye sehemu nzuri itakayopeleka uwekezaji wenye tija kwa sababu tumeshuhudia sehemu mbalimbali watendaji hao walikuwa wanafanya kazi chini ya kiwango lakini tumeendelea kucheka na nyani na mwisho wake Tanzania inaendelea kuvuna mabua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana ndugu zangu nitakapokuja hapa mtupe majibu jinsi gani ambavyo mtaweza kuwezesha Ofisi ya TR ili aweze kuwa na meno na nguvu ya kuweza kuyasimamia mashirika haya ambayo sasa hivi madaraka yake TR anaonekana kuwa ameporwa na sasa hivi anafanya kazi nusu nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ndiyo Mzee!

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Ulega, atafuatiwa na Mheshimiwa Leonidas Gama na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajjandae.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika mjadala huu unaohusu Kamati yetu ya Viwanda na Biashara na Mazingira lakini nikienda sambamba na ile ya Mitaji na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue fursa hii kupongeza sana Kamati yetu, imefanya kazi nzuri yenye kupendeza ambayo imeeleza mambo mbalimbali hasa hii ya Viwanda na Biashara ambayo ningependa nijielekeze kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naomba niwe shuhuda mzuri sana wa Tanzania ya viwanda. Katika Jimbo langu la Mkuranga mpaka sasa nina viwanda 56 vyenye kufanya kazi na nina viwanda 11 ambavyo wakati wowote vitakamilika. Katika hivyo 11, kimoja ni kile kipya na kikubwa kushinda vyote katika Afrika Mashariki na Kati, kiwanda cha *tiles* ambapo tutakuwa na uhakika sasa wa kutokuagiza *tiles* kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa na uwezo sisi wenyewe katika nchi yetu kupata huduma hii bila kuagiza kutoka mahali kokote. Kwa fursa hii kwa kweli kabisa napenda niipongeze sana Serikali yetu kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kuwavutia wawekezaji wale na wakaja katika Jimbo letu la Mkuranga na kuwekeza pesa zao nyingi kabisa juu ya kujenga kiwanda hiki kikubwa cha *tiles*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli uwepo wa viwanda umetuinulia sana uchumi wetu sisi watu wa Mkuranga na nchi kwa ujumla wake. Mwaka jana 2016/2017 mwaka huu ambao tunamalizana nao tuliweka kadirio la kupata *service levy* isiyopungua milioni 500 na sasa tutakuwa na uhakika wa kupata *service levy* isiyopungua bilioni moja katika huu mwaka wa 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima niseme ukweli na hapa ndipo nilipokuwa nataka nisisitize sana, kwamba bado tunayo fursa kubwa zaidi ya kuwa na viwanda vingi zaidi, hasa hususani katika Jimbo la Mkuranga na sehemu zingine katika nchi. Kazi kubwa ambayo ningependa niiseme hapa ni kwa wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini, wajitahidi sana katika kuhakikisha nishati hii ya gesi, ya umeme, iweze kuwa ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimekikosa kiwanda pale Mkuranga cha kutengeneza nguo katika eneo la Dundani. Mwekezaji amekuwa yuko tayari kabisa ataajiri vijana wasiopungua 14,000 lakini sharti la kwanza anataka umeme wa uhakika. Sasa pamoja na jitihada kubwa sana za kuwavuta wawekezaji zinazofanyika na wao wanaitikia, lakini bado tunayo changamoto kubwa ya nishati. Kwa hivyo wenzetu wa nishati wajitahidi wahakikishe mipango yao ya kusambaza gesi katika viwanda vyetu iende sambamba na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani katika viwanda hivi vyote 56 hakuna kiwanda hata kimoja leo kinachotumia gesi na hilo bomba la gesi limepita hapo hapo Mkuranga. Kwa hivyo wenzetu ni lazima watuambie; nimemsikia Naibu Waziri asubuhi anasema kuna zaidi ya bilioni tano ambazo zitaelekezwa katika kwenda kusambaza gesi majumbani katika maeneo ya Tabata na Sinza na kwingine kule Dar es Salaam, lakini hakueleza ni kiasi gani cha fedha ambacho kitatumika kwenda kutengeneza mtandao wa mabomba ya kusambaza gesi katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kupata huduma hii ya nishati kwa bei nzuri na hatimaye uzalishaji wa bidhaa katika viwanda vile uwe ni wa gharama nafuu na hatimaye kumsaidia Mtanzania mlaji wa zile bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vile ili aweze kupata zile bidhaa kwa bei nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu alipokuja katika kiwanda cha Bakhresa aliagiza jambo hili, aliagiza kwa sababu watu Bakhresa *food industry* wameomba wapate gesi kwa muda mrefu na bado hawajafanikiwa mpaka hivi sasa. Jambo ambalo linapelekea uzalishaji wa bidhaa katika viwanda mbalimbali katika maeneo yetu unakuwa ni wa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tuwaombe wenzetu watuambie ni namna gani, viwanda viko vingi sana, vinaingia kila siku ya Mwenyezi Mungu lakini je, tumetengeneza mazingira ya namna gani ya kuweza kuvisaidia kupata huduma hii ya gesi na nishati kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana nawashauri na kuwaomba wenzetu hawa wa nishati na madini waone umuhimu wa kuiweka Mkuranga kuwa hata na *substation* yake ya umeme, uwezekano huo upo na wala hakuna tatizo lolote la eneo wala hakuna tatizo lolote la upatikanaji wa gesi. Gesi *tap* ziko pale *valve* namba 12 na 13 katika maeneo ya Mbezi na Mkiu zinapatikana kwa wingi kwa hivyo tunawaombeni sana mtuweke *substation* pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu wa viwanda ni lazima kama ilivyopendekezwa na Kamati katika ukurasa wake wa 50 juu ya elimu ya ufundi. Vijana wetu wengi sana wanakwenda kuwa vibarua katika viwanda hivi, lakini tunaomba sasa ikiwezekana na wenzetu wa elimu muone umuhimu wa maeneo kama haya ya viwanda kuyapa uwezekano wa kuwa

na vyuo vya elimu, ili vijana wetu waweze kupata elimu na hatimaye waweze kwenda kuwa na uwezo wa kwenda kuajiriwa katika viwanda vile. Hivi sasa unaweza ukakuta ni asilimia ndogo sana ya vijana wa Mkuranga ambao wanafanya kazi katika viwanda hivyo. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri anayehusika pia alitazame hili jambo kama ilivyopendekezwa na Kamati yetu ya Viwanda na Biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza ningeomba sana masuala haya ya ukuaji wa viwanda na sisi tumejiandaa vizuri na tayari maeneo yapo ya kutosha. Mathalani tunalo eneo pale katika Kijiji cha Dundani, zaidi ya ekari 700 na Waziri wetu wa Viwanda na Biashara amekuwa akilitaja kila mara. Sasa afanye kazi ya kuhakikisha wananchi wale zaidi ya miaka minne sasa, asiwe anakuja tu kaka yangu Mwijage kulitangaza lile eneo, awalipe fedha za fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wamezuiwa kufanya chochote katika eneo lao, sasa ni miaka minne hawawezi kuendeleza chochote, hawazalishi chochote, hawasafishi maeneo yao ni kwa sababu wamejitolea eneo lao lile liwe ni eneo la viwanda. Sasa wale wananchi wamekata tamaa, ni lazima tuone ni namna gani *either* hawa wa Mkuranga au ni kwingineko kokote katika nchi watu walikojitolea katika kuhakikisha kwamba Tanzania ya viwanda inapatikana, basi mambo haya yakamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nisisitize tena kwa mara nyingine juu ya kupatikana kwa nishati ya gesi katika viwanda vyetu ili uzalishaji uwe wa gharama nafuu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kama nilivyosema atafuatiwa na Mheshimiwa Gama na Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kukushukuru wewe kwa jinsi unavyoongoza Bunge vizuri, lakini pia kwa jinsi unavyotoa matumaini ya kuendelea kulinda nyumba yako hii kwa adabu na heshima kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 nilipata nafasi ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Katika kampeni zangu, katika matembezi yangu ya ndani ya jimbo kwa maana ya ziara, wanachi wa Jimbo la Chalinze walikuwa wanalalamika sana juu ya uwepo wa ajira. Kwa maana walikuwa wanahitaji sana ziweze kupatikana fursa ambazo zinaweza zikawaajiri. Katika Jimbo la Chalinze kwa kuwa wewe mtani wangu unasimama simama sana Kiwangwa unajua tunazo *raw material* za kutosha, lakini viwanda hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii miaka miwili baadaye, ninaposimama hapa, furaha kubwa niliyonayo ni kwamba baada ya miezi isiyopungua mitatu kuanzia leo tutawaalikeni Wabunge ninyi wote akiwepo Mheshimiwa Rais wetu kuja kufungua kiwanda kikubwa cha kuchakata matunda katika Halmashauri ya Chalinze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeanza kusema hivyo? Kwa sababu tunatambua kwamba sera yetu ya kuwa na Tanzania ya viwanda, ndugu zangu Wabunge wenzangu haiwezi kufanikiwa kwa kumwagalia Bwana Mwijage anavyofanya kazi. Nataka niwaambieni ukweli kabisa, Bwana Mwijage, Mheshimiwa Waziri yeye ni sehemu ya kusukuma mambo hayo; kama ninyi Wabunge hamtokuwa wajanja kutumia mazingira yenu, kutumia mazingira ya maeneo tuliyonayo na kuyageuza yawe fursa, ili Serikali ije kutusaidia kuhakikisha kwamba mambo yake tunayoyataka sisi na wananchi wetu yanafanikiwa; hii sera ya viwanda itakuwa ni sera ambayo hatuiishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Chalinze kwetu sisi tuna fursa kubwa sana, mojawapo ni kuwa na *logistic center*, lakini *logistic center* ambayo siyo tu kwamba itakuwa inakuja ni kama sehemu ya kufanyia biashara ya kubadilishana vitu, pia sehemu ambayo watu watakuwa wanapitishia mizigo, na fursa mbalimbali. Wanachalinze wametenga maeneo, Mheshimiwa Waziri Mwijage akishirikiana na watalaam wake katika Wizara yake nimshukuru sana, ametupa ushirikaino mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba yale mawazo ambayo siku zote tumekuwa tunayalilia wanachalinze yanafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninaposimama hapa *logistic center* ya Chalinze inawezekana. Kiwanda kikubwa cha *tiles* kimeshafunguliwa na sasa ujenzi unaendelea vizuri, lakini sio hilo tu kama nilivyosema kwamba sehemu kubwa ya kufanya biashara kwa kingereza sijui wanaitaje maana yake kwa Kikwere tunasema makutano ya biashara. *Logistic center* ndio mnavyoita?

MBUNGE FULANI : Eeh!

MHE. RIDHIWANI J.KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mama Nagu ameongea *logistic center* kwa Kimbulu wanavyoita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanaweza kufanikiwa kwa sababu Serikali yetu inatuunga mkono katika hilo na mimi binafsi bila hata ya aibu niishukuru sana Serikali, kwa sababu kilio cha Wanachalinze kinaweza kupatiwa jibu. Mheshimiwa Lukuvi nimshukuru pia maana kulikuwa na figisu pia pale la upatikanaji wa ardhi, lakini pia kodi kubwa za ardhi. lakini ule utaratibu wa kurasimisha ardhi, toka kwenye mamlaka ya kijiji ili sasa itoke iende kuwa sehemu tengefu kwa ajili ya viwanda nalo pia linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu ninao ushuhuda huo. Pamoja na hayo pia ziko changamoto ambazo Serikali yetu ni lazima iziangalie tunapokwenda kutimiza yale malengo ambayo tumejipangia ya kuwa na Serikali ya viwanda au kuwa na Tanzania ya viwanda. Kwa mfano moja ya tatizo kubwa ambalo Wabunge wengi wamelalamikia hapa ni jambo zima la upatikanaji wa nguvu ya nishati, kwa maana ya umeme. Tumeshuhudia kwa mfano wenzetu hasa kule kwa wajomba zangu Lindi na Mtwara wanalalamika kwamba umeme unatoka kwa siku masaa manne manne, wanasema kila baada ya dakika 20 kama sio dakika 80 umeme unakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tanzania tunayoitaka ya viwanda, moja ya jambo kubwa ambalo lazima tujihakikishie hapa na kama hili hatutakuwa na hakika nalo hii sera ya

viwanda itakuwa ni hadithi isiyokuwa na mwisho, au hadithi isiyokuwa na majibu kama umeme wa kutosha wa uhakika hautopatikana katika Tanzania. Mheshimiwa Waziri Muhongo alitueleza kwamba katika upande wa gesi, bado michakato ya kuendelea kusambaza gesi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wametuingia kwamba gesi itakuja hadi huku Dodoma, lakini pamoja na hayo yale maeneo ambayo yamekwishaanza shughuli za viwanda, ni lazima yapewe kipaumbele ili kuhakikisha kwamba sera ile inatimia kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mheshimiwa Hawa Ghasia Mbunge wa kule Mtwara ameeleza hapa, juu ya jinsi ambavyo mahitaji ya gesi na umeme yanatakiwa kule Mtwara. Pia Mheshimiwa Mwijage wewe mwenyewe umekuja umeona, kiwanda kile mzee, cha kilometa moja, kiwanda ambacho kitakuwa na *line of processing* mbili, kama hakuna umeme pale itakuwa ni kazi bure na ndoto zako ambazo kila siku umekaa unapiga kelele mpaka wengine ndugu zako akina Nkamia hapa hawaamini, kwa sababu wanaona ni kama hadithi hivi hazitofanikiwa. Kaa vizuri na Mheshimiwa Waziri Muhongo, zungumzeni jambo la sera ya umeme, zungumzeni tuone mambo siyo kwamba yanasemwasemwa tu lakini tuone mambo ambayo yanakwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mnazungumzia kuweka treni ya umeme, Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie mimi mwenyewe ni mshabiki sana wa kupanda vitu hivyo lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri, treni ya umeme hiyo mnayoizungumza na *consumption* ya umeme ambayo inatakiwa kwa ajili ya kuendesha chombo hicho na kukatikatika kwa umeme kunakotokea kila siku sina hakika sana kama tunaweza tukafanikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote Serikali imedhamiria kuhakikisha kwamba ajira zinapatikana katika maeneo hayo. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kipaumbele cha kwanza katika ajira hizo, mnapokaa na hao wawekezaji waambieni wawape kipaumbele cha kwanza wale wakazi wa maeneo yale. Kwa sababu haiwezekani ikajengwa kiwanda kikubwa kama kile pale Chalinze halafu ajira tukasikia wanatoka vijana Dar es Salaam sijui wapi hili jambo haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nitumie nafasi nyingine pia kumwomba sana Mheshimiwa Waziri hebu hii sera ya viwanda isimamie vizuri *brother*, kwa sababu kama mambo yakienda vizuri katika viwanda, nina uhakika kuna nyanja nyingi sana ambazo zitakuwa zimekaa vizuri. Kwa mfano viwanda vinahitaji maji, sijajua kwa maji haya yanayosuasua ambayo mpaka leo wana Chalinze bado hawajaelewa tutafikia lini ule mtandao wa maji ukaweza kusaidia watu wote sina uhakika sana Mheshimiwa Waziri kama tutafanikiwa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo mashirikiano baina yako wewe, baina ya Wizara nyingine ambazo ni wadau katika lile ni lazima tuyaimarishe ili tuweze kwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Gama atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ajiandae.

MHE. LEONIDAS T. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo kwenye eneo hili la viwanda na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nichukue nafasi hii niwashukuru sana na kuzipongeza Kamati zote kwa kazi nzuri walizozifanya ambazo zinatupa matumaini. Vilevile nataka niipongeze sana Serikali yangu kwa dhamira nzuri ya kwenda kwenye nchi ya viwanda Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niombe sana, tunapozungumza viwanda nadhani tuna tatizo moja kubwa sana la mikoa ya kusini, hasa hasa Mkoa wa Ruvuma. Hivi sasa tunazungumza habari ya viwanda, lakini Mkoa wa Ruvuma mwaka 2008 ulitenga eneo maalum kwa ajili ya kuweka viwanda. Eneo hili toka mwaka 2008 hadi leo na liko Songea Mjini wale wananchi hawajalipwa fidia, wanaishi maisha ya shida na Serikali haina dalili ya kuonesha lini wataanza kulipa fidia za wananchi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wenzangu hapa Waheshimiwa Wabunge wanavyozungumza viwanda katika maeneo yao mie mwenzenu mnaniacha gizani kwa sababu hata hilo eneo la viwanda halipo. Kwa hiyo, nataka niombe sana Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha wale wananchi ambao wanafikia 1,085 wanalipwa fidia zao ili waweze kupisha eneo la kujenga viwanda na ili mipango ya Serikali iweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, EPZA imechukua zaidi ya heka 5,000 na Waheshimiwa Wabunge hebu fikirieni mjini kuwa na heka 5,000 kwa ajili ya shughuli za uwekezaji ambazo hazijalipwa mnaona jinsi wananchi wa maeneo yale wanavyoteseka sana na shughuli hiyo. Kwa hiyo, naomba sana, Serikali ione umuhimu wa kuwalipa wananchi hawa. Nitatoa hoja kama haitakuja bajeti ya kulipa watu fidia na basi safari hii nitakwenda sambamba na Mheshimiwa Waziri ili kuhakikisha shilingi ile ya kwake naikamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nataka niombe sana. Wenzetu wengi katika mapinduzi ya viwanda walijali sana wazawa wao. Sisi tunazungumza sana viwanda lakini tunawahamasisha watu na sidhani kama tumejiandaa vilivyo ili kuhakikisha Watanzania wenyewe ndio wanapata nafasi kubwa zaidi ya kuingia kwenye uwekezaji katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya kuwafanya Watanzania waingie katika viwanda yako mambo mengi; lazima tuwe na *program* maalum ya kuwafanya Watanzania wajiandae kisaikolojia kwamba sasa tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda. Lazima tufike mahali tuwe na mitaala maalum ya kuwafundisha wanasayansi na watafiti ili ifike mahali watakaendesha viwanda hivyo na watakaoweza kuvihudumia viwanda hivyo iwe ni Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenzetu katika nchi nyingine kama China wanafikia mahali wananchi wao wanapewa mikopo ya kuweza kuanzisha shughuli za viwanda kwa ajili ya kujenga uchumi kwa wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania lazima tujiandae, tunajua mabenki yetu yalivyo, ni vizuri tukajiandaa tuweke programu maalum ili Watanzania wapewe kipaumbele katika kuanzisha viwanda na wapate mikopo ya kuweza kuanzishia viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo viwanda vidogovidogo *SIDO* na *VETA* tuna wataalamu wetu, ingawaje hawajapata elimu ya kutosha lakini viwanda vile tuna uwezo kabisa wa kutengeneza program za kuhakikisha tunawapandisha viwango na uwezo wataalam wetu *SIDO* na *VETA* ili waje kuwa wawekezaji wazuri katika shughuli za viwanda. Kwa hiyo, nataka niombe sana Serikali iwe na utaratibu mzuri wa kuwafanya Watanzania wenyewe wapate uwezo wa kuwekeza katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka niombe sana Serikali iwe na utaratibu mzuri wa kuwafanya Watanzania wenyewe wapate uwezo wa kuwekeza katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa nataka niangalie upande wa pili vilevile, tumekubaliana kimsingi kwamba hivi viwanda vyetu rasilimali yake kubwa ni kilimo. Lakini tujiulize hivi tumejiandaa vipi kilimo chetu kingia kwenye uzalishaji wa viwanda? Maana hata mtu akianzisha kiwanda cha parachichi leo nina uhakika hatuna uwezo wa kuzalisha maparachichi ya kutosheleza kiwanda cha parachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri kujiandaa kikamilifu kwamba, je, wakulima wetu wanaandaliwa vipi kuweza kuviwezesha viwanda viweze kufanya shughuli zao za uzalishaji? Na kwa maana hiyo, lazima tufike mahali tuangalie mfumo wa benki zetu namna utakavyoweza kuwakopesha wakulima wazalishe mazao ya kutosha mengi, ili mazao hayo yatumike katika kuingiza kwenye shughuli za uchumi wa viwanda; vinginevyo tunaweza tukajikuta tunatengeneza viwanda ambavyo malighafi unaitafuta kutoka nje ya nchi yetu na hii haitakuwa na faida kubwa kwa Watanzania wenyewe. Mwenyekiti, Maana viwanda hivi tunavitazamia vizalishe ndani ya nchi, lakini viwanufaishe wananchi kwa maana ya kutafuta *raw materials*, lakini vilevile viweze kupata soko la uhakika la matumizi ya viwanda hivyo.

Mheshimiwa Nilikuwa naomba Serikali iweke programu maalum na itengeneze mazingira mazuri ya kuwafanya wakulima waweze kuingia kwenye uzalishaji wa mazao ambayo yatakuwa ndiyo malighafi katika shughuli za viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishukuru. Nizishukuru Kamati zote na niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya katika shughuli za kuandaa mazingira ya viwanda; naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, tunaendelea, Mheshimiwa Omary Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kupata fursa ya kuchangia Kamati hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nitoe shukrani kwa Mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uzima hata tumekutana jioni hii ya leo. Lakini pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa sera yake ya viwanda na kwa kuanza kwa vitendo, natoa mfano kwenye

Jimbo langu. Mwaka wa jana wakati nakuja hapa watu wengi majirani zangu hapa walikuwa wananiambia kwamba Mgumba Mkulazi, lakini kilio kile kimemfikia Dkt. John Pombe Magufuli, ameweka mazingira mazuri na tumepata mwekezaji, *Mkulazi Holding Company Limited*, kampuni tanzu ya Mifuko ya Jamii ya NSSF na PPF inawezeza kiwanda kikubwa cha uzalishaji wa sukari katika Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki, chenye uwezo wa kuzalisha tani 150,000 kwa mwaka na kuondoa adha ya sukari hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kwenda kwa vitendo utekelezaji wa sera ya viwanda. Haya sio maneno, kama mtu anabisha aje kule Mkulazi anaona ujenzi unavyoanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa niende moja kwa moja kwenye ushauri. La kwanza, naomba kuishauri Serikali hasa kwenye suala hili la TFA (Shirika la Mbolea) na kama walivyosema Kamati, suala kubwa hili shirika ni muhimu sana hasa kwenye sekta ya kilimo. Hili shirika ndio tunalitegemea kwa ajili ya usambazaji wa mbolea kwenye zana za kilimo, lakini kama Serikali haiwezi kulilea vizuri lazima madeni haya yataendelea kuongezeka na shirika hili litakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu Serikali, leo hii kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati, shirika hili lilianza na mtaji wa shilingi bilioni 17.9 leo wana mtaji wa *negative billion 12.3*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini na sababu ni nini? Ni kwa sababu, mara nyingi Serikali, hasa kwenye taasisi zake hasa inapopata huduma kwenye ulipaji au fidia ya ile ruzuku ambayo inaagiza taasisi zake itumie inachelewa kwa muda mrefu sana, athari yake inakuwa kubwa na matokeo yake haya mashirika yanapoteza uaminifu kwa wadau na taasisi nyingine za fedha, hata kwa wasambazaji wengine wa mbolea kule wanakochukulia mbolea hizi na matokeo yake wanashindwa kukopesheka, athari kubwa inaenda kwa wakulima wetu kutokupata mbolea kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niishauri Serikali inapohitaji huduma kwenye shirika lake, kwa mfano kama hapa, shirika hili linaweza kwenda kununua mfuko labda wa mbolea shilingi 50,000 lakini Serikali kwa ajili ya kurahisisha ipatikane kwa bei nafuu, ikaiambia TFC uzeni shilingi 30,000 nyingine ni ruzuku. Sasa ile ruzuku ambayo Serikali ina *top up* ni vizuri ikaipeleka kwa wakati ili kufidia shirika liweze kujiendesha kibiashara na ziweze kulipa madeni yake kule ambako inakopa. Badala ya kutoa miongozo kwamba toeni ruzuku, shirika linatoa ruzuku, lakini hela haziendi kwa wakati, ndio matatizo haya ya *negative* ya mtaji yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili niishauri Serikali kuhusu kwenye Bodi za Mazao. Bodi za Mazao zimekuwa nyingi na mara nyingi tunavyoziona nyingine hazipo kwa ajili ya manufaa ya kilimo chetu wala kwa wakulima wa Tanzania. Sasa ushauri wangu kwa Serikali, ni vizuri tukaunda bodi mbili tu, moja ikawa kwa ajili ya mazao ya biashara ambayo itasimamia mazao yote ya biashara yale makubwa yaliyokuwa na bodi kwa sasa; kwa mfano labda ile Bodi ya Korosho, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pareto, Bodi ya Pamba, zote zikaunganishwa zikawa bodi moja na bodi ya pili ikawa Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Hizi zikiwa mbili itakuwa ni rahisi, moja inashughulikia mazao mchanganyiko nyingine mazao ya biashara, kwa kufanya hivyo hata menejimenti yake inakuwa ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu Mifuko ya Jamii. Katika hili nakubaliana na mapendekezo ya Kamati, wanapozungumza kwamba Msajili wa Hazina (TR) anatakiwa atambulike kisheria kwenye mifuko hii. Nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuja kufunga hoja yake; bado mimi sijaelewa vizuri. Kwa uelewa wangu mdogo najua hii Mifuko ya Jamii ni mali ya wanachama. Sasa kama mali ni ya wanachama Serikali ipo kama mdhamini

lakini si moja kwa moja kama ilivyo kwenye yale mashirika ya Serikali kwa mfano kama *TTCL* na mashirika kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia mali ya wanachama labda *TR* aingie moja kwa moja kule kama msimamizi mali ya Serikali wakati ile si mali ya Serikali moja kwa moja ni mali ya wanachama, naomba ufafanuzi katika hili ili tuweze kupata uelewa wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa katika kujenga nyumba kwa ajili ya kupangisha na uwekezeji, lakini pamoja na nia nzuri ya kupunguza matumizi, bado utalam na ubora unatakiwa uzingatiwe, sasa kumezuka tabia moja hasa kwenye mashirika haya ya Serikali, iwe *NHC* au *TBA* utakuta mwenyewe ndiye mkandarasi, wakati huo huo ni mshauri mwelekezi wa mradi na pia ndiye msimamizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali hii haipo kisheria, kwasababu pamoja na yote kuna mambo ya Kisheria. Lazima iwe kwamba *engineer* awe mwingine, msimamizi awe mwingine, ili kuonesha kama kazi inayotekelezwa inakidhi ubora unaotakiwa. Tukiachia hali hii iendelee, pamoja na nia nzuri ya kupunguza matumizi, lakini kuna uwezekano mkubwa wa kuja kupata miradi ambayo inakuwa chini ya kiwango, baadaye hata tija au *value for money* ikakosa kuonekana huko mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa, tunaendelea, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia, lakini niseme mimi pia ni Mjumbe katika Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Tumetoa ushauri kwenye taarifa yetu, lakini ni vema basi kuna mambo mengine ambayo tunaweza tukayazungumza angalau Wabunge wenzetu waweze kutuunga mkono katika Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuanza na suala zima la mazingira. Kwa masikitiko makubwa niseme kwamba Ofisi hii ya Makamu wa Rais siku zote imekuwa ikipewa bajeti kidogo sana pamoja na kwamba Wizara ya Mazingira ni Wizara mtambuka, lakini bado Serikali imeendelea kuipa pesa kidogo Ofisi ya Makamu wa Rais ka upande wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na udogo wa fedha hiyo, pamoja na udogo wa bajeti hiyo, bado fedha hii kupatikana kwake haipatikani kabisa. Tangu tulivyokutana mara ya mwisho na Ofisi ya Makamu wa Rais, mwezi Januari, kwa masikitiko makubwa mpaka leo tunavyozungumza hapa hawajawekewa hata shilingi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunategemea mazingira ya nchi yetu ndiyo kila kitu katika ustawi wa nchi yetu, lakini bado katika Ofisi ya Mazingira bado fedha haiendi, watumishi pale wanashindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na uwezo mdogo wa fedha walio nao. Wameishia watu wa *NEMC*, sasa hivi wanachokifanya fedha ambayo wanaitumia ni fedha ya kutoza faini kwa watu. Yaani sasa hivi imefika mahali wanapata fedha kwa ajili ya makosa ya watu, sasa sijui ni Serikali ya aina gani ambayo inaendeshwa kwa fedha ambazo ni makosa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi hali ya mazingira nchini kwetu ni mbaya sana kuliko ambavyo tunaweza kuifikiria. Tumetembea kwenye maeneo mbalimbali, lakini baadhi ya miradi ambayo ilikuwa imepangiwa kwenye bajeti hii hatukuweza kufanikiwa kuiona kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Tumetembelea eneo moja tu ambalo tulikuwa kama vile tumeenda *beach*, tulipelekwa eneo la ufukwe la *Ocean Road*; ndilo eneo ambalo pekee tulipelekwa kama Kamati kwenda kuona sehemu ambayo wanategemea kujenga ukuta kwa ajili kuzuwira mmomonyoko ambao unakuja unasogea mpaka kufikia lkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maeneo mengine yote ambayo yalikuwa yamewekwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka huu ya mazingira hakuna eneo lingine ambalo tumeweza kwenda zaidi ya maeneo ambayo Bunge lilitusaidia tumeweza kufika, kama Mwadui pamoja na Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotembelea Mgodu wa Mwadui tulijionea hali halisi ya mazingira katika mgodu ule na kiukweli wanajitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba maeneo ya mazingira katika mgodu ule yanalindwa pamoja na maeneo ya pembezoni ambayo wananchi wanaishi. Eneo la Mgodu wa Mwadui pamoja na wananchi wake wameweza kupewa elimu ya upandaji wa miti na jinsi ya kuvuna miti ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwadui walichowafundisha watu wanaoishi maeneo ya Kishapu ni kuhakikisha kwamba hawakati miti kama vile inavyofanyika maeneo mengine. Eneo lile wamefundishwa kukata miti kwa kukata matawi na kuacha shina liendeleo ili ule mti uweze kuendelea kuwa mkubwa badala ya kukata mti mzima na kuacha kisiki na kutegemea kwamba watu waendeleo kupanda miti mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea Mgodu wa Geita. Mgodu wa Geita kiukweli kwa kuhusiana na suala zima la maji machafu wamejitahidi kwa namna moja ama nyingine kuweza kuweka bwawa ambalo linahifadhi yale maji machafu. Lakini kwenye maeneo ya mazingira, hasa kwenye maeneo ya miti kwa kweli hawafanyi vizuri kwa sababu hali ni mbaya, wananchi wanakata miti sana, wananchi wanatengeneza mikaa kwa wingi kweli kweli! Kwa hiyo, tuliwashauri angalao kwenye maeneo ambayo yanawazunguka basi waweze kusaidia wale wananchi wa pale waweze kuwa wanapanda miti na kusaidia mazingira yaweze kuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda kwenye Mradi wa Ziwa Victoria. Huku ni masikitiko makubwa sana, kwasababu imefika mahali hali ya mazingira katika Mradi wa Ziwa Victoria kwa kweli si nzuri na hairidhishi. Tungemuomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake hebu ajaribu kutuambia katika huu Mradi wa Ziwa Victoria nini hasa kinachoendelea? Kwa sababu inavyoonekana kama Tanzania tunajitahidi kwa namna moja ama nyingine kuweza kuzuia hali ya mazingira ya Ziwa Victoria kuwa sawa, lakini ukiangalia nchi jirani ambazo zinatuzunguka na tulizoingianazo mkataba bado zenyewe hazitekelezi mkataba ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufike mahali sasa na Watanzania tuangalie na nchi jirani za wenzetu ili yale ambayo tunakubaliana kwenye mikataba yetu yaweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kuhusu suala zima la viwanda, sasa hivi viwanda vingi vya samaki Mwanza vinafungwa na vinafungwa kwa sababu ya ukosefu wa samaki katika Ziwa Victoria. Hali ni mbaya, kiwanda ambacho kilikuwa kinaweza kufanya kazi saa 24 leo wanaweza wakafanya kazi kwa *shift* mbili peke yake, ikizidi sana ni *shift* moja. Leo viwanda vya samaki vya Mwanza baadhi vimefungwa na baadhi vinaendelea kufanya kazi kwa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini kwa kukubali mapendekezo yetu na maoni yetu ya kumuomba waanze kununua transfoma zinazotengenezwa nchini kwetu. Kiwanda cha *Tanelec* kinatengeneza transfoma nzuri na Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamati tumesikia wamesema kwamba, kuanzia sasa wataanza kununua transfoma kutoka nchini kwetu. Hilo ni suala zuri naomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri na tufanye hivyo ili kuweza kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyotangulia kusema Mjumbe mwenzangu, Wizara ya Fedha imetengewa bajeti lakini mpaka leo tunavyozungumza tunakwenda karibu robo iliyobaki kumaliza bajeti, lakini fedha iliyokwenda ni *only 7 point something billion*. Jamani katika bilioni 42, bilioni saba kwenye Wizara ya Viwanda ni kitu gani ndugu zangu! Nafikiri hapa tunafanya masihara, tunaweza tukawa tunalaumu, lakini mwisho wa siku Serikali; Mheshimiwa Mpango na Hazina yako hebu jaribuni kuangalia basi. Zile Wizara ambazo angalao mnasema kwamba zina kipaumbele hebu zisaidieni kuziwekea fedha ili waweze kutekeleza majukumu yao badala ya kukaa mnatusaundisha (mnatushawishi) kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wanapokuja watu wa Wizara ya Fedha ni habari ya kusaundishwa (kutushawishi) tu, lakini utekelezaji haupo. Ilifika mahali tuliwarudisha, tuliwafukuza na tukawaambia hatutakaa tusikilize taarifa yenu kwa sababu haina jipya. Kila wanapokuja wanakuja na yaleyale kumbe tatizo ni ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii kuna kitu kinaitwa *Fair Competition*, hawa watu wanafanya kazi kubwa sana, yaani hawa watu ndio ambao wanazuia bidhaa *fake* kuingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Fair Competition* wanafanya kazi ngumu lakini hawana watu ambao wanafanya kazi hizo. Leo *Fair Competition* kati ya wafanyakazi 125 wanaohitajika wana wafanyakazi 53 tu nchi nzima. Hebu fikiria mtegemeo hawa watu waweze kufanya kazi nzuri, kazi hiyo wanaifanya kutokea wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Angella Kairuki alituelea hapa kwamba, Ofisi yake ya Utumishi imeanza kuruhusu ajira; Mheshimiwa Angella Kairuki, sijui ajira hizo zinakwenda upande gani? Kwa sababu kama kwenye Wizara mbalimbali hakuna watumishi ambao wanaajiriwa! Mheshimiwa Waziri, hebu utatueleza ukweli, hawa watumishi mnawaajiri kwenye idara zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha ni kwamba hawa watu wa *FCC* pia waafanya kazi nyingine ambazo ni za hatari sana, wanaingia bandarini wanakutana na watu, lakini... (*Makofi*)

(*Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Riziki!

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ilikuwa kengele ya kwanza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Riziki Said Lulida.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia hii nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kunipatia afya njema. Ukimuona mtu mzima analia basi ujue amepatwa huyo mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ni-*declare interest* kama mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PIC au Uwekezaji. Kwa kweli, kama ingekuwa Wabunge wote wanapata taarifa za mikataba mibovu ambayo imeingiwa na mashirika mbalimbali basi, humu ndani tusingekuwa pamoja tungekuwa tumepata msiba mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitu ambacho nimejifunza katika kukaa katika Kamati ya Uwekezaji, kwanza ni mikataba mibovu ambayo imeifanya nchi isiweze kwenda. La pili, tumeshindwa kusimamia Sheria ya Uwekezaji. Tatu, kulindana kulikopitiliza, matokeo yake wanapewa watu nafasi ambao hawawezi kuzifanyia kazi, iwe Mwenyekiti wa Bodi au awe Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na ninakotoka, Mkoa wa Lindi na Mtwara. Mkoa wa Lindi na Mtwara tulikuwa na viwanda vya korosho vinane na wawekezaji au ubinafsishaji wakapewa vile viwanda kwa bei ya kutupa. Tangu walipopewa viwanda vile wamevifungia mpaka leo, je, Serikali ipo, haipo? Serikali ina macho, haina macho? Lakini wamelifumbia macho na kuacha viwanda vile vikifungwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamewapa wawekezaji, wale wawekezaji wamevifunga vile viwanda, wametoa mashine na kuzipeleka Mozambique ambako wamefungua viwanda vingine na kuwaacha watu wa Mtwara na Lindi wakiwa hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza watu wale wale wamepewa kazi ya kupeleka korosho nje *as a raw material*, tujiulize tunajitambua? Kama kweli tunakwenda katika uwekezaji wa viwanda kwa mfumo huu hatutoki, maana mnawajua nani anasafirisha korosho nje, anapeleka ajira nje, anapeleka kila kitu nje, viwanda amevifungia kwa sababu ya nani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri mwenye dhamana atuambie kwa nini viwanda hivi vimefungwa zaidi ya miaka kumi wananchi hawana ajira na korosho inapelekwa nje ajira inapelekwa nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikubaliki ni aibu. Lazima tujitambue na tufunguke, kwa hiki tunachofanyiwa ni aibu. Hata kama utasema tunataka kuwekeza kama mikataba mibovu itakwenda hivi, hakuna uwekezaji hapa. Ina maana tunataka kutoa mfumo wa kukandamiza taasisi zetu kuhakikisha watu wa nje wanakuja kuwekeza hapa na kuleta *pollution*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda Amerika ya Kusini; uwekezaji umepelekwa mkubwa sana Amerika ya Kusini; sasa hivi Amerika ya Kusini ni eneo ambalo lina *pollution* ya hali ya juu. Na Tanzania kwa mikataba mibovu tutakayoendelea nayo nina imani baada ya miaka mitano nchi hii itakuwa *polluted* yote; na mazingira yote mnayoyaona haya yatakwishwa. Tujitambue na tusimamie kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na viwanda vya nguo zaidi ya kumi MUTEK, MWATEK, Urafiki, *Sungura Textile*, *Tabora Textile* na *Riziki Textile*, lakini viwanda vile vyote vimefungwa. Na katika kufungwa bahati nzuri Kamati ilitembelea EPZA, tukaenda kuangalia kiwanda ambacho kinatengeneza nguo za *jeans*, tukawauliza je mnapata wapi nyuzi? Wametujibu kuanzia sindano, uzi na kila kitu tunapata kutoka China. Tujiulize kweli tuko *serious* na uwekezaji? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona ndugu yangu Mwijage wamekupa mzigo mzito kwa vile uliokuwa nao chini hawako *serious* kukusaidia, utakuwa unakimbia peke yako wataalam wako huku pembeni hawako *serious* na wewe kabisa. Haiwezekani tumefunga viwanda vya kusokota nyuzi, leo nyuzi zinatoka China, maana yake ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka uchumi endelevu, pana uchumi hapo? Wanawaajiri watu kwa miezi mitatu mitatu, Mtanzania huyo atapata faida gani hapa? Ina maana unamchukua miezi mitatu unamuachisha, miezi mitatu unamuachisha, hii nchi haiwezi kwenda katika mifumo ya namna hiyo ya mikataba mibovu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na viwanda vya kukamua mafuta; tulikuwa na *Tanbond* inatoka Tanzania, *Super gee* inatoka Tanzania, *pride* Tanzania na *Mara ghee* Tanzania; leo viwanda vyote mmefunga. Na wamevifunga tunaagizia *blue band* kutoka nchi za nje, *are we serious?* Halafu unapotaka kutuambia sisi tunakwenda katika mfumo wa viwanda vyote tumevifunga tunategemea vya nje hivi vina kasoro gani hata vimefungwa? Nenda Urafiki ni *ma-godown*, nenda Mtwara ni *ma-godown*, je, maendeleo haya mnayoyafanya mnayadumaza kwa makusudi halafu mnasema sasa hivi tunataka ulimwengu wa maendeleo ya viwanda, tutafika katika mfumo huo? Hatufiki, mikataba mibovu imefikia mahali ambapo sijui dawa yake ni nini, ni msiba kwa Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelewa na Shirika la Madini Tanzania (STAMICO), walikuwa na maeneo yao ya madini Tanzania nzima viwanda vya chumvi Lindi, Mtwara na Kigoma. Vile viwanda vyote vimefungwa na walipewa maeneo mengine kama ya uwekezaji ya Mererani. Mererani ina vitalu 29, STAMICO amepewa vitalu viwili tu. Mle ndani watu ni fujo tu na ndiyo maana unaona leo Tanzania tuna *Tanzanite* lakini inapelekwa nje ni kwa ajili tumesababisha njia za panya. Tunashindwa nini kuwauliza wale watu kwa nini wale watu wote wasishirikiane na STAMICO ili akaweze kupeleka uchumi, lakini imeshindikana yote ni kwa ajili ya mikataba mibovu. Tufike mahali tujiulize tunatakaje maendeleo ya uwekezaji na mikataba mibovu? Hii nchi imekuwa kaputi kabisa kwa ajili ya mitaba mibovu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewa mradi wa uwekezaji na TANZAMOB ambao wamepewa na STAMICO; yule mwekezaji ni tapeli wa kutupa, ameanza kuchimba madini kwa muda toka mwaka 2011 anasema hajapata faida. Tujiulize, kwa nini hajapata faida na kwa nini anaendelea kuchimba? Miradi yote unayoiona Tanzania haina *time frame*, anafanya mtu biashara kwa miaka yotote anayotaka yeye. Sasa je, utasemaje tunaenda katika ulimwengu wa viwanda, ulimwengu wa uwekezaji tukiwa katika mfumo mbovu? Aibu. Tujiulize kweli nchi hii tunataka kuikwamua? Haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea *National Housing*, mwekezaji Kawe alinunua majengo ya Kawe na heka 300 kwa milioni sita, milioni sita Watanzania nawaambia. Kawe ameinunua kwa milioni sita akalipa milioni mbili na laki tano, hakufanya chochote leo ameambiwa ana *share* na *National Housing*. Meneja wa *National Housing* anahangaika kutafuta *fund* yule anachukua hela ya bure na mapato ya bure, tutafika? Kwa mfumo huu tutafika? Kwa nyumba za bei rahisi mtazipata wapi? Huwezi kuzipata Tanzania anatozwa mpaka tozo la vifaa vya kuingiza kutoka nje kwa ajili ya ujenzi wa nyumba halafu unasema zile nyumba za bei rahisi, Mtanzania wa kawaida hawezi kukaa katika nyumba ya *National Housing* kwa vile mmeweka mikataba mibovu ya kumfanya *National Housing* asiendelee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelewa na TANAPA. Kuna wawekezaji wako ndani ya Shirika la TANAPA ambao ni watu wa mahoteli, wake watu ni majambazi sugu ambao hawataki kulipa *concession fee*, halafu wanachokifanya ni kukimbilia mahakamani wakicheza na mahakama kuhakikisha TANAPA haiapati tozo, mahakama iko chini ya nani? Matokeo yake sasa hivi tumeshashinda lakini bado wale watu hawataki kuona Waziri ambaye anafanya kazi wanasema tutamtoa kwa vile anatudhalilisha. Uchumi wa nchi umeshikiliwa na watu wachache ambao wamehakikisha nchi hii haiendi. Tunawajua, tunawafahamu na tunawafumbia macho.

Nchi hata kama mtafika mahali hapo kama hamsimamii sheria zetu, hamuangalii mikataba yetu nina imani kuwa hatutaweza kufika popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelewa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(Tanzania Airport Authority)*; Tanzania tuna airport 58 amepewa airport nane tu; 50 zote zipo kwa watu wachache wanafanya shughuli zao huko, madini yanapotea huko, wanyama wanapotea huko na mali zinapotea huko ni kwa ajili ya mikataba mibovu. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea, Waheshimiwa Wabunge tunaingia kwenye kipindi cha kugombania mpira wa kona. Dakika tano, tano kwa kila nitakayempa nafasi kabla hatujamaliza kuhamia upande wa Serikali. Kama mnaona ni vigumu nitaenda upande wa Serikali. Mheshimiwa Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako na Mheshimiwa Balozi Diodorus Kamala ajiandae, dakika tano tano tu.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwasababu ni dakika tano nitachangia haraka haraka na nitaanza kwa kuchangia mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yetu yameharibika, na sana sana yameharibika kwasababu ya mkaa pamoja na ukataji wa kuni. Watu wote mnajua kuwa Mkoa wetu wa Morogoro, Mkoa wa Pwani na nchi nzima ya Tanzania kwa wastani, mara unapopita utakuta mkaa na utakuta kuni. Kwa hiyo, naomba mikakati iwekwe pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais kuona kuwa itafanyaje ili kuweza kutafuta nishati mbadala badala ya kutumia kuni au kutumia mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni karibu asilimia 90 ya Watanzania wanatumia mkaa na Dar es Salaam tu wanatumia mkaa magunia 200,000 mpaka 300,000. Kwa hiyo, naomba sana hii iweze kupewa kipaumbele kwa kuwa inaleta jangwa, joto, mvua hatupati na tabia nchi inabadilika. Kwa hiyo, naomba itiliwe mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tutakuwa na kiwanda cha sukari Mkulazi lakini ijulikane kuwa viwanda vingi vya Mkoa wa Morogoro havifanyi kazi. Nilikuwa nakuomba tuone jinsi ya kufufua hivi viwanda viweze kufanya kazi, Mkoa wa Morogoro ulikuwa ni mkoa wa viwanda lakini sasa hivi havifanyi kazi. Ni vizuri tuna Kiwanda cha Maji Udzungwa kinafanya kazi, Kiwanda cha Tumbaku kinafanya kazi lakini viwanda vikifanya kazi tutaweza kupata ajira kwa wakina mama pamoja na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili viwanda viweze kufanya kazi ni lazima uwepo umeme wa uhakika, lazima yawepo maji ya uhakika na ni lazima kuwepo na malighafi na hizi malighafi lazima zitokane na kilimo. Kwa hiyo, inabidi tuangalie hayo mambo na tuangalie mikakati ya kuwa na umeme wa uhakika, maji ya uhakika pamoja na kilimo cha uhakika kinachozalisha malighafi ambazo zitaweza kuendeleza viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa sababu umenipatia nafasi hii na ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Kamala na Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru ingawa muda ni mchache niseme mawili tu ya haraka haraka.

Kwanza, Waheshimiwa Wabunge leo tuna taarifa hizi kumi na zote hizi zinazungumzia mapendekezo ya Bunge hili. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ni vyema ungetuongoza kwamba kama walivyosema wenzetu kwenye Kamati ya Uwekezaji ukurasa wa 49 kwamba ni vyema maazimio haya, mengine ni mazito sana, kwa mfano mambo yaliyozungumzwa kuhusu Bandari ya Dar es Salaam kama ni ya kweli basi yataisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hiyo tu wewe mwenyewe kwa sababu ni mahiri kuongoza Bunge hili ningemba sana haya yote maazimio Waheshimiwa Wabunge tukubaliane yasiachiwe kwa Katibu wa Bunge; sisi wenyewe Wabunge tuunde Kamati yetu ndogo ya kuratibu mambo haya ni mambo mazito sana, vinginevyo yatakuwa hayana maana haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukumbushane kidogo, Mabunge mengine yanafanya hivyo kwamba kazi hii tunayoifanya ni kazi muhimu ya Kikatiba; ni kazi yetu kabisa ya msingi ya kuishauri Serikali na kuisimamia, lazima mambo ya msingi yalimo humu pengine si yote, lakini yale ya msingi lazima yadavuliwe, yaandikwe vizuri na Serikali tuitake ije na majibu na kalenda yake ya utekelezaji, vinginevyo itakuwa ni hadithi tu, mambo ni mengi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamezungumzwa humo ndani, ushauri wangu nakubaliana na wenzetu wa Kamati ya Uwekezaji kama walivyoainisha kwamba tuunde Kamati Ndogo na wewe Mheshimiwa Chenge utuongoze tuunde Kamati Ndogo itakayosimamia mambo haya kwa kuwa ni mambo makubwa na mazito sana ambayo haiwezi kuachiwa Ofisi ya Katibu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa niliseme kwa muda uliobaki kidogo huu nizungumzie suala la PPP. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anahangaika sana, hongera. Kaza buti, lazima ufanye *promotion* na lazima uendelee kufanya *promotion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ushauri wangu ni kwamba, ili upate pesa lazima utumie pesa; waswahili wanasema ili ule lazima uliwe, ndiyo maana yake. (Kicheko)

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hii *private* sekta tuisaidie, yenyewe haiwezi kunyanyuka; *private sector* duniani kote inasaidiwa kukua ili hatimaye iweze kuzalisha wafanyabiashara na walipe kodi na hatimaye kodi hiyo ndio inakuja kusaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa mambo mengine yanatisha ukiyasoma humu ndani, kwa mfano kama kesi imeamuliwa ni kwa nini wenzetu wa Maliasili hawatekelezi haya yaliyoamuliwa na Mahakama? Kwa nini Serikali hamfanyi? Tunapotaze shilingi bilioni 10 wakati kesi imeamuliwa na Serikali imeshinda? Hakafu wakati huo tunaambiwa fedha hazipo, fedha si ndizo hizi? *Ten billion* mnai-*surrender* namna gani wakati kuna *court ruling*? Wale matajiri kama hawataki kakamateni mali zao tupate *ten billion* yetu. Sasa mengine humu ndani yanazungumzwa kwa kweli yanatia uchungu sana. Tunatafuta fedha tuna shida ya fedha ya miradi ya maendeleo fedha zingine zimeachiwa kwa matajiri na sababu iliyotolewa humu kwamba eti hakuna Bodi ya *Tanzania National Parks*, alah! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi bodi hiyo iundwe haraka sana na ndio mambo ambayo sisi kama Bunge lazima tusimame kidete na tuitake Serikali iunde hiyo bodi tuokoe *ten billion* yetu na hilo linakuwa halina mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala mwisho ni la kilimo. Mimi tafsiri yangu ya viwanda ni viwanda vya kilimo, vya mifugo na vya sekta ya uvuvi. Hivi viwanda vya Wachina Waturuki,

Waingereza na wengine wanakuja kutusaidia tu lakini the *basic industry* ni lazima itokane na kilimo chetu, kilimo, wafugaji na wavuvi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nizungumzie habari ya wawekezaji; ndugu Mwijage tembea na wawekezaji mfukoni kama wapo walete kwetu tutawapa maeneo ya kufanya shughuli zao. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante unaendelea, Mheshimiwa Balozi Kamara atafuatiwa na Mheshimiwa Komanya.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuzingatia kuwa ninazo dakika tano tu nitaongelea hoja mbili. Naomba nibainishe kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati, sote kwa pamoja tuna nia ya kujenga Tanzania ya viwanda; lakini kwa masikitiko makubwa baadhi ya wawekezaji tunaowakabidhi viwanda hivi ili watusaidie kuviboresha kwa kuleta teknolojia za kisasa, wao badala ya kufikiria kujenga Tanzania ya viwanda wanafikiria kujenga Tanzania ya ma-godown. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni kiwanda chetu cha nguo cha Urafiki. Tulipotemebelea sehemu ile tulishangazwa na tulishtuka kuona Mkurugenzi Mkuu hajui *mission* kwa nini wapo pale na hajui *vision* kwa nini wapo pale, jambo hili lilitusikitisha sana. Lakini baadaye tukabaini kwamba wakati fulani zilitolewa fedha kwa ajili ya kununua mitambo, fedha zilitumia lakini hakuna mtambo hata mmoja ulioletwa, kwa hiyo ulinunuliwa mtambo hewa. Wakati Serikali inahangaika na watumishi hewa wakati umefika pia kubaini mitambo hewa inayonunuliwa, badala ya kuendesha kiwanda, inanunuliwa mitambo hewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tulibaini kuna mpango wa makusudi wa kuhakikisha *spare* ambazo zinatakiwa kutumika kwenye kile kiwanda hazinunuliwi na wala haziagizwi, mashine inapoharibika inabidi sasa ing'olewe kwa sababu hakuna *spare*, huo ni mkakati wa kubadilisha kile kiwanda kuwa *godown*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukabaini kwamba pamoja na kung'oa ile mitambo pale kuna menejimenti mbili; kuna menejimenti inayoongozwa na wazawa na kuna menejimenti inayoongozwa na wawekezaji. Wawekezaji wanajua ya kwao na wazawa wenzetu wanajua ya kwao. Kwa hiyo, ni menejimenti mbili katika kiwanda kimoja, matokeo yake hakuna kinachoendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ambayo ningependa niimalizie na nyingine niziache, tumeona tatizo la kutotenga fedha za kulipa fidia, kaka yangu Mheshimiwa Mwijage anajitahidi kuhangaika lakini kwa mfano pale Omkajunguti tunataka kuweka *Export Processing Zone*, zinatakiwa fedha za kulipa fidia, lakini hadi sasa tumeendelea kuzungumza tu hakuna fedha iliyotolewa. Labda tu nimshauri waziri muhusika kwa kuwa alishaniaidi kulipa fidia hizo, alisema ifikapo mwezi wa kumi atakuwa amelipa na sasa hajalipa, ikifika wakati wa bajeti tusigombane, nitafuata taratibu za Kibunge zinazotakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi, Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae, halafu nitaenda mengine.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda huu niliopewa naomba nijikite zaidi katika mazingira na nitajikita katika mazingira hususan katika Mkoa wa Simiyu. Ni dhahiri kwamba athari za mabadiliko ya tabianchi zinaongeza uwezekano wa kaya kuendelea kuishi katika umasikini. Umasikini huu utaendelea kuongezeka kwa miaka ijayo, hususan kwa mwanamke ambaye ni mkuu wa kaya kama hatua mathubuti na endelevu za kukabiliana na athari za tabianchi hazitachukuliwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke wa Mkoa wa Simiyu amekuwa akikabiliana na njia mbalimbali katika kukabiliana na athari ya tabianchi. Mwanamke amekuwa akijishughulisha katika kilimo cha umwagiliaji ambacho ni kidogo na hakina tija. Nikiongelea Wilaya ya Busega, Kata za Kiloleni, Nyashimo, Kabita, Kalemela, kata hizi ziko kandokando ya Ziwa Victoria lakini mwanamke anatomia ndoo kumwagilia katika kilimo chake ambacho hakina tija. Niendeleo kuiomba Serikali, itakapoanza kutekeleza mradi wa maji ya Ziwa Victoria, na ninaamini utekelezaji wa mradi huu uko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, basi itenge maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili iweze kumsaidia mwanamke huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea Kata ya Gambasingu, Wilaya ya Itilima na Kata ya Mwashata, Jimbo la Kisesa, Wilaya ya Meatu, wanawake wanatumia ndoo kumwagilia maji kutoka Mto Simiyu ambapo kilimo hicho kinakuwa hakina tija. Niiombe basi Serikali kupitia hizi asilimia tano ama shilingi milioni 50 zikianza kutolewa kwa kila kijiji, zianze na Mkoa wa Simiyu ili wanawake waweze kukopesheka na kuweza kununua pampu ambazo zitawasaidia katika umwagiliaji na hivyo waweze kukabiliana na athari ya tabianchi, ikiwemo pia na Kata ya Mwamanimba iliyopo katika Jimbo la Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine wanazotumia wanawake kuweza kukabiliana na athari hizi ni kufanya biashara ndogo ndogo; lakini changamoto wanayoipata ni ukosefu wa mtaji pamoja na kujengewa uwezo. Halmashauri hutenga asilimia tano katika bajeti yake kwa ajili ya kuwawezesha wanawake, lakini fedha hizi zimekuwa hazitolewi, zinabaki kwenye makaratasi tu. Niombe basi kuwe na msukumo wa utekelezaji wa utoaji wa fedha hizi, hata kupitia vikao vya RCC iwe ajenda mojawapo ya kufuatilia utekelezaji wa asilimia tano kwa ajili ya akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, wanawake... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Zainab Katimba atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ya kuweza kuchangia katika hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuleta uchumi wa viwanda kuna mambo ya msingi ambayo Serikali inabidi iendeleo kuweka msisitizo. Katika uchumi wa viwanda ni lazima Serikali iweze kuangalia kwamba kuna upatikanaji wa malighafi. Tunahitaji malighafi ya kutosha ili kuweza kulisha viwanda vyetu. Katika malighafi tunazungumzia upatikanaji. Kukiwa kuna viwanda lakini hakuna upatikanaji wa malighafi ya kutosha kulisha viwanda vyetu basi mwisho wa siku tunakuja kuona viwanda vyetu vinafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nitoe mfano, viwanda vyetu vya sukari hapo awali vilikuwa vinafungwa kwa msimu fulani kwa sababu hakukuwa na malighafi ya sukari ambayo ingeweza kuzalisha sukari. Kwa hiyo, Serikali inabidi iweke msisitizo katika upatikanaji wa malighafi hizi. Na hata tukiangalia nchi ambazo ziliendelea na zimeendelea katika uchumi wa viwanda ilianza kwanza *agrarian revolution* yaani mapinduzi ya kilimo, yalianza yakaweza kuleta *industrial revolution* ambayo ni mapinduzi ya viwanda. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuendeleza jitihada zake inazozifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, tunahitaji malighafi ambazo ni za bei nafuu. Tukiwa tuna viwanda lakini malighafi zinazopatikana nchini ni za bei ya juu na zinatumiya *cost of production* kubwa kuliko zinazotoka nje ya nchi, mwisho wa siku tunaona kwamba hata gharama ya uzalishaji wa mali ambazo zitazalishwa ndani ya nchi zitakuwa zina gharama ya juu zaidi kuliko mali zitakazoletwa kutoka nje ya nchi.

Kwa hiyo, ningependa pia Serikali iendelee na jitihada zake inazofanya kuhakikisha kwamba malighafi zinapatikana kwa bei nafuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, tunahitaji ubora wa malighafi ambao utatokana na ubora tuseme kwa mfano wa mbegu. Kwamfano kama tunazungumzia viwanda vya kutengeneza, tuseme juisi, inahitaji kwamba kuwe kuna ubora wa hata yale matunda yanayopatikana Tanzania. Kwa hiyo je, mbegu zinazotolewa na mbegu zinazotumika zina ubora wa kuzalisha kwa kiwango kizuri cha kuweza kulisha viwanda vyetu? Hilo ni suala lingine ambalo Serikali inabidi iendelee kufanya jitihada zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mbolea, kuna suala zima la teknolojia inayotumika, je, teknolojia inayotumika Tanzania ni ya kizamani au inaendana na wakati, kwa sababu kutumia teknolojia ya zamani kunaleta gharama kubwa zaidi ya uzalishaji na mwisho wa siku hata mali zetu na viwanda vyetu vinakuwa haviendelei vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia katika suala zima la upatikanaji wa mitaji. Upatikanaji wa mitaji au tuseme mikopo lakini upatikanaji wa mitaji hii kwa riba nafuu. Upatikanaji wa mikopo katika taasisi zetu za kibenki tujiulize, je, unaweza kuhimili uchumi wa viwanda? Je, *financial institutions* zinaweza kutoa mikopo kwa ajili ya wawekezaji wetu wa ndani kuweza kuwekeza katika viwanda vyetu? Na hiyo mikopo inayotoka na hizo fedha zinazotoka kutoka kwenye taasisi zetu riba zake zikoje, kwa sababu kuna taasisi za kifedha ambazo zinatoa mikopo, zinatoa fedha kwa riba hadi asilimia 25, je, huyu mwekezaji ataweza kweli kufanya biashara zake, ataweza kweli kuhimili matakwa ya kuendesha kiwanda chake na kikaweza kufanikiwa.

Kwa hiyo mimi napenda kuiomba Serikali kwamba ikae na wadau mbalimbali, viwanda na biashara na taasisi za kibenki, ili iweze kusaidia mchakato utakaoweza sisi kutunga sheria itakayoweza kuweka ukomo wa viwango hivi vya riba kwenye mikopo katika taasisi za kifedha. Kwa sababu tukisema tu tunaacha hivi ilivyo, taasisi za kifedha zinaweka riba za hali ya juu na mimi kama kijana najua vijana wenzangu wanajishughulisha katika shughuli za ujasiriamali na wanahitaji hizi fedha, wanakwenda kwenye taasisi za kifedha na wanapata... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA ...wanapata fedha kwa riba kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, moja kwa moja nimpongeze shangazi yangu, Mheshimiwa Mama Lulida, alichokisema Mheshimiwa Mama Lulida ndiyo kitu ambacho kinatokea Mtwara, lakini pia ndivyo vitu vinavyotokea Lindi. Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo iliingia mikataba ya kuuza maghala ambayo yalikuwa ni viwanda vya korosho Mtwara, Lindi, Newala, kwanza imepoteza ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba basi tu-review upya ile mikataba kwa sababu tunaamini pamoja na ugumu uliopo kule ndani lakini Rais ana nia ya dhati kabisa ya kuwasaidia watu wa Mtwara ili waweze kupata ajira. Sisi Mtwara hatuna shida ya malighafi, tuna malighafi ya korosho ambayo inategemewa sana India. Malighafi pekee wanayoitegemea wale ni kutoka Mtwara ambayo ni korosho na tumeona mwaka huu korosho imeuzwa mpaka shilingi 3,800. Ili kuweza kuongezea wale wananchi kule kipato, tunataka sasa vile viwanda vifufuliwe korosho hii tubangue kule wenyewe. Kwanza ikibanguliwa kule moja kwa moja itauzwa kwa bei kubwa kwa sababu gharama za usafirishaji na tozo nyingine hazitakuwepo, hii pesa atakwenda kuipata mkulima moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeshuhudia maghala haya ndiyo yamekuwa sehemu ambazo zinakwenda kuwafilisi na kuwaibia wananchi, hawapati haki zao stahiki. Maghala haya kule ndani imeingia mikono ya wakubwa ukitaka kugusa biashara za maghala Mtwara basi unatafuta ugomvi na wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tukuombe, hakikisha unapitia vizuri hii mikataba ukishindwa wewe kuisema tupatie sisi tutasema, mpe pale Mheshimiwa Mama Lulida atasema, nipatie mimi nitasema, lakini kimsingi tunachotaka mwishoni wananchi wa Mtwara, wananchi wa Masasi wawe na viwanda vyao vile vya zamani. Viwanda hivi vilijengwa kwa kukopa pesa nchi za nje, ambapo ninaamini bado Serikali hii inaendelea kulipa pesa wakati viwanda vimeuzwa kwa bei rahisi, kwa hiyo nikuombe kabisa upitie hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tena kidogo kuhusiana na suala la biashara ya mafuta. Watu wengi, na hapa ndani tumeona wakiwa wanachangia, sasa hivi tunaona bei ya mafuta imepanda sana, hata kama tunasema imepungua, asilimia 42 ya tozo mbalimbali zilizopo kwenye bei za mafuta zinakwenda Serikalini kuendesha vitu mbalimbali, lakini tunawatengenezea ugumu hawa wafanyabiashara wa mafuta. Kwa hiyo, tuone namna gani tunaweza tukawasaidia, tuangalie hizi tozo na kuzi-review. Haiwezekani asilimia 42 yote iwe kama sehemu tu za kodi, mfanyabiashara apate shilingi 120 au 150 sehemu ya kazi anayoifanya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kimsingi tujaribu kuangalia, tunaposema kwamba watu wa Mtwara sisi tuna shida hatuna shida hasa ya viwanda kama mnavyovisema. Hivi karibuni tu Mheshimiwa Waziri niliongea nawe nikakueleza, tunaweza tukapata juisi kwenye mabibo, tunaweza tukapata nipa kwenye kochoko inayotokana na mabibo, lakini lengo hasa ni kwenda kumuongezea mkulima kipato. Hivi vitu vikiuzwa, hata tukiuzwa korosho shilingi 3,000, lakini tukauza mabibo yetu yanayokwenda kutengeneza juisi, tukauza zile kochoko zinazokwenda kutengeneza *gin*, tukaachana na hivi vitu vya ku-*import* itakwenda kuongezea pia kipato Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa tunasema tunataka kupata mapato kwenye Serikali kwa kutumia vileo, ukiangalia asilimia kubwa ya wananchi vijijini ni wanywa gongo,

wanywa gongo hawa, na hii gongo tunasema ni pombe haramu haijarasimishwa, lakini ndio wengi wanaokunywa gongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiamua sasa kurasimisha ikazalishwa vizuri kwenye vyombo vinavyotakiwa kodi itakwenda kuongezeka kwenye vileo, sawasawa na ilivyo konyagi sawasawa na ilivyo *gin* sawasawa na ilivyo kwenye *K-Vant* watu wa Arusha. Kwa hiyo tutoe leseni za watu kuweza kupika gongo ambayo ipikwe kwenye viwanda vinavyotakiwa, ipimwe vizuri, irudi ikaingizie kipato Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakataa bure, asilimia 75 ya Watanzania wanaoishi vijijini wanakunywa gongo, na hii tutambue kama vyanzo vya mapato kwa sababu tutatoza kodi. Tunasikia sifa kutoza kodi kwenye *grant's*, tunasikia sifa kutoza kodi kwenye konyagi wakati tunajua wazi wanywaji wa konyagi na *grant's* si wengi kama walivyo wanywaji wa gongo. Kwa hiyo tunapoteza mapato, tuangalie namna bora ya kufanya ili tuweze kuzalisha hivi vitu lakini pia itaongeza kipato cha wakulima wetu kama ilivyo kwa wakulima wa miwa. *K-Vant* inatengenezwa kwa kutumiwa miwa, miwa ni mazao ya wakulima, konyagi inatengenezwa kwa kutumia *chemicals* nafikiri, lakini pia nipa inatengenezwa kwa kutumia mabibo ambayo inaongeza kipato wakulima kama tutarasimisha na kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nikuombe utakapohitimisha utuambie sisi watu wa Mtwara mna mpango gani na viwanda vyetu vilivyozwa kiholela holela vya korosho, vinaweza kutoa ajira kwa vijana wetu wote maeneo yale, tunaweza kuongeza tija kwenye korosho. Mheshimiwa Mama Riziki Lulida amesema hapa kwamba hizi ajira zinapeleka India, tunajisifu tume-export tani laki mbili za korosho kupeleka India, lakini hatufikiri kama tumeondoa ajira za watu zaidi ya 10,000 au watu 20,000 kupeleka India, tunataka kuweka viwanda vya aina gani? Tuwaombe Mtwara tunataka tu viwanda vya kuanzia vya korosho, wala hatuhitaji kutengeneza nondo katika hali hii, korosho yetu isitoke na kwenda nje, iwe *processed* palepale ili kuweza kuiongeza thamani, muwashawishi wale wawekezaji waliopo kule waje Mtwara kujenga viwanda sio sisi tuwapelekee kwao malighafi, ninaomba ulichukue hili na tafadhali ulifanyie kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe, nakushauri ukasome *Hansard* ya mwaka 1968 wakati Serikali inawasilisha Muswada Bungeni kuhusu Sheria ya Vileo. Tunaendelea, Mheshimiwa Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa sababu ni dakika tano nitakwenda kuongea kwa kifupi sana. Kwanza kabisa naunga mkono ripoti za Kamati zote mbili, lakini zaidi naomba Serikali ifanyie kazi ripoti ya Kamati ya Uwekezaji kwa yale yote ambayo tumeshauri pale na ambayo tumeyaona *field*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa haraka haraka nisisitize kwa yale ambayo tumeandika kwenye Kamati yetu. Ni kweli kabisa tumeona athari ambazo zinajitokeza kwa kutokuwa na bodi kwenye taasisi na mashirika ya umma. Taratibu zinataka kwamba mchakato wa kuweza kuwa na bodi baada ya ile nyingine kukaribia kuisha walau uanze miezi sita kabla, lakini tumeshuhudia Serikali hii taasisi zinakaa bila bodi zaidi ya miaka miwili hadi miaka mitatu. Na mfano tumetolea Bodi ya TANAPA, imekaa zaidi ya miaka mitatu tunaona kabisa ile kesi ya *concession fee* ilihukumiwa tarehe 12 Septemba, 2014, lakini Serikali ikaona ni bora Taifa liendeleo kupoteza kila mwaka zaidi ya shilingi bilioni 10 kuliko kuunda Bodi ya TANAPA ambayo ingeweza kufanya maamuzi na kuweza kupata fedha ambazo ni takribani zaidi ya shilingi bilioni 20 zimepotea, ambazo zingeweza kwenda kujenga zahanati na vitu vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kumekuwepo na watumishi kukaimu kwenye nafasi za watendaji wakuu kwenye mashirika yetu na taasisi kinyume kabisa na sheria inavyosema. Unakuta mtu amekaimu zaidi ya miaka miwili hadi mitatu, wakati inatakiwa ndani ya miezi sita mtu aweze kupatikana kwa nafasi husika. Hii inasababisha mashirika yetu, taasisi zetu zisiwe na ufanisi katika utendaji na tutaendelea kuona mashirika yakiwa yanajiendesha kihasara kwa sababu hatujaweza kutengeneza *management* ambayo kwanza kabisa imeboba na inajua ni nini inafanya. Ukimkaimisha mtu hawezi akafanya *decision* kwa sababu hajua kwanza *ultimatum* ya nafasi yake ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusu madeni ambayo Serikali inadaiwa na hazi taasisi. Unakuta imepata huduma lakini inashindwa kulipa madeni haya. Kwenye Kamati tumeainisha; mfano ni madeni makubwa kutokana na mifuko ya hifadhi ya jamii, tumeona madeni takribani kwenye PSPF ukiyachukua yote kwenye *categories* zile tatu ni takribani shilingi trilioni 3.47 za wanachama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja Naibu Waziri wa Fedha akatuahidi kwamba watatoa hati fungani ya takribani shilingi bilioni 290 ambayo ilikuwa ni deni linalotokana na miradi, lakini mpaka leo hawajaweza kutoa hiyo hati fungani, hawajaweza kulipa malimbikizo ya madeni ya mwajiri kwenda PSPF, hawajaweza kulipa takribani shilingi trilioni 1.7 ya yale madeni ambayo waliyachukua kwa wastafu wale wa kabla ya mwaka 1999. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuishii hapo tu, Shirika kama DAWASCO ni shirika dogo sana, lakini unakuta linadai shilingi bilioni 16 kutoka kwenye Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hizi shilingi bilioni 16 zingeenda DAWASCO zingeweza kusaidia na kuboresha huduma ya maji Dar es Salaam na Pwani, lakini unakuta hawalipi wakiambiwa hawalipi kwa sababu ni Jeshi basi linaendelea tu wanapata huduma. Ifike wakati hizi taasisi kama hazilipi na zenyewe zikatiwe maji, haiwezekani Mtanzania anashindwa kulipa 20,000 mnamkatia maji, lakini taasisi ya Umma inadaiwa mpaka shilingi bilioni 16 hamuwakatii maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uonevu na Mtanzania wa kawaida akisikia anashangaa sana, yaani akishindwa kulipa bili ya maji ya shilingi 10,000, 20,000 anakatiwa maji lakini unakuta mnadai zaidi ya shilingi bilioni 16 na bado huduma ya maji inaenda. TANESCO wanawadai, TSN wanadai, LAPF wanadai, Serikali mnadaiwa madeni mengi sana. Tuweze kulipa haya mashirika ili yaweze kujiendesha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kwa haraka haraka kabisa, wakati tumepitia kwenye hizi taasisi tumegundua kwamba hizi taasisi zinajiendesha kihasara. Tatizo lingine ni kwamba fedha wanazozipata wanazitumia kwenye matumizi ya kawaida badala ya uwekezaji. Kwa mfano, kama ilivyoainishwa kwenye baadhi ya mashirika; tumeona NSSF walitumia zaidi ya asilimia 17 kinyume kabisa na vile ambavyo matakwa yanataka asilimia 10 kwa mwaka wa fedha 2015/2016; lakini pia kamati imeainisha AICC na mashirika mengine. STAMICO inajiendesha kwa hasara, wanaweza wakawa wanakopa benki wanakuja wanajitumia kwenye matumizi ya kawaida ambayo ni kinyume kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu mikataba ambayo mashirika yetu yanaingia, taasisi zetu zinaingia hasa zikiwa kwenye ubia na wawekezaji wengine. Hii imekuwa inalipeleka taifa letu kwenye shimo siku zote. Na ninashindwa kuelewa wataalam wetu ni kwamba tunakuwa hatujui ni nini tunafanya au hatuna uzalendo wa kutosha. Kwenye taarifa yetu umetolewa mfano wa mkataba wa *Mlimani City*; kwamba sisi tunakubali kuingia mkataba wa kupata gawio la asilimia 10 ya faida na tunasema kwamba tunaingia mkataba mpaka baada ya miaka 50 ndipo tunaweza tukapata ile mali, na ukiangalia ubora wa yale majengo ya

Mlimani City ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kabisa ndani ya miaka 50 tutakuwa tunapata mabua. Yaani wale wawekezaji watafaidika wataondoka sisi wakitupa asilimia 10 tu, Taifa... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Khatib Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kupata nafasi na mimi kuchangia kidogo na nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na shukrani kwa pekee zizidi kwako na nikuhakikishie tu kwamba uwepo wako katika kiti hicho unatupa raha ndani ya roho zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie nikiwa nimejieleza wazi kwamba ni Mjumbe wa Kamati hii ya Viwanda na Biashara na nimpongeze kwa dhati Mwenyekiti wetu. Kati ya Wenyevitini makini wa Kamati hizi za Bunge, Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu naweza kusema ni nambari moja.

Sasa katika Kamati zetu siku moja, alikuja mchumi fulani akatuambia kwamba wawekezaji ni kama ndege, kule wanapokuwa wanaruka angani wanaangalia ni nchi gani inafaa kuwekeza ndipo wanaleta uwekezaji wao. Na kati ya vigezo muhimu sana vinavyowavuta wawekezaji na vivutio muhimu sana, kimojawapo ni amani na usalama katika nchi. Wawekezaji wanaangalia mazingira ya usalama ndani ya nchi, hayo yanawafanya wawe na umuhimu wa kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo tunaokwenda nao sasa hauashirii kuwakaribisha wawekezaji katika nchi yetu. Juzi tu hapa wakati nauliza swali nilimshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kujiaalia nchi yetu kuwa ni miongoni mwa nchi ambazo haziko katika janga, tishio la ugaidi, hili ni jambo la kushukuru sana na tumuombe Mungu azidishe hilo. Lakini jambo la kusikitisha, Mheshimiwa Waziri, ninaemuheshimu sana alikuja akalipinga hilo na akaona kwake yeye ni bora kusema kama nchi yetu ni miongoni mwa nchi zilizo katika tishio hilo, ni kitu cha ajabu sana. Mimi namheshimu sana Mheshimiwa Mwakyembe, lakini ningeweza nikadhani labda sijui kuna kitu kimemvuruga au vipi lakini tuyaache hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hilo dogo, leo hii tunashuhudia vitu vya aibu ambavyo vinafanyika ndani ya nchi. Leo hii mtu mmoja anayejiipa madaraka ambae aliwahi kujiita Mungu wa Dar es Salaam anafikia hadi ya kutaja majina ya wawekezaji na wafanyabiashara wakubwa kwamba hao ni *drug dealers* wakubwa sana, kitu ambacho wale wawekezaji tayari wanatafakari upya na kuendelea kuwekeza kwao, je, hawa walioko nje watajifikiriaje kuja kuwekeza katika nchi yetu? Upande mmoja tunahimiza wawekezaji waje kuweka viwanda, upande wa pili tunawa-harass wawekezaji juu ya uwekezaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina mfumo kamili wa ulinzi wala sidhani kama umetetereka. Kuna Jeshi la Polisi, kuna Waziri wa Mambo ya Ndani makini sana tunayemuamini, mchapa kazi, kuna vyombo vya ulinzi wa usalama makini sana, kuna Usalama wa Taifa tunaamini ni makini sana, kuna Jeshi la Ulinzi ni makini sana. Leo vyombo vyote hivi vimeonekana havina maana, *father god* wa Dar es Salaam aliyejiita Mungu wa Dar es Salaam ndiye amejipa jukumu la kusema kila kitu katika nchi hii? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu wa Dar es Salaam leo anaweza kumtaja yoyote na isiwe lolote siku ya pili anatoa amri aje *central police*, ni nani huyu katika nchi hii? (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilipopewa jukumu la kusimamia mambo haya muhimu ya ulinzi na usalama, dawa za kulevya na *everything* vimelala wapi? Vinamuachia Makonda aliyejibatiza kujita Mungu leo anafanya kila kitu, ni nini, *what for*, tunakwenda wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nataka niliseme hili kwa sababu azma ya kuwekeza kwenye viwanda haiwezi kwenda kwa matamshi ya ajabu ajabu na maamuzi yanayotolewa na mtu mmoja kwa sababu yeye kauli yake inaonekana inasikilizwa sana na Mheshimiwa Mtukufu Rais, haiwezekani. Mimi nadhani sasa kila mmoja atajua wajibu wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la mwisho mimi nataka kumwambia ndugu yangu Waziri, Mheshimiwa Waziri nia yako nzuri ya kuimarisha viwanda na mimi nakubaliana na wewe lakini Mheshimiwa Waziri kila mchezo una sheria zake. Kwenye riadha ile kuna mbio za vijiti. Huwezi kukimbia tu ukafika..... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. *order, order.*

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti!...

MWENYEKITI: *Order, order in the house.* Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi niseme kutoka awali kwamba naunga mkono taarifa za Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda halina mjadala, Bunge lako Tukufu hili limekubali kama Serikali inavyotaka kwamba ili tufike nchi yenye kipato cha kati ni lazima tupitie kwenye viwanda. Lakini nataka niwambie kwamba kama tunataka tufaulu kwenye viwanda lazima tuwe na uwezo wa ushindani kwa sababu bidhaa za viwanda zitashindana na bidhaa za nchi nyingine.

Kwa hiyo, nataka niwaeleze wale waliokuwa wanataka viwanda vya miaka ya 1960 na 1970 vifufuliwe, inaweza ikawa hasara kwetu kwa sababu uwezo wa ushindani utakuwa mdogo, ila tutake viwanda vipya vya korosho na sehemu zingine vianzishwe. Tusipoangalia hilo tutajingiza na mimi nafurahi sana Serikali hii ya Awamu ya Tano inalijua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme jambo moja ambalo lilishaanzishwa na sisi tusipolipeleka mbele tunaweza tukajirudisha nyuma. Kupitia *SIDO* na Wizara ya Viwanda kulikuwa na mradi wa *MUVI* ambao unajua kila Wilaya inaweza ikawa na viwanda vipi ili tuwe na uwezo wa kubadilishana ndani ya nchi ambamo viwanda vingi ni vya kuchakata mazao ya kilimo katika kuongeza thamani.

Kwa hiyo, naomba mradi huu wa *MUVI* muuangalie upya kusudi kusiwe na Wilaya ambayo haina viwanda, ama sivyo tutaifanya nchi iwe na sehemu nyingine ina viwanda, sehemu nyingine haina viwanda halafu wengine wakawa nyuma na wengine wakawa wamepiga hatua. Kwa hiyo, naomba sana, hili liangaliwe, tuwe na nchi ambayo ina uwezo wa kuwa na viwanda nchi nzima na kwa kuangalia kwamba kila Wilaya ina-*specialize* kwanza *issue* ya *division of labour* na *specialization* lazima iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi nataka kusema habari ya mikataba. Mikataba ya nchi hii imetayarishwa na wataalam na wataalam ni binadamu. Inawezekana kwamba kuna

maeneo yamekosewa, lakini sidhani kama mikataba yote ni mibaya kiasi hicho. Kwa hiyo tuwe watu wa kuangalia mikataba ipi inaupungufu na mikataba ipi ambayo ni mizuri iendelezwe na ile ambayo ina upungufu iweze kuangaliwa na kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema kwamba tuhakikishe kweli viwanda vinafanikiwa. Ili viwanda vifanikiwe kuna kitu kinaitwa *basic industries* au viwanda mama. Viwanda vya chuma, viwanda vya *chemicals*, viwanda ambavyo vinaweza vikafanya vingine vikazaliwa na vikaendelea kuzaliwa. Tusipofanya hivi tunaweza tukaanzisha viwanda ambavyo havitasonga mbele. Kwa hiyo haya yote tuyaangalie na suala la uwekezaji lazima tulitilie mkazo. Watu wasipowekeza ndani ya nchi, nchi itatawaliwa na watu wengine wa nje. Tulianzisha *forum* ya uchumi katika kila mkoa, naomba Waziri uendeleze zile *forums* ili kila mkoa ujue kwamba wanaweza kuwekeza sehemu gani ili nchi yetu iwe na maendeleo sawia kwa kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Livingstone Kaboyoka, dakika tano.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze wenzetu wa Kamati zote kwa kazi nzuri walizofanya. Najua ukiwa wa mwisho itakuwa *point* zako nyingi zimechukuliwa lakini nimebaki na chache ili nisirudie rudie zile ambazo wenzetu wamezisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa tu nataka ni-observe mambo mawili, kwamba katika nchi yetu nafikiri tunatakiwa tuongeze uzalendo zaidi maana naona kwamba kila wakati tunasema tukaangalie wawekezaji kutoka huko nje. Hatuweki misingi ya kusema tujenge uwezo wa watu wetu wa ndani. Kama wenzangu waliotangulia waliosema Wachina, nakumbuka hata kile kisiwa cha *Hong Kong* wakati wazungu wale wa Uingereza wakitakiwa waondoke, *10 years before*, waliwawezesha watu wao wawe na mitaji mikubwa waweze kuwekeza kwenye vie viwanda vikubwa na wawe *board members* ili waweze kujifunza na kupata uzoefu, ndiyo maana wenzetu mpaka leo China wamekwenda mbele sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu tunajua kwamba kuna aliyesema *50 percent* ya mafuta yanaingizwa kutoka nje, *infact* ni *70 percent* ya mafuta ya kula wakati alizeti zinalimwa sana na *infact* tungeongeza *pressure* au misaada kwa wakulima wetu wa zile alizeti tungehakikisha kwamba hatu-*import* mafuta ya kula. Wenzetu kutoka Kenya wanakuja kuchukua vitunguu hapo Singida wanavi-*re-export*, sisi tunabaki tunaangalia wakati vitunguu vinatoka kwetu. Tunadharau vitu vidogo vidogo, lakini tungeangalia *bottom up* tungejikuta tunasaidia wakulima zaidi *as a result* tukaboresha na umaskini tukauondoa katika *level* ile ya chini kwa kuweza kuunganisha viwanda vyetu na malighafi kutoka kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunaangalia *institutions* zetu, tuna *TEMDO, CARMATEC, CBE, Dar Tech, Arusha Technical*; wote hawa wanafanya kazi ambazo wangewekwa pamoja, wakasaidiwa, wangeweza ku-*invent* vitu vizuri na ushauri mzuri kwamba tu-*invest* kwenye nini na waweze kuweka utaalum wao pale. Hivi vyote vimewekwa pembeni tunaangalia watu wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalizi wetu wametumwa nje, wanaambiwa muangaie wawekezaji, samahani sikumbuki labda imesemwa hiyo; lakini ningetegema nchi iwe ime-*identify* ni mazao gani tunaweza ku-*export* ili kila Balozi anayekwenda nchi fulani tumwambie atuangalilie soko la kitu hiki na kile na kile. *For example*, vitu vinavyolimwa Tanzania ambavyo tunaweza kupeleka nje ni vitu kama nini? Tunaweza kusema ni mzaha mzaha lakini tangawizi

ambayo tunaweza kuiboresha, ni nchi yetu ina-produce tangawizi *the best* katika Afrika, lakini hivyo vyote hatuviangalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaangalia maziwa tuna-import mengi, kwa nini hatuboreshi viwanda vyetu watu wakasaidiwa, wafugaji wakazalisha maziwa kuliko ku-import maziwa, viwanda vile vikakuzwa. Unaona kuna ASAS Iringa, kuna kiwanda cha maziwa cha Tanga hatutaki kuviboresha badala yake tuna-import maziwa ya unga, yanakuwa *imported* sijui madawa gani kutoka *South America* yanakuwa *packed*, tunapata maziwa ya hovy hovy. Sasa kuna mambo mengi sana, kwamba bado uzalendo wetu haupo kuangalia kwamba tukuze *from the bottom up* halafu tuwe na *inward looking* badala ya kila siku tunasema kalete wawekezaji, wawekezaji ambao wakija wanatunyanyasa. Tunajua kuna viwanda watu wamewaweka huko hawajui hata Kiswahili sasa ndiyo tunayoyataka hayo. Mimi nafikiri ifike *high time* ambayo tutaweza kuangalia kwamba tunasaidiaje watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie suala la mitaji, *banks* zinaweka riba kubwa sana kwa nini tusiwe na *strategic plan* ya kuona kwamba tuna-identify viwanda gani ambavyo tuwaboresha watu wetu na tuwape.....(Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana tunaendelea, Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia maneno mawili, matatu hususani kuhusu viwanda na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote mimi nimpungeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini nitoe masikitiko yangu makubwa, kama leo Baba wa Taifa ingekuwa kuna jambo la kusema anaweza akasimama akauliza, angeuliza habari ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tuna mateso sana, tulikuwa na viwanda vifuatavyo kwa sababu ni dakika tano lakini nilikuwa nimejipanga kwa dakika kumi ningeeleza nadhani leo Mheshimiwa Waziri yangemuingia.

MWENYEKITI: Weka akiba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tuna Kiwanda cha Nyuzi na Mheshimiwa Riziki amesema, kiwanda hiki kimehujumiwa na wawekezaji. Wamechukua kila kitu hata kama tunakwenda kwa *science* na teknolojia wameondoa vifaa vyote na wametapeli, mimi ninasema kwa lugha nyepesi, wametapeli. Tangu wamechukua hawajafanya chochote; kwa hiyo hata tukisema zao la pamba liweze kuimarishwa hakuna, tulikuwa tunatengeneza nyuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti lakini tuna Kiwanda cha kusikitisha sana cha Manonga, Mheshimiwa Waziri anajua kipo Igunga. Kiwanda hiki alikuwa amechukua Rajan. Mimi mwaka 2006 nikiwa Mbunge niliwahi kuuliza swali, lakini huyu mwekezaji Rajan amefariki, wamechukua watoto wake, bado kuna usumbufu mkubwa tangu mwaka 1999 kiwanda kile kimefungwa. Ni uchungu mkubwa sana wa unyanyasaji wa Mkoa wa Tabora. Lakini pamoja na hayo, Mheshimiwa Waziri anajua, tulimuomba awakutanishe Rajan pamoja na Igembe Nsabu, hajafanya hivyo na alitoa ahadi ya kwenda kuongea nao, nina uchungu sana, inasikitisha na inakatisha tamaa.

Mheshimiwa mwenyekiti, si hilo tu, Mheshimiwa Waziri alisema katika Bunge lako hili wakati tunauliza swali na alisema wawekezaji wa Kichina wameishia *airport*, sasa hivi mpaka leo bado wameishia *airport*? Inasikitisha, leo nipate majibu kama kweli wawekezaji hawa wapo au hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vya kutafuta wawekezaji Tabora inayo, jinsi ya kuiiza Tabora ipo. Tuna masuala ya tumbaku, tuna masuala ya urinaji wa asali. Hivi asali yote inayotoka nchi nzima hii inatoka Tabora bado hakuna uwezekano wa kuweka kweli? Mheshimiwa Waziri, namheshimu sana naomba aangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie habari ya mazingira. Tabora inalima tumbaku, lakini hawa wanunuzi hawana mpango wa kuhakikisha mazingira endelevu yapo katika Mkoa wa Tabora. Kwa nini nasema hivyo? Wanabeba mbegu za miche, wanatupa kuwapa.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, kabla sijaanza kuita upande wa Serikali kusaidia kutoa maelezo nina matangazo ya wageni ambao tunao hapa, kwa sababu muda unaenda na wenyewe inawezekana wanataka kurejea makwao.

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni watatu wa Mheshimiwa Cosato Chumi kutoka *Open University* Jijini Dar es Salaam, Dkt. Emmanuel Malya na Ndugu Shedrack, wako wapi? Haya kokote mliko karibuni sana.

Halafu tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kundi la kwanza, tunao wanafunzi 90 kutoka *St. Peter Clever High School* mkoani Dodoma. Karibuni sana vijana, someni kwa bidii sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) tunafurahi sana kuwaona hapa. *(Makofi)*

Hao ndiyo wageni, sasa nianze upande wa Serikali kwa hawa wafuatao; Mheshimiwa Mpina dakika tano, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango dakika tano, Mheshimiwa AG dakika tano, Mheshimiwa Makamba dakika kumi na Mheshimiwa Mwijage dakika kumi. Tunaanza, Mheshimiwa Mpina.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hizi dakika tano ulizonipa, lakini pia nichukue nafasi hii kuipongeza sana Kamati. Kamati imetoa taarifa nzuri sana na imenikumbusha enzi hizo nikiwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo na Kamati kwa kweli taarifa yenu ni nzuri na mmetushauri vizuri sana Serikali. Sasa kwasababu ni dakika tano nilizopewa, niseme kwa kifupi haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la jinsi ambavyo Serikali ilishughulikia suala la magwangala hasa upande wetu wa mazingira kwa taasisi yetu ya *NEMC*. Tulichokihakikisha sisi kimefanyika ni kwamba *NEMC* walishiriki kutoa mwongozo, kwa maana ya kuhakikisha kwamba mahali ambapo yataondoshwa haya magwangala kuna mtaalam na kuhakikisha kwamba wanawapa masharti na vigezo vya kuzingatia kadri ya magwangala hayo yatakapohamishwa kutoka eneo fulani kwenda mahali fulani, na kuhakikisha kwamba kwa namna yoyote ile hakutakuwa na uharibifu wowote ule wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, limezungumzwa suala la ujenzi wa mradi huu wa *climate change adaptation program*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema na kuliambia Bunge lako kwamba mradi huu tayari mkandarasi yupo kwa ajili ya miradi yote ya *Ocean Road*, Pangani, Kilimani pamoja na ya Kisiwa Panza, yote hii mkandarasi ni huyu isipokuwa kwa sasa hivi ndiyo yupo hapo Dar es Salaam pale *Ocean Road* ndiyo ameanza. Maeneo mengine haya yote ana *mobilise resources* ili kuweza kupeleka kwenye maeneo hayo ili miradi hii iweze kuanza. Kwa kifupi sana unaweza kuona kwamba huyu *contractor* anaitwa *DEZO Contractor Limited* na alianza toka mwezi wa kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kutekeleza miradi hii tunazo. Fedha za kutekeleza miradi hii ninayozungumza, mkandarasi yuko *site* na ataenda kujenga kuta zote zinazotakiwa, sehemu za kujenga mitaro na yenyewe tayari inajengwa kama maeneo yale ya Kigamboni kule kwa Mwalimu Nyerere, Buguruni, mitaro ile inaendelea kujenga; na sehemu zingine tayari tumeshatekeleza kwa mfano Rufiji tayari tumeshapanda mikoko iliyokuwa itakiwa zaidi ya hekta 792 tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wabunge wote wa maeneo mengine ambayo mradi huu unajumuisha kama Pangani, Kilimani, Kisiwa Panza ambako tayari na kwenyewe mikoko tumekwisha kupanda wakae wakijua kwamba mkandarasi yupo na muda wowote ataanza kazi ya ujenzi mara moja. Kama nilivyosema mkandarasi yupo na fedha tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu suala la Mfuko wa Mazingira. Suala la Mfuko wa Mazingira, hali iliyopo mpaka sasa hivi ni kwamba tayari tumeshapeleka maombi yetu Hazina tena kwa ajili ya kupitisha zile tozo ambazo zinatakiwa zitozwe, lakini vile vile tayari Waziri ameshateua ile Bodi ya Wadhamini ya kusimamia mfuko huu na tayari kikao cha kwanza kimekaa. Kwa hiyo, tunachoomba tu ni kuendelea kuungwa mkono ili tuweze kutekeleza mambo makubwa ya kimazingira kama ambavyo Wabunge mlivyoyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitake kuwahakikishia kwamba kwa kweli tunajua tatizo la mabadiliko ya tabianchi na nchi hii ya Tanzania inavyosakamwa sasa hivi na mabadiliko ya tabia nchi. Tunajua uharibifu wa mazingira unaoendelea, tunahitaji *support* ya Bunge hili ili tuweze kufanya kazi hiyo ya kuhakikisha kwamba tunayarejesha mazingira kwenye hali yake, tunayazuia mazingira kwenye uharibifu wake na mimi na Waziri wangu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii hatuwezi kulala hadi pale mazingira ya Tanzania yatakapokuwa yamerekebishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Leah pale amezungumzia suala la mradi ule wa maji wa Ziwa Victoria ambao unakuja mpaka Jimboni kwangu na mpaka Meatu. Niseme kwamba mradi huo wa umwagiliaji ukweli ni kwamba katika dunia hii ya mabadiliko ya tabianchi, bila wakulima wetu kuwaelekeza katika miradi ya umwagiliaji, bila wakulima wetu kuwaelekeza katika matumizi ya mbegu zinazovumilia ukame na mbegu ambao zinakomaa kwa muda mfupi hatuwezi kufanikiwa katika mapambano haya ya kilimo. Nimhakikishie kwamba mradi huu unaotekelezwa ambao unasimamiwa na Wizara ya Maji na kuratibiwa na Ofisi ya Makamu ya Rais,....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Mheshimwa Dkt. Mpango, dakika tano.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumzie suala la fedha kidogo ambazo zimepelekwa kwa ajili ya maendeleo ya viwanda. Nisisitize tu kwamba utoaji wa fedha unategemea sana upatikanaji wa mapato. Kwa kifupi *revenue effort* yetu kwakweli bado haitoshi kubeba mzigo mkubwa wa mahitaji yetu kitaifa. Tumefanya vizuri, nilieleza upande wa *domestic revenue* lakini tumepata changamoto upande wa misaada na mikopo katika nusu ya kwanza lakini tunaendelea kulifanyia kazi na *prospects*, matumaini yetu ni makubwa katika nusu ya pili ya mwaka iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nisisitize kuwa fedha hizi zilizotolewa si kwa ajili ya kujenga viwanda. Fedha hizi ni kuiwezesha Wizara kufanya *facilitation*, ni kuiwezesha Wizara kuweza kuelekeza sekta binafsi wapi wawekeze. Kwa hiyo, hizi sio fedha kwa ajili hiyo, msimtegemeo kwa kweli Waziri kujenga viwanda na Mheshimiwa Ridhiwani amelieleza vizuri lakini pia Mheshimiwa Mary Nagu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kweli miezi saba ni kipindi kifupi sana kuweza kufanya *evaluation* kwamba Serikali imepiga hatua kujenga viwanda. Utaratibu wa kujenga viwanda hii ni *long term* na tujielekeze zaidi kwamba sekta binafsi katika kipindi hiki imejenga viwanda gani na Serikali ime-*facilitate* kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa kweli Serikali imejitahidi kufanya vitu ambavyo ni msingi wa viwanda, kwa hiyo, mnapo *evaluate* kwamba Serikali imefanya nini kujenga viwanda muangalie *effort* ya Serikali upande wa umeme, upande wa miundombinu mingine ya maji na usafirishaji, lakini pia jitihada mbalimbali ambazo zimefanyika katika kuhamasisha uwekezaji wa ndani ya nchi. Ningeweza kueleza kwa kirefu lakini niishie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu madeni ya mifuko. Niseme tu kwamba ilikuwa muhimu kwanza Serikali ifanye uhakiki wa yale madai ya kwanza yaliyowasilishwa; na kwa kweli hali ilikuwa si nzuri hata kidogo. Yale madai yaliyowasilishwa tuligundua kwamba kulikuwa na sehemu kubwa ambayo si madai halali na hasa kwa upande wa miradi ya ujenzi ambayo ilitumia fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaangalia sasa upya ule mkakati wetu wa kulipa yale madeni, ikiwa ni pamoja na *issuance* ya ile *special cash bond* ya shilingi bilioni 290 na tunatarajia kwamba hizi taratibu zitakamilika hivi karibuni ikiwa ni pamoja na jitihada za kupata fedha pia mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia kutusaidia kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kukosekana Bodi ya Wakurugenzi wa Mashirika na hasa ilisemwa TANAPA, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tumefanya jitihada na tumeshakamilisha uteuzi wa bodi za taasisi mbalimbali ikiwemo hii ya TANAPA na Bodi hii ya TANAPA inaongozwa na Bwana George Waitara. Kwa hiyo, tumefanya jitihada mbalimbali katika kukamilisha shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme lingine pia ni kuhusu bajeti ndogo ya ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, ni kweli fedha hizi ni kidogo, na niseme tu kwamba si ofisi peke yake ambayo haijapatiwa fedha, tatizo kama nilivyosema ni sungura mdogo. Sasa hivi tunakamilisha mapitio ya utekelezaji ya nusu mwaka na kwa hakika tutalitazama hili kwa kuzingatia unyeti wa sekta ya mazingira na athari ambazo zinaonekana wazi. Lakini ukweli unabaki pale pale kwamba kwa kweli mahitaji yetu ni makubwa, tunahitaji sana kujiwekea vipaumbele vya dhati ndani ya sekta na kwa Taifa letu kwa ujumla ili kuweza kuelekeza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Vizuri sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *Attorney General*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kupata fursa ya kuchangia. Nikushukuru wewe mwenyewe, lakini pia niwashukuru Wenyeviti wa Kamati wa kuwasilisha hizi taarifa zote mbili ambazo ni taarifa muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme tu kwamba na mimi naunga mkono hoja za taarifa zote hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tumepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati yao kuhusu uwepo wa mikataba mibovu na mingine inayodaiwa kuwa mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliambie Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali imechukua hatua, inaipitia na inaendelea kupitia mikataba hii na inaendelea kuipitia. Ushauri wangu ni kwa Wabunge, popote pale walipo, wanapopata taarifa za uwepo wa mikataba mibovu basi wawasiliane na Wizara za kisekta ili walete kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuzipitie wote kwa pamoja ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba yote kwa kawaida huwa na vipengele vya marekebisho (*amendment clauses*) ndiyo inayotoa fursa kwa wahusika wa mikataba hiyo kuirekebisaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo naomba kushauri ni hiki ambacho mmeshauri kuhusu Sheria kama ya *EWURA* na *TCRA* kutokuwa na utaratibu wa *succession plan*. Ukweli ni kwamba ziko *succession plan*, ukisoma jedwali la kwanza la hizi sheria zote mbili, jedwali la pili limeweka muundo wa ile bodi na namna gani ambavyo hawa Wajumbe wanapatikana. Kwa mfano hii ya *EWURA*, imeweka kwenye Ibara ndogo ya kwanza *Chairman* anakaa miaka minne, *Director General* miaka minne, Mjumbe mmoja anakaa miaka mitatu, Wajumbe wawili wanakaa miaka mitano. Halafu ana fursa ya *reappointment*, na vivyo hivyo hata ya *TCRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Sheria zote za bodi zinatoa fursa ya *reappointment for one more other term*, hii yote imewekwa mahsusi kwa ajili ya kuendeleza ile *succession plan* na *institutional memory* ya wale wajumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambayo nilikuwa naomba kushauri ni hili suala la Msajili wa Hazina. Ukisoma ile Sheria ya Msajili wa Hazina, kifungu cha 8 na kifungu cha 10 kilifanyiwa marekebisho mwaka 2010 na kupitia Bunge lako Tukufu kupitia Sheria Namba 15 ya mwaka 2015 tumefanya mabadiliko pia kifungu cha 10 tukaongeza 10(a), vifungu vyote hivi vinampa mamlaka Msajili wa Hazina hata kusimamia hii Mifuko ya Hazina kwasababu inataja juu *public corporation* na *statutory corporation* havikuiondoa hiyo mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunatambua pia kwamba mifuko hii kuna wasimamizi wengine kama *SSRA* na Benki Kuu. Tutakachofanya ndani ya Serikali ni kukaa namna gani sasa tumuwekee mipaka huyu Msajili wa Hazina kusudi tusije baadae tukaleta mgongano, lakini kwa ukweli ni kwamba anayo mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru tena. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunaendeleana Mheshimiwa Januay Makamba, dakika kumi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hoja hii ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Kamati na Mwenyekiti na Kamati nzima kwa kweli kwa ripoti nzuri waliyoandika, kwa mapendekezo mazuri, lakini pia kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayoifanya kuisadia Serikali wakati wote ambapo tumekuwa tunafanya nao. Kamati hii imesheheni wanamazingira, wanafahamu changamoto zilizopo na wamekuwa wanatusaidia vizuri sana katika kufanya kazi zetu. Nawapongeza na nawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tumepokea mapendekezo ya Kamati, ni mazuri na mimi nayaunga mkono, lakini pia tumesikia michango ya Wabunge kuhusu masuala ya mazingira. Wabunge wote waliochangia kuhusu eneo hili wamesema hali ya mazingira nchini ni mbaya na mimi nataka niseme kwamba hali ya mazingira nchini ni mbaya sana, si tu ni mbaya, ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji katika nchi yetu ni rasilimali kubwa, ukitazama mito, vijito, mabwawa, chemichemi, kila mwaka unaopita tunapata changamoto ya upatikanaji wa maji, kwenye ardhi rutuba inapungua, matumizi yasiyozingatia kanuni za masingira, misitu inateketea, mvua hazitabiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka hapa tunakutana kupanga maendeleo na kupanga maendeleo na kupanga fedha za maendeleo. Ie shughuli za kupanga maendeleo na kupanga fedha za maendeleo itakuwa haina maana kabisa kama hatutazingatia umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwenye sekta zote. Ukitaja kilimo, hakiwezekani kuwa na manufaa kama hakizingatii mazingira. Afya, elimu, maji, utalii, hakuna sekta isiyoguswa na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya nchi yetu yana mahusiano moja kwa moja na hifadhi ya mazingira lakini pia hata uwezeshwaji wa wanawake (*women empowerment*) na yenyewe moja kwa moja ina uhusinano wa hifadhi ya mazingira. Tunapozungumza ukosekanaji wa maji unaotokana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi wanaoathirika zaidi ni akina mama. Tunapozungumza suala la nishati ya kupikia, wanaotumia muda mrefu kwenda kutafuta kuni na hata wakati mwingine kuingia katika mazingira hatarishi huko porini ni akina mama na ndiyo maana sikushangaa kwamba Wabunge waliochangia kwa sehemu kubwa kwenye mazingira ni akina mama, Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa dada yangu mpendwa sana Hawa Bananga, Dkt. Christine Ishengoma, Mama Mwanne Mchemba kwa sababu ni jambo linalowagusa akina mama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba tumepokea mapendekezo na tumeyakubali na tunapenda Bunge litusaidie kwa sababu Bunge ndilo linalogawa fedha, Bunge ndilo linaloamua fedha kiasi gani ziende katika maeneo gani. Waheshimiwa Wabunge, mkiamua ninyi kwamba Mfuko wa Mazingira katika mwaka ujao wa fedha uwe na shilingi bilioni 200 badala ya sifuri mnaweza kufanya hivyo. Sisi tulipanga katika bajeti iliyopita, tulijadiliana ndani ya Serikali lakini na hapa Bungeni kuhusu uwezekano wa mfuko wetu kupata vyanzo vya moja kwa moja kwenye tozo mbalimbali ili uweze kuwa na fedha nyingi zaidi ili mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Mazingira nikipita kwenye majimbo nikiona unahitaji miche 10,000 niwe na uwezo wa kukupatia miche 10,000. Nikiona unahitaji kwa kupitia Mfuko wa Mazingira, vyanzo vya maji vitunzwe kwenye jimbo tuweze kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo napenda nirudishe changamoto hii kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba tunaelekea kwenye bajeti na kama kweli tunaamini mazingira ni muhimu basi pale tuoneshe kwa vitendo kwamba Mfuko wa Mazingira upate vyanzo vyake vya moja kwa moja kama ambavyo mfuko wa barabara unapata vyanzo moja kwa moja, kama ambavyo Mfuko wa Nishati unapata vyanzo moja kwa moja na mifuko mingineyo, mtakuwa mmetusaidia na mtakuwa mmeisaidia nchi yetu sana. Kwa hiyo ndugu zangu bila fedha hifadhi ya mazingira ni jukumu la moja kwa moja la msingi la Serikali. Sekta binafsi inaweza kushiriki kwenye hifadhi ya mazingira lakini hatuwezi kubinafsisha hifadhi ya mazingira. Lazima sisi kama Bunge tupange fedha ili zitumike huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu tatizo la mkaa. Tumeamua sisi kama Serikali kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kukabiliana na changamoto hii. Sasa hivi tutaleta mapendekezo; tozo kwenye kila gunia la mkaa ni shilingi 16,000 za TFS; labda Halmashauri inaweza na yenyewe inaweza ikacharge shilingi 2,000. Tunataka tuongeze kodi kwenye mkaa ili tuweze kupata fedha nyingi zaidi na tutapenda fedha hizo ziingie kwenye mfuko wa mazingira. Tungependa Wabunge mtusaidie tuamue na Waziri wa Fedha yuko na mazungumzo yanaendelea Serikalini; kwamba zile teknolojia ambazo zinasaidia uhifadhi wa mazingira basi zisamehewe kodi ili gesi iwe bei rahisi, majiko ya gesi yawe bei rahisi ili wananchi wa kawaida waweze kuyamudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa maji Simiyu, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza vizuri ila nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba moja ya nyenzo ambazo tumeamua kuzichukua kama Ofisi ya Makamu wa Rais ni kutumia hii mifuko mikubwa ya kifedha ya kimataifa kupata fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi lakini fedha hizo kuziingiza kwenye miradi ya maendeleo. Kwa mfano, kwa uhakika kabisa Mkoa wa Simiyu utapata shilingi bilioni 200 kwa ajili ya upatikanaji wa maji kutokana na Mfuko wa Mazingira wa Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kwenye maeneo yote yenye ukame kama Serikali tujenge hoja kwamba ukame ule unatokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, fedha inazosaidiwa Tanzania kwenye kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi tuzipeleke kwenye maeneo kama hifadhi ya maji, kilimo cha umwagiliaji na kadhalika. Tukifanikiwa katika mwezi huu wa tatu unaokuja kupata fedha hizo shilingi bilioni 200 itafungua mlango wa kupata dola milioni 800 kwa ajili ya maji katika nchi yetu. Huu ni mradi ambao tunaufatilia kama Ofisi ya Makamu wa Rais na tutafanikiwa, tutakapofanikiwa basi wetu tutakuwa tumewapunguzia kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukataji wa miti na kilimo cha kuhamahama, nimesikia nilipata nafasi ya kufanya ziara ya mikoa kumi katika nchi yetu na baada ya Bunge hili tutazunguka katika mikoa yote siyo tu kukagua hali ya uharibifu wa mazingira bali kuchukua hatua wakati ule ule tutakapoona kuna uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye tumbaku Tabora, tumeamua sasa kupiga marufuku matumizi ya yale mabani ya zamani ya kienyeji ambayo yanatumia magogo mengi na kupelekea ukataji wa miti na misitu ya nchi yetu. Ningependa Bunge lako liwe ni Bunge la wanamazingira. Naomba tusaidiane sana, Waheshimiwa Wabunge mkiishika ajenda ya mazingira tutatoka, pamoja na kwamba inawezekana athari za uharibifu wa mazingira zisionekane papo kwa papo lakini madhara yake huko mbele yatakuwa maisha magumu sana kwa Watanzania. Kwa hiyo, tuna uwezo wa kuweka historia kama Bunge la kwanza lililoweka fedha nyingi zaidi kwenye hifadhi ya mazingira na kuyaokoa mazingira ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja hapa kila mwaka tunaomba fedha nyingi kwenye bajeti ya maji, lakini unaweza kuomba fedha na kujenga miundombinu ya maji kama

hatukupanga fedha za kuhifadhi vyanzo vya maji tutakuwa tumepoteza fedha kwenye kujenga mabomba ya maji wakati kule maji yanakotoka hatujayahifadhi.

Kwa hiyo, katika shughuli zote ambazo tunazipanga katika Bunge hili mazingira ndiyo msingi wake na Serikali tunaishukuru sana Kamati kwamba jambo hili imeliona na inalishughulikia, tunategemea sasa *spirit* hii ya Kamati basi Bunge zima na yenyewe italichukua ili itakapofika wakati wa bajeti basi wote tuzungumze kwa kauli na sauti moja ili tuweze kuisaidia nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa fursa hii, nashukuru tena Kamati na ninawashukuru wote mliochangia kwenye hoja hii. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo una dakika kumi, *kutik mwamba* (vipi jabali).

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nadhani wasemaji wengi tumechukua mawazo yenu, suala ni umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hiyo, nadhani kuna hivi viwanda vya mbolea cha Mtwara na cha Kilwa. Ukweli ni huu, *tender* ilifanyika, *Ferrostaal* ya Kilwa ikashinda *tender*. TPDC ikaanza kufanya kazi na kampuni iliyoshinda *tender*. Kampuni iliyoshindwa *Helm* ikaamua kufanya taratibu zingine kwenda kujenga kiwanda Mtwara, huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hayo yote sisi hatujatenga kampuni yoyote, niseme tu kwamba tulikaa kikao na Makamu wa Rais, nikapeleka wataalam wangu Mtwara, viwanda vyote vinapewa gesi, sitaki kwenda zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha Mkuranga *Goodwill* cha vigae, mitambo mabomba yamefika, yeye aliyekuwa anaomba gesi hajamaliza kujitayarisha na yenyewe ninaiachia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la umeme, Waheshimiwa ni kwamba umeme tukubaliane kwamba popote duniani ukitaka kuanza kiwanda sehemu zote duniani, ardhi inakuwepo, maji yanakuwepo, umeme unakuwepo na mambo ya usafirishaji. Tukiri kwamba saa zingine tunavutia watu wanajenga viwanda wakati hivyo vitu vyote vitatu havipo. Kwa hiyo, siyo sahihi kusimama na kuanza kusema Wizara hiyo na hiyo lakini wakati unaenda kujenga kiwanda hukuiuliza Wizara. Japokuwa tuna majukumu ya kupeleka umeme pale, hilo nalo lifahamike hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama tunavyojenga vyumba watu wanachelewa kutoa viwanja, watu wengine wanaenda kujenga milimani, halafu wanataka mabomba ya maji yaende milimani, umeme uende milimani, kwa hiyo ndiyo hali kama hiyo. Tujenge viwanda kwa mpangilio, badala ya kulaumu kwamba Wizara zina usingizi, katika Wizara inaheshimika duniani ni Wizara ya Nishati na Madini. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme ni mtizamo naomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tuache mtizamo kwamba dunia ya leo umeme utazalishwa na TANESCO peke yake, haiwezekani. Kwa sababu nikiwapa hapa bajeti yaani makisio ya umeme kati ya mwaka jana na mwaka 2020 tunahitaji dola bilioni 11.6. Kati ya mwaka 2021 na 2025 tunahitaji dola bilioni 5.9, haya mahesabu yatakuja kama Wizara imelala? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *power per capital* twende tunapiga hesabu sasa, *power per capital* sasa hivi ni *unit* 138 kwa mtu kwa mwaka. Wakati tutaingia kwenye kipato cha kati mwaka 2025 tukiwa watu milioni 70 na *GDP per capital* ikiwa 3000 inaamaanisha *GDP* yetu lazima iwe bilioni 211, *power per capital* lazima iwe zaidi ya *unit* 500 lakini ni bora ikawa 1400. Kwa hiyo, ndugu zangu nataka kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge huku Wizara ya Nishati na Madini tunaenda kwa mahesabu kweli kweli. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine hatutazalisha tu umeme ndani, ndiyo maana sasa hivi tumemaliza *transmission lines*, Mheshimiwa Rais akipata muda itabidi azindue, tumeongeza umeme mara mbili unaotoka Iringa, Dodoma, Shinyanga ndiyo maana umeme haukatikikatiki sasa hivi. *Transmission line* ile imetoka 220kv kwenda 400kv. Unataka matayarisho gani zaidi ya hayo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tunajenga *transmission line* kubwa vilevile, mmeona kutoa Singida, Arusha kwenda Kenya, lakini hii ya Kenya, Kenya watajenga kilovolti 400 kuunganisha na Ethiopia, Ethiopia itaunganisha na Egypt n kilovolti 500. Tumeshanza hata mahesabu ya kununua umeme wa bei ndogo kutoka Ethiopia. Duniani kote kuna kitu kinaitwa *power trade* hata ingekuwa na Mtanzania anatuuzia umeme wa bei mbaya miaka michache inayokuja hatutanunua. Umeme wa Ethiopia bei ya kwanza bado tunajadiliana nayo ni 7.5 *US cents per unit*, hatujasaini kwa sababu tutatumia miundombinu inayopita Kenya inaitwa *willing charges* hatuwezi kusaini hiyo mpaka tujue Kenya watatu-charge kiasi gani kwa *unit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo umeme wa Ethiopia unaweza kwenda mpaka huku Zambia watautumia na sisi tutawa-charge, halafu tunajenga *transmission line* ya kutoka Tanzania kwenda Zambia tuungane na *power pool* ya Kusini. Hakuna usingizi Wizara ya Nishati na Madini hamna kitu kama hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu upande wa Kaskazini huku Bukoba sasa hivi wanatumia umeme wa Uganda ambao ni megawati 18. Ndugu zangu wengine wa Sumbawanga wanatumia umeme wa Zambia megawati Nne, Kenya wanaleta megawati moja. Sasa tunachokifanya na hivi karibuni tutaenda kuzindua ni Rusumo megawati 70 kwa nchi tatu, lakini tunajenga *transmission line* ya kutoka Rusumu kuja Nyakanazi. Wakati huo huo tunajenga kutoka *transmission line* kubwa kutoka Mbeya kuingia Sumbawanga mpaka Nyakazani, sasa haya nilivyosema ni mabilioni. Kwa mfano, *transmission line* kwa miaka minne ninahitaji dola bilioni 3.7. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, yote haya tunayafanya Wizara na Nishati na Madini tukiwa tunajua kwamba tunakuwa nchi ya kipato cha kati, lakini lazima uchumi ukue na uchumi kukua ni umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapinduzi ya uchumi (*industrial revolution*) mwaka 1746 yalichukua miaka 100 na yalihatiji vitu vitatu; yalikuwepo makaa ya mawe, chuma zamani ilikuwa ni viwanda vya pamba, baadaye ikaja *revolution* ya pili ndio ambayo ilienda kwenye mambo ya usafirishaji. Mapinduzi ya viwanda hayasimami, sasa hivi wakati sisi tunang'ang'ana na hivi viwanda vya chuma mapinduzi ya viwanda sasa hivi duniani ni *non-technologies*. Vitu ambavyo vina size ya unywele wako, ndiyo *revolution* iliyoko duniani sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii ya kuweka *solar panels* inaanza kupitwa na wakati, majaribio yanafanyika Sahara watu wachukue umeme kutoka kwenye mchanga. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nataka kuwathibitishia kwamba umeme wa uhakika utakuja na ndiyo maana napenda nirudie, ndiyo maana mimi nilikataa bei ya umeme kupanda kwa sababu huwezi ukajenga viwanda. Sasa niliyekataa bei ya umeme kupanda halafu eti nashtakiwa tena. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Profesa. Mheshimiwa Mwijage Waziri wa Viwanda.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi kuchangia taarifa mbili za Kamati. Kipekee niwapongeze Wenyeviti wa Kamati hizi mbili, Wajumbe wa Kamati lakini kipekee Waheshimiwa Wabunge ambao mmeshiriki kuchangia hizi Kamati mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma sana taarifa hizi mbili, lakini nimesoma kipekee taarifa iliyohusu mahsusii suala la viwanda, biashara na uwekezaji. Ninawaunga mkono, nataka niwaambie pale ninapotofautiana na ninyi. Serikalii haina mpango wa kutwaa kiwanda na kukiendesha, haijaandikwa mahali popote wala sijawahi kuelekezwa na mkuu wangu wa kazi au tajiri namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaambia wenye viwanda, vile viwanda vihakikishe vinafanya kazi, wasipofanya kazi tutawapa wengine waviendeshe. Ndugu yangu wa Tabora, kwetu kuna methali moja inasema asiyemhurumia chura anasema chura hafi kwa mpini ukimpiga. Nimekwenda kwa Ndugu Rajan mimi, Rajanialikufa nikamfuata mtoto wake wa Uingereza nikaongea naye, kiwanda cha nyuzi kitaanza. Ndugu Gulamali kila siku ananifuata ili kusudi turudishe Manonga. Igembe Nsabo wanakuja hapa kesho kutwa nifanye nini Mwijage? Kwa hiyo, huo ndiyo msimamo wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msiwaoneshe Watanzania kwamba tuna hali mbaya, nimepewa dhamana hii Novemba, 2015 ngoja niwape taarifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, TIC wamesajili viwanda 170, BRELA viwanda 180 nina taarifa. Mbali na taarifa ya Kamati na mimi nina taarifa yangu nimefanya nini na nitaiwasilisha. Unapozungumza EPZA viwanda 41, NDC viwanda saba na vitatu vikiwa ni vya dawa. Unapokuja SIDO wameratibu viwanda 1,843 mpaka sasa ninapozungumza nina viwanda 2,169; ndivyo hivyo viwanda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwaeleze Watanzania nimefurahishwa na jambo moja kwamba Watanzania tunawahamasisha watu wa nje tunawaacha watoto wa ndani, siwezi kufanya hivyo. Hata nilipokuja hapa saa nane nilikuwa nawahamasisha Watanzania, niwaeleze ndugu yangu Mavunde, kesho kutwa tunakwenda kuzindua kiwanda cha chaki chenye uwezo wa kuzalisha chaki hapa Dodoma, kimetengenezwa kwa gharama ya milioni 20 kitaweza kuzalisha na kiwanda kipo hapa.

Kwa hiyo, ningependa tuzungumze ukweli. Msiwatie hofu ushauri wote utazingatiwa msiwatie hofu Watanzania kwamba hatuendi...

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda mbele.

MWENYEKITI: Taarifa, kaa kidogo Mheshimiwa Waziri.

TAARIFA

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe Waziri taarifa kwamba kwa mpango mkakati wa Serikali wa miradi mikakati yote iliyoletwa mwaka huu wa fedha ikiwepo Mchuchuma, ikiwepo *General Tyre* na miradi mingine hakuna hata mradi mmoja ambao Serikali sasa imeshaelekeza fedha.

Kwa hiyo, kama kuna viwanda vidogovidogo vinavyoanzishwa tunataka mkakati wa Serikali ule ambao unaseme ni shilingi ngapi imepelekwa kule, kwa sababu hakuna fedha zilizopelekwa, asitudanganye hapa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waziri unasemaje?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni Mjumbe wa Kamati yangu, taarifa uliyonipa naikubali na naipokea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu zilindwe, kuna kitu kinaitwa *mis-conception*...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, utulivu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kinaitwa *misconception*.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu!

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Mpango amewaeleza, Serikali haijengi viwanda ila Serikali inaweka mazingira ya kujenga viwanda. Mchuchuma na Liganga ametueleza, Mheshimiwa Ridhiwani amekuambia anakualika ukienda Chalinze usimame uangalie, Mkuranga umealikwa. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa hizo nyanya unazolima mimi nina fursa ninaweza nikakupa kiwanda. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu niwaambie kitu kimoja Wabunge waelewe, unajua Wabunge mnajichanganya, mnasema Watanzania wazawa wawezeshwe, wapewe fursa msiagize wageni, lakini ninyi wazawa kuna mzawa kuliko Mbunge, unyanyuke wewe Mbunge. Asubuhi nimejibu swali kuhusu zile taulo za akina dada, niwaeleze kuna Waheshimiwa Wabunge wawili hapa tunahangaika kuleta teknolojia ya kutengeneza vitu, msilogope kuwa na utajiri ilimradi huo utajiri usiuipe. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mjiandae kumiliki useme kiwanda hiki ni changu na hiki ni changu. Mheshimiwa hapa tumekubaliana alete *proposal*. Juzi nimeitisha semina hapa ya *venture capital* nikawaleta hapa, wanasema pesa wanazo. Kuna Wabunge walijitolea wakaja wakaangalia, waliposema dola bilioni kumi kumpa mwekezaji nikawaambia msiwadanganye Wabunge. Mtu akasimama akasema we *have money* mjitokeze. Hauwezi kulala kitandani ukapewa *lift* lazima uingie barabarani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie viwanda vilivyobinafsishwa, hali siyo mbaya hivyo, ila yeyote aliyepewa kiwanda kulingana na masharti viwanda vitatwaliwa. Ninayo ripoti ya viwanda kumi ambavyo vinakwenda kwa AG na viwanda vitatwaliwa, Lakini safari yetu ni miaka mitano, ndiyo naanza kazi sasa hivi mnaanza kusema. Hivi unategemea unaweza kujenga viwanda kwa shilingi bilioni 42. Kiwanda cha Mkuranga mnachosikia ni bilioni zaidi ya 80. Serikali haijengi viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la EPZA. Tunalitambua suala la EPZA! EPZA inayoniama ni *Special Economic Zone* ya Bagamoyo. Maamuzi yametolewa na Serikali namna gani wananchi wa Bagamoyo watakavyoweza kufidiwa. Liko suala la EPZA, *Special Economic Zone* ya Bunda, timu yangu imekwenda, nimshukuru Mjuku wangu, wamekwenda Bunda, wamepeva ushirikiano, wale waliokula pesa za Serikali watakamatwa na watajuana na Mheshimiwa Mwigulu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe kitu kimoja Waheshimiwa Wabunge, viwanda tunavyojenga ni kwa ajili yetu, kamateni maeneo kwa ajili ya familia zenu. Mheshimiwa Simbachawene ametoa maelekezo namna gani katika Serikali ngazi za vijiji na mikoa mtakavyoweza kutunza maeneo na kuweza kuwapa vijana wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kilimo nusu. Katika viwanda vilivyotengeneza ninavyowaambia kuna Kiwanda cha TAMCO, tumeshakibadilisha kuwa kiwanda cha kuunga matrekta na ninavyozungumza sasa vifaa vya kutengeneza matrekta 340 vimeshafika Kibaha na tunalenga kutengeneza matrekta 2004 Kibaha kabla ya mwisho wa mwaka huu na yote nimepeva dhamana nitayagawa mimi. Sasa kama ulikuwa unalima na jembe, nitakupa trekta, ndiyo namna ya kuongeza tija katika kilimo. Kwa hiyo, viwanda ninavyovihasabu ni cha Urususi cha matrekta kiko TAMCO. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kipekee ambalo baadhi ya Wabunge mmezungumza ni viwanda vya dawa na dhamana hiyo iko chini ya Makamu wa Rais. Makamu wa Rais amenielekeza pamoja na Waziri wa Afya, tuandae wawekezaji juu ya kuwekeza kwenye viwanda tiba, ndiyo kazi ambayo tunawaita wawekezaji kutoka Misri, ndiyo kazi ambayo tunawaita wawekezaji kutoka Uturuki, China *and the response is good*. Kwa hiyo, Waheshimiwa msijione wanyonge Watanzania, ninyi Wabunge mkijiona wanyonge wananchi wenu watanyong'onyea! Tanzania sasa tunajenga viwanda, msidhani kwamba hamuwezi na mjifunze kumiliki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru watu wa Kigoma. Tunasaidiana na watu wa Kigoma kwenye kilimo cha michikichi na miwa, nichukue fursa hii pia wawekezaji wote waliochukua maeneo ya kulima miwa, kufikia mwezi wa nane atakayekuwa hakufika *site* nitampeleka kwa Mheshimiwa Lukuvi, tutamnyang'anya eneo, ikiwemo *Kibondo Sugar*, ikiwemo *Kigoma Sugar*. Waheshimiwa kazi zinafanyika, lakini kama nilivyosema hii ni ripoti ya wenyewe na ripoti ya kwangu iko hapa, siku mtakapoiona mtacheka na kufurahi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mambo mahsusuni, suala la Urafiki. Ubinafsishaji wa Kiwanda cha Urafiki una masharti. Upande wangu kwa dhamana yangu, nilishazungumza na watu wa *Foreign Affairs* yule mwekezaji aondoke, aletwe mwingine kusudi awekeze kwa malengo. Ule ufisadi mnaozungumza ni historia na mimi nimeukuta, lakini mimi siyo *expert* wa kufukua makaburi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu viwanda vya kilimo, uvuvi na mifugo. Nakushukuru Mheshimiwa Nsanzugwanko, ndivyo Mpango wa Pili wa Miaka Mitano unavyosema. Ndiyo maana kuna mkakati mmoja wa mwaka jana niliou-*launch* mimi na Ndugu Mwigulu, unasema *cotton to clothing*, unasema *leather and leather by products*, unasema kuhusu maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Njombe anajua, leo nimempa muhtasari wa Kikao cha SAGCOT ambapo ng'ombe 3,000 wataletwa kupelekwa Njombe ili watoe maziwa, ili maziwa hayo yaweze kutosheleza viwanda vya maziwa vya ASAS na viwanda vya Njombe vya

maziwa. Tunafanya kazi, lakini kama nilivyosema asiyehurumia chura, anasema hata ukimpiga kwa jiwe hawezi kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikataba ya Viwanda vya Korosho, kwa kipekee nilikuwa nalishughulikia suala hili, lakini suala hili nakwenda kulimiliki na nitakufa navyo. Viwanda vya Korosho nitakufa navyo, naviperemba nikimaliza nampelekea Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana. Viwanda vyote vilivyobinafsishwa mwenye navyo ni *Treasurer Registrar*, kwa hiyo, viwanda vyote tutavishughulikia. Hii kazi nirudie tena, siyo kazi ya mtu mmoja, tukishinda Taifa letu limeshinda na tukishinda tushinde wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kwa mara nyingine niwaeleze; Serikali yetu ya Tanzania katika Taarifa ya Kamati kwamba, Serikali ina matatizo na wawekezaji. Mimi ndiye *receptionist*, wawekezaji wote wanakuja kwangu kila siku, nimehamia Dodoma kila siku wanakuja hapa. Hakuna mwekezaji amekuja kwangu akashindwa kuhudumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie pale wanapokosea, usijidanganye kwenda kwa tajiri namba moja au Makamu wa Rais au kwa Waziri Mkuu...

MHE. HALIMA J. MDEE: Dakika kumi zimeisha! Anatupotezea muda huyo!

WAZIRI WA VIWANDA NA BIAHARA: ...kama unataka kuwaona wakubwa uje unione mimi. Mimi ndiyo nitakufanyia mpango ukamuone Mheshimiwa Rais, huwezi kutoka huko ukaenda kwa baba bila kupita kwa mwana, njooni hapa nitawafanyia mipango, huo ndiyo utaratibu. Kwa hiyo, Serikali hii ni *friendly*, inapenda wawekezaji. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE: Muda!

WAZIRI WA VIWANDA NA BIAHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru binti Katimba kwa sababu ya upatikanaji wa malighafi. Mheshimiwa Katimba ngoja nikwambie, nimepata mwekezaji, muulize dada yako wa Uvinza, tunakwenda kule Itamigaze na ndugu yako Mheshimiwa Zitto, tutapanda Migaze Kigoma, lakini Migaze ya leo haiwezi kuzidi ya kesho. Kuna kipindi kirefu, tutafanya kazi sisi ambayo ni manufaa kwa vijana wetu. Waheshimiwa Wabunge, watu wasikate tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru watu wa Kamati mmenipa changamoto, lakini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana, tunaendelea. Namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ahitimishe hoja yake kwa muda usiozidi dakika 15. Mheshimiwa Dkt. Kafumu, karibu. *(Makofi)*

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIAHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nihitimishe hoja hii muhimu sana katika historia ya maisha ya Tanzania yetu. Tunataka nchi yetu iwe nchi ya viwanda ifikapo 2025.

Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge mliochangia, tulikuwa na wachangiaji 37, kumi na sita wamechangia kwa maandishi na kwa maneno wamechangia Waheshimiwa Wabunge 21 pamoja na Mawaziri, ahsanteni sana kwa michango yenu. Kamati tunashukuru sana kwa hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, suala la kujenga viwanda katika Tanzania ni suala la kufa na kupona na ndiyo maana liko kwenye awamu hii ya Mpango wa Maendeleo. Tulianza kama Mbunge mmoja alivyosema kuweka mazingira. Tulitakiwa tuwe tumeshamaliza kuweka mazingira ya miundombinu halafu tuanze ku-*industrialise* lakini hatukuweza. Kwa hiyo, sasa tuna-*industrialise* wakati huo huo tunaweka mazingira. Kwa hiyo, ni jambo letu sisi wote ni jambo la kufa na kupona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kusema ni jambo la *coordination*, Serikali inafanya kazi *individually* mmoja-mmoja. Nishati na Madini yuko kwake, Kilimo yuko kwake, kila mtu yuko peke yake. Mimi nilitarajia maprofesa pamoja na madaktari, Serikali ina madaktari na maprofesa, mkutane wote, Wizara zote mkutane mtengeneze *road map* ambayo itatupeleka, lakini mnapofanya kazi kila mtu peke yake hatutafika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Waziri wa Nishati umeeleza vizuri sana juhudi ambazo tunataka kuleta umeme, lakini uko peke yako, hufanyi kazi na wenzako. Mheshimiwa Profesa Waziri wa Kilimo ni Daktari wa Kilimo yule na yeye yuko peke yake. Msipokutana tukatengeneza kitu kimoja hatutafika. Kamati tunadhani mkakati wa pamoja wa Serikali nzima unatakiwa ufanyike, vinginevyo hatufiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sekta binafsi kuhamasishwa mmesema vizuri sana, Waziri wa Fedha amesema vizuri na baadhi ya Wabunge, huo mtazamo, pamoja na Waziri wa Viwanda hapa, mtazamo wa kwenda kwenye ujamaa hatuutaki. Sasa hivi *we are not going back to ujamaa*, tunataka sekta binafsi ijenge uchumi. Serikali inaweza kuwa na viwanda vya kimkakati vichache, lakini mnavyofikiria kutwaa viwanda na kuviendeleza, nashukuru Waziri wa Viwanda na Biashara amesema hapa, yeye ni *coordinator* ili sekta binafsi iweze kujenga viwanda pamoja na Serikali kwa namna ya pekee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pesa kutokupelekwa limesemwa sana. Waziri wa Fedha ameeleza vizuri pale, wanahangaika na kukusanya, lakini ni jambo ambalo tumelipata kwa wadau, tumelipata kwenye Mawizara ni tatizo letu sisi sote, ni lazima tulichukulie kwa upana wake kwamba, fedha lazima zipatikane na zipelekwe. Tunapopanga Bungeni humu, basi tupange bajeti ambayo ni *realistic*, tutaweza kupata fedha na kuzipeleka, lakini tunapopanga tu bajeti ambayo haina fedha tunakuwa kama tunawadanganya wananchi, siyo jambo zuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu limesemwa sana na wadau. Tunamuomba Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, pamoja na juhudi zote hizi lakini tatizo bado lipo. Ukienda kwenye kiwanda chochote utakuta wanasema umeme unakatika katika kweli na wengine mpaka wanafunga viwanda, wengine mitambo inaharibika, kwa hiyo, ni jambo lipo. Pamoja na mikakati ya kisayansi na nini, lakini umeme bado ni shida. Tukubaliane kwa kweli, pamoja tuende ili tufike mahali panapohitajika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Wabunge wamesema ambalo nataka nili-echo tena, malighafi tutumie, tunapojenga viwanda tutumie malighafi ambazo zinagusa watu, kilimo, uvuvi na mifugo. Ukianzisha kiwanda cha *tiles* kama cha ndugu yangu kule unaweza ukawanavyo 200, lakini wananchi umaskini unaendelea. Kwa hiyo, kuna suala la maendeleo (*growth* ya uchumi), lakini kuna suala la *economic development* pia, maendeleo ni tofauti na kukua kwa uchumi, unaweza ukakuza uchumi, lakini wananchi bado wanahangaika.

Kwa hiyo, ni lazima tutumie hizi bidhaa, malighafi za Tanzania za kilimo, mifugo na uvuvi na zingine tuzijenge viwanda. Hii itatusaidia sana na Wabunge wengi wamesema na mimi naunga mkono jambo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira rahisi ya kufanyia biashara wamesema Wabunge sana. Narudia tena kwa kusema ni lazima mwekezaji akija awe wa ndani au nje, ajisikie amepokelewa. Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mheshimiwa Mwijage, wawekezaji wengi bado wanalalamika, pamoja na kwamba upo vizuri, lakini wenzako sasa, mtu akienda ardhi kule anaweza akakimbia, akienda madini kule anaweza akakimbia, akienda kilimo anakimbia, wewe uko vizuri. Kwa hiyo, *coordination* ni muhimu, lazima m-*coordinate* mfanye vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya kufanya biashara wadau wamelalamika sana. Kwa kweli ni jambo letu sisi sote na sisi Kamati hatukutoa hii ripoti kwa sababu ya kuipiga Serikali, hapana. Tumetoa hali halisi tu inavyoonekana huko kwa wadau ili tushughulikie jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu namaliza, jambo kubwa la mazingira. Mazingira ni jambo kubwa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, uharibifu wa mazingira ni mkubwa kuliko tunavyofikiria. Tuna mpango wa kupanda miti lakini hautekelezeki. Tuliliomba Bunge mwaka jana uanzishwe mfuko na fedha za tozo zote ziingie kwenye mfuko. Tumeweka pendekezo, tumeweka Azimio la Bunge kwamba bajeti ijayo tozo zote za kimazingira ziingie kule na mfuko huu uwe na fedha ili tuweze kutunza mazingira, vinginevyo tutaimba sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ziwa Victoria ni vizuri niurudie, unakamilika mwezi wa 12, lakini *effect* yake ni ndogo. Naishauri Serikali kama mnaweza kuanzisha mradi mwingine katika viunga vya Afrika Mashariki utakaoshughulikia zaidi mito hii mikubwa ambayo inaleta maji, tunaweza kulitunza ziwa letu vizuri zaidi, lakini uvuvi haramu ni tatizo kubwa sana. Serikali lazima mliangalie hili, Wizara ya Kilimo, wote tushirikiane ili tuweze kuondokana na jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi ni jambo kubwa pia. Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema, Tanzania ya mwaka 68 na Tanzania ya leo ni tofauti. Mito imekauka, maziwa yamekauka, vitu vingi vimekauka na sisi wote ni mashahidi. Kwa hiyo, ni lazima tulitazame jambo hili kwa namna ya tofauti na ninaiomba Serikali katika kutengeneza miradi na katika kuzungumza na wadau wa maendeleo ni lazima tupate fedha kwa ajili ya *curb* jambo hili, tusipolitazama vizuri mambo yetu yataendelea kuwa mabaya zaidi. Nasema suala la mazingira ni mtambuka na lazima tushirikiane kama nilivyosema awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni maazimio. Haya maazimio tuliyoyapita, naomba ni-echo yale aliyoyasema Mheshimiwa Nsanzugwanko na mimi wakati nawasilisha hapa nilisema. Maazimio haya ni maazimio muhimu sana, hatutaki yakabaki kwenye *shelf* za Bunge, hebu tutengeneze utaratibu wa kuyafuatilia kama Wabunge. Tukiunda Kamati Ndogo ya kuyafuatilia, tunajadiliana na Serikali maana hili ni jambo letu wote siyo kwamba tunapingana ni jambo letu wote, tusigombe fito. Tutengeneze Kamati ambayo itafuatilia na Serikali itakuwa inatupa mambo kwa uzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nizungumzie viwanda ambavyo vimesemwa na Wabunge. Mbunge wa Mkuranga kasema ana viwanda sijui vingapi 56 na viwanda 11 jumla 67, pia Waziri anasema ana viwanda 1,149 sijui, kama namba nimeishika vizuri.

WAZIRI WA VIWANDA, BIAHARA NA UWEKEZAJI: Ni viwanda 1,169.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE VIWANDA, BIAHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda 1,169.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi Mheshimiwa Waziri, Kamati yangu haina taarifa kabisa. *Interpretation* yetu kama Kamati ni kwamba Waziri hushirikiani na sisi vizuri. (Makofi/Kicheko)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mjibu msanii huyo. (Makofi/Kicheko)

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama kungekuwa na ushirikiano tungekuwa tuna habari, hata kufunguliwa kwa kiwanda cha Mkuranga au wapi, hata Mwenyekiti tu angeenda. Hata Mjumbe mmoja tu hizi habari tungekuwa nazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, ninatamuomba Mheshimiwa Rais labda amuongeze Naibu Waziri inawezekana ana shughuli nyingi sana ili tuweze kumpata Waziri kirahisi zaidi. Vinginevyo, Kamati tunafanya kazi peke yetu Mheshimiwa Waziri, sasa hii siyo sawa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba Bunge lako lipokee Taarifa ya Kamati na kuwa maamuzi ya Bunge. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Toa hoja.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Haya, *order!* Waheshimiwa Wabunge, utulivu! Hoja imetolewa, imeungwa mkono na Wabunge zaidi ya 10. Kwa hiyo, sasa naitoa kwenu kwa uamuzi!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja inayofuata, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha Hoja ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kama tulivyoiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze wewe Mwenyekiti kwa kuongoza vizuri, lakini naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri waliochangia hoja hii, pia nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuchangia tena hoja hii. Tumepata wachangiaji 16 kwenye hoja hii na wengine 14 wamechangia kwa maandishi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata hoja za wachangiaji tofauti na mchangiaji wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Joseph Haule ameongelea mikataba ya Chuo Kikuu na *Mlimani City*, ameongelea mikataba ya *TANESCO*, ameongelea mikopo inayodaiwa na *TANESCO* na *PSPF*. Kamati inakubaliana na yeye kwamba hii mikataba kama tulivyosema kwenye ripoti yetu

iweze kuangaliwa upya kwa sababu tunaamini kwamba hii asilimia kumi wanayoipokea katika miaka 50 ni ndogo sana, huenda thamani halisi baadae ikawa siyo nzuri. Kwa hiyo, tunaamini kwamba mapendekezo ya Kamati yaweze kuzingatiwa na yaweze kufanyiwa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba ya TANESCO kama Mheshimiwa Waziri alivyoongea na Kamati yetu imeongea vizuri, ni mategemeo yangu kwanza kipengele cha mikataba kama AG alivyosema nayo Kamati inashauri iweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ambayo Serikali inadaiwa na PSPF tunakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeongea, ni concern ya Kamati kwamba speed inayotumiwa kuhakiki na kulipa madeni ni ndogo sana. Kwa hiyo, Kamati inaona kwamba Serikali bado hapa haijafanya juhudi kubwa, tunaomba kwamba Serikali iweze kuendelea na juhudi kubwa zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wameongelea vile vile Ofisi ya TR kwamba kwa nini Ofisi ya TR iwe ni msimamizi wa mifuko. Waheshimiwa Wabunge ndiyo tuliotunga sheria hii mwaka 2010, Cap. 370 tulitunga ambayo mifuko inawekeza fedha nyingi na TR ndiye msimamizi wa Serikali. Kwa hiyo, ni wajibu wa TR kuhakikisha kwamba shughuli zote za Serikali na mashirika yake inaziangalia, na ni hakika kwamba Msajili ni kazi yake kuziangalia hizi sheria. Ukiangalia sheria inayounda Mifuko ya Hifadhi inaangaliwa vile vile na Benki Kuu na SSRA, lakini ni kazi ya TR tena kufanya uhakiki wa mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wengi wameongelea kuhusu bodi na wengine wameenda mbele zaidi kuongelea mambo ya TANAPA. Kamati tumesema bayana, hatujaficha, Serikali ni wavivu katika kuteua bodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Mamlaka ya Uteuzi nafikiri haipelekewi mapendekezo mapema kiasi kwamba, mfano kwenye mashirika 41 tuliyokutana nayo; mashirika 13 yalikuwa hayana bodi na yapo mashirika mengine tuliamua kuyarudisha kwa sababu Mwenyekiti wa Bodi hakuwepo. Kwa hiyo, ni vizuri mamlaka zinazohusika ziweze kuteua bodi. Hata hivyo, tunaipongeza Serikali mmeanza kuchukua hatua, tunaomba hiyo hatua iendeleo ili muweze kukamilisha mashirika yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa suala la *National Housing*, Mheshimiwa Omary Mgumba amesema haiwezekani *National Housing* ijenge, isimamie yenyewe, ikague ubora na kila kitu. Kwa hiyo, Wajumbe wana wasiwasi kwamba lazima kuwe na chombo kingine cha kuihakiki *National Housing* ili kuangalia *accountability* kwa sababu ni shirika hilo hilo linaloshughulikia mambo yote. Kamati imependekeza na iko kwenye mapendekezo ili Serikali iweze kuyaangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata mchango mwingine unaohusiana na TBA kwamba sasa hivi kuna mwamko TBA iweze kujenga majengo, je, nani anaikagua hii kampuni na haitoi gawio kwa Serikali. Kwa hiyo, nalo hilo Wajumbe wamelichangia nalo tunahisi kwamba Serikali iweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo walioonesha masikitiko makubwa. Waheshimiwa Wabunge, Serikali hii ina mashirika na taasisi 264 na mtaji wa mashirika haya yote ya Tanzania ukiyajumlisha ni trilioni 23 lakini faida kwa mwaka kwa mashirika yote ya Tanzania yenye mtaji wa trilioni 23 yanaleta faida ya bilioni 422 ambayo ni asilimia 1.83 ambayo Kamati hairidhiki. Huwezi kuwa na mtaji wa trilioni 23 ukaleta faida kidogo namna hii. Hata kama ingeweza kuleta *ten percent* ingeweza kuiingiza Serikali trilioni 2.3 ikaweza ku-boost mapato ya Serikali. Kwa hiyo,

TR anayo kazi kubwa kuhakikisha kwamba mchango wa mashirika haya lazima uongezeke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wameongelea tena mashirika mengine kama STAMICO ambayo kwa kweli na sisi ni kampuni ambayo tulihoji inaenda kwa hasara, inatumia ruzuku ya Serikali na huku ni msimamizi wa madini. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kama Wizara iweze kuipa nguvu hili Shirika la STAMICO na kuipa mitaji ili iweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lulida ameongelea jambo moja pale la kusema pale kuna mwekezaji kwenye national housing pale Kawe ni kweli. Kamati tumetembelea pale ule uwekezaji wote uliopo Kawe wa *National Housing* yuko mwekezaji mmoja mmbia ambaye viwanja vile kweli alinunua kwa milioni sita mwaka 1995 nafikiri. Lakini yeye ameingia ubia na *National Housing* kwa *fifty fifty*, miradi ile ni mikubwa lakini yeye ametumia bilioni sita kuingia kwenye mikataba mikubwa. Haya ni mambo ambayo yanaendelea kwenye uwekezaji wa mitaji ya umma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru tena Wizara kwa kuteua Bodi ya TANAPA, kama Mheshimiwa Nsanzugwanko alivyosema kuna kesi iliamuliwa pale ambayo ilitakiwa shilingi bilioni 10 ziwe zimeletwa Serikalini kwa ajili ya kutoza, lakini nashukuru kwamba imechelewa kwa miaka mitatu hatujui Kamati tunajiliza kesi inaamuliwa kwamba shilingi bilioni 10 ziingie Serikalini lakini bodi haiteuliwi ili iweze ku-effect hizo fedha zije, zinakaa miaka mitatu, Kamati inajiliza kulikuwa na nini? Kwa hiyo, tunashukuru sana kwamba Mheshimiwa Waziri amesema sasa bodi imeteuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni; Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameyaongelea vizuri lakini yapo madeni ya majeshi, maji kwenye taasisi za Serikali, hayo nayo ni muhimu sana muweze kuyafanyia malipo ili kunasua hizi taasisi za umma ziweze kujiendesha. Kwa kweli ukikutana nao wanasikitika, tungeomba muweze kuwasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mwongozo wa TR ambao unasema mashirika ya umma yaweze kutumia asilimia kumi tu ya mapato yote, lakini yapo mashirika katika uchambuzi wetu tumekuta yanatumia zaidi ya asilimia kumi. Kwa hiyo, ni mategemeo yetu kwenye mapendekezo kwamba Serikali itaweza kuyachukua.

Lipo pendekezo moja la Mheshimiwa Elibariki Kingu ambaye ameenda kinyume, anasema haafiki kabisa kwamba TR aweze kusimamia mifuko ya jamii kwa sababu TR anayo mashirika mengi. Tukumbuke Mheshimiwa Kingu ni kwamba tulishatunga sheria, mpaka sheria itakapobadilishwa. Ni haki ya TR kuhakikisha kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nayo anaiangalia kwa sababu inaweka uwekezaji na Serikali ndiyo inadhamini hata kama watakuwa wameshindwa kulipa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha sasa naomba Bunge lako likubali maazimio na mapendekezo ya Kamati kama yalivyopendekezwa kwenye kitabu chetu. Baada ya kusema hayo nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitaitoa kwenu hoja hiyo muiamue.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninawashukuru sana kwa kazi kubwa mliyoifanya kwa siku ya leo kwa hizi hoja mbili. Nianze kuwashukuru Wenyeviti wenyewe na Wajumbe wa Kamati hizo mbili, ni taarifa nzuri. Pia majibu ya kufafanua yaliyotolewa na Serikali nadhani hoja kubwa ni hiyo ambayo imesemwa kwenye ya Kamati *follow-up* ya maamuzi haya. Sasa hili suala zito pamoja na kwamba Kanuni ya 117(18) inaruhusu kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuunda Kamati Ndogo kufanya shughuli ambazo zitatolewa na Kamati husika. Sidhani kwamba huo utakuwa ni utekelezaji bora wa maazimio hayo. (Makofi)

Sasa suala hili nadhani tulichukue tulipeleke kwa ngazi zinazohusika kwa maana ya kwamba Kamati ya Uongozi, maana mapendekezo haya yamo kwenye maazimio ambayo tumepitisha sasa hivi, yanaenda Serikalini lakini kwa vile hoja hizi ni za Kamati na Wenyeviti ndiyo Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, tuone namna nzuri sasa ya kupendekeza kwa Spika na baadae sasa hoja ikiiva irejeshwe Bungeni humu, turekebishe Kanuni zetu ili kuweza kutoa fursa hiyo. *Otherwise* tutakuwa tunaimba kila mwaka mawazo mazuri tu, Serikali inakuja na maelezo ya jumla kupitia kwenye hotuba za bajeti na kujibu maswali lakini tunabaki pale pale, lazima tuende mbele. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumekwenda vizuri sasa mniruhusu nitumie madaraka niliyonayo niongeze muda usiozidi dakika 30 tufanye kazi moja ya msingi ambayo asubuhi niliwasomea Kanuni ya 30(4) ambayo inaweka mpangilio wa shughuli za Bunge. Haki za Bunge huwa zinakuja mapema, ukiisoma ile Kanuni ya 30(4) unashuka nayo kama zipo zile shughuli ambazo zimetajwa, kama hazipo kwenye *Order Paper* hiyo ndiyo inakuwa *slotted* mapema.

Sasa niliruhusu twende namna hii kwa leo kwa sababu nilikuwa nataka nijiridhishe na mambo fulani fulani kama mwenye hoja hiyo ametimiza, nimejiridhisha ametimiza. (Makofi)

Kwa hiyo, namuita Mheshimiwa Waitara Mwitara awasilishe hatua ya kwanza ya yale maombi halafu tuone niipime haraka, nikiridhika twende; utawasilisha kwa muda usiozidi dakika tano ili nione kama tunaenda sawa kwenye haki za Bunge, karibu Mheshimiwa. (Makofi)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, wakati nimesoma Sheria ya Haki, Hadhi na Mamlaka ya Bunge Sehemu ya Pili kifungu cha tatu na kama ulivyosema nikaenda kutumia Kanuni ya 51(1) nikaona kwamba hii ni maeneo ambayo haki na hadhi ya Bunge itakuwa imekiukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa tulifanya mjadala na tukapendekeza baadhi ya mambo ambayo yaliwasilishwa hapa Bungeni na kwa hiyo yakaridhiwa na Bunge kama Taarifa Rasmi ya Bunge. Lakini baada ya pale ilionekana kwenye mtandao wa *facebook* na *clip* hii nimempa Joshua ambaye ni miongoni mwa watumishi wa Bunge hili, kama ungeruhusu angeweza kuweka ile *clip* ili Wabunge wakaona kilichozungumzwa na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru anaitwa Alexander Pastory Mnyeti. Mkuu wa Wilaya anasema; "Huu ni upuuzi mtupu, Wabunge hawa hawajielewi nawashauri fanyeni kazi zenu." Hiyo ni taarifa ambayo ilitoka kwenye mtandao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ndio pia yamejirudia wakati nikiangalia *Clouds tv* Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akisema sisi humu tunasinzia na kwa hiyo unaweza kuona kama muendelezo.

Lakini ukisoma Katiba Ibara ya 63(2) inasema hili Bunge ndio chombo kikuu kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali. Lakini hiyo kama haitoshi hawa wanaosema maneno haya ni watu ambao Bunge hili Tukufu linatunga bajeti kuwalipa mishahara na vitendea kazi ikiwepo na magari yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisoma pia ibara ya 100(1) pia tulikuwa na uhuru wa kujadili humu ndani bila kuingiliwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na ukisoma taarifa ya Kamati yetu ya Utawala na Serikali za Mitaa ukurasa wa 37, 38 na 39 tulielezea kwa ujumla wake mambo ambayo yanafanyika, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kuweka Wabunge ndani Waheshimiwa Madiwani, watumishi wa umma na huu utawala ambao kimsingi haufuati utawala wa kisheria na haki zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia pia sheria ambayo inawapa mamlaka ya kukamata na kuweka ndani Wakuu wa Wilaya, kwenye Sheria ile ya Serikali za Mitaa Ibara ya 7(1) na (2) na Ibara ya 15(1) na ya (2) kwa ma-DC. Mambo haya yote ukiyaangalia kwa maoni yangu nikaona kwamba Bunge na kwa uwezo wako kama mtu ambaye umekuwa kiongozi mkubwa nchi hii, umekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sasa hivi umekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, umebobea katika Bunge hili na mwanasheria mbobezi kimsingi ni kipindi ambacho Bunge linaingia katika majaribu makubwa ya kudharauliwa na kusiginwa haki zake kwa kiasi ambacho hata kwa kauli hizi ambazo zinatolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekanaje Kamati ya Bunge inajadili tumekuja tumewasilisha, tunakula kiapo humu, tunaomba Mungu atujalie tuamue vizuri kwa niaba ya Watanzania wetu halafu Mkuu wa Wilaya anasema hawa ni wapuuzi na Mkuu wa Mkoa anasema hawa wanasinzia tu, hawanitishi na hawanibabaishi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaruhusu yupo Mbunge mwingine alipigiwa simu pia na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akasema hawa Wabunge, ukimpa nafasi atasema; hawa Wabunge sisi hapa hatuna lolote na hatumtishi hatumbabaishi. Kwa mtazamo wangu nijiridhishe kwamba tulikaa kwenye Kamati kwa muda wote ambao tumetoka tukajadili nikaona kwamba kwakweli tumeradhaurika na hii inakiuka kabisa Sheria hii ya Haki, Hadhi na Madaraka ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuomba kwa heshima kubwa uniruhusu nitoe hoja kama itakupendeza ili Wabunge waweze kujadili na tupate Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ndiyo maana nilikupa ueleze kwa kifupi tu kwanza ili nipime kama kweli hayo unayoyasema kwa kifupi yanaangukia kwenye Haki za Bunge kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano.

Sasa nimeridhika na hiyo ila na maeneo ambayo yanahusu kinga ya Bunge hili kama taasisi na wajumbe wake, ile sheria ya *Regional Administration* inasimama peke yake, kwa hiyo, nielekeze katika maelezo yako sasa jielekeze katika sheria yenyewe ambayo unasema sasa na uunganishe na kufafanua sasa ili hoja unayoitoa itakapoungwa mkono mimi ntaitoa kwa Wabunge hawa kwa muda mfupi wachangie halafu tuamue. (Makofi)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na ndiyo maana Mbunge mmoja akasema ukiwa kwenye hiki kiti watu wanakuwa na amani sana, mimi ni miongoni mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru niachane na ile Sheria ya Madaraka ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kukamata na kuweka ndani. Kama nilivyosema ni kwamba taarifa hii kimsingi bahati nzuri sio ya kwangu peke yangu, ni taarifa ambayo tulijadili kwenye Kamati na Wajumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa wanajua. Tumekuja hapa yakatokea matamko ambayo Mkuu wa Wilaya ameyasema na kimsingi kwenye taarifa hii hatukumtaja mtu lakini yeye kwa kujishuku, kwa kujihisi akaenda hadharani akaingia kwenye mitandao na akasema sisi ni wapuuzi kwa namna ambavyo nimemnukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inasema vizuri, kama nilivyosema, Sehemu ya Pili Ibara ya Tatu, kwamba sisi kama Wabunge tukishajadili jambo humu ndani haiwezekani mtu mwingine yeyote awae akaenda kuhoji tena mtaani huko, eti Wabunge walijadili kitu gani katika eneo hili. Na niseme tu kwamba hili jambo Waheshimiwa Wabunge sio jambo la Mheshimiwa Waitara, sio jambo la Upinzani, kama alivyosema Mwenyekiti, ni jambo la hadhi ya Bunge sisi kwa ujumla wetu. *(Makofi)*

Kama Waheshimiwa Wabunge tunapewa heshima kubwa, unapewa Bendera ya Taifa unapeperusha barabarani, unataka heshima kwa Waheshimiwa Mapolisi na wengine, kama kauli hizi zinatolewa na viongozi ambao kimsingi wanajua kwamba kwenye Bunge hili tunaye Waziri wa TAMISEMI ambaye anawajibisha watu hawa ambao wanasema maneno pale nje, wanajua kwenye Bunge hili amekaa Waziri ambaye anashughulika na mambo ya Utumishi Bora na Utawala wa Kisheria humu ndani kwenye hili Bunge. Wanajua bila shaka kwamba humu ndani yupo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiyo msimamizi wa shughuli za Serikali hapa, wanajua kwamba humu kuna Spika wa Bunge na ni mhimili ambao unajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nisiwachoshe Waheshimiwa Wabunge, uniombe nitoe hoja waniunge mkono, wapate fursa ya kutoa maoni yao na baadaye tupate Azimio la Bunge hili ili kulinda hadhi na heshima ya Bunge hili ili tuweze kuheshimiana kwa vizazi vya leo na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Endelea, sasa kwa sababu ya muda mimi nakupa, maana utarudia hayo hayo, lakini usizidi dakika kumi.

MHE. MWITA M. WAITARA: Anasema?

MWENYEKITI: Aah! Hapana, ngoja. Mngekuwa mnanielewa Waheshimiwa Wabunge, lakini basi kama mnataka kuwahisha, mimi huwa napenda tujifunze wote, yeye hatua ya kwanza ilikuwa aeleze kwa kifupi amefanya ile ya kwanza, ya pili ilikuwa kufafanua, utoe hoja sasa aweze sasa muone kama tunaelekea kwenye haki za Bunge. Ameeleza marefu, mimi nadhani kama mmeunga mkono mimi sasa nataka niitoe tu kwamba mujadili. Na kwa sababu ya muda nitaruhusu Wabunge wawili upande huu na huku wawili, tutatenda haki. *(Makofi)*

Tuanze na Mheshimiwa Chifu Kadutu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa hii. Kwanza nimpongeze mdogo wangu na binamu yangu Mheshimiwa Waitara kwa kuleta hoja yenye mashiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimehuzunika sana kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge tunafika mahali tunadharauliwa halafu watu tunaangalia tu. *(Makofi)*

Haya ambayo yametokea Dar es Salaam na kule alikosema Mheshimiwa Waitara hivi karibuni yametokea Manispaa ya Dodoma. Mkurugenzi anaongea na Wabunge kama watoto wadogo, anafinya midomo na kusema anamuweka ndani Meya, tunakwenda wapi kama Wabunge? Wenzetu mliokuwemo humu Bungeni kwa miaka mingi, dharau za namna hii hazikuwahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linakuwa jambo la kushangaza Wabunge ambao tunategemea kupata heshima na kwa sababu tunafanya kazi, pesa zote wanazochezea chezea hawa mikoani mpaka tuziidhinishe sisi hapa, kama hatukuidhinisha pesa yoyote hapa halafu mtu anasema tunasinzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hata ile sheria wenzetu kule Marekani, kila anayeteuliwa kwa ngazi zile kubwa lazima aletwe Bungeni, watu wa namna hii tuweze kuwamaliza hapa hapa, hatuwezi kukubali Mkuu wa Mkoa haheshimu Bunge, Mkuu wa Wilaya haheshimu Bunge, Mkurugenzi haheshimu Bunge, mimi sijawahi kuona. *(Makofi)*

Sisi ndio tunayoifanya Serikali hii, kwa mfano, sisi wa Chama cha Mapinduzi tumepambana kuhakikisha Serikali hii inaingia madarakani, hivyo hivyo, CHADEMA, CUF, wamepambana kivyao kuhakikisha wanafika hapo walipo, bila mapambano haya hata hao Wakuu wa Mikoa wasingepata uteuzi. Kwa sababu Rais wa CCM, mgombea wa CCM asingeshinda hawa wangetokezea wapi? *(Makofi)*

Watu tumetumia gharama zetu na hizi gharama tulizotumia ndiyo zinafanya Serikali au Chama cha Mapinduzi kipate ruzuku ya kutosha kuendesha Chama au Serikali hii iliyopo sasa isingekuwepo. Lakini watu wanadhani wao wako juu yetu sisi, mimi hapana, nadhani ifike mahali watu wawajibishwe. Tunaposema tumbuatumbua, haiwezekani, lazima Bunge liwe linaazimia watu watumbuliwe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kifupi najua watu wengi wanapenda kuchangia – mimi nilitaka kusema hivi; Bunge lifike mahali sasa tuazime, Bunge likisema linaishauri Serikali hii ni lugha nyepesi, lazima lugha ibadilike, Bunge linaazimia huyu atolewe kazini, hatuwezi kujenga Serikali ya watu wenye kiburi, haiwezekani watu wafanye kiburi kwa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza kwa taratibu zilizopo, kama niko sahihi au siko sahihi lakini lazima lugha ya Bunge ibadilike wakati mwingine tusiwe na lugha nyepesi ya kusema Bunge linashauri. Unapotaka kulitoa pepo, pepo halibembelezwi, unataka kupunga majini huwezi kubembeleza lazima ukazane kulipunga jini litoke, na hatuwezi kutoa pepo tuna lugha nyepesi nyepesi, pepo toka, haiwezekani, lazima pepo tulikemee. *(Makofi/Kicheko)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kadutu. Mheshimiwa Ester Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Musukuma. *(Makofi)*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja muhimu sana katika mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri jambo moja, nilipokuwa Chama cha Mapinduzi...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane bwana.

MHE. ESTER A. BULAYA: ...nilipokuwa Chama cha Mapinduzi nilipikwa, nikafundishwa *how to be a good political leader.* (Makofi)

Nimeomba niliseme hilo, na huku pia niliko nimeendelea kufundishwa hivyo, na moja ya sifa ya kiongozi ni kuwa na akiba ya maneno. Na jambo lingine tuliweza kufundishwa ni namna gani kila mhimili una majukumu yake na unapopewa madaraka usitumie madaraka yako vibaya usitumie madaraka yako kwa kujinufaisha wewe, tumia madaraka yako kwa kunufaisha Taifa na Watanzania kwa ujumla. (Makofi)

Sasa tumeona hivi karibuni vijana wanaoaminiwa, nasikitika sana kama Mbunge kijana, nasikitika sana wanatumia madaraka yao vibaya Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya na wengine wanakwenda mbali zaidi wanasema tuko karibu na bwana mkubwa tutaendelea kuwachafua, ninyi Bunge si lolote si chochote na tutawashughulikia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki kitukufu kina Waziri Mkuu kama kiongozi wetu wa Bunge, kina Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kina Spika ambaye anatuongoza pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kukubali chombo hiki kikashushiwa hadhi na watu ambao tunawapitishia bajeti hapa, eti kwa majigambo kwamba wako karibu na mabwana wakubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Waitara amezungumzia hapa suala la Mkuu wa Wilaya, hivi tunavyoongea, wakati tunachangia mjadala wa Kamati ya UKIMWI, mimi Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam amenipigia simu na kunitisha kwamba yeye yuko karibu na bwana mkubwa, atatushughulikia, sisi Waheshimiwa Wabunge si lolote si chochote na amesema ataanza na Mheshimiwa Musukuma, atakwenda kwa Mheshimiwa Halima Mdee, atakwenda kwa Mheshimiwa Ester Bulaya na amewataja baadhi ya Waheshimiwa Wabunge; kwa Mheshimiwa Sugu, kwa Mheshimiwa Msigwa, kwa Wabunge wengi tu, amewataja. Amesema ana mamlaka hayo, na amesema mnashangaa nini yeye kwenda Marekani, na alimpigia simu hata Mheshimiwa Esther Matiko akamwambia ameshakaa Ufaransa sana hakuna atakayemtisha, Bunge ninyi si lolote si chochote, amesema Wabunge hawana akili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makonda ni mdogo wangu mimi nilimwachia Idara ya Uhamasishaji na Chipukizi, alipita tu UVCCM hakutengenezwa kuwa kiongozi mzuri. Haiwezekani umepewa mamlaka ya namna hiyo, na ndiyo maana anafika hata katika mkutano wa hadhara unapiga simu unamuweka kiongozi wa nchi, Amiri Jeshi Mkuu kwenye *loudspeaker!* Ni dharau kubwa sana. Na sisi tunasema hatuwezi kama Bunge likadhalilika lakini pia hatutakubali kama kiongozi mkuu naye akadhalilika kwa kuwekwa *loudspeaker* katika mikutano ya hadhara, hilo lazima tuliseme hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyo huyo, wakati katika mwendelezo hawa Wakuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara aliendelea naye akasema Bwanausi, Mheshimiwa Chuachua, Mheshimiwa Mwambe si lolote si chochote na wenyewe wakamatwe. Mambo kama haya hatuwezi kuyaruhusu Waheshimiwa Wabunge tukiwa tunatekeleza majukumu yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Bwanausi alikuwa Meya wa Temeke, Mbunge wa chama chake pia, angesema Mheshimiwa Mwambe tugesema amefanya siasa, kwa hiyo tunaona ni namna gani wanavyotumia mamlaka yao vibaya. Sasa sisi tunasema... (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante!

MHE. ESTER A. BULAYA: ...na vyombo vya uteuzi... (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, ahsante! Basi! (Makofi)

Mheshimiwa Zitto!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dakika ngapi? Dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongea kwa dakika mbili na nusu tu halafu dakika mbili na nusu nyingine nitakuomba rufusa yako nimuachie Mheshimiwa Kubenea ameniomba nimgawie kidogo naye ana jambo anataka kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili na nusu zangu ni mambo yafuatayo:-

Kwanza, hoja ambayo iko hapa inahusiana na kifungu cha tatu cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ambacho kinazungumzia *freedom of debate* kwamba Mkuu wa Wilaya wa Arumeru na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wameongelea mambo ambayo yamejadiliwa na Bunge, jambo ambalo linakatazwa na Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge. Sio tu wao, hata Mahakama imezuiwa kufanya jambo hilo, sio tu *individuals* kama Wakuu wa Mikoa au Wakuu wa Wilaya, hata Mahakama imezuiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninapenda ninukuu maneno yako ya leo asubuhi wakati unatoa Mwingozo wa Mheshimiwa Heche, kwamba ni lazima tulinde hadhi ya Bunge kwa wivu wa hali ya juu sana, kwa sababu tusipolinda hadhi hiyo tutadharaulika sana. Na ndiyo maana leo Waheshimiwa Wabunge kote huko wanakopita ni rahisi sana DC kumjibu Mbunge anavyotaka, itafikia wakati hata Watendaji wa Vijiji watatujibu wanavyotaka. Na hata haya mambo ambayo tumeyashuhudia hivi karibuni ambayo tuliyajadili siku ya jana ya ukamataji na kadhalika, *guts* ambazo mamlaka nyingine zinapata kufanya hivyo ni kwa sababu hatujalinda hiyo hadhi ya Bunge kwa namna ambavyo inatakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba, na wewe mwenyewe umeona *atmosphere* ya ndani ya Bunge, hili jambo ni *cross party*, hili jambo ni la Waheshimiwa Wabunge kutaka hadhi yao kuweza kulindwa.

Lakini pili ni lazima tufuate taratibu zetu pia, kwa hiyo hatuwezi kuwa na azimio ambalo litaamua moja kwa moja kabla ya taratibu zetu zinazotakiwa ziweze kufuatwa.

Kwa hiyo, nina mapendekezo mawili; pendekezo la kwanza, napendekeza kwamba Bunge liazimie kwamba Kamati ya Bunge ya Maadili iwaite wahusika wanaotajwa katika mjadala huu na kama kuna Mbunge mwingine yeyote ana lingine lolote ambalo limetokea katika utendaji wa kazi ili waweze kuhojiwa na ku... (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kukubali na mimi nichangie hoja hii iliyopo mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI na mjadala huu juu ya Mkuu wa Wilaya, pamoja na kwamba ulianza kwenye ripoti ya Kamati, lakini ulitokana na mchango wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza na Mheshimiwa Juma Nkamia ambaye alizungumza kwa uchungu sana jinsi ma-DC walivyojitangaza Marais katika Wilaya zao.

Sasa suala hili ni suala zito sana, ma-DC wamekuwa wanafanya kazi bila kufuata utaratibu, wamekuwa wanakamata Wabunge wakiwa katika shughuli zao za Kibunge kwenye majimbo yao, wamekuwa wanatoa amri kana kwamba wao ni Polisi na Mahakama bila kufuata utaratibu. Bunge hili limejengwa kwa nguvu kubwa sana, Bunge limekuwa na hadhi kubwa sana. Wabunge hawa wametumia nguvu kubwa sana kuingia Bungeni, mchakato wa kuwapata Wabunge haukuwa rahisi kwenye vyama na kwa wananchi. Kwa hiyo ni lazima hadhi ya Bunge, heshima ya Bunge, utu wa Bunge ni lazima ulindwe kwa gharama yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmoja ya hawa wanaotajwa, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam anawapigia simu Wabunge akiwataja Mawaziri kwamba ndiyo wanaotuma Wabunge wamtukane yeye. Mmoja wa Waziri aliyetajwa ni Mheshimiwa Nape Nnauye. Huyu Mkuu wa Mkoa anagombanisha Serikali na Bunge, anajenga fitna kati ya Rais na Waziri Nape, anajenga fitna kati ya wananchi na wafanyabiashara na anajenga fitna kati ya wananchi na Wabunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa heshima kabisa, nakubaliana na hoja iliyopo mezani kwako na ninaunga mkono taratibu za Kibunge zifuatwe ili Mkuu huyu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya hawa waletwe kwenye Kamati ya Maadili, ajadiliwe bila kuangalia sura ya mtu kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru sana na niwatake radhi sana Wabunge pengine haya yote mimi ndiyo nimeyasababisha kwa kusema ukweli, lakini naomba wana CCM mnielewe, nimefika hapa kwa sababu ya kuwaambia wababishaji mambo ya ukweli.

Waziri wangu Mkuchika alikuwa shahidi nilipokuwa Mwenyekiti wa Halmashauri, niliwaambia watu ukweli na wakaniondoa. Mama Ghasia amekuwa Waziri wangu wa TAMISEMI, anajua. Kwa hiyo ukweli ndiyo umenifikisha hapa na nataka niwambie wana CCM na wana CHADEMA na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mimi ndiyo nimetajwa mchekeshaji, lakini ndugu zangu mimi ni Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa, nilishinda Mkoa mzima kasoro Madiwani wawili. Huyu anayeniita mchekeshaji hata Mwenyekiti wa Taifa upime na Katibu Mkuu na viongozi wengine, alikuwa DC Kinondoni, kilichotokea ni nini? Nani anakuwa mchekeshaji kati ya Makonda na Musukuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye *point*; ninaomba taratibu za Kibunge zifuatwe kwa RC huyu. Kama kweli anaweza akasema sisi tumekuja kusinzia, sijawahi kulala Bungeni. Yeye maana yake ana kamera zinazompelekea sisi kutuona tumesinzia humu ndani. Kama Wabunge wote tumeambiwa hivyo tunalala, kifuatacho ni nini? Tuna sababu gani ya kulipwa posho wakati tumekuja kusinzia, kwani *guest* hatuzioni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri amezidi kipimo na si hivyo tu, ni yeye anayemchonganisha hata Rais na wafanyabiashara. *Tension* iliyoko kwenye nchi hii Dar es Salaam siyo ya kawaida. Haiwezekani RC anafanya kazi za Intelijensia, RPC ana kazi gani? RSO ana kazi gani Dar es Salaam kama kila kitu anafanya RC? Halafu baadae anakuwa na kiburi cha kusimama na kulijibu Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu wa CCM, Serikali ni ya wananchi. Ibara ya 8 imetueleza, Serikali ni mali ya wananchi na Wabunge waliomo humu wameletwa na wananchi, kwa nini tutukanwe na wananchi wetu? (Makofi)

Wananchi waliowaamini Wabunge hawa bila kujali vyama vyao, tumo humu kwa ajili ya kura, mimi nilipata kura 55,000 niliwashinda Maprofesa kibao watano halafu mtu ananiambia nimekuja kulala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani mapendekezo yangu; Wewe ni kiongozi Mkubwa sana kwenye hili Bunge. Iitishwe hata Kamati ya dharura ili kuonesha msisitizo wa hii kazi. Kamati ya Uongozi ikae dharura mtoe tamko kama Bunge vinginevyo nataka niwaambie bora mtunyang'anye hata hizi bendera hazina maana tutaenda kuzomewa vijijini. (Makofi)

Ushauri wangu mimi ninaomba Bunge lichukue maazimio ya kuazimia, tumeona wakati hatujawa Wabunge. Mliambiwa ninyi ni wajinga wakati wa Jairo, *Hansard* zinakumbukumbu, mlimuazimia Jairo humu ndani alitoka, leo Makonda ni nani kwenye hii nchi? Kama Jairo alitoka leo Makonda ni nani ayeweza kutufanya Wabunge tukaacha kufanya kazi zingine za Kibunge kujadili Makonda mtu mwenye barua ya Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana niliyoysema yaingie kwenye *Hansard* na mimi niko tayari kwa mapambano na Makonda hata tukitoka humu. Ninaomba taratibu zifuatwe ili tuweze kutoa tamko kama Bunge, suala la Musukuma na Makonda tutakutana mtaani, nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa AG dakika mbili. No, in all fairness dakika tatu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tuna Mwongozo kwenye katiba yetu, ibara ya 13(6) inasema; "Wakati haki na wajibu wa mtu yoyote inapotakiwa kufanyiwa maamuzi na Mahakama au chombo kingine chochote kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na pia haki ya kukata rufaa ya kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamesema kwa uchungu sana juu ya baadhi ya viongozi wa Serikali ambao wanadaiwa kukiuka Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge. Na Bunge hili Tukufu lina Kamati yake ya haki, Kinga na Madaraka. Na namna pekee kwa mujibu sasa wa masharti ya Katiba kuwawezesha hawa watu wanaotuhumiwa nao waweze kusikilizwa ni kwa kupata fursa ya kuenda kwenye hiyo Kamati wakasikilizwe na kwa sababu hiyo naomba kushauri, badala ya Bunge kuazimia kwamba wanaotuhumiwa wawajibuishwe na Serikali na Mamlaka ya uteuzi, kwanza wapewe fursa ya kusikilizwa na itakapokuwa Kamati imejiridhisha.

(Hapa Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge...

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge...

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Kuhusu Utaratibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:.....Kamati itakapokuwa imejiridhisha.....

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: ...kwamba hawa wanaotuhumiwa wamekiuka Haki na Madaraka ya Bunge...

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: ndipo Bunge linaweza kuazimia kumshauri Mamlaka ya uteuzi wamchukulie hatua za kinidhamu. Naomba kushauri.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa dakika moja/mbili hivi za kuzungumza jambo hili. Ninasimama kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ninaomba kutambua kwamba Bunge linayo haki ya kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa Kanuni ambazo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ninaomba tu niliarifu Bunge hili; ninawashukuru Wabunge wote waliochangia hoja hii katika jambo hili ambalo limezungumzwa na kuchangiwa na Wabunge, ninaomba kukubaliana nao kwamba Mheshimiwa Rais atasimama yeye mwenyewe peke yake kwa mujibu wa Katiba na madaraka aliyonayo na hawa watendaji ambao Mheshimiwa Rais anawateua na kuwakabidhi madaraka kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 34(4) watatekeleza majukumu yao wakimwakilisha Rais kwa utaratibu ambao unatambulika Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea majukumu waliyokabidhiwa wawakilishi na watendaji wa Mheshimiwa Rais ninaomba kuendelea kusesitiza, nikubaliane na Wabunge kwamba jambo hili kila mtendaji basi atapewa haki ya kufuatiliwa mienendo ya utendaji wake, lakini kushughulikiwa katika mambo aliyoyafanya kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu bila kumuhusisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo sasa, kwa kuwa hoja hii imeletwa mbele ya meza yako, sasa wewe utakuwa na haki ya kuiongoza na kuihitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madaraka ya kiti chako utaiiongoza hoja hii na kuihitimisha kwa kuzingatia haya niliyoyasema ambayo...

(Hapa Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Malizia, malizia.

WABUNGE FULANI: Unamuelekeza Spika wewe nani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti ambayo....

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane basi

MHE. HALIMA J. MDEE: Amuelekeza nani bwana? Achangie hoja zake.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:...Mheshimiwa Mwenyekiti ambayo.....

MHE. HALIMA J. MDEE: Kwani unafikiria Mwanasheria Mkuu...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: ...Mheshimiwa Mwenyekiti, ambayo ni lazima Mheshimiwa Rais aendelee kulindwa kwa mujibu wa Katiba tuliyonayo.

MBUNGE FULANI: Kwani nani aliyemtaja Rais?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mtoa Hoja.

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara mtoa hoja.

MBUNGE FULANI: Anatuharibia hoja yetu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: *President is okay on this one, President is okay on this one.*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana na nawashukuru sana waheshimiwa Wabunge kwa kuniunga mkono kwa nguvu zote katika hoja hii ya muhimu sana ambayo ni kwa ajili yetu sisi sote, lakini niwashukuru wale wote ambao wamepata fursa ya kulisemea jambo hili kwa uchungu mkubwa.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi nikujibu tu kwamba hakuna mtu amemtaja Mheshimiwa Rais hapa na naendelea ku...na katika kutoa hoja tumezingatia hilo, tunajua kwamba Rais hajawatuma hawa ndiyo maana tukasema Bunge liazimie dhidi yao wao. Wamepewa fursa, wameshindwa kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mapendekezo ya maazimio. Ninapendekeza kwamba Bunge liazimie kuwa DC wa Arumeru na RC wa Dar es Salaam ambao ni Paul Makonda waitwe kwenye Kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge wajieleze na itakapothibitika basi wachukiliwe hatua za kinidhamu kwa sababu wanaweza kushtakiwa kwa sababu wamevunja sheria ya kudhalilisha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili; niombe Bunge liazimie kwamba Waziri mwenye dhamana hii atoe maelekezo mahsusi kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya namna ya

kufanya kazi zo bila kuingilia mihimili mingine na hasa kudhalilisha Wabunge katika maeneo yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza azimio la tatu la Bunge kwamba vyombo vingine vyote vilivyokuwa vinafanya kazi, mamlaka nyingine inapokuwa inafanya kazi na ikihitaji Wabunge kwa mashitaka ya aina yoyote ile, Bunge liazimie itakuwa ni muhimu au ni lazima, Spika wa Bunge hili ajulishwe kwa ajili ya Mbunge fulani kupelekwa au kushitakiwa katika maeneo fulani kwa maana ya *notification*. *(Makofi)*

Azimio la nne na la mwisho, ninapendekeza kwamba mamlaka za kinidhamu baada ya kuitwa kwenye Kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge wakapewe fursa ya kusikilizwa kama alivyopendekeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wawajibishwe kinidhamu ikiwa ni pamoja na kuachia nafasi hizi ikiwa ni pamoja na kuachia nafasi hizi kwasababu wameshindwa kuzitumia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ili kuungwa mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya, Waheshimiwa Wabunge muda mnajua tunafungwa na Kanuni, lakini mnaona pamoja na kujifunza mnaona kwanini nilikuwa nataka nijiridhishe na hatua ya kwanza.

Sasa Bunge tumeletewa maazimio hapa ambayo ninyi mmemsikiliza tu mwenye hoja lakini hamnayo hapa, ndiyo tatizo hilo nilikuwa nawaambieni. Ni uamuzi wa Bunge lakini hii ingelikuwa imeandikwa wewe utakuwa umeona kwamba hii...

MBUNGE FULANI: *Hansard*.

MWENYEKITI: *Hansard* ndiyo, lakini ninyi ni Wabunge huwezi kusingizia *Hansard*.

Kwa hiyo, sasa mimi nitawahoji muamue hoja hii ambayo azimio hili lina maeneo manne, sasa nitawahoji. Wanaoafiki azimio kwanza linalopendekezwa na Mheshimiwa Waitara kwamba Waziri mhusika wa TAMISEMI atoe waraka kwa wahusika namna ya utekelezaji wa majukumu yao, pili, waitwe wahusika kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

La tatu, endapo itaridhika na kuridhika itakuwa baada ya kamati ile kuwasilisha taarifa Bungeni na Bunge likaridhia kwamba kuna *criminality*. Sasa Sheria yetu ya Bunge inatoa Madaraka kwa AG kufuatilia na vyombo vingine vya dola, sisi hatuwezi kufika huko, tunaishia hayo yatakayoletwa na Kamati na suala hilo la uwajibikaji linaenda pamoja na hayo ambayo yatakayoletwa na Kamati. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya *modification* hiyo ya azimio sasa nawahoji. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

WABUNGE FULANI: Chenge, Chenge, Chenge. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa azimio hilo, tuendelee hivyo sasa nina tangazo.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba kesho tarehe 9 Februari kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu mpango wa kunusuru Kaya masikini. Semina hiyo itaratibiwa na TASAF na itafanyika katika Ukumbi huu huu wa Bunge saa saba mchana baada ya shughuli za Bunge kusitishwa. Baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

MBUNGE FULANI: Mtemi Chenge.

*(Saa 2.15 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 9 Februari, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*